Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Tatu – Tarehe 12 Aprili, 2012

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kusimama. Waheshimiwa Wabunge tutakumbuka kwamba tumepata misiba mikubwa hivi karibuni, kama ilivyo ada nitaomba tusimame kwa heshima ya mwakilishi wa Jimbo la Bububu Mheshimiwa Salum Amour Mtondoo. Lakini vile vile Mkuu wa Majeshi Mstaafu Jenerali Mwita Kyaro, lakini vile vile Mkuu wa Jeshi la Polisi Mstaafu, Marehemu Harun Mahundi naomba tusimame kwa dakika moja tukiwakumbuka.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kuwakumbuka waliotutangulia mbele ya haki)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shughuli za asubuhi ya leo naomba niwakumbushe Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla kwamba leo tarehe 12/04/2012 ni siku ya Kumbukumbu ya kifo cha mpendwa wetu aliyekuwa Waziri Mkuu Ndugu yetu Edward Moringe Sokoine na Kumbukumbu yake Kitaifa leo itafanyika kule Morogoro ambako kutakuwa na ibada kwa ajili hiyo.

Kutakuwa na basi ambalo litaondoka hapa kwenye saa nne. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao watapenda kufanya hivyo tuingie katika usafiri huo.

## KIAPO CHA UTII

Wabunge wafuatao waliapa Kiapo cha Utii na kukaa katika nafasi zao ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso
Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari

*(Hapa Wabunge walishangilia na kupiga vigelegele baada ya Kiapo)*

**NAIBU SPIKA:** *Order.* Katibu hatua inayofuata.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA URATIBU NA BUNGE:** Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia Tarehe 30 Juni, 2011. *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statements of the Local Government Authorities for the year ended 30$^{th}$ June, 2011)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY GEORGE TEU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kupitia kwako kabla ya kuwasilisha Hati Mezani naomba nitoe taarifa fupi ndani ya Bunge lako Tukufu kwamba katika mkutano wa Umoja wa Mataifa *(The United National General Assembly)*, uliofanyika Novemba, 2011.

Mkutano huu uliridhia kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Tanzania Ndugu Ludovick Utoah, *(The Controller and Auditor General of the United Republic of Tanzania)* na ofisi yake kuwa mmoja wa Wajumbe wa Bodi ya Ukaguzi wa Mahesabu pamoja na *programs* mbalimbali za Umoja wa Mataifa kuanzia tarehe 1 Julai, 2012 kwa kipindi cha miaka 6 mfululizo.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Tanzania ataungana na wenzake kutoka *Supreme Audit Institution ya China* na *Supreme Audit Institution* ya Uingereza kuunda Bodi ya ukaguzi wa umoja wa Mataifa kwa kipindi chote cha miaka 6. Kupitia uteuzi huu Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itapata fursa nzuri na uzoefu wa kujenga uwezo wa kushiriki *issues* mbalimbali za ukaguzi wa kimataifa na hii ni motisha kubwa kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Hii ni heshima kubwa kwa ofisi na nchi kupata fursa hii ambayo nchi nyingi wanachama wa Umoja wa Mataifa walikuwa wanainuia. Kupitia Ukaguzi huu nchi yetu itapafa fedha za kigeni yaani forex kupitia ada za ukaguzi zitakuwa zinalipwa na Umoja wa Mataifa. Serikali itatoa *support* kwa kadri itakavyoona inafaa katika kutekeleza jukumu hili la ukaguzi wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba sasa uniruhusu kuweka Mezani Hati zifuatazo:-

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu kwa Mwaka ulioishia Tarehe 30 Juni, 2011 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statements of the Central Government for the Year Ended 30th June, 2011).*

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Juu ya Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya

Umma kwa Mwaka 2010/2011 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year 2010/2011).*

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi Jumuifu wa Ufanisi na Upembuzi kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Machi, 2012 *(Report of the Controller and Auditor General of Tanzania on the Performance and Forensic Audit conducted for the period ending 31st March, 2012).*

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Juu ya Hesabu zilizokaguliwa za miradi ya Maendeleo kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 *(Report of the Controller and Auditor General of Tanzania on the Audit of the Financial Statements of Donor Funded Projects for the year ended 30th June, 2011).*

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ripoti ya Ufanisi inayohusu Ukaguzi wa Magari na Udhibiti wa Mwendo wa Magari katika kupunguza Ajali za Barabarani *(A Performance Audit Report on the Management of Traffic Inspections and Speed Limits in Tanzania).*

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi wa Ofisi za Balozi *(Report of the Controller and Auditor General of Tanzania on the Audit of the Financial Statement of the Tanzania Embassies/Mission for the Year ended 30th June, 2011).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Tanzania kwa Mwaka 2010/2011 *(The Annual Report and Accounts of the National Audit Office of Tanzania for the Period 2010/2011).*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha tunakushukuru sana. Swali la kwanza kwa siku ya leo litaulizwa na Mheshimiwa Mariam Ruben Kasembe.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, …

**NAIBU SPIKA:** Nitakupa nafasi baada ya kipindi cha Maswali na Majibu nitakupa nafasi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Samahani, Kiongozi wa Kambi Upinzani Bungeni ndio anatakiwa kuanza kuuliza swali.

**NAIBU SPIKA:** Kiongozi wa Upinzani Bungeni alisimama? Kiongozi wa upinzani Bungeni una swali? Sikukuona samahani.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuomba/kutoa pole kwa Watanzania wote ambao wamefikwa na misiba ambayo ilikumba taifa siku za karibuni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa muda mrefu yamekuwepo matamko mbalimbali yanayotokana na Viongozi wa Serikali na mengine yakitoka kwa Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kwamba maeneo ambayo Watanzania wanachagua Vyama vya Upinzani kuwa wawakilishi wao katika vyombo vya maamuzi kama Madiwani na Wabunge hayatapata mgao wa fedha za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba sasa kauli yako kama kauli ya Serikali uwaeleze Watanzania kupitia Bunge hili kama ni kweli Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi ina Sera ya Ubaguzi katika mgao wa pato la taifa na kama kweli Sera hiyo ipo ni kikao gani kinachokaa kufanya mgao huo zaidi ya Bunge la Bajeti ambalo sisi wote tunakaa hapa kwa maana ya wawakilishi wetu wa Tanzania kutoka Vyama vyote

ambavyo vimepigiwa kura. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba utupe majibu hayo. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima nionyeshe masikitiko yangu sana kwenye swali hili kwa sababu limeulizwa kijumla na linatoa picha kana kwamba anayoyasema ndio mambo yanayotekelezwa wakati anajua kabisa kwamba hiyo si kweli. Hakuna mahali popote hapa nchini ambako hatujapeleka fedha kulingana na mgao wa taifa bila kujali kama eneo hilo ni la CHADEMA la CUF au la Chama kingine chochote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kidogo nimestushwa na hiyo kauli lakini basi labda niishie hapo tu. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na masikitiko yako napenda kukufahamisha kwamba kauli kama hizi zimekuwa zinatolewa mara kwa mara na ninaweza nikatoa mifano halisi na mfano wa kwanza kauli hizi zimetolewa na Waziri Mheshimiwa Mary Nagu wakati wa Kampeni za Uchaguzi katika Jimbo la Arumeru Mashariki.

Kauli kama hizi zimetolewa na Naibu Waziri wa Ardhi katika Jimbo la Arumeru Mashariki, Mkoani Arusha. Matamshi kama haya yaliwahi kutolewa na Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Magufuli katika kampeni za Igunga. Mheshimiwa Waziri Mkuu ahadi kadhaa zimekuwa zinatolewa na Serikali wakati wa kampeni kipindi ambacho kinajulikana kabisa kwamba ni marufuku kwa watendaji wa Serikali kutoa kauli kama hizo na umarufuku huo unatiwa halali na hukumu iliyofanyika katika Jimbo la Kigoma Mjini kufuatia kauli iliyotolewa na Serikali pamoja na ziada ya Rais Mheshimiwa Mstaafu Mzee Mwinyi wakati wa ziara katika uchaguzi wa Jimbo la Kigoma Mjini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge sasa swali.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu unatuambia vipi tutakapoweza kukudhihirishia kwamba kauli hizo zimetoka na utachukua basi hatua gani kwa Mawaziri wako ambao wametoa kauli hizo? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri Watanzania tuendelee kujenga demokrasia yetu tumejitahidi sana. Serikali hii itaendelea kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Nchi hii katika mgao wake wote wa fedha.

Sasa kama kuna kauli nyingine, kauli zinatoka, nyingine kwenye mapambano wakati wa chaguzi na nini mimi nasema tutaendelea kuheshimu Katiba na Sheria. (*Makofi*)

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kuwapa pole sana Wakulima wa Zao la Korosho popote walipo nchini na hasa wale wakulima wangu ninaowawakilisha katika jimbo la Masasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali iliandaa utaratibu mzuri wa stakabadhi ghalani ili kuwasaidia wakulima wetu wa zao la korosho waweze kuuza korosho zao kwa uhakika na kuleta tija kwa wakulima ili waweze kuendesha maisha yao vizuri.

Kwa misimu miwili ya mwanzo stakabadhi ghalani ilikwenda vizuri na wakulima waliupokea utaratibu huu kwa furaha sana kwa sababu ulileta tija na ulikuwa na mwelekeo wa kuleta maisha bora. *(Makofi)*

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu katika msimu huu, kibao kimegeuka, wakulima wetu hawajauza korosho zao, hawajalipwa pesa zao na hivi sasa ninavyozungumza msimu mwingine wa palizi za korosho na kupulizia unakaribia na wakulima hawana hata fedha za kununulia pembejeo.

Sisi Wabunge wa Mkoa wa Mtwara tumekuwa tukijitahidi sana kuja kwako wewe Waziri Mkuu ili usimamie suala hili; kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na hatimaye kwa Mheshimiwa Rais, lakini hadi hivi sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kwa ajili ya kuwalipa wakulima wetu.

Je, Serikali hadi hivi sasa inawafikiria nini wakulima hawa au ina utaratibu gani wa haraka zaidi ili kuwalipa wakulima wetu wa zao la korosho waweze kujikimu katika maisha na ukiangalia hali ya ukali wa maisha ilivyo, watu hawa wako katika hali ngumu sana! Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la korosho ni eneo moja ambalo ni kweli limeleta matatizo kwa wakulima safari hii kama ilivyotokea kwenye pamba, ilitokea kwenye zao la tumbaku. Moja ya sababu ni ule utaratibu wa upangaji wa bei dira. Kwa hiyo, tunapopanga bei dira halafu gafla bei ya soko ikabadilika mnaingia kwenye mgogoro wa namna ya kuuza mazao hayo. Lakini kwa upande wa korosho kwa uzalishaji uliokuwa umefanyika katika kipindi cha msimu huu, Serikali iliweza kulipa fedha kwa kiwango cha karibu asilimia sabini kwa wakulima.

Kwa hiyo, tulibaki na asilimia thelathini ambayo tulikuwa hatujalipa na kulikuwa na korosho ambazo zilikuwa bado mikononi mwa wananchi, lakini kwa sababu fedha hizi ni fedha ambazo zinatoka kwenye mabenki kwa kutumia mfumo wa mikopo, kwa hiyo, tulilazimika kuingia katika utaratibu wa kuomba vyama vya ushirika vipewe mkopo mwingine kuweza kugharamia korosho zilizobaki pamoja na asilimia thelathini. Kwa hiyo, tulichelewa kidogo kwa sababu ya ukusanyaji wa takwimu kutoka kwenye matawi mbalimbali nchini, Mtwara walifanya vizuri waliharakisha. Lakini Lindi kidogo walichelewa sana kuwasilisha hizo takwimo. Lakini zoezi hilo limemazilika na inakadiriwa kwamba zitahitajika kiasi cha shilingi bilioni 29. Kwa matumaini yangu ni kwamba leo au kesho takwimu zile

zitawasilishwa kwa Gavana wa Benki Kuu ili fedha zile ziweze kutolewa kwa ajili ya malipo ya korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, korosho hizo *ofcourse* zimetolewa kwa mkopo kwa maelewano na Benki Kuu kwamba tutadhamini mkopo huo kwa asilimia mia moja na ilikuwa na ilikuwa kidogo ndiyo eneo lililokuwa na mvutano kidogo lakini hatimaye Ganava wa Benki Kuu amekubali. Kwa hiyo, nataka nimwombe tu Mheshimiwa Kasembe pamoja na Wabunge wote wa Mikoa hiyo na wananchi kwa ujumla kwamba jambo hili limesimamiwa, limechukua muda kidogo, lakini hatimaye tumelimaliza.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa sasa tumekuwa tukiona hali ya kuyumba kwa mazao ya wakulima wa korosho, pamba hata mahindi na sasa hivi tuko kwenye muelekeo wa bajeti. Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kutenga fungu ambalo tulifanye kama ni fungu la dharula ili inapotokea tatizo kama hili Serikali iweze kukabili mara moja? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazo zuri lakini sisi tunafikiri utaratibu mzuri ingekuwa kwa wakulima wa mazao haya kwa kutumia vyama vyao vya ushirika, wao kukaa chini na kuamua kuwa na mfuko maalum ambao utachangiwa kutokana na zao hilo, usimamiwe na wao wenyewe ili inapotokea jambo kama hilo, basi uwepo utaratibu wa kuweza kuziba lile pengo kwa kiasi watakachokubaliana. Kwa hiyo, rai yake ni ya msingi lakini na sisi upande wetu tunafikiri Serikali itajaribu kuzungumza na vyama hivi kuona uwezekano huo na kwa bahati nzuri upande wa zao la pamba tayari walishaanza mazungumzo haya naamini hata kwa mikorosho tunaweza tukazungumza kwa kutumia mfumo huo huwo ili tuweze kuondokana na hili tatizo la bei kupanda na kushuka.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ningependa nimwulize

Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja hasa ukizingatia nimeamka saa tisa alfajiri nilishangaa ilivyoanza vinginevyo nilitaka kusikitika lakini nashukuru nimepata nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wastaafu wa Shirika la *TAZARA* wamekuwa wakidai mafao yao kuanzia mwaka 2007 na wamekuwa wakipewa ahadi mbalimbali za Serikali wakati wa Bajeti pamoja na viongozi mbalimbali waandamizi wa Serikali kwamba watalipwa malipo yao muda si mrefu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wastaafu hawa ni Watanzania, wametumikia nchi yao kwa uadilifu na uaminifu mkubwa, ningependa kujua kauli ya Serikali ni nini kuhusiana na malipo ya wastaafu hawa wa *TAZARA?* Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na tatizo hilo la malipo ya mafao ya wastaafu wa *TAZARA,* lakini yako matatizo mengine mengi vile vile kwenye Shirika hili la *TAZARA* ambayo tunaendelea kuyashughulikia, lakini hususani hili la mafao kwanza tulitaka tuwashukuru sana wafanyakazi hawa kwa sababu katika mkutano wao wa mwisho na Serikali baada ya majidiliano nao walikubali sasa kwamba basi Serikali ijaribu kuona namna itakavyolipa zile bilioni 22 na wamekubali kwamba zilipwe kwa awamu. Kwa hiyo tumekubaliana kwamba tutatoa fedha hizo kwa awamu tatu, bilioni 7 awamu ya kwanza, bilioni 7 awamu ya pili na bilioni 7 awamu inayofuata. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kairuki jambo hilo tunalikamilisha sasa hivi na tutalipa hizo fedha kwa awamu kama tulivyokubaliana na tunaomba tu wavute subira kidogo ili tuweze kulimaliza.

Lakini wakati huo huo Serikali imeona ni vizuri tutazame tatizo la *TAZARA* kwa upana wake. Kwa hiyo, tumeomba Mawaziri wanaohusika upande wa Zambia na Tanzania wakutane ili tuweze kwa kweli kuona namna bora zaidi ya kuimarisha chombo hiki kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza matatizo ambayo yanawakabili. (*Makofi*)

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Waziri Mkuu kwa majibu yako, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu kauli kama hizi na ahadi kama hizi, zimekuwa zikitolewa kuanzia tarehe 26 mwezi wa kumi mwaka 2011 kupitia kikao cha Mheshimiwa Waziri na wastaafu hawa, lakini vile vile tarehe 29 mwezi Desemba mwaka 2011 kupitia Katibu Mkuu wa Uchukuzi, Wastaafu, Menejimenti ya *TAZARA* pamoja na Menejimenti ya pensheni ya Bima.

Lakini vile vile pamekuwa na kikao kupitia maamuzi mbalimbali ya Serikali ya mwezi Novemba mwaka 2011 kupitia Waraka Na. 2 wa mwaka 2011. Napata tabu, ningependa nisikie leo hii *commitement* ya Serikali kila awamu ya bilioni 7 italipwa lini? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Kairuki nimesema fedha hizo zitalipwa na tutazilipa kwa awamu. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ningependa kumwuliza Waziri Mkuu hali ya maisha ya Watanzania sasa hivi ni ngumu sana kutokana na mfumuko wa bei hasa katika vyakula.

Je, ni hatua gani ambazo Serikali itachukua kwa haraka ili kuweza kuokoa maisha ya Watanzania ambao wanahangaika sana kutokana na mfumuko huu wa bei wa ajabu kabisa? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa kwamba hali ya maisha kwa ujumla hapa Tanzania lakini hata nchi nyingine nyingi ni dhahiri kabisa kwamba ipo na kila nchi inajaribu kuhangaika kutafuta suluhu ya matatizo yake.

Sasa kwa upande wa Tanzania tunachoweza kusema tu ni kwamba bei ya vyakula ndiyo hasa inachangia kwa kiasi kikubwa sana katika tatizo hili la mfumuko wa bei na ndiyo

maana umeona Serikali imetumia nguvu zake nyingi kujaribu kutafuta kila mbinu, tuone kama tunaweza tukauza sukari kwa bei ambayo ni nafuu. Tuone kama wananchi wanaweza wakapata mpunga. Kwa mfano mchele kwa bei nafuu, unga vile vile kwa bei nafuu, lakini bado tatizo hili halijapata ufumbuzi wa moja kwa moja na wakati huo huo tunaendelea sasa kukabiliana na tatizo la ongezeko la bei ya mafuta ambayo hata karibuni imepanda tena. Kwa hiyo, ukiyachanganya mambo yote haya, ni kweli kabisa kwamba tatizo linalotukabili ni kubwa na hili linataka kwa kweli ushirikiano wa karibu wa watu wote, vyombo vyote na ndiyo maana tutaendelea kuwasii Watanzania tujaribu kwa pamoja kushirikiana hasa pale ambapo Serikali inachukua hatua za kujaribu kudhibiti mfumuko huu wa bei unaotokana na vyakula.

Tunawaomba vile vile hasa wafanyabiashara ambao baadhi yao sio waaminifu sana, hata pale ambapo Serikali imejitahidi kujaribu kuchukua hatua za kusaidia bado unakuta baadhi ya wafanyabiashara hawakutimiza wajibu wao inavyotakiwa, wameendelea kutoza bei kubwa. Kwa hiyo, kwa kweli kinachohitajika ni nguvu ya pamoja katika kujaribu kusimamia eneo hili.

Kwa hiyo, kwa upande wetu tutaendelea kama Serikali kutazama njia mbalimbali za kusimamia jambo hili la mfumuko wa bei na kuna zile *interventions* za moja kwa moja kupitia Gavana wa Benki Kuu kwa maeneo yanayomhusu, lakini lazima na sisi tuendelee na hizi jitihada. Wakati huo huo ni lazima tukubali kwamba ili tuweze kwa kweli kuwa na bei ndogo kwenye vyakula hivi ni lazima vizalishwe kwa wingi sana, lazima tupate vyakula hivi kwa wingi ili visambazwe nchini. Kwa hiyo, kazi kubwa ni Watanzania vile vile kufanya kazi kwa bidii zaidi hasa katika maeneo yale ambayo yanatuhusu. Kwa hiyo, tukichanganya nguvu nyingi pamoja hili jambo linaweza hatimaye likapungua na likatoa nafuu kwa Watanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu kwa kifupi sana, orodha yangu ni ndefu Waheshimiwa kama mtu angeweza kufupisha kidogo ningeweza kupata watu wengi, hivyo kifupi sana.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yanaeleweka, lakini ningependa kujua ni lini Serikali itakubali kupunguza uagizaji wa vyakula. Kwa mfano, mchele sasa hivi unatozwa ushuru asilimia 75.

Je, hatuwezi tukaangalia kwa kipindi hiki cha mpito tukapunguza gharama hii ya ushuru ambayo itapelekea kushusha kwa bei katika soko?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunayo baadhi ya mapendekezo ambayo tunayafanyia kazi sasa hivi kujaribu kuona ni maeneo gani pengine tungeweza tukachukua hatua za namna hiyo hasa upande wa vyakula. Ndiyo maana nimesema kubwa kwa kweli ni kujitahidi Watanzania kuwa watu ambao tunazingatia maslahi ya watu. Kwa sababu kwenye sukari tumejitahidi, tumeagiza sukari kutoka nje, tukaondoa ushuru wote. Lakini bado sukari iliyoletwa huoni ina unafuu wowote, bado bei ni kubwa licha hatua hizo ambazo tumechukua. Kwa hiyo, unaona changamoto hapa wala si suala tu la kusema upunguze ushuru, lakini inataka dhamira vile vile kwa wale ambao wameshika nyenzo hizi za utoaji wa huduma na wao kuwa watu ambao ni waelewa. Kwa hiyo, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mangungu, tutajaribu kutazama maeneo mengine. Lakini mimi bado nadhani ufumbuzi mkubwa utategemea zaidi sisi Watanzania.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka wa kibajeti wa 2011/2012 uko ukingoni kukamilika, Wizara nyingi tu takribani Wizara zote,Idara zote, Halmashauri, Mahakama zinalalamika ukosefu wa fedha, ufinyu wa Bajeti. Mheshimiwa

Waziri Mkuu, je ni kweli Serikali imefilisika? Au imekuwa na vipaumbele vingi na mipango mingi ambayo haitekelezeki?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rajab Mohamed kwa swali lake, lakini nataka nimhakikishie tu Serikali haijafilisika maana hata wewe usingekuwepo Bungeni hapa. (*Kicheko*)

Bado tupo, bado tupo ila ni kweli kwamba Bajeti yetu ni kali kidogo, kubanana ni kukubwa sana na tulilazimika hapo katikati kuchukua hatua zaidi za kubana matumizi hasa kwenye maeneo yale ambayo sio ya lazima sana kwa kupunguza kiasi fulani cha Bajeti yetu. Sasa lile *ofcourse* limesababisha kidogo kubanwa kukubwa kwenye maeneo haya.

Lakini ni jambo ambalo limeelezwa vizuri kwa vyombo vyote vinavyohusika na tumewaomba sana wajitahidi ndani ya Bajeti ambayo sasa tunaenda nayo basi wahakikishe fedha zile zinazopelekwa zisaidie kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Serikali. Hatutakwama, lakini tutafika mwisho wa mwaka tukiwa tumefunga mikanda kwa nguvu sana. Lakini lengo ilikuwa ni lazima tubaki katika utaratibu unaotuwezesha kuwa na Bajeti ambayo imezingatia uhalisia badala ya kujidanganya kwamba mna Bajeti kubwa ambayo kumbe ndani yake yaliyomo si ya uhalisia ndiyo hasa tunachojaribu kufanya sasa hivi.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeshuhudia matatizo katika sekta ya elimu ikiwepo watoto kukaa chini na walimu wapya kukosa malipo na kuishi katika maisha magumu. Serikali ilikuwa inafuatilia fedha ambazo ziko kwa jina la chenji ya rada na taarifa tulizokuwa nazo ilikuwa zitumike katika kuboresha sekta ya elimu na taarifa nilizozipata kutoka Uingereza ni kwamba ile chenji imerudi. Sasa swali langu kama ni kweli ni kiasi gani kimerudi na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lini hizo fedha zitapelekwa kwenda kunusuru sekta ya

elimu na zitagawanywa kwa utaratibu gani ili kuhakikisha kwamba zinatimiza kusudio lililokusudiwa? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru kwanza Mheshimiwa Mchemba kwa jambo hili na naomba nitumie dakika kidogo kulieleza. Ni kweli kwamba baada ya kesi ile kumalizika Uingereza, tuliingia katika mazungumza ya namna ya kurejesha zile fedha hapa nchini na hatimaye nadhani mwezi wa tatu tulifanikiwa kukubaliana nao *BAE,* kampuni ile halafu pamoja na kile chombo chao ambacho ni cha uchunguzi wa makosa makubwa SFID wakatoa zile fedha nadhani ilikuwa paundi za Uingereza 29.5 milioni ambayo ni karibu Shilingi bilioni 72.3.

Kwa hiyo, zile fedha zimeshapatikana tayari kupitia Benki Kuu na tunazo. Lakini tulikubaliana kwamba fedha hizi zikipatikana zisaidie katika uimarishaji wa sekta ya elimu na tulilenga hasa elimu ya msingi kwa sababu ndiyo kwenye matatizo makubwa zaidi. Kwa hiyo, tumekubaliana kupitia maelewano ambayo tumewekeana saini kwamba fedha hizi ziende sasa zikaimarishe ule mfumo wa kutoa ruzuku, fedha ambayo ilikuwa inatumika kwa ajili ya ununuzi wa vitabu kwa ajili ya wanafunzi.

Kwa hiyo, tumeshaelewana juu ya jambo hilo na fedha zile zitagawiwa sehemu itakwenda TAMISEMI ambao ndiyo wanasimamia eneo hili, lakini kuna fedha nyingine ambazo tumeomba zibaki Wizara ya Elimu pale kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zinahudumia sasa zoezi zima kwa ujumla.

Matumaini yangu ni kwamba zoezi hili tukilifanya vizuri, tutapunguza sana ile nakisi iliyopo ya vitabu katika shule za msingi. Na vitabu hivi tunazungumza vitabu vya ziada, kiada, tunazungumza vile vile mitala, tunazungumza miongozo ile kwa ajili ya walimu, vyote hivi ni sehemu ambayo tutatumia kwa ajili ya fedha hizo.

Lakini kwa maana ya usimamizi na ufanisi wa fedha hizo, tumeona kwamba tufungue akaunti maalum pale Benki Kuu na fedha hizi zitatolewa kwa utaratibu maalum kwenda kwenye maeneo yanayohusika na tumeomba hatimaye kwamba ni vizuri Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali apewe na yeye nafasi mwisho wa zoezi hili kufanya ukaguzi wa kina kuhakikisha kwamba zimetumika inavyotakiwa.

Kwa hiyo, naomba tu nitoe rai hasa kwa Watanzania kwamba fedha hizi zitakapokuwa sasa zimeanza kutoka kwenda huko kwa ajili ya ununuzi wa vitabu basi tuhakikishe tunapata vitabu, vitabu vyenye sifa na ubora unaotakiwa ili watoto wetu waweze kuvitumia kwa njia nzuri zaidi.

Lakini tuliona vile vile kwamba pengine tutumie kiasi cha fedha kidogo kwa ajili ya Halmashauri kama tisa hivi ambazo zina upungufu mkubwa sana wa madawati. Kwa hiyo, tutatumia kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa madawati kwenye Halmashauri kama tisa hivi, lakini kwa sehemu kubwa kiasi kingine chote kinachobaki kitakwenda kwenye vitabu.

Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Mchemba kwa jambo hili, tulikuwa tumefikiria baadaye tuje tutoe kauli Bungeni lakini nadhani hii itasaidia kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na mimi hapa kwa hatua hii nimshukuru sana Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Cheyo na mimi mwenyewe ambaye kwa niaba ya Bunge, Serikali na wananchi wa Tanzania tulienda kule Uingereza tukajitahidi fedha hii imekuja. Tupigieni makofi basi angalau. *(Kicheko/Makofi)*

Ahsante sana. Swali linalofuata linatoka kwa Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi nimwulize Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi sasa ni takriban miaka mitatu hadi minne tangu Serikali ianzishe mfumo huu wa kutoa pembejeo kwa wakulima. Lakini utaratibu wa kutoa hizo pembejeo umekuwa ni wa utata sana.

Kwanza pembejeo hizo zinachelewa kuwafikia wakulima kwa wakati. Sio tu wakulima wa Mkoa wa Manyara wanalalamika, lakini hata juzi tulikuwa katika Jimbo la Arumeru Mashariki, nilikuwa katika Kata za King'ori na Leguruki nimeona wakulima wanapalilia lakini Serikali ndiyo inapeleka pembejeo.

Swali, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lini sasa Serikali itagundua kwamba msimu wa kilimo unatakiwa kuanza mapema na hizo pembejeo zifike kwa wakati ili wakulima waweze kuzipata na walime kwa msimu unaotakiwa badala ya kuwapelekea wakati wao wanapalilia. Ni lini hili tatizo litakwisha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lini? Majibu sasa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tukubaliane kwamba Serikali ilibuni utaratibu huu kwa nia njema kwa sababu lengo lilikuwa ni kuwawezesha wakulima wadogo hawa waanze kutumia utaratibu huu ili waweze kuongeza tija katika uzalishaji.

Kwa hiyo, ni jambo jema na tumeanza nalo vizuri. Lakini ni kweli kabisa msimu uliyopita tulipata tatizo la ucheleweshaji wa vocha na ilitokana na hasa na taratibu zetu za manunuzi. Mkandarasi aliyekuwa amepatikana awali ilibidi baadaye tukamkataa.

Kwa hiyo, ikabidi kuanza upya tena. Kwa hiyo tukachelewa kutoa zile vocha na matokeo yake tukawa tumechelewa hata kwenye taratibu nyingine. Lakini tumelizungumza sana kwa upande wetu. Kwa sababu hilo ni moja ya tatizo lakini yako matatizo mengi sana kwenye mfumo wa vocha ambayo vile vile tumeyagundua.

Kwa hiyo, tulimwomba Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali atusaidie na yeye kufanya ukaguzi maalum wa vocha kwa sababu hoja ya kuchelewa tunaiona lakini tunataka vile vile kujiridhisha kama kweli wakulima hawa wanapata faida hasa kutokana na utaratibu huu? Au wajanja pale katikati ndiyo wanafaidika zaidi kuliko mkulima. Kwa sababu hili ndiyo limejitokeza katika baadhi ya maeneo.

Kwa hiyo, tumemwomba *CAG* na ameshaianza hiyo kazi nina hakika mwisho wake tutapata ushauri nzuri zaidi namna ya kuimarisha ikiwepo na hilo ulilolitaja. Nataka nikuhakikishie safari hii hatutachelewa hata kidogo na Mheshimiwa Jumanne Maghembe, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ameshaambiwa na tumesema tunataka jambo hili msimu unaanza tuhakikishe na vocha zenyewe zipo tayari kwa ajili ya zoezi hilo. Kwa hiyo, naamini tutalikabili vizuri katika kipindi hiki cha mwaka huu.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho kwa leo Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa ninavyo vielelezo ambavyo vinaonyesha Chuo Kikuu kimoja cha Mjini New York, Marekani ambacho kilifanya utafiti kuhusu minofu ya samaki wa Ziwa Victoria na ikaonyesha kwamba samaki wanaouzwa nchi za nje kutoka kwenye nchi ambazo zinazunguka Ziwa Victoria zina thamani ya milioni 344,500,000 (milioni mia tatu arobaini na nne na laki tano) hizo zikiwa ni dola za Kimarekani kwa mwaka.

Tanzania ikiwa ina nafasi kikubwa zaidi ya asilimia 50. Lakini taifa kubwa hapo katikati ambalo ndilo linanunua samaki hawa na kuwauza nje lenyewe linapata dola za Kimarekani bilioni moja na milioni arobaini na nane mia mbili sabini na mbili na mia tano thelathini. Ikiwa ni zaidi ya mara tatu ya pesa ambazo nchi zetu pamoja na Tanzania tunapata katika mauzo haya. Je, Serikali inalifahamu hili? Swali la kwanza hilo.

Pili, kama jibu ni ndiyo, kwa nini Serikali sasa isione kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuliondoa hili Taifa la katikati ambalo ndilo linafaidi minofu ya samaki wa Ziwa Victoria na kutafuta kila jitihada za kuuza hawa samaki sisi wenyewe Ulaya na Marekani ili kwanza tuboreshe maisha ya wananchi wa Kanda ya Ziwa pamoja na Taifa kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba majibu yatayoridhisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mataifa haya yanayoendelea kama Tanzania, eneo moja ambalo lina changamoto kubwa sana ni hilo alilolitaja Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwamba bado nchi nyingi hizi tunauza mazao yetu bila kusindikwa. Kwa hiyo huko tunakouza ndiyo wanaofaidika zaidi kuliko sisi wenyewe ambao tunauza mazao bila kusindika na pale tunapofanya jitihada za kusindika inakuwa ni usindikaji lakini ambao si kamilifu. Kwa hiyo, bado sehemu kubwa watakaofaidika ni wale walioko nje. Ndiyo maana jitihada za Serikali sasa ni kujaribu kuimarisha viwanda vyetu hapa ndani kwa nguvu zaidi kwa kutumia mfumo huu wa *Export Processing Zones* ambao tunadhani utatusaidia kuweza kuongeza thamani ya mazao yetu kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mfano alioutoa wa samaki ambao wengi wanavuliwa kutoka Ziwa Victoria ni kweli na mimi taarifa hizo nimezipata, ninazo. Kwa hiyo, nataka niungane na

Mheshimiwa Mama Malecela kwamba tupange utaratibu sasa ambao utatuwezesha, si kuuza minofu, lakini tuone kama tunaweza kutumia utaratibu ambao utatuwezesha. Minofu ile iweze kusindikwa ifungwe na kuuzwa moja kwa moja kwenda kwa mlaji baada ya kuzingatia taratibu zile za ubora unaotakiwa, mimi naamini linawezekana.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mama yangu Anne Kilango Malecela pale kwamba jambo hili nimelipokea na juzi nimewaandikia Wakuu wa Mikoa wote wa Kanda ya Ziwa kwamba watafute katika kikao chao cha pamoja cha uwekezaji wanadi hili wazo la namna ya kuongeza thamani ya zao hili la samaki kwa kuona uwezekano wa kuwa na mwekezaji katika Kanda ile ambaye atafanya kazi si ya kuuza minofu lakini kazi ya kuitengeneza hiyo minofu kwa kiwango kinachotakiwa ili kiweze kuuzwa nje bila kupitia kwa mtu mwingine ambaye anafaidika zaidi kuliko sisi wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawashukuru sana wale maprofesa wa Marekani ambao ndiyo wamefanya uchunguzi huo, utafiti huo na baadaye wametuletea mawazo haya. Lakini nikushukuru vile vile Dada Anne Kilango Malecela kwa sababu na wewe ulilifuatilia kwa nguvu sana jambo hili na ndiyo maana nikatoa majibu na maelekezo haraka sana kuhakikisha kwamba jambo hili sasa tunalipa nafasi kubwa katika Taifa letu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kimeisha. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yako fasaha, kama kawaida yako. Ahsante sana. *(Makofi)*

Katika kipindi hiki cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumepata maswali kutoka kwa kiongozi wa Upinzani Bungeni na Wabunge wengine sita. Kwa hiyo, kwa ujumla tumeweza kupata Wabunge saba. Naomba niwashukuru wale wote mliopata nafasi ya kuuliza maswali. Kwa wale wengine

ambao hawakupata nafasi, Kwa kweli muda wetu haukuweza kuruhusu tutajitahidi wakati mwingine. Kama utaratibu wetu ulivyo kwa hao waliouliza leo wiki ijayo hawatapata nafasi itakuwa ni zamu ya *grou*p lingine. Katibu tuendelee na *Order Paper. (Makofi)*

**MASWALI YA KAWAIDA**

Na. 30

**Viti Maalum Zanzibar Kutoshirikishwa Katika Mfuko wa Jimbo**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Zanzibar ni nchi na sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

(a) Je, ni kwa nini Wabunge wa Viti Maalum Zanzibar hawashirikishwi katika mfuko wa Maendeleo wa Jimbo?

(b) Je, kwa nini Wabunge sio Wajumbe wa Baraza la Madiwani kama ilivyo kwa wenzao walioko Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Na. 16 wa mwaka 2009 unahusu maendeleo ya majimbo ya uchaguzi, iliyopo haijawajumuisha Wabunge ambao hawawakilishi majimbo ya uchaguzi

yaliyoanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 75 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wabunge wanaotoka Tanzania Zanzibar kutokuwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani kama ilivyo kwa Wabunge wa Tanzania Bara. Jambo hili linatokana na Sheria zinazosimamia uanzishaji, muundo na majukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa upande wa Mabaraza la Madiwani Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ifahamike kuwa Sheria ya Serikali za Mitaa Namba 8 ya mwaka 1982 Mamlaka za miji na Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 ya mwaka 1982 Mamlaka za Wilaya siyo Sheria za Muungano. Hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge kuwasilisha suala hili kwenye Baraza la Wawakilishi ili kama italazimu kufanya hivyo Sheria za Tanzania Zanzibar zirekebishwe kuwajumuisha Wabunge katika Mabaraza ya Miji ya Tanzania Zanzibar.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri yenye matumaini. Kwa kuwa pesa za mfuko wa jimbo kwa upande wa Zanzibar zimekuwa zina mzuko mwingi, hata hawa wabunge wa majimbo hawazipati kwa wakati muafaka.

Je, Serikali ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mtahakikishaje hizi fedha za Mfuko wa J imbo zinawafikia walengwa na kwa wakati muafaka? *(Makofi)*

Swali la pili. Kwa kuwa wanawake wengi wamekuwa ni chachu ya maendeleo katika jamii na katika mikoa. Je, Serikali mtahakikishaje wanawake hawa wanashirikishwa katika mfuko wa jimbo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi kilichopita kwenye Bunge hili lililopita Mwanasheria Mkuu

wa Serikali alikuwa anakuja hapa na mabadiliko ambayo yangesaidia katika kuhakikisha kwamba hela zinazokwenda kwa wenzetu wanaotoka Zanzibar yanakwenda vizuri ili kuondoa hili tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge analizungumzia.

Lakini baadaye kama mtakumbuka hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipokuwa anataka kuleta ile kukawepo na ile hali ya kusema kwamba turudishe. Kwa hiyo, tuliporudisha mle ndani kulikuwa kuna hayo mabadiliko ambayo Mheshimiwa Maryam anazungumzia hapa. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba itakapokuja tena sasa lile tatizo tutakuwa tumeliondoa pale na kwa hiyo hili tatizo halitakuwepo tena na hapo ndipo kwa kweli tunatakiwa tusimame imara kama kuna tatizo bado linaendelea basi pale tuzungumze vizuri ili kuondokana na hilo tatizo ambalo linasemwa hapa. *(Makofi)*

Sasa hili swali la pili hili, jamani mimi nilizaliwa na mama. Hayuko hapa duniani lakini najua mama ndiye alinizaa na baba. Kwa hiyo, umuhimu wa mama mimi haunipi tabu kabisa, wala sina tatizo, wala sitaki niingie hapa kwenye mgogoro hapa umuhimu Mbunge ni mbunge siyo jumla na moja wala hatua moja. Mheshimiwa Waziri Mkuu tulipokutana siku ile alipokuwa anafanya *briefing* pale alitamka pale ndani akasema kwamba hili jambo amelisikia, ataliangalia tena kwa uzito wake ili tuone jinsi ambavyo tunaweza tukali-*accommodate* jambo hili linalozungumzwa hapa. *(Makofi)*

Sasa jamani nikisema tuwe na kitu kingine na Mkuu mwenyewe ameshasema hivyo, hivi kweli mnanitakia mema kweli nyinyi hapa. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Fedha. Swali litaulizwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa.

Na. 31

**Ruzuku ya Fidia ya Vyanzo vya Mapato**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato iliondolewa bila maelezo. Je, Serikali haioni kuwa Halmasdhauri zitashindwa kutekeleza malengo yaliyopangwa kutokana na vyanzo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato katika Halmashauri ilipunguzwa kwa jumla ya shilingi 49.1 bilioni kutoka shilingi 59.9 bilioni mwaka 2010/2011 hadi shilingi 10.8 bilioni mwaka 2011/2012. Punguzo hilo lilitokana na mpango wa Serikali kupitia mchakato wa Bajeti ya mwaka wa 2011/2012 wa kurejesha utaratibu wa kulipa ada ya leseni za biashara kila mwaka katika ngazi za vijiji, kata, wilaya, miji, manispaa na majiji.

Mapendekezo haya yalitarajiwa kuongeza mapato ya Halmashauri kwa jumla ya shilingi 120.0 bilioni. Kiasi hiki ni kikubwa ukilinganisha na ruzuku iliyokuwa inatolewa na Serikali Kuu ya shilingi 59.9 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baada ya kutathimini athari za kupunguzwa kiwango hicho cha ruzuku na kwa kuwa Halmashauri zimeshindwa kufikia malengo yao, Serikali italeta pendekezo kwenye Bajeti ya kurejesha tena ruzuku ya fidia ya mapato ya Halmashauri katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Hatua hii ya kurejesha ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato kama ilivyokuwa mwaka 2010/2011 pamoja na kuendelea kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vya ndani itaziwezesha Halmashauri zote kuwa na mapato zaidi yatakayoongeza uwezo wao wa kutekeleza majukumu yao ya kisheria.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Naomba pia kabla sijauliza maswali yangu mawili niipongeze Serikali kwa kukubali kurudisha tena ruzuku hii ya vyanzo vya mapato. *(Makofi)*

(a) Kwa kuwa Serikali wakati inatoa pendekezo la kukatwa au kupunguzwa ruzuku hii haikutazama kwa kina chanzo cha ada za leseni kuwa kinatofautiana sana kutoka katika Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji. Hivyo kufanya Halmashauri kama ya Namtumbo yenye wakulima wengi zaidi ya wafanya biashara kuyumba na kusitisha shughuli zake za kimsingi na za kisheria.

Je, Serikali baada ya kuona athari zilizojitokeza ipo tayari sasa kuzifidia Halmashauri zisizofikia lengo kwa kipindi hiki ili waweze kutimiza majukumu yao ya msingi na kisheria?

(b) Kwa kuwa Serikali imesema italeta pendekezo la kurejesha tena ruzuku hii hapa Bungeni katika kipindi hiki cha Bajeti ya mwaka 2012/2013. Je, Serikali inaweza kuona sasa wakati umefika kwa Manispaa na Majiji ambayo yanaweza kutoza ada za leseni na zikawa kubwa zaidi ya ruzuku hiyo wakaachiwa watoze halafu Halmashauri kama za Namtumbo wakaongezewa ruzuku hiyo ya fidia ya vyanzo vya mapato?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ningependa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa ufuatiliaji wake mzuri wa ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato kwa Halmashauri zote hapa nchini ikiwemo na Namtumbo. Vile vile kufuatilia uwiano wa mapato yanayotokana na ada ya leseni kama alivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kuhusu fidia; ningependa niseme kwamba, kuhusu fidia, panapojitokeza kwamba ipo haja ya kulipa fidia, Serikali huwa inabainisha chanzo cha fidia hiyo kulipwa na namna ya kutatua tatizo hilo kwa njia ya muda mfupi au muda mrefu na hasa kwa kuzingatia uwezo wake wa kifedha, kwa maana ya bajeti. Sasa kwa hili la Halmashauri kupewa fidia kwa kuziba mapengo yaliyojitokeza, tunaangalia pengo hili au tatizo hili lilitokeaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba, Halmashauri nyingi zimeshindwa kukusanya mapato kupitia hii ada ya leseni. Sasa mtu aliyeshindwa au Halmashauri iliyoshindwa leo tena ipewe fidia kwa kushindwa, inakuwa ni vigumu. Ukizingatia uwezo wa bajeti kwa hivi sasa kwa kipindi hiki cha muda mfupi uliobaki wa miezi miwili, mitatu na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati akijibu swali hapa kwamba, tuna upungufu wa bajeti finyu sasa hivi; kwa hiyo, itakuwa vigumu sana kutoa fidia kwa Halmashauri hizi ili kuziba mapengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa swali la pili la ruzuku ni kwamba, Manispaa, Majiji au Miji Mikubwa, kwa sababu wao wana fursa nzuri ya kukusanya ada ya leseni, wapunguziwe ruzuku na ruzuku hiyo iende kwenye Halmashauri hizi ndogondogo ambazo fursa ya kukusanya ada ya leseni ni ndogo. Ninafikiri huu ni ushauri mzuri sana na ningependa kumwambia Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwamba, hili tutazidi kushauriana au tutaomba ushauri wa

wadau wanaohusika kwa maana ya Miji na Manispaa, tuweze kuangalia jinsi ya kutekeleza wazo hili zuri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, kwa sababu ya muda naomba tuendelee na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula.

Na. 32

**Uanzishwaji wa Programu ya Uvuvi Nchini**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015, Serikali imeahidi kutengeneza Programu Kabambe ya Uvuvi kama ilivyofanyika katika kilimo:-

(a) Je, uanzishwaji wa Programu hiyo umefikia hatua gani na ni lini Programu hiyo itaanza kufanyika?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha maalum kwa ajili ya ruzuku kwa wavuvi kwa ajili ya mitaji na zana bora kama ambavyo ilivyo katika Sekta ya Kilimo, wakulima hupewa ruzuku za pembejeo na matrekta?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 – 2015/2016 ambapo Sekta ya Uvuvi imepewa umuhimu unaostahili. Mpango huo umeingizwa

kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano ambao umeshazinduliwa na Mheshimiwa Rais. Programu hiyo, itatekeleza pamoja na mambo mengine, uendelezaji wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji, matumizi endelevu na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi na mazingira. Vile vile, Programu hii itahusisha ukuzaji wa teknolojia ya uvuvi, pamoja na uimarishaji wa huduma za ugani, utafiti, mafunzo na upatikanaji wa takwimu sahihi za uvuvi. Aidha, Programu itaboresha miundombinu ya uvuvi pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwenye Sekta ya Uvuvi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiwawezesha wavuvi wadogo kwa kuwapatia mikopo kupitia Miradi na Programu mbalimbali zinazotekelezwa chini ya Sekta ya Uvuvi. Kupitia Mradi wa *MACEMP,* jumla ya shilingi 1,303,950,355 zilitolewa kama ruzuku kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi, ambapo jumla ya Miradi midogo 125 ya uzalishaji ilitekelezwa tangu Mradi huo ulipoanza kutekelezwa mwaka 2006 hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu, Serikali imetekeleza Mpango wa kubadilishana zana haribifu na zana bora za uvuvi endelevu katika maeneo tengefu ambazo zimetolewa kama ruzuku. Chini ya utaratibu huo, jumla ya wanajamii 275 kutoka Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia wamepatiwa majarife 102 na wanajamii 436 kutoka Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma, wamepatiwa majarife 716.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada nyingine, Serikali imeendelea kuhamasisha jamii kujiunga kwenye vikundi vya kuweka na kukopa ili waweze kujijengea uwezo katika kutekeleza Miradi ya Kiuchumi kwa ajili ya kuboresha maisha yao.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Tarehe 18 Novemba, 2010, wakati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anazindua Bunge hili alisema na ninaomba kunukuu; "Ni makusudio yetu kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015, kutengeneza Programu Kabambe ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi Nchini kama tulivyofanya katika kilimo." Mwisho wa kunukuu.

(i) Kwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano hauoneshi bayana na kwa udhahiri dhamira hii ya Mheshimiwa Rais. Serikali ipo tayari sasa kuona umuhimu wa kuelekeza nguvu katika Sekta ya Uvuvi? *(Makofi)*

(ii) Takwimu za ukuaji wa hali ya uchumi zinaonesha kwamba, kwa mwaka uliopita Sekta ya Uvuvi imekuwa kwa asilimia moja tu. Hiki ni kielelezo kwamba, hatujafanya vya kutosha katika Sekta ya Uvuvi. Serikali ipo tayari sasa kuelekeza nguvu zake kuhakikisha tunaiboresha Sekta hii ili kuwaondolea umaskini uliokithiri wananchi wanaoishi katika maeneo ya uvuvi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kitandula, kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kama Mheshimiwa Rais alivyosema hapa, alitoa maelekezo kwa Wizara yangu tuandae Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi na Programu hii imeshakamilika na ipo katika Mipango ya Wizara, inayopaswa kutekelezwa kwa miaka hii mitano.

Mkazo katika Programu hiyo ni kushughulikia suala zima la miundombinu kwa maana ya bandari ya uvuvi, lakini pia mialo ya kuweza kuwarahisishia wavuvi kuwa na mahali pa kuja kufanya *landing* wanapovua wawe na mahali pa kufikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Programu inakazania pia kujenga uwezo wa wavuvi wadogowadogo. Kwa hiyo, Programu imeendeleza mawazo ambayo yalianza katika kipindi cha nyuma mfano katika Wilaya ya Mkinga, jumla ya zaidi ya shilingi milioni 600 zilitolewa kuwajengea uwezo wavuvi wadogowadogo ili waweze kuvua na waweze pia kufanya *fish farming* na kutumia kama mitaji kuboresha maisha yao.

Niseme tu, Programu hii imekamilika na tunatarajia kwamba, itapatiwa fedha na mkazo utakuwepo katika Sekta ya Uvuvi.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, ukuaji umekuwa mdogo kama tulivyosikia, kinachovuliwa kutoka Ziwa Viktoria, wananufaika wengine, lakini pia *Deep Sea Fishing Authority,* wananufaika wengine zaidi yetu. Mpango wa sasa unajaribu kuziba mianya inayowanufaisha wengine na kuhakikisha kwamba, sisi tutanufaika zaidi.

Nitamwomba Mheshimiwa Mbunge na nikuombe wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Programu itakapokuja kuombewa pesa tuipatie fedha za kutosha kwa sababu tutanufaika zaidi kutegemeana na kiasi cha pesa tutakachokuwa tunaweka kwenye utekelezaji wa Programu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, nitaomba sana maswali ya leo wauliza maswali wawe wale wenye maswali ya msingi tu basi. Tunaendelea na Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

No. 33

**Wananchi Kupewa Mashamba ya Mbalizi kwa Kilimo**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE** aliuliza:-

Serikali katika mpango wake wa miaka mitano haijaonesha kwamba ina dhamira ya kufufua Kiwanda cha Nyama cha *Mbalizi Tanganyika Packers*:-

Je, kwa nini Wananchi wa Mbalizi wasipewe mashamba hayo ambayo hayatumiki ili wayatumie kwa ajili ya kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Nyama cha Mbeya ni mojawapo ya viwanda vya nyama vya iliyokuwa Kampuni ya *Tanganyika Packers Limited (TPL),* vilivyoorodheshwa na Serikali kwa ajili ya ubinafsishaji na wawekezaji wamekuwa wanatafutwa na *Consolidated Holdings Corporation (CHC)* katika kipindi kirefu. Kiwanda hicho kimekwishatangazwa mara mbili hadi sasa na hakuna mwekezaji aliyejitokeza.

Serikali kupitia Shirika lake la *CHC* imeshakamilisha tathmini ya mali ya kiwanda hicho ili kujua hali halisi ya sasa na kiasi cha thamani ya kiwanda pamoja na ardhi yake kwa sasa. Ripoti ya tathmini imewasilishwa kwa Msajili wa Hazina ili kuipitia na kutoa ushauri kwa lengo la kukitangaza tena wawekezaji waweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kiwanda na majengo lina ukubwa wa Hekta 102, linatambulika kama Shamba Na. 760, lenye hati Na. *LO/188772/3* ya miaka 33 kuanzia tarehe 1 Septemba, 1999 na hilo eneo lipo kwenye eneo la Mbalizi. Eneo la pili katika Mradi huu ni la malisho na lina ukubwa wa hekta 1999 linalotambulika kama Shamba Na. 761 na lipo eneo la Nsalala. Shamba hili limetengwa kwa ajili ya malisho kwa mifugo itakayotumika kiwandani; hivyo, haitakuwa busara kuligawa kwa wananchi kwa sababu punde kiwanda kitakapoanza kazi, mifugo haitapata eneo la kuchungiwa ama kunenepeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016, Serikali imedhamiria kufufua Kiwanda cha Nyama cha Mbalizi na kujenga viwanda vingine vipya kwa kushirikiana na sekta binafsi.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Naibu Waziri ameyajibu lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa katika jibu la msingi Serikali yenyewe inakiri kwamba, shamba hilo limewekwa katika soko zaidi ya mara mbili lakini hakuna mwekezaji yeyote aliyepatikana kununua shamba au kiwanda hicho. Je, Serikali sasa inatamka nini na ina mpango gani kwa sababu katika Mpango wa Miaka Mitano Serikali haikuonesha kama itakifufua kiwanda hicho; sasa inawatangazia nini Wananchi wa Mbeya Vijijini na Tanzania kwa ujumla; Kiwanda hicho kitaanza kufanya kazi au kitawekwa katika mpango lini?

(ii) Kwa kuwa shamba la zaidi ya ekari 2000 lipo pale na limekaa halilimwi. Je, ni kwa nini, Serikali isiwapatie Wananchi wa Mbalizi kwa mkataba waweze kulima kwa mkataba na kisha kiwanda kikifunguliwa waweze kulichukua kwa urahisi wasipewe wananchi hawa walime?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Luckson Mwanjale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la lini kiwanda kitafanya kazi; inakuwa vigumu kutoa muda maalum hapa, lakini niseme tu ni mapema kadiri itakavyowezekana. Hivi karibuni wamekuja pia watu wa Kampuni ya *Beef* ya Zambia wanaitwa *ZAM-BEEF* wakaonesha *interest* ya kutaka kuwekeza katika kiwanda hicho. Kwa hiyo, tayari mawasiliano yameshakuwepo na *CHC* maana hapo nyuma jitihada zilifanyika za kurudisha kiwanda Wizarani haikuwezekana, bado kipo chini ya *CHC* ambao wanasema kwamba wao watakibinafsisha na hivi karibuni kumekuwepo na *interest* kama nilivyosema, kampuni hiyo ya Zambia wana *interest.* Tunatarajia kwamba, maadam wametokea wawekezaji ambao wanaonekana wapo *serious,* tunatarajia Mheshimiwa Mchungaji uvute tu subira, kwa sababu kitaanza kufanya kazi mapema inavyowezekana, japo sikuweza kutaja ni tarehe ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuruhusiwa wananchi wa eneo lile kulima shamba hili kwa mkataba kabla halijaanza; hapa tunaingia katika mahitaji ya kiikolojia na kama lengo ni kutumia eneo lile kwa malisho ya kunenepesha mifugo watakaochinjwa. Unapolima tayari umeshabadilisha *composition* ya ardhi na hivyo huenda mazao yatakayolimwa pale hayatakuwa rahisi tena kuweza kutumia eneo lile kama malisho kama ilivyokusudiwa hapo awali. Kwa hiyo, ningeomba niseme kwamba, labda niende na wazo hili alilolitoa Mheshimiwa Mchungaji, litazamwe ili tupate kidogo maelezo ya kitaalamu na maelekezo kabla hatujasema kwamba hilo linawezekana likafikiriwa ama hapana. Kitu kitakachoamua zaidi ni ardhi ile baada ya kulima, itafaa tena irudi kwa malisho ama hapana.

No. 34

**Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED** aliuliza:-

Mwaka 1968 Serikali ilianzisha Kitengo cha Umwagiliaji ili kuendeleza hekta 10,000 za mashamba; na mwaka 1986 na 1995 Serikali ilipatiwa msaada kutoka *UNDP/FAO* wa kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji kwa skimu 147 kwa kipindi cha miaka 20 hadi kufikia mwaka 2014:-

(a) Je, hadi sasa ni skimu ngapi zimeendelezwa na ni katika maeneo gani?

(b) Je, ni changamoto gani zilizojitokeza na ni mafanikio gani endelevu yaliyopatikana?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 1988 na 1999, Serikali ilitekeleza Mradi wa Umwagiliaji kwa msaada wa Mashirika ya *UNDP* na *FAO.* Malengo makuu ya Mradi huo, yalikuwa kujenga uwezo wa Kitengo cha Umwagiliaji, kupanga na kutekeleza Miradi ya Umwagiliaji katika nchi nzima na kukarabati baadhi ya skimu zilizokuwa zimechakaa katika Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 1994, Mradi huo uliisaidia Serikali kuandaa Mpango wa Kitaifa wa Kuendeleza Umwagiliaji *(National Irrigation Development Plan – NIDP),* ambao uliweka lengo la kuendeleza skimu 147 ifikapo mwaka

2014. Hadi kufikia mwaka 2002, skimu 60 zenye jumla ya hekta 191,900 zilikuwa zimeendelezwa. Aidha, mwaka 2002, Serikali kwa kushirikiana na *JICA,* ilitumia matokeo na mafanikio ya *NIDP* kuandaa Mpango Kabambe wa Umwagiliaji *(National Irrigation Master Plan – NIMP),* uliobainisha kuwepo kwa hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kumwagiliwa. Mpango huu *(NIMP),* ndiyo unaoendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP).* Hadi Machi, 2012 skimu 2006, zenye jumla ya hekta 381,000 zimejengewa miundombinu ya umwagiliaji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio endelevu ambayo yapo ni pamoja na uwezo uliojengwa wa Wahandisi wetu wa Umwagiliaji kusanifu, kusimamia na kujenga miundombinu, ikilinganishwa na huko nyuma ambapo tuliwategemea sana wataalamu wa kutoka nje hasa India. Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto zinazotokana na uwekezaji mdogo katika kilimo cha umwagiliaji kwa sekta za umma na binafsi, uhaba wa wataalamu na vitendea kazi hasa katika ngazi ya Halmashauri na mabadiliko yanayosababisha ukame na mafuriko ya mara kwa mara.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

(i) Kwa kuwa Mradi wa *ASDP Basket Fund* ambo ulikuwa kwa ajili ya kugharimia uendelezaji wa skimu hizo na ulianzisha Mifuko ya *District Irrigation Development Fund* na ule wa *National Irrigation Development Fund.* Je, ni Halmashauri ngapi za Wilaya ambazo zimeendelezwa na Mradi huo?

(ii) Kwa kuwa Serikali ilichelewa kuweka Sera ya Taifa ya Umwagiliaji hadi mwaka 2010 na kwa makusudi kudharau Agizo la Rais la Uundwaji wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo ilikuwa na majukumu ya kusimamia kwa ukamilifu shughuli za umwagiliaji na kuandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Umwagiliaji; na kwa kuwa hivi karibuni

Wizara hii iliingia makubaliano na kampuni moja ya Kihindi ya Jayan katika kuendeleza mifumo ya umwagiliaji. Je, Mheshimiwa Waziri utalihakikishiaje Bunge hili pamoja na wananchi ya kwamba makubaliano hayo siyo bomu linaloweza kuliingizia Taifa katika mrorongo wa mikataba feki ili Taifa lisije kuingia katika hasara nyingine?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mhandisi Chiza karibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, inaonekana kama Mheshimiwa Mbarouk kuna baadhi ya mambo hajayaelewa vizuri; ningependa nimkaribishe ofisini kwangu ili nimpe elimu ayaelewe kwa sababu mpangilio wenyewe wa kuuliza haendi kama yalivyo. Ninapenda niseme kwa kifupi tu kwamba, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ambayo ndiyo ambayo tunaitekeleza hivi sasa imeweka Mifuko hiyo; kwanza, kuanzia ngazi ya Wilaya tunayo mipango ya kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans),* ambako ndiko huko tunakoanzia kupanga mipango ya kilimo cha umwagiliaji na ina kiwango cha fedha ambapo Halmashauri zote hujipangia mipango hiyo na kuomba fedha hizo.

Baada ya hapo tunakwenda katika ngazi ya *District Irrigation Development Fund* kama fedha hiyo ipo kati ya kiwango cha bilioni 500 mpaka milioni 800, zinapozidi hapo tunaweka Mfuko unaoitwa *National Irrigation Development Fund* kama fedha hizo zinazidi shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinajadiliwa katika Halmashauri zote kulingana na mipango ambayo Halmashauri imejiwekea. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbarouk ashiriki katika Vikao hivyo vya Halmashauri, wanapopanga mipango hii ya maendeleo ya kilimo ili aweze kuelewa mipango inavyopangwa. Kwa kifupi ni kwamba, Halmashauri

zote za Wilaya zinaleta mipango hii na mipango yote ambayo inapitishwa vizuri inapewa fedha.

Kuhusu Sera ya Umwagiliaji ya Taifa; ni kweli tumeandaa Sera ya Umwagiliaji ambayo imepitishwa mwaka 2010 na ipo tayari na hivi sasa tupo katika mchakato wa kuanzisha Kamisheni ya Umwagiliaji, sambamba na Kamisheni ya Ushirika. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba vyombo hivyo havijaundwa, vyombo hivi vinachukua muda kuandaliwa na ndiyo maana sasa tupo katika mchakato na tupo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kuandaa Kamisheni ya Umwagiliaji ambayo muda si mrefu tutaileta tena hapa Bungeni na itajadiliwa.

Kuhusu *Memorandum of Understanding (MoU),* ambayo Serikali imeingia na Shirika la *Jayeen Irrigation System* la India, haya ni hati ya makubaliano wala siyo mkataba kwamba tunakwenda kuwalipa muda fulani. Hii ni kampuni ya kitaalam, ambapo tumekubaliana kutumia uzoefu wao na hasa katika maeneo ya *drip irrigation* katika mikoa kame hasa ya Dodoma, kuonesha jinsi tunavyoweza kutumia *drip irrigation* kuhakikisha tunatumia maji yetu kwa ufasaha kama wenzetu walivyofanya. Kwa hiyo, sidhani kama ni bomu na ndiyo maana nilisema Mheshimiwa Mbarouk, ningeomba utumie muda wakati mwingine uje na mimi nikuelimishe uweze kuelewa jambo hili.

Na. 35

**Utekelezaji wa Mpango wa Kilimo Kwanza**

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA)** aliuliza:-

Mpango wa Kilimo Kwanza unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao na kuwapatia wakulima soko na bei nzuri na kwamba Kasulu ni miongoni mwa Wilaya zilizopo katika mpango wa utekelezaji:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kujenga kituo maalum cha manunuzi ya mazao ya Wakulima wa Kasulu?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza pembejeo za kilimo kama vile matrekta, mbolea na mbegu zitakazosaidia kuwa na kilimo bora?

**NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mpango wa Ujenzi wa Masoko ya Kimataifa na Mazao ya Wakulima katika maeneo mbalimbali nchini. Kuanzi mwaka 2002/2003 hadi sasa, masoko 188 yamejengwa nchini kupitia Mradi wa Masoko ya Kilimo *(AMSDP)* na Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani *(DASIP).*

Hivi sasa ujenzi wa masoko hayo unaendelezwa kupitia Mradi wa *DASIP* na Mradi mpya unaoitwa *Marketing Infrastructure Value Addition and Rural Finance*. Katika Wilaya ya Kasulu, Serikali imetenga shilingi milioni 575 za kujenga soko katika Kijiji cha Mnanila. Taratibu za kusaini mikataba na wataalam elekezi na wasimamizi wa ujenzi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Kilimo Kwanza na kufikia Mapinduzi ya Kijani itafikiwa iwapo wakulima wataongeza matumizi ya pembejeo hususan mbolea, mbegu bora, viatilifu na matumizi ya zana bora za kilimo yakiwemo matrekta. Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa ruzuku ili kuwasaidia wakulima kumudu gharama za pembejeo hizo. Kupitia utaratibu huo, katika mwaka 2009/2010 jumla ya kaya 42,680, kaya 46,063 katika mwaka 2011/2012 zimenufaika na ruzuku hiyo. Aidha, matumizi ya zana bora za kilimo nchini

yameongezeka, kwa mfano, matumizi ya matrekta yameongezeka kutoka wastani wa asilimia 10 mwaka 2005 hadi asilimia 14 mwaka 2012 wakati matumizi ya wenye makazi yamepanda kutoka asilimia 20 hadi asilimia 22 katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, habari njema kwa wakulima, Shirika la Suma JKT limepunguza bei za matrekta ili wakulima waweze kuzimudu. Kwa mfano, trekta aina ya *farmtrack 60 (50 HP:2WD)* lilikuwa linauzwa shilingi 25,635,759 sasa linauzwa shilingi 16,480,952, sawa na punguzo la asilimia 35.71.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba wanajenga soko katika eneo la Mnanila. Sasa ninachopenda tu kuijibu Serikali ni kwamba Mnanila siyo sehemu ya Wilaya ya Kasulu, isipokuwa Mnanila ni sehemu ya Wilaya mpya ya Buyigwe. Sasa swali la Mheshimiwa Buyogera ambalo ni *current* kabisa lilikuwa linauliza Serikali haioni umuhimu wa kujenga soko katika Wilaya ya Kasulu. Sasa nilikuwa naomba Serikali itoe kauli ni lini itaweza kujenga soko katika Wilaya ya Kasulu kama swali lilivyokuwa limeulizwa? Kwa hiyo kipengele hakikujibiwa kama ilivyotakiwa.

(ii) Pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali kuweza kutoa takwimu kuanzia mwaka 2009/2010 kuhusiana na suala zima la kuboresha upatikanaji wa pembejeo za kilimo; lakini leo hii tunapozungumza, Wilaya ya Kasulu ni miongoni mwa Wilaya ambazo *suppliers* wa pembejeo za kilimo kama vile mbolea, hawajalipwa mpaka dakika hii, kiasi kwamba hata mbolea ilichelewa kuanza mwaka jana. Ninaomba kauli ya Serikali ni lini wafanyabiashara wote ambao waliweza ku-*supply* wataweza kulipwa katika

mfumo wa vocha ili waweze kupata pesa hizo na waweze kuwa na moyo wakati mwingine wasisite kuwahudumia wakulima wetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Soko la Mnanila lipo nje ya Kasulu lakini siyo mbali sana Mheshimiwa Machali kwa sababu huwezi ukazalisha hapo hapo Kasulu, ukauza hapo hapo kila kitu. Soko hili lipo katika eneo ambalo ni karibu kabisa na Kasulu na naamini hata Wakulima wa Kasulu watafaidi kwenye soko hili. Pamoja na hayo, bado nadhani swali lake ni zuri tu kwamba, ipo haja ya kuwa na mchakato wa kuwa na soko lingine pale Kasulu; na ni vizuri basi Halmashauri iandae mchakato mwingine tena kwa ajili ya kujipanga kupata soko kwa ajili ya wakulima wa pale Kasulu.

Soko hili la Mnanila bado litawahudumia Wananchi wa Kasulu. Ninaomba pia nimfahamishe Mheshimiwa Machali kwamba, sisi tumeanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, ambayo itakuwa pia ikanunua mazao yote bila kujali zao gani katika Halmashauri zote hizi na sasa hivi tunajijengea uwezo na pindi itakapoanza kazi basi hata Kasulu bodi hii itawafika kwa ajili ya kununua mazao hayo.

Kuhusu Mawakala ambao hawajalipwa, siyo wale wa Kasulu tu, wapo na wengine na hivi sasa nimepewa taarifa kwamba wapo wengine huko Rukwa bado hawajalipwa. Tunachokifanya hivi sasa, tunatafuta fedha na tunataka tujitahidi kabla ya mwisho wa mwaka huu, mawakala wote hawa ambao wanatudai tuwe tumewalipa, wengine hawakulipwa kutokana na matatizo ambayo yamejitokeza kwao wenyewe maana kuna ujanja ujanja uliofanywa na baadhi ya mawakala na baadhi ya watendaji na kusababisha mitafaruku. Hilo nalo limechangia mawakala kuchelewa, wengine wamechelewa kutokana na fedha zenyewe kupatikana lakini tunafanya kila juhudi mawakala hawa walipwe fedha zao.

Na. 36

**Kuboresha Miundombinu ya Kambi ya JWTZ - Potoa - Unguja**

**MHE. JADDY SIMAI JADDY** aliuliza:-

Askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kambi ya Potoa iliyopo Jimbo la Mkwajuni – Kaskazini Unguja wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo miundombinu mibovu hasa majengo ya ofisi, hali inayosababisha askari hao kushindwa kufanya kazi hasa kipindi cha mvua:-

(a) Je, Serikali inaelewa hali ngumu ya kuitendaji waliyonayo askari hao?

(b) Je, ni lini sasa Serikali imepanga kuboresha miundombinu ya kazi kwa askari wa Kambi hiyo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa, Kambi Potoa inakabiliwa na tatizo la uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi. Kufuatia hali hiyo, tayari Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa pamoja limeshafanya tathmini ili kubaini mahitaji ya ukarabati huo unaohitajika. Kulingana na tathmini hiyo iliyofanyika, kinahitajika kiasi cha shilingi 109,190,000.00 ili ukarabati wa Kambi hiyo uweze kufanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hicho cha fedha kimejumuishwa katika makadirio ya fedha za maendeleo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Fungu 38 - NGOME kwa

Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 yatakayowasilishwa katika kikao kijacho cha Bunge la Bajeti.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekubali kabisa kuwepo kwa uchakavu wa majengo katika Kambi hiyo. Je, sasa Waziri atakuwa tayari kufuatana na mimi ili kwenda katika eneo hilo na kuweza kujionea baadhi ya mambo mengine ambayo yatahitaji uwepo wake yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jaddy, kama ifuatavyo:-

Nitakuwa tayari kufuatana naye ili kwenda kuangalia matatizo yanayokabili miundombinu katika Makambi yetu. Hata hivyo, kazi hiyo tayari nimeshaifanya, niliwenda kwenye *brigedi* zote na baadhi ya vikosi vyetu nilipata nafasi ya kutembelea na nafahamu fika matatizo ya miundombinu yanayokabili majengo ya ofisi pamoja na makazi; ndiyo maana tumeweka mpangilio maalum wa kuweka bajeti katika Wizara, bajeti katika Voti ya Ngome. Vilevile tunao mpango wa muda mrefu wa kukopa fedha kutoka China kwa madhumuni ya kujenga nyumba katika maeneo yote ya jeshi kwa sababu hali ya makazi maeneo mengi siyo nzuri. Niseme tu kwamba, nitakuwa tayari kufuatana na Mheshimiwa Mbunge.

Na. 37

**Kuinua Sekta ya Utalii – Kigoma**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuinua Sekta ya Utalii Kanda ya Magharibi hususan Mkoa wa Kigoma?

**NAIBU SPIKA:** Swali zito hili, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige, majibu, kwa uchumi wa nchi hii. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kupunguza utegemezi wa utalii wa mbuga za wanyama na kupanua wigo wa utalii ikiwemo Kanda mbalimbali za Utalii. Kanda ya Ziwa Tanganyika ni eneo mojawapo lilipo katika mipango ya kuipanua Sekta ya Utalii. Kwa kuanzia, Wizara imetumia kiasi cha shilingi milioni 680 kuboresha Kituo cha Kumbukizi Kigoma. Aidha, Wizara inakamilisha hatua ya kuingiza njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa kwenye orodha ya urithi wa dunia. Njia inayoanzia nchini Kigoma Ujiji hadi Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zaidi zimechukuliwa na Shirika la Hifadhi la Taifa *(TANAPA),* ambalo limefungua ofisi zake Kigoma Mjini, kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma na taarifa mbalimbali za watalii. Pia Shirika hilo limeweka boti ambayo huweza kukodishwa kwa watalii ambao wanapenda kutembelea Hifadhi za Taifa za Gombe na Mahale.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016, suala la kuboresha miundombinu katika Mikoa ya Magharibi limezingatiwa. Kuboreka kwa hali ya usalama na miundombinu kutachangia maendeleo ya Sekta ya Utalii katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Bodi ya Utalii itaendelea kuhamasisha Wakala wa Utalii kuuza safari za Ukanda wa Magharibi ikiwemo Kigoma. Ninapenda kutoa pongezi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, kwa hatua ilizochukua katika uendelezaji na utangazaji utalii kwa kufungua ofisi na kuteua afisa anayeshughulikia masuala ya utalii.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Mji wa Ujiji ni wa kihistoria kama ulivyo Mji wa Bagamoyo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuutangaza Mji huo ndani na nje ya nchi?

(ii) Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma tuna meli ya MV. LIhemba; ni meli ya kihistoria; je, ni mkakati gani sasa sekta yako imeweka kuhakikisha kwamba meli inakuwa ni kitovu na *source* ya utalii ndani na nje ya nchi? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba, moja ya malengo tuliyojiwekea katika miaka hii mitano ya Ilani ya CCM ya mwaka 2010/2015, ni kupanua wigo wa utalii kwa kuingiza kanda zingine ambazo hazina utalii mkubwa kwa sasa. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kupitia Bodi ya Utalii, imekwishabuni mpango wa utangazaji utalii ambao umegawanywa katika Kanda. Wakuu wa Mikoa katika Kanda hizo ukiwemo Mkoa wa Kigoma, wamekwishaarifiwa na tayari kila Mkoa umeshaanza kuandaa orodha ya vivutio ambavyo vinafaa kutangazwa. Kwa Mkoa wa Kigoma, Mji wa Ujiji, meli ya MV. Lihemba, pamoja na vivuto vya asili ikiwemo Hifadhi ya Mahale na Gombe ni miongoni mwa maeneo ambayo yapo kwenye orodha ya vivutio vya Mkoa huo.

Hatua inayofuata kwa sasa hivi ni kuanza kutangaza vivutio hivyo. Changamoto ambayo tumekuwa nayo kwa kiasi

kikubwa ni fedha lakini vilevile kiasi kingine ni changamoto ya kimiundombinu kwenye maeneo hayo; kwa sababu ikumbukwe kwamba, watalii ni watu ambao ukiacha *adventurers* wanaokwenda kwenye maeneo magumu, walio wengi wanakwenda kwenye maeneo ambayo miundombinu imeimarika sana, ambayo kazi hiyo inafanyika kwa kiasi kikubwa hasa uwekezaji unafanywa na sekta binafsi. Kwa hiyo, jinsi miundombinu inavyoimarika sisi tutaendelea kutangaza na ninaamini kwa mazingira ya Kigoma kwa sasa hivi utalii wake utaanza kukua kwa kasi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho kwa leo linaelekezwa Wizara ya Ujenzi na linaulizwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 38

**Mkandarasi wa Barabara ya Manyoni – Singida**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:**-**

Barabara ya Manyoni – Singida iliyokuwa inajengwa na Kampuni ya SIETCO imeshakamilika na kufunguliwa rasmi:-

(a) Je, Mkandarasi anatakiwa kuwepo kwa uangalizi wa barabara kwa muda gani?

(b) Je, Mkandarasi anatakiwa kufanya kazi nyingine zipi zaidi ya uangalizi na marekebisho madogomadogo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Isuna – Singida (km 63), ambayo ni sehemu ya Barabara ya Manyoni – Isuna – Singida, muda wa uangalizi baada ya barabara kukamilika ni miaka mitatu. Ujenzi ulikamilika mwaka 2008 na muda wa uangalizi wa miaka mitatu uliisha mwezi Juni mwaka 2011. Aidha, sehemu ya Manyoni – Isuna (km 54) imejengwa na Kampuni ya *China Geo Engineering* kutoka China na barabara bado haijafunguliwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kipindi hiki cha uangalizi, Mkandarasi anaruhusiwa kufanya kazi za mikataba mingine ya kazi za ujenzi wa barabara kulingana na uwezo wake.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa katika swali la msingi Waziri amejibu kwamba Mkandarasi alishamaliza muda wake wa uangalizi na kwa kuwa mkataba ulishakwisha alitakiwa awe ameshaondoka; lakini hivi ninavyozungumza hapa Mkandarasi huyu ameanzisha biashara nyingine ya kuchimba kokoto na kuuza kwa makampuni mengine ya ujenzi wa barabara. Je, ni lini Serikali iliipatia Kampuni ya *SIETCO* mkataba mpya au leseni ya kufanya biashara ya kuchimba kokoto na kuuza kwa makampuni mengine?

(ii) Kama Serikali iliipatia Kampuni hii ya *SIETCO* ya kuchimba na kuuza kokoto bila kushirikisha wananchi; je, kampuni hii inalipa kodi stahiki kwa Serikali ya Kijiji cha Utaho na Halmashauri ya Wilaya ya Singida kama ambavyo Sheria ya Madini inataka?

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi. Swali la mwisho litatoka kwa Mheshimiwa Diana Chilolo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kwa pamoja na kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mkandarasi *SIETCO,* ambaye alipewa kujenga kipande cha barabara kutoka Isuna kwenda Singida, chenye urefu wa kilomita 63 aliweka kambi yake sehemu hiyo anayoisema Mheshimiwa Mbunge ya Utaho na pale akajenga vilevile mtambo wa kokoto kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Kama tulivyosema, barabara ilishakamilika mwaka 2008 lakini akawa ana kipindi cha miaka mitatu kuitengeneza hiyo barabara kwa kutumika kokoto hiyo lakini vilevile ilibidi aendelee kutumia kokoto hiyo kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha barabara cha kilomita 25, yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge anakielewa kutoka Misigiri hadi Kiomboi.

Mheshimiwa Naibu Spika, machimbo hayo ya kokoto anayoyasema Mheshimiwa Mbunge ni ya Serikali, yaani *it is a Government query*. Tatizo linalojitokeza hata mimi naliona, ikiwa Mkandarasi amenza kufanya biashara ya kokoto na makandarasi wengine siwezi kubishana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu hili. Ninaomba kuchukuchua fursa hii kumwagiza *Regional Manager* wa *TANROADS* Singida alifanyie uchunguzi wa haraka sana suala hilo na kwa kuzingatia mkataba tuliosaini naye *TANROADS* na huyo mkandarasi na ikigundulika mwenzetu ameacha kujenga barabara na kuanza kuuza kokoto kwa kweli ni lazima Sheria ifuatwe, alipe ushuru na mimi nitalifuatilia kwa karibu pamoja na Mheshimiwa Mbunge nitakutaarifu matokeo yake. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Diana Chilolo swali la mwisho kwa siku hii ya leo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la barabara

kuharibika kipindi cha mkandarasi akiwa kwenye uangalizi; mfano, Barabara ya Misigiri – Shelui imeharibika vibaya na Serikali ilishamwagiza mkandarasi kuikarabati barabara hiyo ndani ya kipindi cha uangalizi lakini mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea na ajali sasa zimeanza kutokea kwenye eneo hilo.

Je, Serikali inasema nini katika barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulishasema hapa Bungeni kwamba, kwa barabara zinazoharibika mapema kutokana na udhaifu wa mkandarasi, tunachukua hatua za kumlazimisha Mkandarasi kujenga upya hiyo barabara kwa gharama zake kama ambavyo tumefanya kwa Barabara ya Kilwa. Vilevile mnaelewa hapa tumeshatoa taarifa kuhusu Barabara ya Nangurukuru na Mbwemkuru, ambapo mkandarasi *CHICO* anaifanyia tena ukarabati upya barabara aliyoijenga lakini kaona na mwezi Septemba atakuwa amemaliza. Vilevile Barabara ya Kyamrorwa na Buzirayombo, tulishatoa taarifa kwamba tayari tumechunguza na tuna mazungumzo pamoja na mkandarasi kuweza kuijenga upya.

Sekenke Diversion mpaka Shelui, ambayo mimi mwenyewe nilipita hiyo barabara mwaka jana nikaagiza *TANROADS* wafanye uchunguzi, mara moja. Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, uchunguzi huo umefanyika na imegundulika kwamba mkandarasi *CHICO* alikuwa na makosa katika utendaji wake wa kazi. Ametaarifiwa hilo lakini kampuni hiyo, mkandarasi naye amejitetea kwamba angetaka mazungumzo kati ya *TANROADS*, yeye mwenyewe pamoja na Mhandisi Mshauri ambaye ni Kampuni ya *BCOM* ya Ufaransa waweze kukaa; nafikiri wanakaa mwezi huu waweze kuangalia nani abebe mzigo wa kuikarabati barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalifuatilia hilo suala kwa ukaribu sana na si kwamba tumeliachia hivi hivi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, mtaona tumepita kidogo muda wetu wa kawaida, moja ya sababu ni kwamba, tulianza na mambo mengi kidogo ya kuweka mezani na kuwaapisha Wabunge wetu wapya; kwa hiyo, ikachukua kama nusu saa ambayo ndiyo tumeifidia.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaanza kutambulisha wageni wetu waliopo Ukumbini, kwanza, nitoe taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusiana na kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, anasema kwamba, atakuwa nje ya Dodoma kwa shughuli za kikazi kuanzia leo tarehe 12 mara baada ya kipindi cha maswali Bungeni na anatarajia Kurejea Jumatatu tarehe 16 Aprili, 2012.

Kwa kipindi ambacho hatakuwepo hapa Dodoma, atakayekaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi wakati huo ni Mheshimiwa Samuel J. Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa hiyo, naomba tumpe ushirikiano Mheshimiwa Samuel J. Sitta. *(Makofi)*

Baada ya hilo, naomba sasa niingie kwenye matangazo ya wageni wetu. Kwanza, waliopo Bungeni ni Ndugu Ludovick Utouh, ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali akiwa ameambatana na Wakuu wa Idara, Afisa Masuuli na Maafisa wa Ofisi ya *CAG*. Karibu sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hapa Bungeni na leo kazi yako imewekwa mezani tumeipokea sisi Wabunge na kupitia Kamati tutaifanyia kazi vizuri. Tunaipongeza sana Ofisi yako kwa kazi nzuri ambayo mnatufanyia na tunawaomba mwendelee kufanya kazi nzuri zaidi siku zijazo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi la pili ni wageni wetu kutoka *DFID,* Shirika la Misaada la Uingereza, ambao ni Dkt. Marshal Elliot, Kiongozi wa Msafara, akifuatiwa na Mr. Mark Montgomery - *Governance Adviser*, Ndugu Richard Moberly - *Senior Economic Adviser* na Ms Getrude Mapunda ambaye ni *Social Development Adviser.* Karibuni sana na walipita ofisini kwangu jana tukaongea nao pamoja na mambo mengine, wanapendekeza kutusaidia kuanzisha kitu kinachoitwa *Parliamentary Score Card,* ambayo ita-*truck* mwenende na ushiriki na *perfomance* ya Mbunge katika miaka ambayo anakuwepo Bungeni ili mwisho wa miaka mitano wananchi waweze kujua. Kwa hiyo, tunaendelea kuongea tuone kama jambo hili linawezekana au vipi, lakini tutapenda vilevile kupata ushauri wenu. Ahsanteni sana *and you are welcome. (Makofi)*

Naomba kuwatambulisha Wabunge wa Afrika Mashariki, nianze na Wabunge watatu; Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, Mheshimiwa Sebtuu Mohamed Nassor na Mheshimiwa Said Gharib Bilal. Hawa ni Wabunge wa kutoka upande wa Zanzibar, vilevile nimtambulishe Mheshimwa Janet Deo Mmari. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Janet. Katika ile *group* nzima ya Wabunge wa Afrika Mashariki waliomaliza muda wao, kwa upande wa Tanzania Bara, yeye peke yake ndiye aliyebakia. Sasa katika masuala ya kumbukumbu za kitaasisi yaani *Institutional memory,* mimi sina cha kusema. *(Makofi)*

Tunaendelea na wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni 90 wa Mbunge Mteule wa Arumeru Mashariki, Mheshimiwa Joshua Nassari wakiongozwa na mzazi wake Bwana na Bibi Mchungaji Samwel Nassari. Karibuni sana kutoka Arumeru, kijana wenu amefika hapa. Mzee Samwel nyoosha mkono, ahsante sana na karibu sana baba yetu. (Makofi)

Wapo wageni 22 wa Mbunge Mteule wa CHADEMA, Bibi Cecilia Paresso wakiongozwa na wazazi wake pamoja na mumewe Ndugu Stephen Mbogo. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Cecilia na yeye vilevile ameshafika safari yake. Bwana Stephen pia karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Cecilia amekuja na amemtambulisha kabisa mume wake Bwana Stephen yupo, ameolewa! Karibuni sana. *(Kicheko/Makofi)*

Wageni wa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo ni Daktari Albina Chuwa ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ameongozana na Maafisa wengine watatu. Karibuni sana na tutawatambulisha baadaye zaidi kwenye kikao kitakachofuata. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Bi. Junita Nabanjo, ambaye ni Mwakilishi wa *Development Partiners,* ameongozana na Wajumbe wengine wanane kutoka Shirika la Idadi ya Watu. Popote walipo wanakaribishwa sana. *(Makofi)*

Baada ya hao, naomba niwatambulishe wageni wawili muhimu sana kwangu; kwanza ni Ndugu Mussa Chiwanga, ambaye ni Katibu wa Uchumi na Fedha Wilaya ya Kongwa. Karibu sana. Ameambatana na Mchungaji Wiliam Chidumuka Magawa kutoka Kongwa. Mzee Chidumuka Magawa, simama kidogo nikutambulishe. Mchungaji William Chidumuka Magawa, alikuwa Mbunge wa Mpwapwa kati ya mwaka 1968 - 1970, Jimbo ambalo leo lina Wabunge watatu ambao ni Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Gregory Teu na mimi pia.

Yeye alikuwa peke yake akiwa Mbunge wa Jimbo hilo wakati huo, lakini pia akaendelea kuwa Mbunge wa Kongwa kati ya mwaka 1970 – 1975. Sasa hivi ni mstaafu yuko kijijini amenitembelea na ametutembelea kuonesha kwamba bado

wapo Waheshimiwa Wabunge ambao waliitumikia nchi yetu na bado wapo. *(Makofi)*

Katika wakati wake Mchungaji Magawa akiwa Bungeni, moja ya mambo ambayo aliyatetea sana na yakafanikiwa ni kutetea hoja ya kwamba, wakati ule wafungwa Tanzania walikuwa hawaruhusiwi kuvaa viatu na alitetea sana hoja hiyo mpaka serikali ikakubali kwamba wafungwa sasa waruhusiwe kuvaa viatu. Tunakushukuru Mchungaji na karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la semina; Mkurugenzi Msaidizi wa Shughuli za Bunge, Ndugu Mrema, ameomba niwatangazie Wabunge wote kwamba, kutakuwa na semina inayohusu Sensa ya Watu na Makazi leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hiyo muhimu itakayotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na itatolewa na Maafisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria. *(Makofi)*

Nawaomba wale ambao mna vikao muda huo muwaone sasa kwani nitatangaza matangazo ya vikao vyenu lakini muone namna gani mtafanya kwa sababu jambo hili la sensa ni jambo muhimu sana la Kitaifa, ninaomba tulipe kipaumbele.

Kwanza, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, anaomba Wajumbe wake wakutane saa tano mara baada ya matangazo haya Ukumbi Namba 227, Jengo la Utawala. Mmeruhusiwa kufanya hivyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Brig. Gen. Mstaafu Hassan Ngwilizi, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa tano, pia nimeruhusu jambo hilo liendelee katika Ukumbi Namba 231, Ghorofa ya Pili.

Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, anaomba mkutane katika Ukumbi Namba 231, saa saba, lakini kama nilivyosema basi mtaambiana wenyewe ni muda gani mkutane kwa sababu ni muhimu mkawepo katika semina ya sensa na makazi.

Mheshimiwa Angellah Kairuki, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba mkutane katika Ukumbi wa *Basement,* saa saba. Kama nilivyoeleza, vilevile angalieni muda mwafaka ili muweze kuhudhuria kwenye semina muhimu.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John M. Cheyo, anaomba wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali waku tane leo tarehe 12/4/2012 saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa B. Vilevile na ninyi muangalie wakati mwafaka mtakaofanya shughuli yenu hiyo ili msiweze kukosa katika Semina itakayokuwepo katika ukumbi wa Msekwa.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa nimwite Mwenyekiti Sylivester Masele Mabumba ili aendeleze jahazi lililo mbele yetu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester Massele Mabumba) Alikalia Kiti*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania wa Mwaka 2011 (The Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011)*

*(Kusomwa kwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada uliopo mbele yako unapendekeza kuanzishwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(Tanzania Livestock Research Institute Act – TALIRI)* kwa lengo la kuifanya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kutambulika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(TALIRI)* inayopendekezwa kutungwa, ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mpango Mkakati wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa mwaka 2008/2009 – 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Mifugo inatamka kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahamasisha, itahimiza, itaendeleza na kuwezesha uwekezaji katika utafiti wa mifugo na itaimarisha miundombinu, vifaa, huduma za kitaalamu, ushirikiano katika utafiti, ugani na wafugaji na uratibu na ushirikiano wa wadau. Aidha, Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2008/2009 – 2010/2011 unazingatia matumizi ya teknolojia bora, sahihi na endelevu katika uzalishaji wa mifugo kwa kuimarisha Taasisi za Utafiti wa Mifugo nchini ili kuongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa uzalishaji na uendelezaji wa mifugo hapa nchini, kwa sasa, unafanyika katika Vituo vya Mpwapwa, Tanga, West Kilimanjaro, Kongwa, Mabuki, Naliendele na Uyole chini ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo (*National Livestock Research Institute – NLRI*) Mpwapwa na kwa upande wa utafiti wa magonjwa ya wanyama unafanyika na Maabara Kuu ya Mifugo *(Central Veterinary Laboratory - CVL)* Temeke, Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Malale Tanga na Kituo cha Utafiti wa Mbung'o Kigoma chini ya *CVL*, wakati uratibu wa utafiti unatekelezwa na Kurugenzi ya Utafiti, Mafunzo na Ugani, Makao Makuu ya Wizara; vyote vikiwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa, hakuna chombo kilichoundwa kisheria cha kufanya, kusimamia na kuratibu utafiti wa mifugo unaotekelezwa katika Taasisi na Vituo hivyo ikilinganishwa kwa mfano; na utafiti wa uvuvi ambao unasimamiwa kisheria na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (*Tanzania Fisheries Research Institute-TAFIRI*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwa na chombo cha kisheria, kumesababisha udhaifu katika kutekeleza, kusimamia, kuendeleza na kulinda matokeo ya utafiti wa mifugo. Aidha, kutokuwepo kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo inayotambulika kisheria kunapunguza kasi ya mafanikio katika kazi za utafiti wa mifugo hapa nchini na ushirikiano kati ya Taasisi za utafiti hapa nchini na za nje ya nchi.

MheshimiwaMwenyekiti, Taasisi nyingi za utafiti hapa nchini kama vile Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi *(TAFIRI);* Taasisi ya Utafiti wa Wanyama Pori *(TAWIRI)* na nje ya nchi kama *Kenya Agricultural Research Institute (KARI)* ya Kenya; Ethiopian *Institute of Agricultural Research (EIAR)* ya Ethiopia na kwingine duniani zimeundwa na kuendeshwa kisheria kwa lengo la kuhuisha teknolojia zinazozalishwa na kusambazwa. Vilevile, Sheria za Utafiti Duniani kote zinasisitiza kulindwa (*Intellectual Property Rights*) kwa matokeo ya teknolojia zilizozalishwa kwa manufaa ya nchi na watafiti wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutungwa kwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania kunatarajia kuleta matokeo yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa ufanisi wa shughuli za utafiti wa mifugo na uendelezaji wa mifugo nchini;

(ii) Kuongezeka kwa teknolojia sahihi za tasnia ya mifugo;

(iii) Kuwepo kwa muundo madhubuti wa kitaasisi ukilinganishwa na muundo uliopo sasa; na

(iv) Kuimarika kwa ushirikiano kati ya Taasisi, mashirika na wadau wengine wanaoshughulikia utafiti wa mifugo na uendelezaji wa mifugo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuweka muundo wa utafiti utakaowezesha uzalishaji, upatikanaji na usambazaji wa teknolojia sahihi za mifugo nchini;

(ii) Kuweka muundo utakaovutia wataalam wa mifugo kujiunga na kubaki katika kazi za utafiti wa mifugo kwa kuwapatia mafunzo kwa wakati, maslahi bora na motisha *(rewarding system)* tofauti na hivi sasa ambapo wengi wao huacha kazi na kuhamia katika taasisi zingine ndani na nje ya nchi;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya utafiti na vitendea kazi ili watafiti watekeleze majukumu yao kulingana na viwango vya kimataifa kwa kuzingatia sayansi na teknolojia;

(iv) Kuweka mfumo utakaowezesha kushirikisha wadau wengine kama vile Vyuo Vikuu, Taasisi zisizo za Kiserikaili *(NGOs, CBOs)* na watu binafsi katika kuzalisha na kusambaza tekinolojia kulingana na mahitaji;

(v) Kuweka wazi kazi na majukumu ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania na zile za Taasisi zitakazokuwa chini yake**;**

(vi) Kuweka wazi kazi, mamlaka na majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania**;**

(vii) Kuweka taratibu za kuwezesha sheria kuzingatiwa na kutekelezwa *(Enforcement mechanism)* kwa kuwaweka Wakurugenzi wa Taasisi za Utafiti zilizo chini ya *TALIRI* na kuweka kipengele kitakachomwezesha Waziri mwenye dhamana ya kuendeleza mifugo kuandaa kanuni za utekelezaji wa sheria inayopendekezwa kutungwa;

(viii) Kuainisha Vituo vya Utafiti wa Mifugo *(Livestock Research Centres)* zitakazosimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania**;**

(ix) Kuweka wazi uhusiano kati ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania na Taasisi zingine zinazojihusisha na utafiti wa mifugo**;** na

(x) Kuweka mfumo wa utawala na usimamizi wa fedha *(financial provisions)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kutokana na umuhimu wa mambo yaliyozingatiwa katika Muswada huu, Muswada umegawanyika katika sehemu kuu sita. Sehemu ya Kwanza inaeleza jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, matumizi yake, ufafanuzi wa maneno na misemo yenye maana maalumu katika sheria inayopendekezwa pamoja na kuainisha dhana na misingi ya utafiti wa mifugo.

Sehemu ya Pili, inapendekeza kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania na majukumu yake; na inaweka bayana utaratibu wa namna ya kuanzisha Vituo vya Utafiti wa Mifugo vitakavyotelekeza majukumu ya Taasisi.

Sehemu ya Tatu, inatoa mapendekezo juu ya kuanzishwa kwa Bodi ya Taasisi. Katika sehemu hii zipo Ibara zinazohusu kazi za Bodi, mamlaka ya Bodi kuunda kamati mbalimbali. Pia, maelezo juu mamlaka ya Bodi kukasimu madaraka yake na mamlaka ya Waziri yameelezwa katika sehemu hii.

Sehemu ya Nne, inaelezea kuhusu masuala ya utawala na uendeshaji wa Taasisi. Aidha, sehemu hii ina Ibara zinazohusu uteuzi na kazi za Mkurugenzi, Naibu Mkurugenzi, Maafisa Waandamizi wa Taasisi, ajira kwa watumishi wa kada mbalimbali za Taasisi. Pia, sehemu hii inaainisha maeneo ya shughuli za utafiti, tafiti zinazofanywa na watafiti wa ndani ya nchi, makosa yatokanayo na kushindwa kuwasilisha taarifa za utafiti.

Vilevile, sehemu hii inatoa maelezo juu ya utafiti unaofanywa na watafiti wa nje ya nchi. Mamlaka ya Taasisi kuitisha taarifa, uvumbuzi, uwekaji wa mfumo wa motisha kwa watafiti na uratibu wa tafiti zimeelezwa katika sehemu hii.

Sehemu ya Tano, imeelezea kuhusu masuala ya fedha. Zipo Ibara zinazohusu mishahara, pensheni za watumishi, ukaguzi wa hesabu za Taasisi, uwasilishaji wa taarifa mbalimbali za Taasisi.

Sehemu ya Sita, inapendekeza masuala ya ujumla kama vile kubainisha makosa na adhabu chini ya sheria inayopendekezwa na Mamlaka ya Waziri ya kutunga Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** baada ya maelezo haya, naomba sasa Bunge lako Tukufu lijadili Muswada huu na kuupitisha ili uweze kuwa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe mwenyewe binafsi, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, atoe maoni ya Kamati.

**MHE. SELEMANI S. JAFO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, 2011 *(The Tanzania Livestock Research Institute, Act, 2011).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yanayohusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania wa mwaka 2011 *(The Tanzania Livestock Research Institute-(TALIRI) Act, 2011).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo wa mwaka 2011 (*The Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011),* ili Bunge lako Tukufu liupitie na hatimaye kuwa sheria baada ya kupitia hatua zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo katika sekta yoyote ile yanatokana na kuwekeza katika utafiti. Kwa Muswada huu, Sekta ya Mifugo iliyokuwa imesahaulika kwa miaka mingi katika utafiti, sasa itaweza kufikia malengo ya kuchangia kwa asilimia kubwa katika Pato la Taifa kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi Barani Afrika. Hata hivyo, uwingi huu haushabihiani na mchango wake katika Pato la Taifa. Hali hii inatokana na ukweli kwamba zaidi ya asilimia 98 ya mifugo yetu ni ile ya kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati yangu inaafiki kuwa Bunge lako Tukufu katika kikao hiki, sasa lijadili na kupitisha Muswada huu wenye lengo la kuanzisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kufikia hatua hii muhimu na ya kihistoria, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu. Aidha, kwa namna ya pekee, nawapongeza wadau na Taasisi zote zilizohusika na kukusanya mawazo tangu hatua za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** pamoja na maelezo haya ya utangulizi, Kamati inatoa maoni ya jumla kwa Serikali katika maeneo yafuatayo:-

- Serikali ione uwezekano wa kuongeza bajeti ya utafiti ili angalau ifikie lengo la 1% ya Pato la Taifa kama ilivyoahidi;

- Serikali iangalie umuhimu wa kukamilisha Sera ya Utafiti ya Taifa kwa kuwa mpaka sasa nchi haina Sera ya Utafiti;

- Utafiti utakaofanywa ulenge kutatua matatizo ya magonjwa, uzalishaji, malisho na maji kwa mifugo;

- Serikali kupitia *TALIRI* iweke utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya ufugaji wenye tija;

- Bodi ya *TALIRI* iwe makini katika kuhakikisha kuwa utafiti haufanyiki kwenye maabara peke yake, bali ufanyike pia katika eneo husika (*On Farm Research*) kwa kuwa kwa kufanya hivyo utaleta ushirikishwaji na matokeo chanya;

- Serikali idhibiti uingizwaji holela wa mazao ya mifugo nchini ili kulinda soko la ndani; na

- Kamati inashauri *TALIRI* ihakikishe kuwa matokeo ya utafiti utakaofanywa yanawafikia wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Miswada. Kamati yangu ilipitia Sehemu na Vifungu vya Muswada na kuishauri Serikali kurekebisha maneno na sentensi na jedwali la marekebisho liletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Baadhi ya maneno yaliyoainishwa na Kamati ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jina refu la Muswada `*Long Title,´* yatumike maneno `*Livestock Research´* badala ya *´Livestock Production´.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, Ibara ya 3 ambayo ni tafsiri ya maneno:-

- Katika kutafsiri neno `*laboratory*', neno *facility* litumike badala ya neno *´institution*'.
- Maneno *Livestock by-products´* yapewe tafsiri.
- Katika kutafsiri neno `r*eseacher´* neno *'person´* litumike badala ya `*graduate´.*
- Kwenye tafsiri ya neno *'Centre´,* maneno *'deemed to have been established´* yafutwe.
- Neno `*member´* liongezewe maneno *'of the board´* ili isomeke *'Member of the Board´.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Ibara ya 5(1), Kamati inashauri kuwa usambazaji wa matokeo ya utafiti kwa wadau iwe mojawapo ya majukumu ya Taasisi.

- Ibara ya 5(1)(a)(iii) maneno `*nutrition including feeding'* yafutwe na badala yake neno `*feeds* ` litumike.

- Ibara 5(1)(a)(vi) maneno `*animal health'* yaongezewe maneno `*and diseases'* ili isomeke `*animal health and diseases'.*

- Ibara ya 5(1)(g), Kamati inashauri kuanzishwe mfumo wa kutunza taarifa za utafiti *(Research Data Base and Backup Facility).*

- Ibara ya 5(n) liongezwe neno *'regional'* baada ya neno *Institutions'* na pia neno *'Stakeholders'* litumike badala ya neno`*Individuals.'*

- Ibara ya 6(2), Kamati inashauri majina ya vituo yabebe jina la Taasisi; mfano *TALIRI-Mabuki Centre*.

- Ibara ya 7 neno `*units* liondolewe na badala yake yatumike maneno *'Technical Committee.'*

- Ibara ya 8(1) Kamati yangu inashauri kuwa kwenye Bodi ya *TALIRI* wawepo wawakilishi kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, Ibara ya 9(2)(c), Kamati inashauri mamlaka ya kuajiri ibaki kuwa Bodi ya *TALIRI* badala Sekretarieti ya Ajira. Vilevile, katika Ibara hiyo yaongezwe maneno `*employment and termination of staff'* baada ya neno *authorize* ili kukifanya kifungu hiki kisomeke `…*employ or authorize employment and termination of staff…'*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Ibara ya 13(1), Kamati inapendekeza vyeo `Director General**'** na `Deputy Director General**'** vitumike badala ya `*Director'* na *'Deputy Director.'*

- Ibara ya 13 (2), Kamati inapendekeza ukomo wa kumteua Mkurugenzi Mkuu utajwe katika sheria hii.

- Ibara ya 17 Kamati inasisitiza kuwa kinga kwa Wajumbe wa Bodi iwe kwa nia njema.

- Ibara ya 18, Kamati inashauri kuwa baadhi ya majukumu yaliyomo katika Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 yatazamwe ili ikiwezekana yajumuishwe katika majukumu ya Bodi ya *TALIRI*.

- Ibara ya 18(1) (a) badala ya kuorodhesha maziwa yatokanayo na wanyama mbalimbali kifungu hicho kisomeke `*Milk Production'.*

- Ibara ya 18 (1) (b) badala ya kuorodhesha nyama zitikanazo na wanyama mbalimbali ibara hii isomeke *'meat production'*.

- Ibara ya 18(1) (c) kisomeke `*livestock by- products'.*

- Ibara ya 18(1)(g) maneno `*and behaviour***'** yaongezwe baada ya neno `*welfare'* ili isomeke… `*Animal welfare and behaviour'.*

- Ibara ya 18(2) (a) lifutwe neno `*the'* na badala yake yawekwe maneno `*Ethics and***'** ili kuifanya Ibara isomeke `…*with ethics and standards* …'.

- Ibara *ya* 18 (2) (b) (i) *maneno 'research outputs'* yatumike badala ya neno *'study'.*

- Ibara ya 18 (2) (ii), isomeke `c*oordinating researchers at various centers'*.

- Ibara ya 19 (2) *Research Proposal format* iwe pana kama za *COSTECH* na *SUA*.

- Ibara ya 19 (3), Kamati inashauri siku kumi na nne (14) za kupitisha *'research proposal'* ziongezwe ziwe ndani ya siku thelathini (30).

- Pia Kamati inashauri Ibara za 20 na 21 zibadilishane nafasi, Ibara ya 20 iwe ya 21 na ile ya 21 iwe ya 20 ili kuleta maana na mtiririko mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano. Ibara ya 26, Kamati inashauri iongezwe Ibara itakayotamka `*Establishment of Livestock Research Fund'.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine ni kama yatakavyoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Kamati kuwa baada ya Muswada huu kuwa Sheria, Serikali itaweka utaratibu mzuri kwenye Kanuni ili Sheria hii iweze kueleweka kwa Wananchi na inapowezekana tafsiri ya Kiswahili ni muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kuwa, Muswada huu umebeba maoni mengi ya wadau na bila shaka utakapokuwa Sheria kamili, mabadiliko ya kweli yatadhihirika katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitumie nafasi hii, kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Daktari David M. David (Mb), Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Benedict Ole-

Nangoro (Mb), Katibu Mkuu Daktari Charles Nyamurunda, Naibu Katibu Mkuu Daktari Yohana Budeba na Wataalamu wote wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa kutoa maoni yao katika kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mwenyekiti na Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Makamu Mwenyekiti.

Wengine ni Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mheshimiwa Daktari Christine Gabril Ishengoma, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Sylevester Mhoja Kasulumbayi, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mheshimiwa Abdulsalaam Seleman Amer, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Mansoor Sharif Hiran, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mheshimiwa Daktari Titus Mlengeya Kamani, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni na mimi kijana wenu mtiifu, msikivu Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Jimbo la Kisarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge Daktari Thomas Kashililah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Elieka Saanya na ndugu Chacha Nyakega kwa kuratibu vikao vya Kamati hadi maoni haya kutoka katika muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nipende kuwashukuru sana wazazi wangu walionilea na kunipa maadili mema, lakini nipende kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu mkubwa. Hali kadhalika nipende kuwashukuru wafanyakazi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe pamoja na Madiwani wote ambao sasa hivi wako katika mchakato wa bajeti. Wote nawapenda sana, lakini kubwa zaidi napenda sana kuwashukuru wananchi wangu wote wa Jimbo la Kisarawe kwa kuniombea na kunihakikishia kwamba maendeleo ya Kisarawe yanazidi kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, naomba kuunga mkono Muswada na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafo kwa taarifa ya Kamati yako. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kuwa hapa mahali nilipo na kuweza kusoma maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria na Kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo wa Tanzania kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 86(6), toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nikutakie afya njema na busara iliyotukuka ili uweze kuliendesha Bunge hili kwa kufuata misingi ya kanuni na haki. Aidha, niwashukuru viongozi wangu wote wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) sambamba na Makamanda wakuu wa Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuongeza jembe kali Bungeni baada ya kujizolea ushindi mkubwa katika Jimbo la Arumeru Mashariki na kuongeza Madiwani. Hongereni sana Makamanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama nitashindwa kutambua mchango wa viongozi, wanachama pamoja na wananchi wote wa Wilaya ya Maswa kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge nje na ndani ya Bunge. Nasema ahsanteni sana, nami nitaendelea kupambana na uonevu wowote na manyanyaso kwa wana Maswa. Hivyo kwa dhamira hiyo, kitendo cha kuchakachuliwa kwa Makao Makuu ya Mkoa wa SIMIYU kulikofanywa na Serikali hivi majuzi, hizi ni mbinu chafu zilizotengezwa ili sisi wanandugu tugombane na tugubikwe na malumbano yasiyo na tija. Nawaomba tulieni katika kipindi hiki tunapoandaa utaratibu mzuri, mzidi kuwa watulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, niwashukuru wajumbe wenzangu wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji inayoongozwa na Mwenyekiti wetu Prof. David Mwakyusa, kwa ushirikiano katika utendaji wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kabla ya kuanza kupitia na kutoa maoni yake kwenye baadhi ya vifungu, inapenda kutokukubaliana na dhana hii ya Serikali ya kuongeza taasisi ambazo kwazo zinatakiwa zipatiwe ruzuku ili kujiendesha na hivyo kuzidisha mzigo mkubwa kwa walipa kodi, kwani fedha hizo ni za matumizi ya kawaida na si za matumizi ya maendeleo. Kwa maana rahisi ni kwamba, taasisi hizi zinasaidia kuongeza ukubwa wa Serikali badala ya kupunguza ukubwa wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa, vituo hivi vya utafiti, vilikuwepo miaka yote na vinaendelea kutimiza majukumu yake ya msingi kulingana na

matakwa ya uanzishwaji wake. Swali la kujiuliza, ni kwa nini majukumu ya Taasisi yasiwe ni sehemu ya majukumu ya Wizara? Au ni kwa nini taasisi zote za utafiti zisiwe chini ya *Commission* ya Sayansi na Teknolojia-*(COSTECH).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka kumbukumbu vizuri ni kwamba, Februari 17 mwaka 2009, Serikali kupitia Rais Jakaya Kikwete, ilitangaza azma ya kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa kwa ajili ya maendeleo ya utafiti. Fedha hizo zilitakiwa ziende moja kwa moja kwa *Commission* ya Sayansi na Teknolojia. Kwa nukuu hiyo ni kwa nini Serikali inashindwa kuoanisha dhana nzima ya Rais na kuiweka katika hali halisi ya kiutendaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5(1) cha Sheria No. 7 ya 1986 iliyoanzisha *COSTECH* kinaeleza wazi majukumu na mamlaka ya *Commission* hiyo kuwa itakuwa ndiyo Mshauri Mkuu wa Serikali kwa mambo yote yanayohusiana na tafiti zote na maendeleo ya teknolojia katika nchi. Kambi ya Upinzani inaona kwamba ili kuonyesha dhamira ya kweli ya kupunguza matumizi makubwa ya Serikali, lingekuwa jambo la busara kuwa, taasisi zote zinazofanya tafiti kwenye sekta mbalimbali kuwa chini ya *COSTECH* kwani *Commission* hii ndiyo inayotengewa fedha kwa ajili hiyo, au kuwa chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6(1) cha Muswada huu kinasema kuwa "Waziri baada ya kusahuriwa na bodi, ataanzisha vituo kadhaa vya taasisi kwa madhumuni ya kutekeleza kazi za taasisi kama itakavyohitajika". Aidha kifungu cha 6(4) kinasema kuwa, "Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Bodi kwa amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, kuanzisha vituo vingine na kuipa Taasisi udhibiti na usimamizi wa shughuli za vituo hivyo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya rasilimali ya malisho kwa maeneo ambayo ardhi ni kubwa mara nyingi ardhi hiyo

inakuwa inamilikiwa kimila na vijiji husika au humilikiwa na watu binafsi. Malisho ya pamoja mara nyingi ndio yanayopelekea wafugaji kuhama toka eneo moja kwenda lingine kwa lengo la kutafuta malisho yaliyo bora pamoja na maji kwa ajili ya mifugo yao. Uhamaji huo ndio chanzo kikuu cha ugomvi baina ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, aidha ndicho chanzo kikubwa cha ueneaji wa magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi endelevu ya maeneo ya malisho kwa wafugaji yanaathiriwa na kubadilika mara kwa mara kwa misimu ya mvua na hivyo kusababisha ubora wa malisho katika maeneo mbalimbali kutofautiana na hivyo mzunguko wa kuhama kuanza, pili ni kutokuwepo kwa sheria na utaratibu wa kuwamilikisha wafugaji ardhi ili waiendeleze wao (kutokuwepo kwa mpango makini wa matumizi ya ardhi kwa wafugaji). Kwa ufupi nchi yetu kinadharia ina eneo kubwa la ardhi lakini ukweli ni kwamba eneo hilo ni dogo sana kuweza kuhimili idadi ya wakulima, mifugo, wanyamapori na wachimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli uliowazi kuwa, migogoro mingi iliyopo baina ya wananchi na Serikali inatokana na ardhi, naomba kufanya marejeo kwa vituo viwili vya tafiti za mifugo kama mfano wa jinsi vituo hivyo, utafiti unavyohitaji ardhi na eneo la kutosha na tuone ni ardhi kiasi gani inayomilikiwa na kila kituo, pengine vituo hivyo vinahitaji ardhi zaidi ili kufanikisha tafiti zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Utafiti wa Mifugo Kilimanjaro Magharibi - *Livestock Research Centre (LRC)* kilianzishwa mwaka 1948 kikimiliki ekari 5000 sawa na hekta 2,023. Tu lakini kwa sasa kituo hicho kinamiliki takribani ekari 24000 sawa na hekta 10000. Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Mpwapwa kina mashamba matatu kwa ajili ya utafiti yenye ukubwa wa jumla ya hekta 7,000, kama ifuatavyo, shamba

kubwa likiwa na hekta 5,080, Kiboriani hekta 1800 na Ilolo likiwa na hekta 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi hiyo inayomilikiwa na vituo hivyo ilipatikana miaka ya nyuma, wakati idadi ya watu katika maeneo husika ikiwa ni ndogo na pia kipindi hicho hakukuwa na tabia iliyopo sasa ya watu wachache kupora ardhi za vijiji kwa udanganyifu jambo ambalo limesababisha kuwepo kwa kesi nyingi sana hapa nchini zinazohusu ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona ni wazi kwa mifano tajwa hapo juu kifungu hiki kinaweza kutumiwa vibaya na hivyo kuleta madhara makubwa sana kwa wananchi na mwishowe nchi ikaingia kwenye mapambano ya wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 15(1) kinasema kuwa nanukuu, "Bodi inaweza kuajiri waajiriwa wengine wanataaluma na wasio wanataaluma wa Taasisi kama itakavyoonekana ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora na wenye ufanisi wa kazi za taasisi", mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu zile zilizotolewa na wadau katika kifungu cha 9(2)(c) cha Muswada huu kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma (*Public Service Amendment Act No.18 ya mwaka 2007)* ilianzisha na kuipa mamlaka ya kutoa ajira Sekretarieti ya Ajira kuwezesha ajira katika Utumishi wa Umma kifungu cha 29 (4). Hivyo kifungu hiki cha 15(1) cha Muswada huu kinakinzana na kifungu cha sheria hiyo ya uanzishwaji wa Sekretarieti ya Ajira. Sambamba na hilo, ni kwamba, Bodi ni mamlaka ya nidhamu kwa maana kwamba kazi yake kubwa ni kutoa usimamizi kwa shughuli zinazofanywa na utawala wa taasisi na sio mamlaka ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 20 cha Muswada kinachosema kuwa, kwa mtu yeyote atakayeshindwa kuwasilisha kwenye Taasisi taarifa ya mwisho ya utafiti wake

atakuwa ametenda kosa na Kifungu cha 20(a) kinataoa adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kwenda jela kwa kipindi cha miezi sita. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kingeweka wazi zaidi kuwa adhabu hiyo ingehusu wale watafiti ambao wamepata ufadhili toka kwenye Taasisi au chombo chochote kinachotumia fedha za walipa kodi, kwani kuna uwezekano kwa mtafiti kutumia fedha zake na kwa bahati mbaya fedha zikaisha kabla ya kupata matokeo ya utafiti aliokuwa akiufanya. Je, kwa mazingira ya mtu anayefanya utafiti kwa fedha zake, naye anastahili kulipa faini au kwenda jela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 27 cha Muswada kinampa Waziri mwenye dhamana na mifugo kwa kushauriana na Bodi kupanga marupurupu kwa Wajumbe wa Bodi. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kifutwe na badala yake utaratibu wa kupanga na kutoa marupurupu kwa Wajumbe wa Bodi uwe ni mmoja kwa Wajumbe wa Bodi zote kwa taasisi na wakala za Serikali. Kwani tunaamini kuwa kazi ya bodi zote ina lengo kuu la kusimamia jinsi utawala unavyoendesha taasisi husika na hivyo hakuna sababu kwa Wajumbe wa Bodi hizo kuwa na marupurupu tofauti, jambo hilo linaweza kusababisha Wajumbe wa Bodi kujiingiza katika kazi ambazo hawastahili kuzifanya kwa mujibu wa kanuni na taratibu za utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba kunukuu sehemu ya taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na marupurupu kwa Wajumbe wa Bodi, "Ada za Wakurugenzi na gharama za Bodi za Wakurugenzi zimekuwa zikiongezeka kila mwaka kwa baadhi ya Mashirika ya Umma. Hali hii inaonyesha kutofuatwa kwa kanuni za utawala bora. Kazi mojawapo ya Bodi za Wakurugenzi katika taasisi ni kusimamia majukumu ya Menejimenti ya kuongeza mapato na kupunguza matumizi. Kwa upande mwingine matumizi yamepanda kwenye baadhi ya Mashirika kwa sababu ya ongezeko la gharama za Bodi na ada za Wakurugenzi ambazo hupangwa na Wakurugenzi

wenyewe. Hii imedhihirika katika ukaguzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA).* Katika mkutano wake wa Bodi uliofanyika mwaka 2006, Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliamua kwamba ada za Wakurugenzi zipangwe kwa njia mbili; njia ya kwanza - Wakurugenzi walipwe ada kwa kupungua *(on a reducing basis):* Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti walipwe Sh.milioni 1.75 kwa mwaka, wakati Wakurugenzi wengine walipwe Sh. milioni 1.5 kwa mwaka. Njia ya pili, iwapo faida ya mamlaka kabla ya kodi ni sawa au zaidi ya bilioni moja, ada za Wakurugenzi zitakuwa zinalipwa asilimia 4 ya hiyo bilioni moja au zaidi na itagawanywa kama ifuatavyo, asilimia kumi (10%) ya asilimia nne (4%) ya faida kwa Mwenyekiti na Wakurugenzi wengine watagawana asilimia tisini (90%) ya asilimia nne (4%)". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ushahidi tosha kuwa badala ya Serikali kuwekeza kwenye taasisi zinazozalisha na hivyo, kuiondolea Serikali mzigo wa kukopa kila kukicha yenyewe, inawekeza kwenye taasisi zinazotumia kile kidogo tulichonacho. Uanzishwaji wa taasisi hii ni mwendelezo wa matumizi yasiyokuwa na tija kwa walipa kodi wa nchi hii na jambo hili Kambi Rasmi ya Upinzani inazidi kulikemea kwa nguvu zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mawasilisho ya Kambi ya Upinzani juu ya Muswada huu, sasa tunaingia kwenye majadiliano. Napenda niwataje ambao tutaanza kuchangia. Kwanza Mheshimiwa George Simbachawene atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Julius Masele na Mheshimiwa Prof. Peter Msolla wajiandae.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pili, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kibakwe kwa

ushirikiano wanaonipa katika kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo yanayostahili kulingana na wakati na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kwanza kuwapongeza sana Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na hasa Waziri na Naibu wake kwa kuleta Muswada huu wa sheria hii muhimu katika kipindi cha sasa kuhusu Taasisi ya Utafiti wa Kituo cha Mifugo Tanzania. Niwapongeze sana, sheria hii nimeisoma, imeandaliwa vizuri, imezingatia sana mazingira ya sasa ya ushindani wa kibiashara, mazingira ya sasa ya ushindani katika kanda yetu ya *East Africa* na kwa hivyo unapozungumzia mifugo au ufugaji unazungumzia uchumi moja kwa moja. Tunaamini kabisa kwamba kilimo na mifugo ndio sekta ambazo zinaajiri Watanzania wengi takriban asilimia 80, lakini hakutakuwa na maendeleo ya mifugo kama hakutakuwa na utafiti wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani sasa ufugaji si ule wa kwetu wa kizamani. Ufugaji umebadilika kwa ajili ya kuleta tija inayostahili na hili litawezekana tu kama tutakubaliana Watanzania kutumia tafiti mbalimbali ambazo kwa hakika zimekuwepo na vimekuwepo vituo vya utafiti hapa nchini lakini sasa vinakuja na sura iliyobora zaidi ambapo sasa kunaundwa Taasisi ya Utafiti Tanzania ambayo itajitegemea. Hii ni hatua kubwa sana kwa nchi yetu. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa kazi nzuri ambayo unafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vituo hivi vya tafiti na vimekuwepo kikiwepo kituo cha Mpwapwa cha Utafiti wa Mifugo na ndiyo iliyokuwa Makao Makuu ya Utafiti ya Mifugo Tanzania. Kituo hiki pamoja na vingine vimekuwa vikifanya kazi nzuri ingawa bado kuna changamoto ya namna ya matumizi ya tafiti hizo. Vilikuwepo vituo vingine na ambavyo vimeonyeshwa kwenye *schedule* ya kwanza navyo ni kama Kituo cha Mpwapwa, Kituo cha Kongwa, Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mabuki, Kituo cha Naliendele, Tanga, Kilimanjaro

Magharibi na Uyole na bado vinatajwa hata katika Sheria hii kwamba vitaendelea kuwa vituo vya utafiti wa mifugo kama taasisi moja yenye *autonomous*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nijikite kuzungumzia Kituo cha Utafiti cha Mpwapwa. Kituo hiki labda tu kwa faida ya Watanzania, niseme tu kwamba ni kituo cha kwanza katika *East Africa and Central* na kilianzishwa na Wajerumani mwaka 1900 na josho la kwanza katika *East Africa and Central* lilijengwa Mpwapwa. Kwa hiyo, unapata sura kwamba Mpwapwa ni sehemu ya namna gani. Kihistoria hata kabla ya Uhuru kituo kilikuwepo. Chanzo cha utafiti wa mifugo katika *East Africa and Central* tunaweza tukasema ni Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Sheria hii nimeona wamejaribu kuvitaja kwa ujumla wake ingawa hawasemi ni wakati gani pengine watasema na katika Sheria hii hawajasema sasa Mpwapwa itakuwa ikoje, nilitaka hapa nipate kueleweshwa kwamba sasa Mpwapwa itatajwa kwamba bado ni Makao Makuu ya Utafiti wa Mifugo nchini au mnaanza mchakato mpya. Kama itakuwa hivyo tuanze kukaa mkao wa kujiandaa kuwa Makao Makuu, tuanze kuandaa mazingira mengine ya kufanya hali hiyo ifanane na chombo ambacho ni *autonomous*, tusije tukafika mbele huko tukapigana chenga Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachofahamu ni kwamba Mpwapwa itaendelea kuwa Makao Makuu ya Vituo hivi vyote vya Utafiti katika Tanzania na sababu zake kwa nini nasema hivi? Sio kwa sababu mimi ni Mbunge ninayetoka Wilaya ya Mpwapwa, Kituo cha Utafiti cha Mpwapwa kina mazingira ya aina tofauti na Vituo vingine vyote vilivyoko Tanzania na pengine hata katika *East Africa*, tuna uwanda wa aina tatu wa tafiti za mifugo na unaposema utafiti wa mifugo humaanishi chochote, unachomaanisha ni hali ya hewa ya mifugo lakini hali ya hewa yenyewe itakayowekwa ile mifugo

lakini pia hali ya hewa itakayootesha nyasi au majani ya malisho ya mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Mpwapwa tuna nyanda tatu. Tuna Kiboriani ambayo hali yake ya hewa ni ya baridi kali kabisa ambayo ni tofauti kabisa na Iringa, ni tofauti na Mbeya na ni tofauti na Kilimanjaro, ni hali kama ilivyo Ulaya. Kwa hiyo, unaweza ukajaribu kufuga wale kondoo wa manyoya mengi kama ilivyo Ulaya. Kwa hiyo, hali ya hewa ile inayopelekea kuwa na mimea hata ambayo haipatikani katika sehemu nyingine ya Tanzania inafanya tuwe na *a class* ya utafiti mifugo ambayo itakuwa tofauti na mazingira ya sehemu zingine ambako viko vituo hivi. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba eneo lile la Mpwapwa kwa ujumla wake kwa sababu hizo basi liwe ni eneo ambalo kwa kweli litapewa fursa ya pekee hata kubaki kuwa bado ni Makao Makuu ya Utafiti. Hiyo ni Kiboriani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishuka chini utakuta Kikombo. Kikombo ni eneo la ileile *Research Institute* lakini ni eneo ambalo lina hali ya hewa ya baridi ya wastani ambayo inalingana sasa na maeneo mengine kama ya Morogoro. Kwa hiyo, kiutafiti unapata Ukanda mwingine wa Utafiti ambao ni tofauti na maeneo mengine yenye joto la Kanda ya Kati ambayo kuna ukame na hili unalipata kulekule Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Kikombo ambako kuna hali ya baridi ya wastani na uoto wa tofauti na ule wa Kiboriani lakini unaupata uoto ule mwingine wa ukanda wa ukame unapata Ilolo ambako kuna hali ya hewa ya ukame ambako unalinganisha na Dodoma kwa ujumla wake, Singida, Tabora, Shinyanga kwa hiyo unapata hali za hewa tatu katika eneo moja. Hii inanipelekea mimi nishawishi kwamba kusije kukatokea mabadiliko yoyote ya Makao Makuu ya Taasisi hii inayoundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotaka kulizungumzia hapa ni suala zima la Bodi ya Utafiti. Tumesema katika hii Sheria kwamba kutakuwepo na Bodi. Katika hii Bodi imeanisha na kutaja baadhi ya Wajumbe wa Bodi hiyo. Sasa bila kuzitaja mojamoja niende tu kwenye sehemu ya tatu, kifungu cha 8(2)(f). Nimezisoma zile zote lakini nilipofika kwenye (f) nimeshindwa kuelewa inamtaja nani. Inasema miongoni mwa watakaounda Bodi hiyo ya Taasisi ya Utafiti ni pamoja na wawakilishi wawili toka mashirika ya sekta binafsi yanayojishughulisha na masuala ya mifugo, hakifafanui zaidi. Kifungu hiki kina utata kwa sababu hapa umewataja wawakilishi hawa wengine wote watakaoingia kutokana na nafasi watakazoingia nazo lakini hapa nilitegemea ndipo wafugaji wapatikane na wafugaji nao lazima wawepo kwenye Bodi kwa sababu Bodi hii itakuwa ni Bodi ambayo itaendesha chombo ambacho kina *autonomous* basi hata angalau wale *beneficiaries* kwa maana ya walengwa ambao ndiyo wafugaji na wao wawepo katika uwakilishi ule. Sasa kwa ujumla wake hiki kifungu kinavyosema unashindwa kuelewa. Unaposema mashirika ya sekta binafsi inamaanisha nini? Ni *NGO* au ni hawa watumiaji wa *product* za mifugo kwa maana ya *processors*, yaani hawa wazalishaji wa bidhaa za mifugo au una maana wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukijaribu kuangalia kwa sababu pengine idadi hii ipo kwa mujibu wa Sheria inayounda hii Bodi basi nadhani hapa kuna haja hapa tukaongeza, tunataka kuona hawa Wawakilishi wa *NGO* waingie humu kwa sababu *NGO* nyingi zinatusaidia sana katika kufanya tafiti. Mkiwa na mtu anayefanya utafiti kwenye Bodi inawasaidia sana kupata habari ambazo ni za kitafiti juu ya hali ilivyo ya mifugo nchini. Pia kuna hawa wazalishaji wa bidhaa, hawa wanaozalisha bidhaa za mifugo ni vizuri wakawa na wawakilishi lakini pia wafugaji ni vizuri wakawemo. Sasa Waziri mjaribu kuona ni namna gani tunaweza tukafanya marekebisho hapa tukaweza ku-*accommodate* hawa wawakilishi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilipenda kulizungumzia ni tatizo letu la kutokutumia matokeo ya tafiti. Hili ni tatizo sugu na hata katika Sheria hii haisemi kwamba hii Taasisi sasa itaenda *to what extent*, itaenda mpaka wapi katika kuhakikisha kwamba ule utafiti wao unatumika? Maana wamekuwa wakifanya kazi za tafiti na taarifa za tafiti sio kwamba hazipo, zipo. Hapa kinachobadilishwa ni muundo tu, lakini tumekuwa na tatizo la kutokutumia tafiti na hili ni tatizo kubwa na Serikali mimi nadhani ni vyema wakaliangalia tatizo hili kwamba tukiwa na tafiti peke yake tukaweka kwenye ma-*shelves* hazitusaidii chochote bali matumizi yake ndiyo jambo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri katika Sheria hii, Taasisi hii hebu ikasogea hata kuhakikisha inasukuma kwa kiasi chochote ingawa kusiwe kukawa kuna *interference* ya *implementation* maana kila mtu ana sehemu yake. Hawa kazi yao ni kutafiti lakini wanaokwenda kusimamia utafiti ni wengine lakini basi iwe na kamkono fulani kawe kanaingia na kuhoji kwa nini bwana hizi tafiti zinaenda hivi. Maana wasiishie kwenye majaribio halafu wakaweka taarifa zao, nilijaribu kupendekeza namna inavyoweza kuwa nikaona ninashindwa kupata moja kwa moja lakini nadhani unaweza Mheshimiwa Waziri hata kupitia Kanuni utakazozitengeneza ukasema basi taasisi sasa iende *at the extent* ya kuona utafiti wake unaanza kusimamiwa na unatekelezwa na hata kushawishi au kukushauri wewe kupitia Kanuni utakazopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa ni huu nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. MASELE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia kwenye mjadala huu wa Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo. Kwanza na mimi ni-*declare interest* kwamba natoka katika jamii ya wafugaji hususani Wasukuma

eneo la Shinyanga. Kwa hiyo, tunapojadili hapa tunashukuru kwamba Serikali sasa imewakumbuka wafugaji wote Tanzania kwa kuanzisha Taasisi hii muhimu ambayo kimsingi italeta mageuzi makubwa kabisa katika ufugaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwapongeze sana Wizara pamoja na Kamati ya Bunge ya Kudumu kwa kuleta Muswada huu na kuufanyia kazi nzuri sana. Kwa kweli ni Muswada ambao umeandaliwa vizuri japokuwa kuna mambo madogo madogo ambayo tutajaribu kuzungumza hapa kwa ajili ya kuyaboresha hasa katika kuhakikisha kwamba sekta hii ya mifugo inakuwa sekta muhimu katika kuchangia Pato la Taifa na kuendelea kutoa ajira kwa watu wengi wa jamii ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nilikuwa naangalia muundo wa Bodi katika Muswada huu, imeelezwa kwamba kutakuwa na wawakilishi kutoka sekta binafsi. Napenda kufahamu baadaye Waziri atakapokuwa anajibu kwamba hii sekta binafsi inayojishughulisha na sekta ya mifugo ni watu wa namna gani? Ni makampuni ama ni taasisi zingine binafsi ama vyama vya wafugaji? Nilitaka nifahamu vizuri hapa kwa sababu katika muundo wa Bodi ni muhimu sana kushirikisha vyama vya wafugaji na tunafahamu katika Tanzania tuna vyama vya wafugaji vingi. Tuna vyama vya wafugaji Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini na tuna vyama vya wafugaji Kanda ya Mashariki. Kwa hiyo, ningependa nifahamu ushiriki wao katika muundo wa bodi katika kusimamia sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Muswada yamezungumzwa sana kuhusu biashara, uongezaji wa thamani na masoko. Kwa kipindi kirefu sana tumekuwa tunalalamika Bungeni hapa na Wabunge wengi na leo nimeshuhudia Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwamba Tanzania na nchi nyingine za Afrika zinashindwa kusindika bidhaa zake na zinauza bidhaa ghafi nchi za nje. Sasa ukitazama ni sekta gani ambayo tunaweza kuanza nayo maana kila siku tutakuwa

tunasema tu kwamba tunashindwa kusindika lakini tunatakiwa tuthubutu sasa kuanza kusindika, tunaanzia wapi? Kama tumeshindwa kwenye sekta ya mifugo ambayo ni sekta nyepesi zaidi ambayo tukiwekeza nguvu pale tunaweza tukaanza kusindika bidhaa za mifugo na tukaweza kuuza bidhaa ambazo zimefanyiwa kazi na bidhaa za mwisho badala ya kuuza bidhaa ghafi ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye hili nilitegemea kabisa kwenye taasisi ile ieleze wazi ni namna gani itasimamia viwanda ambavyo vitajishughulisha na mifugo. Hapa nazungumzia viwanda kwa mfano vya nyama. Kiwanda cha nyama kwanza kinashughulikia nyama yenyewe kwa maana ya yule ng'ombe au mbuzi lakini baadaye kinaendelea zaidi na mazao mengine yanayotokana na mifugo kwa mfano maziwa, ngozi na vitu vingine vinavyotokana na mifugo. Sasa kwenye eneo hili haijaeleza vizuri sana; imeeleza tu kwamba itaongeza thamani, itatafuta masoko lakini nitataka ufafanuzi baadaye kwamba ni namna gani watasimamia eneo hili la viwanda ambalo inaonekana tumeshindwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano pale Shinyanga ambapo ndiyo Mkoa unaongoza kwa kuwa na mifugo mingi kuliko Mkoa wowote Tanzania, sisi tuna takribani ng'ombe milioni sita, mbuzi na kondoo milioni 10, kuku ndiyo usiseme lakini pale tuna kiwanda cha nyama ambacho kilijengwa tangu mwaka 1974, kiwanda kile hakijawahi kufanya kazi hata siku moja na sioni jitihada kabisa za Wizara juu ya kukifufua kile kiwanda na mifugo ile ambayo iko ukanda ule waweze kupata soko la kuuza mifugo ile kwenye kiwanda kile na kutoa ajira kwa vijana wengi wanaohangaika ajira. Leo ndugu yangu Simbachawene alikuwa anazungumzia Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti yawe Dodoma, lakini na mimi naweza kusema kwa nini yasiwe maeneo ya Shinyanga na Kanda ya Ziwa ambapo ndio kuna mifugo mingi? Sasa tunapozungumzia sekta ya mifugo lazima tuangalie maeneo ambayo kuna mifugo mingi na tujaribu

kupeleka sasa taasisi kama hizi maeneo yale ili zikafanye kazi kwa karibu na wadau wengine wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo unakuta *ranch* zinajengwa labda Ruvu, pesa nyingi zinawekwa Ruvu, lakini Ruvu pale nani mfugaji zaidi ya ndugu zangu wale kutoka Arusha Wamasai ambao wanahamia kule kama sisi Wasukuma tunavyohamia maeneo ya Rufiji, Ifakara na kwingine. Tunahamia kule kwa sababu mazingira tunakotoka hayajatengenezwa vizuri. Sasa swali ambalo nataka kuuliza tunaposema tupunguze idadi ya mifugo, hapa tatizo ni idadi ya mifugo ama hatujatengeneza mazingira mazuri ya kutumia sasa ule wingi wa mifugo yetu kwa faida zaidi? Kwa sababu Ulaya au nchi nyingine tunazozisifia kwamba zimefanikiwa kwenye mifugo si kwamba zina idadi ndogo ya mifugo. Sisi hapa tuna mifugo milioni 20, tunashika nafasi ya tatu kwa Afrika lakini Ufaransa pale wana mifugo zaidi ya kwetu, ile mifugo ambayo ni mbegu bora, ng'ombe yule mwenye tani nyingi, ng'ombe ambaye ana uwezo wa kutoa maziwa mengi lakini wanao wengi kuliko idadi tuliyonao sisi. Shida hapa si idadi ya mifugo, ni namna gani tuna-*manage* mifugo tuliyonayo na hizo *bleeding* nzuri ambazo tunazitengeneza ili ziweze kuleta tija na faida kwa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiweza kutengeneza na kusimamia vizuri viwanda maana yake tutakuwa tumetengeneza soko la uhakika kwa wafugaji na hawawezi kukimbilia sehemu nyingine kuleta vurugu na wakulima kama kule wanakotoka, kule kwenye *source* tayari kuna soko la uhakika, kuna kiwanda, kuna bidhaa za ngozi zinatengenezwa. Kwa hiyo, watu watapewa elimu ya kuhakikisha kwamba mifugo yao wanaiboresha kwa kuilisha na kunenepesha na kwenda kuuza sehemu ambayo wanauhakika nayo. Lakini sasa hivi tunavyosema punguza, haitusaidii sana kwa sababu unapunguza unapeleka wapi? Leo tunafahamu kila Mkoa takwimu zinaonyesha idadi ya matumizi ya ng'ombe kwa siku,

kama wanapungua au kuongezeka ni watano tu lakini tunaposema punguza unawapeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa mdogo nakumbuka Serikali ilikuwa na kampuni yake ambayo ilikuwa inajishughulisha na biashara ya mifugo, ilikuwa inatambulika kama KABIMITA. KABIMITA ilikuwa ni Kampuni ya Biashara ya Mifugo Tanzania ambayo jukumu lake kubwa ilikuwa ni kufanya biashara yaani Serikali ilikuwa ina-*coordinate* biashara ya mifugo, KABIMITA imekufa, haipo. Sasa Waziri kama atatueleza kama pamoja na kuongeza thamani na kutafuta masoko, je, tunaelekea kule kwenye kufufua kampuni ile ili iweze kusimamia hata kama tunauza ng'ombe, kama kwenye baadhi ya nchi ambazo zinahitaji ng'ombe hazihitaji nyama basi iwepo kampuni ambayo ina-*coordinate* na kujua idadi ya ng'ombe wanaokwenda kuuzwa nje na hatupaswi kuogopa. Tunachotakiwa kufanya ni kuelemisha wafugaji wetu wajue kwamba wale ng'ombe tunaweza tukatumia fursa ya nchi jirani ambazo zina uhaba wa ng'ombe tukafanya biashara badala ya kusema punguza, tunapunguzaje? Wakulima na wafugaji wa ng'ombe tutambue hawana ujuzi wa biashara. Wengi ni watu wanaokaa vijijini ambao utaalam wao kwenye mambo ya biashara ni mdogo. Sasa tunaposema badilisheni ng'ombe zenu mfanye biashara hiyo taaluma ya biashara hawana. Kwa hiyo, nasisitiza suala la elimu pia ni muhimu sana, wakulima na wafugaji wa ng'ombe wapewe elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, lazima Serikali iandae na iwe na *Database* ya wafugaji, ijue wafugaji wake nchini wako wangapi, ng'ombe wako wangapi na sehemu gani ili kurahisisha hata wanaoweka programu za elimu, iwe rahisi kuwafikia na kuwapa elimu ya matumizi bora, ufugaji bora ambao tunauzungumzia kama Sera ya Taifa ya Kupunguza Mifugo. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kufanikiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa ujumla, Muswada huu ni mzuri na ukipitia baadhi ya vipengele, baadhi ya kasoro hizo ndogo ndogo ambazo zinahitaji ufafanuzi, kwa mfano kama kwenye suala la viwanda, naomba Wizara iweke msisitizo kweli, kwenye kuanzisha viwanda. Nami ningependa sana kiwanda cha Shinyanga kiwe mfano kwa sababu ni rasilimali, ni pesa imetumika pale, haijafanya kazi. Tukiangalia *value for money* pale, ni kwamba tumepoteza. Lakini ningependa sana Serikali ianzie pale Shinyanga kuweza kufufua viwanda vile kwa ajili ya matumizi ya masoko ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilikuwa nataka tu niongezee la mwisho hili la Makao Makuu ya "*Centre*". Ninavyojua, Tanzania hapa tuna Mikoa kama 10 ambayo inajihusisha na ufugaji na sina ubishi na *proposal* anayoisema ndugu yangu Mheshimiwa Simbachawene kwamba Mpwapwa imekuwa ni sehemu moja muhimu sana kwa ufugaji na hasa tafiti za mifugo. Kwa hiyo, ningependelea Serikali inapoleta sera kama hizi, pia waangalie eneo ambalo lina wadau wanaohusika na sekta hiyo. Ukienda kwenye sekta nyingine, inasikitisha kuona hata Viwanda vya Almasi vilipelekwa Iringa huko – *TANCUT* wakati Alimasi iko Shinyanga tu pekee. Kwa hiyo, ni muhimu sana tunapoanzisha vitu kama hivi tuwe tunazingatia pia maeneo ambayo wadau wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, afanye ziara Shinyanga. Watoke, wafanye ziara kule, wakutane na wadau wa mifugo, wasikilize matatizo yanayowasumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu wanaofuga, wananyanyaswa sana hapa Tanzania. Mpaka imefika mahali mtu kutoka eneo moja kwenda lingine ni kama vile anaomba *visa* ya kwenda nchi nyingine. Leo wafugaji wakitaka kwenda Ifakara au Rufiji, humu njiani wananyanyaswa. Kuna kesi nyingi sana, wananyang'anywa mifugo yao, wengine wanaonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isimamie kabisa kuhakikisha kwamba inawalinda wafugaji kwa sababu bila wafugaji, hakuna Wizara.

Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri ufanye ziara Shinyanga, najua hujafika bado, mimi nakukaribisha. Njoo ukutane na wafugaji, wana manung'uniko mengi ambayo wangependa wakueleze na yangekusaidia kufanya kazi yako.

Mimi hapa kama mwakilishi nayataja machache, lakini huko njiani kuna dhuruma, kuna kero kubwa sana ambayo wafugaji wa Tanzania wanapata na hawana msaada mwingine, lakini Wizara ndiyo inaweza kusaidia kwa kuboresha utaratibu mzuri wa masoko na maeneo ya malisho na hasa suala lile la *mapping* ni muhimu sana. Mzingatie kabisa kutengeneza maeneo ya wafugaji ambao watakuwa wanafuga kama mlivyofanya Longido kule. Maeneo mengine pia tunahitaji mtenge maeneo kupitia Halmashauri, mhakikishe kabisa maeneo ya wafugaji yanatambulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine sisi tunahoji kwamba ng'ombe au mifugo ambayo tunafuga kwa ajili ya chakula haipewi ule umuhimu na thamani kubwa ukilinganisha na mahitaji ambayo tunayo kwa ng'ombe yule. Nilikuwa nawatania ndugu zangu kwamba ukiangalia kwa upande wa nyuki kwenye Wizara ya Maliasili ana Mamlaka ya Nyuki na Wakurugenzi na nini, utadhani mtu anaweza akachinja nyuki watu wakala, lakini ng'ombe anapuuzwa. Ukisikia mfugaji ni kama mtu ambaye hana haki. "Nyie wafugaji ondokeni rudini huko kwenu, wafugaji mnafanya nini, wafugaji sijui nini!" Mfugaji ana haki na ngombe ana thamani kubwa na anaweza kutusaidia kutatua tatizo la ajira na ameajiri watu wengi sana hususan kwa jamii ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu ulio mbele yetu. Lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kilolo ambao wameendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vile vile kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kuweza kuleta Muswada huu muhimu leo katika Bunge letu ambao ni mategemeo yangu kwamba hatimaye baada ya kujadiliwa na kufanyiwa marekebisho, utapitishwa kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umekuja kwa wakati muafaka kwa sababu kama, ilivyoelezwa awali, hata pamoja na Waziri Mwenyewe na Kamati ya Kudumu kwamba Sekta hii ya Mifugo imebakia kwa muda mrefu bila kuwa na chombo chake cha utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ikumbukwe kwamba kwenye miaka ya 1980 kwa kweli kulikuwa na chombo cha utafiti kilichokuwa kinaitwa *Tanzania Livestock Research Organization*. Kiliundwa sambamba na kile kilichokuwa kinashughulikia utafiti wa mazao ya kilimo *(Tanzania Agricultural Research Organization)*. Kwa sababu ambazo hazijulikani kamili, vyombo hivi viwili vyote havikuweza kuendelea. Kwa hiyo, utafiti wa mifugo ukawa umeachwa bila kuwa na chombo rasmi cha kisheria, ukilinganisha na vyombo vingine, kwa mfano wanyamapori kama *TAWIRI*, ukilinganisha misitu – *TAFORI*, uvuvi – *TAFIRI*, afya ya binadamu – *NIMRI* na vingine vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashukuru kwamba Muswada huu umekuja na umekuja kwa wakati muafaka na

nina hakika utakuwa na manufaa makubwa kama wengi wetu walivyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ikumbukwe vile vile, maendeleo yoyote katika nchi yoyote ile yameletwa kwa sababu wamewekeza katika utafiti katika nyanja mbalimbali. Sisi hatuwezi kuwa tofauti. Kwa muda mrefu utafiti umekuwa ukitengewa fedha kidogo sana tena sana. umekuwa ukitengewa asilimia 0.038 ya pato ghafi la Taifa. Mpaka mwaka juzi ambapo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliagiza kwamba sasa tuanze safari ya kuelekea kufikia angalau asilimia moja ya pato ghafi la Taifa, itumike kwa ajili ya utafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo hii haingeweza kunufaika kwa hiki kiasi ambacho kinatengwa bila kuwa na chombo halali ambacho kinafanya kazi hiyo. Mimi napenda kuipongeza Serikali kwa kuanza safari ya kutenga fedha ili kuweza kutufikisha kwenye asilimia moja ya pato ghafi la Taifa kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utafiti peke yake hautoshi, lazima uwe utafiti na maendeleo. Kwa hiyo, katika hii safari ambayo imeanza, kwa upande wa sekta ya mifugo, mimi nina hakika kabisa tutaweza kufikia mahali pazuri kwa sababu sasa tunacho chombo rasmi chenye malengo ambayo yataweza kubadilisha tija ya mifugo yetu katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyozungumzwa na wazungumzaji wengine, Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo hususan ng'ombe. Tanzania ina ng'ombe milioni 21.3, ni karibu kila Watanzania wawili wana ng'ombe mmoja.

Sasa, acha mbuzi ambao ni milioni 15, kuku milioni 54, lakini nchi ya kwanza katika Bara la Afrika kwa wingi wa ng'ombe ni Ethiopia yenye ng'ombe milioni 44.3, ikifuatiwa na

Sudan yenye ng'ombe 40.4. Lakini ukilinganisha mchango wa sekta hii ya mifugo kwa nchi yetu bado ni mdogo. Sekta ya mifugo inachangia asilimia 3.8 ya pato ghafi la Taifa, ukilinganisha na nchi nyingine ambazo zina mifugo michache sana hususan Botswana ambao wana ng'ombe milioni 2.7. Sekta hii ni sekta ya tatu kule Botswana kwa kuchangia katika pato la Taifa, ya kwanza ikiwa ni dhahabu, yanafuata mafuta halafu inakuja mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina imani kwamba kwa sasa, kwa sababu tumeanza hii safari ya kufanya utafiti ulio dhahiri, tutaweza kufika mahali pazuri tukawa na ng'ombe ambao watakuwa wanazalisha kwa tija zaidi na nchi ikanufaika zaidi. Sio wananchi tu, lakini hususan wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mdogo wa mifugo katika pato ghafi la Taifa unatokana na mambo mengi na mengine wamekwishazungumza tayari. Lakini kubwa zaidi kuliko yote ni ukosaafu wa mifugo yetu. Ukosaafu, maana yake ni *low genetic potential*. Tuna ngombe wengi, lakini kinachozalishwa ni kidogo. Vile vile matatizo ya malisho katika sehemu ya mwaka. Ikifika kiangazi ng'ombe wanatembea nchi nzima na mifugo mingine kwa ujumla, matatizo ya maji na magonjwa mbalimbali na magonjwa haya yanazidi kuenea zaidi hasa ule wakati ambapo wafugaji wanalazimika kutoka sehemu moja kwenda nyingine ili kupata mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa sasa tunaanzisha chombo hiki rasmi *(TALIRI),* mimi nina hakika hizo changamoto zote zitapatiwa ufumbuzi ili hatimaye tuweze kuwa na mifugo yenye tija kubwa zaidi na kupunguza kiasi cha mazao ya mifugo ambayo tunaingiza hapa nchini.

Kwa mfano, sasa hivi katika bidhaa ya maziwa peke yake, tunaingiza takriban maziwa ya gharama ya dola milioni nne kwa mwaka. Lakini siyo kwamba hapa nchini

hatungeweza kuwa na maziwa ya kutosha kiasi hicho, lakini hatuna miundombinu ya kukusanya haya maziwa na kuyapeleka *Milk Collection Centres* na kupeleka katika masoko na kusindika na hatimaye yaweze kuwafikia wananchi. Ni maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaingiza vitu vingi sana hata mayai. Juzi juzi tu mmesikia mayai mengi yaliyoingia kutoka Kenya ni mabovu. Tunaingiza kuku kutoka Brazil na nchi nyingine. Ndugu zangu nimesema tuna kuku milioni 54 hapa na hawa kuku wako hapa Dodoma, wako Singida na Mikoa mingi, lakini hatuna miundombinu, hatuna *system* ya kuweza kuvuna mifugo yetu sisi wenyewe tukaweza kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa na hii taasisi, mimi ni imani yangu kubwa kwamba itafanya utafiti katika maeneo ya uzalishaji na usindikaji ili tuweze kujitosheleza kwa mazao haya badala ya kuleta mazao mengine kutoka nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tukizalisha vizuri, tuna masoko. Tuna masoko ya kutosha kabisa. Kwa muda mrefu tumekuwa tukiombwa kupeleka mazao ya mifugo na mifugo ambayo ni hai nchi za Urabuni. Hapa *DRC* wanaleta nyama kutoka Brazil, lakini wako mgongoni kwetu tu. Ukienda hapo Mauritius wanahitaji nyama. Kwa hiyo, masoko yapo, lakini tuwe na miundombinu ya humu ndani ili tuweze kuimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia sana juu ya viwanda vya kuchinjia mifugo yetu huko Shinyanga na Mbeya. Mimi nafikiri haya yawe katika mpango wa kuweza kuboresha ili kusudi tuweze kutafuta masoko yaliyo mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi kama lilivyozungumzwa na watu wengine kwamba utafiti huu uwafikie walengwa ili walengwa waweze kunufaika. Lakini katika taarifa zilizotolewa inasisitizwa kufanyia utafiti mahali palipo na mifugo yenyewe *(on farm research)*, hiyo ni njia

mojawapo, lakini yale yanayofanyiwa kwenye maabara, basi ni vizuri yakafikishwa kwa watumiaji wa mwisho ili waweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, tunazungumzia juu ya sera ya utafiti, lakini sera ya utafiti ya Kitaifa haipo mpaka leo. Kwa hiyo, kila sekta wanaandika sera yao. Iko sera ya mifugo, lakini hakuna sera ya jumla ambako ndiko ingekuwa *umbrella* na wengine wote wakaweza kuingia pale. Unapotengeneza sera ya mifugo, unasema sehemu yangu ya ku-*fit in* ni hapa, lakini kila mmoja anakaa anaandika ya kwake bila kuwa na ile inayokuwa kama *road map* ya Taifa katika jambo la utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo sijaliona kamili katika sheria, tayari kwa sasa hivi tuna vituo vinavyofanya kazi za utafiti wa magonjwa na mambo mengine.

Pale Dar es salaam tunacho chombo kinaitwa *ADRI (Animal Disease Research Institute),* huku Mikoani pamoja na Mpwapwa, Iringa, Tabora na sehemu nyingine Mwanza, tunazo *VICs* (*Veterinary Investigation Centres)*. Hizi hazijaonekana kamili katika Muswada huu kwamba zenyewe zitakuwa wapi. Kutakuwa na *TALIRI* peke yake na baadaye kuweko na hivi vingine? Kwa maoni yangu ilikuwa kwamba, hivi vyote vingeingia chini ya hii Taasisi ya Utafiti kwa sababu hata hizo zinafanya tafiti za magonjwa ya mifugo ambayo ni sehemu tu ya utafiti wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo machache, naunga mkono hoja. Tumechelewa sana kuanzisha chombo hiki, na maadam sasa kimefika hapa, ninaamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wataunga mkono ili hatimaye ipite iwe sheria ili Sekta ya Mifugo iweze kubadilika tusiendelee kwa namna tunavyoendelea kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Profesa kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Amina Mwidau, na Mheshimiwa Blandes ajiandae na baadaye Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, kwanza nachukua nafasi hii na mimi kuwapa pole Watanzania wote kwa misiba mizito ambayo imetokea katika nchi yetu hasa ukizingatia msiba wa kijana kabisa ambaye ni msanii, ni Balozi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nichukue nafasi hii adimu kukipongeza chama changu cha wananchi – *CUF* kwa ushindi mkubwa ambao kimepata Tanga katika Kata ya Msambweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi ni ushindi mkubwa kwa sababu wakati wa Msambweni wametuhakikishia kuwa hawakufanya makosa kukichagua kwa mara ya kwanza na wametuchagua tena kutuhakikishia kuwa wanatuamini. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nitakuwa sikujitendea haki nisipoipongeza timu yangu ya Simba kwa ushindi iliyopata kwa goli la ugenini. Ninachoomba ni uzalendo, kwani sasa hivi Simba inawakilisha nchi. Naomba watani zetu wote na timu nyingine tushirikiane kuweza kuhakikisha kuwa tunawakilisha ipasavyo. Mimi mmojawapo nimeonyesha mfano, nimeweza kuwa mzalendo kwa kuvaa rangi za watani zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest*. Mimi ni mvuvi, lakini nachangia Muswada huu wa mifugo kwa sababu kwanza tuko Wizara moja, lakini pia Mheshimiwa Masele hapa alisema sasa hivi wafugaji wanahama kutoka

sehemu za bara mpaka kuelekea huko Rufiji na sehemu nyingine ambapo kunakuwa na matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara kwa Muswada huu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa sababu itasaidia kwa njia moja au nyingine kuweza kuhakikisha kuwa wafugaji hawa wanapatiwa miundombinu ambayo ni muafaka kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kama walivyosema wasemaji waliotangulia ni tajiri sana kwa mifugo, ni ya tatu katika bara la Afrika, lakini pia katika sensa ya mwaka 2007/2008 inaonyesha kuwa Tanzania kwa takwimu za 2011 tuna mifugo ya ng'ombe takribani milioni 21, mbuzi takribani milioni 15, kondoo milioni tisa, kuku kama alivyosema Profesa takribani milioni 54, ukichanganya kuku wa asili na kuku wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha ni hali ya wafugaji. Hali ya wafugaji ni mbaya sana, ila mategemeo yetu baada ya kupitisha Muswada huu utasaidia kwa njia moja au nyingine kuweza kuinua hali za wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, nimeusoma, ni mzuri. Namwomba Waziri pia tukimaliza Muswada huu vile vile kwa sababu Wizara ndiyo hiyo hiyo, basi tupate na utafiti wa Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi iendane na sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, nitachangia katika sehemu tatu, katika sehemu ya pili inayohusu utafiti wa mifugo Tanzania Ibara ya 5 (1)(a) kinahusu kazi za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zote ambazo zimeorodheshwa pale ni muhimu sana, lakini vile vile kuna upungufu kidogo katika kazi zilizoorodheshwa hazikugusia

utafiti juu ya maji kwa ajili ya mifugo. Hii naisema kwa sababu ukiangalia kuwa tarehe 28 Februari, Mbunge wa Kilwa Kusini, Mheshimiwa Suleiman Bungala alijaribu kugusia hapa Bungeni kuhusu suala ambalo lilitokea katika Jimbo lake ambapo wananchi waliweza kupoteza mifugo yao kutokana na maji ambayo wanyama wale walikunywa. Ilisadikiwa kuwa kulikuwa na wasiwasi kuwa maji yale yalikuwa na mabaki ya gesi asilia. Kwa hiyo, kukiwa na utafiti katika masuala ya maji pia itasaidia siyo tu kutambua maeneo mahsusi ambayo mifugo ile itaweza kupata maji mazuri, lakini pia katika magonjwa ambayo yanaenezwa kwa njia ya maji kwa jina la kitalaam ni *water born disease* itasaidia sana. Kwa hiyo, ningeomba na hilo pia liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika ibara ya sita kwenye Vituo vya Taasisi, vituo vile kwa mujibu wa jedwali la kwanza la sheria itakayotungwa vile vitakavyoongezwa na Waziri kwa kushauriana na Bodi, kwa mujibu ilivyo katika maelezo ya vifungu hivyo, inalenga kuanzisha vituo vya kudumu vya utafiti na siyo vinginevyo. Mimi naunga mkono katika hilo.

Vile vile napendekeza katika vituo vile vya kudumu, kwanza kabisa pawe na kituo katika maeneo ya wafugaji wengi. Kuna wafugaji wengi katika Mkoa wa Arusha na Manyara. Lakini vile vile ni vyema uanzishwaji wa vituo ukaboreshwa na kumruhusu Waziri kwa kushauriana na Bodi kuanzishwa vituo vya kudumu kwa jina la kitalaam *Adhoc Centre* na vituo vinavyoweza kuhama kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine *(mobile centres)* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa vituo hivyo ni muhimu kwa sababu vitakuwa mahsusi kwa kukabiliana na utafiti wa magonjwa ya milipuko. Kwa hiyo, kukiwa na vituo ambavyo ni *mobile* na hizo *Adhoc Centres* zitasaidia kwa njia moja au nyingine. Kuna magonjwa ya mlipuko ambayo ni *East Coast fever* na magonjwa mengine yanaweza kuthibitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napenda kuchangia katika ibara ya 13(1) ya Muswada ambayo Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi watateuliwa na Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mimi napendekeza kuwa ndiyo kuna utamaduni ambao upo wa kuteua kwa mujibu wa sheria zilizopo, lakini utamaduni huu ningeomba katika hili katika taasisi hii uweze kutoa nafasi ili sheria iweke wazi kabisa nafasi hizi ziweze kutangazwa na wale ambao wana sifa kwa mujibu wa sheria waweze kuomba washindanishwe badala ya kuteua mtu, kwa sababu watu wanabweteka wanapoteuliwa, lakini tukishindanisha tutapata mtu ambaye ni *competitive* na ambaye ame-*qualify* katika hizo nafasi ya Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza tena Wizara kwa Muswada huu na niombe tuupitishe, bado hatujachelewa sana. Lakini vile vile namwomba Waziri ajaribu kuangalia na kwenye uvuvi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Amina. Sasa namwita Mheshimiwa Blandes na Mheshimiwa Dokta Kamani ajiandae, na baadaye Mheshimiwa Zarina Madabida atafuata.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi, binafsi nianze kumpongeza Waziri, Naibu Waziri wake na Watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wameleta hapa. Napenda kusema waziwazi kwamba Taifa lina imani kubwa sana na Waziri wa Mifugo na sekta hii aliyopewa ni sekta nyeti sana na kwa umri wake. Tunataka atengeneze historia kubwa ya mapinduzi ya mifugo katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanzia kwanza kwenye *definition section* ya Muswada huu. Nilikuwa naangalia neno *'livestock',* wameelezea kwa upana maana yake ni nini,

wameorodhesha wanyama ambao wamewekwa katika *definition* hii, lakini nimeona *definition* hii siyo pana. Kuna wanyama wengine wamekuwa *excluded,* kwa mfano, sioni hapa ngamia, farasi, sungura, bata na kadhalika. Najua kwamba ameweka *general* lakini kama ametaja wanyama, basi ni vizuri na hawa wakaingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye upande wa Wajumbe wa Bodi, sina ugomvi mkubwa sana, lakini hapa nilikuwa namwona Mjumbe mmoja wa Bodi anayetoka kwenye Wizara yenye dhamana ya mazao, bila shaka hapa amekusudia kuweka mtalaam ambaye atatoa ushauri katika mazao kama ni kunde na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeshindwa kumwona mtu muhimu sana katika Bodi hii na ninadhani mtu huyu asipokuwepo katika Bodi hii, naomba niseme ukweli kwamba Bodi hii itakuwa imepwaya sana. Mtu huyu ni muhimu ambaye anatokana na vituo vyetu vya uhamilishaji *artificial insemination,* kwa sababu huyu mtu ndiyo muhimu katika kuzalisha mifugo. Nilidhani kwamba mtalaam au Mkurugenzi wa Kituo cha Uhamilishaji cha Arusha ingekuwa ni vizuri awepo katika Wajumbe wa Bodi, na sababu iko wazi kwa sababu yeye ndiye anatoa utalaam katika kuzalisha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama wenzangu walivyosema, Bodi hii imesheheni watalaam, lakini wale walaji wa mwisho au watumiaji wa utafiti huu mimi siwaoni. Wapo wafugaji wenye uwezo, wenye ujuzi, ni vizuri wangekuwepo na wenyewe tukawaona hapa. Lakini pia tunao watalaam wanaotengeneza madawa ya mifugo, tunao watu kama akina Bagita kule Arusha, tunao watu wanaotengeneza vyakula vya mifugo, basi na wenyewe tungeangalia uwezekano wa kupata Mjumbe mmoja wa Bodi katika Bodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo limekuwa likiikumba Sekta ya Mifugo, ni pamoja na rasilimali watu.

Nimefurahi kwamba katika Muswada huu, suala la rasilimali watu limepewa kipaumbele, lakini napenda kusema kwamba mpaka sasa hivi tunao Maafisa Mifugo jina tu, kwa sababu hawa Maafisa Mifugo hawako kule kwa wafugaji, utakuta wapo mijini na wale ambao wapo vijijini hawana nyenzo za kuwafikia wafugaji. Utakuta Afisa Mifugo hana pikipiki, hana mafuta, hana hata *allowance* ya kuzunguka. Kwa hiyo, ningependa sheria hii katika suala la rasilimali watu, basi ijikite vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ibara ya 13 ya Muswada huu inahusiana na *appointment* ya *Director,* Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hii, suala langu mimi hapa ni kwamba sheria inapendekeza Mkurugenzi Mtendaji ateuliwe na Waziri mwenye dhamana, lakini pia Naibu wake ateuliwe na Waziri mwenye dhamana. Kwanini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumpe Waziri kazi ya kuteua Mkurugenzi Mtendaji? Nadhani hii siyo kazi yake. Tuweke ushindani, watu washindane. Watalaam tunao wengi katika nchi hii, tuwashindanishe kwa ujuzi wao wafanye *interview* ndiyo tuwapate Mkurugenzi Mtendaji na Naibu wake, na hii itakuondolea kelele nyingi sana kwamba umeweka ndugu yako, umemweka rafiki yako, umweka mtu hana uwezo, na pia kumwondolea kiburi Mkurugenzi Mtendaji, kwa sababu akijua nimeteuliwa na Waziri mwingine anashindwa hata kuwajibika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza nitaleta *schedule of amendments* kwamba kipengele hiki kibadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna Naibu Mkurugenzi Mtendaji naye pia atateuliwa na Waziri. Naibu Mkurugenzi Mtendaji ni wa nini? Tunaye Mkurugenzi Mtendaji mwenyewe, sasa huyu Naibu Mkurugenzi ukiangalia kazi zake inasema atapangiwa kazi na Mkurugenzi Mtendaji. Ni kazi zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunasema watakuwepo watalaam wengine. Ningependekeza huyu Naibu Mkurugenzi Mtendaji aondolewe. Hii ni gharama tu, tupunguze gharama za Serikali, kwa sababu watakuwepo Wakuu wengine wa Idara, labda Mkuu wa Mipango, Mkuu wa Fedha, Utawala na kadhalika. Kwa hiyo, huyu sioni umuhimu wake hata kidogo kuwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika Muswada. Muswada umependekeza mambo mengi sana. Kuna masuala ya malisho, masuala ya vyakula, mimi nakubaliana nao kabisa kwa asilimia mia moja kwamba Muswada ni mzuri mno. Wasiwasi wangu ni utekelezaji wake hasa hapa ndiyo utakapopata tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza rafiki yangu hapa Mheshimiwa Masele, Mbunge wa Shinyanga amezungumza kwa kutamba sana kwamba Mkoa wa Shinyanga unaongoza katika ufugaji hapa nchini. Nadhani inawezekana akawa na takwimu za miaka ya nyuma sana, kwa sababu sensa ya mifugo haijafanyika miaka mingi. Lakini nakuhakikishia kabisa Mkoa wa Shinyanga unaweza usilingane na Mkoa wa Kagera kwa wingi wa mifugo. Mkoa wa Kagera una mifugo mingi na pengine inaweza ikawa ni mara mbili ya Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nasema hivyo? Mkoa wa Kagera umepakana na nchi ya Rwanda na Uganda, ninaposema Mkoa wa Kagera una mifugo mingi. Hii ni mifugo ya kutoka nchi mbili, Rwanda pamoja na Uganda ndiyo mifugo ambayo sisi tunajivunia, siyo mifugo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mifugo anatamba na kutembea kifua mbele kwa kujidai na mifugo ya nchi jirani. Sasa wewe unachunga mifugo ya wenzako, na mifugo hii nimekuwa nikizungumza kwa muda mrefu kwamba imekuja hapa kuchukua malisho ya Watanzania na tumeshazungumza

sana kwa muda mrefu. Kwa sababu tunaposema tunatunga sheria na kuweka malisho mazuri kwa faida ya akina nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Wilaya ya Karagwe Mkoa wa Kagera. Ukienda Biharamulo, Karagwe, Muleba pote pamejaa mifugo kutoka nchi jirani. Sasa tukitunga sheria hii ya kutowafaidisha Watanzania mimi nakuwa na wasiwasi, ndiyo maana nikasema utekelezaji wake unanipa mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nchi hii tuna eneo kubwa sana, tumejaliwa na Mwenyezi Mungu kupata eneo kubwa. Maeneo yapo wazi, kwanini tusitenge *block* tukawagawia wananchi kila mtu achunge mifugo yake kwenye eno lake, na kila mtu akachunga kwa ukubwa wa eneo lake badala ya kusema fulani apunguze? Ukiwa na ng'ombe kumi utachunga katika eneo lako linalohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niseme ni soko la mifugo yetu. Sasa hivi tuna minada ile ambayo ng'ombe wanauzwa kwa kumwangalia tu kwa macho. Hakuna vipimo maalum kusema kwamba labda kilo fulani ya ngo'mbe *live* anauzwa kwa kiasi fulani. Hilo ningetaka liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninapendekeza, kwanza, naishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo ilifidia ndugu zetu wa Arusha ambao wamepata majanga ya kufiwa na mifugo yao. Ningependekeza uwepo mfuko maalumu wa Taifa wa kupambana na majanga kama haya ili ukame unapotokea Kagera, Sumbawanga na sehemu nyingine, basi mfuko huu utumike katika kuwafidia Watanzania wote bila kubagua maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na madawa ya mifugo hasa chanjo. Kituo chetu cha Temeke kimelemewa. Tungependa chanjo zitengenezwe kwa wingi na hasa chanjo za mifugo kama *FMD*, Sotoka ya miguu na

midomo ili iweze kusaidia kwa nchi nzima na ikiwezekana chanjo hizi zitolewe kwa ruzuku kwa sababu zimekuwa ni gharama kubwa sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Mifugo wawe wanatembea. Nadhani Wizara ya Mifugo labda pengine ufinyu wa bajeti, lakini mimi kila Desemba huwa natembelea nchi jirani zinazofuga. Nimekwenda Uganda, nimekwenda Mbarara, nimekwenda Masaka, nimekwenda Kenya Mji wa Naivasha, nimeona kabisa kule ufugaji jinsi ambavyo umezingatiwa, wana soko, wana viwanda vya maziwa, wana ng'ombe wa kisasa ambao wanakidhi haja, ng'ombe mmoja ukimkuta Kenya uzito wake ni sawa sawa labda na ng'ombe kumi wanaopatikana hapa Dodoma. Sasa ufugaji huu hauwezi kuwa na tija hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa sana, ni lazima tubadilike. Kwenye Muswada nimeona kwamba unapendekeza uzalishaji wa kiteknolojia, nakubaliana nalo sana. Lakini tuna kituo chetu cha Uhamilishaji pale Arusha kimefeli. Kinazalisha mbegu ambazo haziwezi kukua, ni mbegu ambazo ni nusu mfu. Sasa kituo kile pengine kiboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi dunia imetoka katika *artificial insemination,* imeshaanza kwenda kwenye kitu kinaitwa *embryo transfer*, kwa maana kwamba yule ng'ombe jike anatolewa mayai mengi aliyonayo, yanapelekwa kwenye mashine, yanazalishwa, mtu anachagua, niwe na ndama majike wangapi au madume wangapi? Sasa sisi hapa bado tunasuasua, mambo hayaendi na wakati mifugo hii inatakiwa itukomboe sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nilitaka niseme kwamba nina-*declare interest* kwamba mimi ni mfugaji mkubwa sana hapa nchini na ninajitahidi lakini nakwamishwa pamoja na haya yote ambayo nimeyasema na humu ndani wapo Wabunge wengine na wananchi wetu tungetaka

wafuge kwa ubora, lakini napenda kurudia tu kwamba wenzetu wa mifugo wajitahidi kulisaidia Taifa hili. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, naomba kumwita sasa Mheshimiwa Dokta Kamani na muda ukiruhusu Mheshimiwa Madabida atafuata.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia na mimi nafasi kuchangia katika Muswada huu muhimu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muda huu. Mimi naweza kusema kwamba tumechelewa kiasi kwa sababu Sekta ya Mifugo haikuwa sekta ya kuonekana, ni sekta nyembamba. Wakati wa bajeti, tunasema kasungura kadogo, inapewa bajeti ndogo kwa sababu inaonekana kama ina mchango mdogo sana katika uchumi wa Taifa letu. Sekta hii ni *giant* aliyelala tu na kama angetumika vizuri angeweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana kubadilisha hali ya umaskini wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungumzaji wengi wamezungumzia sana ufanisi wa Sekta ya Mifugo katika nchi nyingine kama Botswana, nchi ndogo na zenye mifugo kidogo zaidi kuliko Tanzania. Lakini hata hapa jirani zetu Kenya wana mifugo, ng'ombe ni kama milioni 12.5. Lakini Kenya ni *giant* katika sekta ndogo ya nyama, maziwa. Sasa ndiyo waingizaji wakubwa wa maziwa katika nchi yetu. Ngozi nyingine ambazo wao wanajivunia kama ni za kwao zinatoka Tanzania. Ni kwa sababu sisi hatujaweza kutumia fursa tulizonazo vizuri tukaweza kuyatumia mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ufanisi huo wote ni kutokana na kwamba wanatumia vizuri utafiti, wana taasisi imara sana za utafiti katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu, tunapozungumza mifugo kwa kweli hata baadhi ya maeneo inaonekana kama ni sekta ambayo haitakiwi hivi! Mwanzoni ng'ombe walipoanza kuingia kule Mkoa wa Rukwa kuna baadhi hata ya wawakilishi wa wananchi walisema hawa waondoke hatuwataki. Lakini hata walivyoanza kuhamishwa, yale maeneo katika kuhifadhi, bonde la Mto Ruaha walionekana kama ni watu wasiotakiwa ndani ya nchi. Namna walivyohamishwa kule Kilosa, zinawekwa kodi za ajabu ajabu kwa wafugaji. Viongozi wanatafuta utajiri kwa kutumia wafugaji hawa. Kwa kweli inaleta hali ya kusikitisha sana kwa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifikiria kwamba hawa wafugaji wasingekuwepo ndani ya nchi yetu Serikali ingetumia fedha kiasi gani kuagiza nyama kulisha Watanzania? Kwa hiyo, ni vizuri sana watu tukaiangalia sana sekta hii kwa mtazamo chanya. Lakini bahati mbaya sana kwa hali ya sasa ufugaji umekabiliwa na changamoto nyingi. Kwanza wafugaji wenyewe wanaonekana ni watu maskini na duni. Kimsingi, wanakuwa watumwa wa mifugo yao. Lakini ufugaji wetu vile vile unaambatana sana na uharibifu wa mazingira na unasababisha mtafaruku mkubwa sana wa kijamii. Migogoro mikubwa inayojitokeza kila wakati na hata kupelekea mauaji kati ya wakulima na wafugaji ni kwa sababu ya Sekta yetu hii ya Mifugo ambavyo hatuipangilii vizuri. Kuna uhamaji holela wa mifugo kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine hadi watu wanaonekana kama ni wakimbizi ndani ya nchi yao.

Kama hili lililosemwa na Mheshimiwa Blandes, mimi nilikuwa sehemu ya Kamati Ndogo iliyokwenda kule Kagera. Kuna wimbi la mifugo kutoka nchi jirani kuingia ndani ya nchi yetu na kutumia ardhi yetu na hatimaye wakati wa kuwavuna wale mifugo wanakwenda kuvunwa tena nchi nyingine bila nchi yetu kunufaika kwa namna yoyote na kodi wala mazao mazao ya mifugo hiyo. Kwa kweli huo ni unyonyaji wa namna

fulani ambao kama nchi, kama Taifa, lazima tutafute namna ya kukomesha mara moja. *(Makofi)*

Pia tuna matatizo makubwa ya maeneo ya kuchungia ndani ya nchi yetu kwa sababu hatuipangilii ardhi vizuri. Hatuna mipango ya *land use plans*. Kule Jimboni kwangu kwenye Kata za Lamadi, Lutubika kule Mwakiloba na Kijirishi wakati wa kiangazi ni matatizo sana. Inabidi wafugaji walazimike kuingiza mifugo ndani ya Hifadhi za Taifa na kusababisha migogoro mikubwa kwa sababu malisho yanakuwa yamekwisha. Lakini yote hayo ni kwa sababu ya kutopanga matumizi bora ya ardhi. Wakati wa kilimo nafikiri sasa linaanza kuwa kama ni tatizo la kitaifa. Utaona ng'ombe wengi wanachungia kando kando ya barabara kwa sababu maeneo yote mengine yanakuwa yamelipwa. Sasa matokeo yake kwamba ng'ombe wetu watakuwa duni sana na hivyo hawezi wakapata soko zuri.

Vile vile kuna tatizo kubwa la maji. Tuna matatizo ya masoko kule kwangu Busega, Wakenya wanakuja na malori wanapakia mbuzi na kondoo wanasafirisha kupeleka kwao, wanakwenda kuchinja kule. Kwa hiyo, mazao yote yanaonekana kama ni ya Kenya. Mfugaji wetu aliyemfuga mbuzi, kondoo kwa miaka minne haachwi na chochote cha maana, kumbe wale mifugo wangeweza kuchinjwa huku na kupakiwa kama nyama na mazao mengine yale ya ngozi, damu ingeweza kuwa ya manufaa na vile vile kujenga ajira kwa Watanzania.

Vile vile mifugo inakabiliwa na tatizo kubwa la utafiti na ndiyo hasa mada ya Muswada huu. Utafiti wa mifugo ulikuwa duni kama alivyosema Profesa. Zamani kulikuwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo *(TALIRI),* lakini kwa sababu ya sera ambazo zinaamuliwa kutoka nje ya nchi, hii *TALIRI* ilikufa na utafiti ukaanza kuwa kitengo tu ndani ya Wizara na unajua kabisa kwamba masuala ya menejimenti na utafiti haviendani

pamoja. Kwa hiyo, urasimu uliua utafiti wa mifugo katika nchi yetu. Kwa hiyo, kuletwa kwa *TALIRI* ni wakati muafaka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nishauri kabisa japo imezungumzwa katika Muswada huu kwamba ule mwelekeo finyu wa utafiti lazima ubadilike. Kuangalia magonjwa peke yake na mbegu siyo jibu la mahitaji ya mifugo katika nchi yetu. Kwa mfano, zamani tulikuwa tukizungumza masuala ya mbegu bora Tanzania, kuna wakati ilikuwa na mbegu yake ya ng'ombe iliyokuwa inaitwa *Mpwapwa Breed.* Alikuwa ni ng'ombe mkubwa, anakua kwa haraka na ana nyama nyingi. Mbegu hii imekwisha, haikuweza kuendelezwa kwa sababu ya kutokuwa na vitengo imara vya uzalishaji na utafiti ambao ni endelevu.

Sasa tunazungumza uhamilishaji *(artificial insemination),* lakini tunavyozungumza uhamilishaji katika ng'ombe wa kienyeji, ina maana ni kazi ngumu. Tunahitaji vituo vile vya madume bora ambavyo zamani vilikuwepo kama kule kwangu Igalukilo, na Waziri alisema kwamba kinafanyiwa ukarabati; sasa wafugaji wa kienyeji hawana mahali pa kupandikiza ili wapate mbegu bora. Kwa hiyo, Muswada huu ni muhimu sana, umefika, lakini ni vizuri vile vile tukajielekeza katika suala la uwakilishi katika ibara ya 8.2. Nilifikiri kwamba uwakilishi wa Wabunge ni muhimu sana katika Bodi kwa sababu wanasiasa ndio wagani muhimu. Kama unataka kuingiza sera yoyote katika jamii, bila kuwashirikisha wanasiasa utapata taabu sana. Kwa hiyo, nilifikiri kwamba kuwepo kwa Wabunge katika Bodi hii ni muhimu sana ili kuleta kiungo kati ya watalaam na wananchi wafugaji.

Vile vile ni muhimu sana tukaangalia kwamba sekta hii ukubwa wake ingeweza kabisa kushindana na madini na utalii kwa sababu ya ajira inayojenga. Kwa sababu siyo wale wafugaji, lakini vile viwanda vyote vinavyoongeza ubora wa mazao ni kwamba vyote hivyo vinatengeneza ajira na hivyo kupanua uwigo wa kuchangia katika uchumi. Lakini vile vile

bahati nzuri nchi yetu Watanzania wamependa sana matumizi ya kuku wa kienyeji badala ya kuku wa kisasa. Kuku wa kienyeji hawaangaliwi kama ni zao muhimu sana.

Hivyo ningependekeza kabisa katika taasisi hii mpya inapoundwa wajielekeze sana katika kuboresha ufugaji wa kuku wa kienyeji kwa masoko yake. Kuna wanyama kama sungura, hata mbuni, kwa soko la kimataifa nchi kama Botswana zimeweza kunufaika na Tanzania na mazingira sahihi ya kuweza kunufaika na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili waweze kufanikiwa zaidi, lazima hali ya haya wanayoyafanyia utafiti kuwe na namna ya kuwafikia walengwa. Taasisi kama hizi *Livestock Multiplication Unit* wanapofanya utafiti wa mbegu bora, *National Ranching Company* lazima zitumike sasa kuweza kusambaza matokeo ya utafiti huo. Ni vizuri vile vile Bodi za mazao zikaimarishwa. Hizi nchi tunapozungumza zimefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Kenya, Botswana na nchi nyingine, Bodi za mazao yanayohusiana na mifugo ziko imara sana, kwa mfano Bodi za Maziwa, Bodi za Nyama, Bodi za Ngozi na kadhalika. Ndio maana Kenya wako imara sana hata kulinda soko lao la ndani kwa sababu Bodi yao ya Maziwa inafanya kazi vizuri. Sisi Bodi yetu ya Maziwa hapa Tanzania wajumbe wa Bodi ni wengi kuliko watendaji. Sasa sijui hiyo Bodi inafanyaje kazi kama ina watendaji wachache kuliko Wajumbe wa Bodi wenyewe ambao wanapanga sera tu. Kwa hiyo, hivi vitu vyote namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie suala hili liwe na manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MWENYEKITI:** Tuna dakika kama 12, naomba nimwite Mheshimiwa Zarina Madabida awe msemaji wa mwisho.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru. Nitajitahidi kutumia hizo dakika kumi nimalize ya kwangu. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuja na Muswada wa Kuanzisha Taasisi hii ambayo mimi naiona ni muhimu sana ambayo kama kweli ikifanya kazi vizuri, basi itaboresha mazao ya mifugo, itaongeza pato la watu, mmoja mmoja na Taifa. Lakini vile vile itaondoa huu uharibifu wa mazingira kwa kuwa na mifugo mingi isiyokuwa na tija na kuhamahama. Kwa sababu ni ukweli kabisa kwamba wanapohama kutoka sehemu moja kwenda nyingine pale wanapoondoka wanakuwa tayari wameshavuruga na ndiyo maana kumekuwa na kelele kwamba wafugaji wasije kwetu kwa wale ambao kwa kawaida siyo wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye huu Muswada. Kwanza, nimesoma katika sehemu ya pili, ibara ya (5) ambayo inaonyesha kutakuwa na utafiti. Pale katika kazi za Taasisi imeonyesha na ninatumaini kama nimeisoma sawa sawa yale yaliyoandikwa pale ni kwa ajili ya utafiti tu wa mauzo, na kwamba siyo mauzo, sitarajii kwamba taasisi hii itakuwa inafanya biashara. Kwa sababu ikiwa kama Taasisi, hii itaingia kwenye biashara. Inamaanisha kwamba itakuwa inakinzana na Taasisi nyingine ya Serikali ya *NARCO* ambayo inafanya kazi hiyo hiyo.

Kwa hiyo, nafikiri biashara hiyo itakuwa ni aidha katika kazi zile za utafiti au kama ilivyoelezwa kwamba ni research *on marketing and so on, and so forth.* Kwa hiyo, hiyo nafikiri itakuwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, nimeangalia, hakuna mahali popote ambapo inaonyesha jinsi gani utafiti huu utafikishwa moja kwa moja kwa mlaji, mlaji huyu nikimaanisha kwamba hawa wafugaji wadogo wadogo. Mara nyingi sana kwa sababu huku nyuma tumekuwa na tafiti mbalimbali katika kilimo pamoja na ufugaji, lakini unakuta

matokeo ya tafiti hizi zinabakia katika makabrasha au katika makabati.

Sasa nimeangalia humu ndani sioni mahali gani ambapo wameandika kwamba tafiti hizi zile *results* zake zitamfikiaje huyu mkulima ambaye nafikiri ndiye mlengwa. Kwa sababu, ni katika matumizi tu ya tafiti hizi ndiyo Serikali itapata faida, nikimaanisha kwamba, kwa kuongeza pato la mtu binafsi na ambayo *eventually* itakwenda kwa Serikali. Kwa hiyo, nafikiri kwamba, basi ingeonyesha katika Muswada huu mahali gani ambapo huyu mkulima mdogo itamsaidia. Naweza kuambiwa kwamba tutaonyeshwa kwenye kanuni, lakini mimi siamini katika kanuni kwa sababu mara nyingi sana kanuni zinategemea mtendaji aliyeko mezani. Mtendaji akiwa ana utashi wa kutaka kufuata kanuni zinafuatwa. Lakini ikiwekwa moja kwa moja kwenye sheria itamlinda yule mkulima mdogo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hiyo ionyeshwe moja kwa moja. Lakini jinsi gani nyingine ambayo ingeweza kufanywa ili kusudi iweze kumpata huyu mlaji moja kwa moja. Ukiangalia katika muundo wa Bodi, unakuta wote ni Wawakilishi wa Wizara, Wawakilishi wa Taasisi, hakuna mtu yeyote ambaye anawakilisha walaji kwa maana kwamba hawa ambao ndio walengwa wa ule utafiti, kwa sababu huo utafiti mwisho wa yote ni lazima utumike. Sasa kwa nini basi kwenye Bodi kusiwe aidha na *let say* Chama cha Wafugaji au kama kuna wafugaji ambao hawatatumia tafiti zile au matokeo ya tafiti kwa maslahi yao binafsi na badala yake yatatumika kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

Kwa hiyo, naomba muundo wa Bodi basi ungeonyesha hivyo ili kusudi tuweze kupata na nafikiri hii taasisi itapata faida kwa sababu Bodi inakutana mara kwa mara.

Kwa hiyo, na taasisi inaweza ikapata *feedback* kutoka kwa huyu mwakilishi; kama ni matokeo ya utafiti, umefanya kazi na *results* zikoje? Zimepokelewaje? Kuna kitu chochote cha kubadilisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika Sehemu ya Nne, ibara ya 19, inaeleza masharti ya mtu binafsi ambaye anataka kufanya utafiti, na ibara ya 20 inatoa adhabu kwa mtafiti binafsi ambaye hakuwakilisha matokeo yake kwenye taasisi. Lakini nilikuwa najiuliza, sawa huyu mtafiti binafsi ameshafanya utafiti na amepata *results,* anaziwasilisha kule. Zinalindwa vipi na yeye anapata nini? Kwa sababu naona hizi hela siyo kwamba amepewa na Serikali, ametumia *finance* yake kufanya utafiti. Analindwa vipi ili kusudi kazi yake isiibiwe? Hii iko katika sehemu nyingine kwamba mtu anafanya kazi yake, anapata matokeo mazuri lakini anapopelekwa kule, mtu mwingine anaweza kwenda kuyaiba yale matokeo kule na kuyatumia bila hata yule mwenye kazi yake kupata chochote.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri pale tungeongeza kwamba huyu mwenye utafiti wake analindwa vipi. Lakini hata Taasisi pia inaweza kuwasaidia kuwalinda kwa sababu mtu mwingine anaweza kuchukua matokeo ya utafiti akaenda kuyafanyia kazi nje ya taasisi. Inalindwa vipi Taasisi na wale wote ambao wanafanya utafiti ambao wanajigharamia wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda niliopewa, naona niishie hapo. Lakini narudia tena kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu na kwa kweli naona kabisa kama itatumika, vizuri itaweza kuleta tija kwa wananchi mmoja mmoja na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno haya, nasema naunga mkono hoja ila tu naomba kazi ifanyike. Kwa hayo machache niliyoyatoa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mbunge.

Kwa vile muda pia umetuishia, nina matangazo mawili. Mosi, napenda niwataje ambao watachangia baada ya kurudi saa 11.00 jioni, tutaanza na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, atafutiwa na Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na wengine watatajwa.

Pia naomba niwakumbushe kuhusu Semina saa 7.00 baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Kutokana na umuhimu wa semina hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tushiriki wote.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni. Ahsanteni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji waliobaki kwa idadi ninayoiona inawezekana kabisa wote walioomba wakapata nafasi ya kuchangia. Sasa niwataje tu wale watakaoanza, yuko Mheshimiwa John Momose Cheyo atafuatia na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi na baadaye Silvester Muhoja Kasulumbai lakini na wengine nitawataja kadri tunavyoendelea. Sasa nitamuita Mheshimiwa Daktari Binilith Mahenge.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niwe ni mmoja ya wachangiaji katika Muswada huu muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi

yetu. Lakini kabla sijaanza kuchangia kuna jambo zuri limetokea kwa wananchi wangu wa Makete ambalo linastahili kabisa kwa niaba yao kulisema hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuishukuru Serikali yetu na hususan Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutupatia Mkoa mpya wa Njombe. Kwa niaba ya wananchi wa Makete wameniomba nitoe shukurani kubwa sana, lilikuwa ni ombi la muda mrefu, wamelisubiri kwa hamu na hatimaye Mheshimiwa Rais amehitimisha kwa kuwasikiliza wananchi na kuwapa Mkoa mpya wa Njombe wananchi wa Makete, Ludewa, Njombe na Njombe Magharibi Ngwageng'ombe.

Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alianza kushughulikia haya maombi tangu alipokuwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI hadi na inahitimishwa sasa hivi akiwa Waziri Mkuu. Nimshukuru yeye pamoja na viongozi wote wa Serikali kwa kusikia kilio cha wananchi wa Mkoa huu wa Njombe kuwapa Mkoa wao mpya, tunashukuru sana, tena sana. Nina hakika wananchi wa Mkoa huu mpya watatumia fursa hii kutoa shukurani kwa viongozi wetu kwa kuchapa kazi ili kuleta mabadiliko katika maendeleo ya Mkoa wetu wa Njombe kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, kwa kuleta hoja hii ya kuundwa kwa taasisi muhimu ya utafiti wa mifugo. Nampongeza sana, imeletwa kwa muda muafaka na ni muhimu sana sisi tukaijadili na tukaipitisha ili shughuli zianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hii ni changamoto na nzuri nikichukulia mfano wa shamba la ng'ombe la Kitulo, shamba ambalo lilianzishwa miaka ya 1965 kwa kuwa na kondoo wa manyoya na baadaye likawa la ng'ombe wa nyama na miaka ya 1975 likabadilishwa na kuwa la ng'ombe

wa maziwa wa aina ya *Friesian*. Shamba hili lina uwezo kwa leo hii wa kuchukua au kuwa na ng'ombe 2000, lakini hivi niongeavyo, shamba hili lina ng'ombe 800. Kwa hiyo, ni wazi kwamba ziko changamoto ambazo tunadhani taasisi hii isaidiane na Serikali kuona kwamba zinatatuliwa na kuona kwamba idadi ya ng'ombe pale inaongezeka kutoka 800 kwenda mpaka hiyo 2000 ya uwezo wa shamba, lakini ni changamoto zipi ambazo ziko pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ambayo imesababisha kupungua kwa idadi ya ng'ombe kulingana na uwezo wa shamba lenyewe ni tatizo la mbegu ya ng'ombe wenyewe aina hii ya *Friesian*. Mbegu hii haipatikani Tanzania, mbegu hii inapatikana *South Africa,* Ulaya na kwa wenzetu, Idara hii ya *DAFCO* imepeleka maombi kwenye bajeti ili iweze kuongeza kupewa fedha na hatimaye kununua hizi mbegu, lakini kulingana na uwezo imekuwa ikishindikana au kwa sababu ya kutopewa kipaumbele maalum kwamba lazima ipewe fedha za kutosha kuweza kununua mbegu hizi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ni changamoto ya kwanza ambayo tunadhani wenzetu wa taasisi hii, watashirikiana na Serikali kuona kwamba inatatuliwa, mbegu zinapatikana ili kuona namna ya kuongeza hawa ng'ombe wa maziwa waliopo kwenye shamba la ng'ombe la Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto ya pili ni malisho. Shamba hili mwaka 1975 wenzetu walipanda majani, haya majani mbegu yake nayo inatoka Ulaya na mwaka 1975 mpaka leo hii ni muda mrefu kwa hiyo ni wazi kwamba yale majani yamechakaa na hivyo kuhitaji majani mengine kupandwa, kwa maana nyingine ipatikane mbegu nyingine kutoka Ulaya. Kwa hiyo, tunarudi pale pale kwamba kutokana na ufinyu wa fedha au kutokana na katika vipaumbele vyetu, hatukuweka mkazo zaidi kwenye hili, basi inaonekana kwamba hatuna sehemu ya kulisha hawa ng'ombe. Kwa hiyo, hata

kama tungekuwa nao 2000 tukapata mbegu za hawa ng'ombe, bado tuna changamoto ya malisho ambayo hayatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji sasa hivi pale Kitulo maombi ambayo yanapatikana kwa mwaka ni maombi ya mitamba 1000, lakini wana uwezo wa kutoa mitamba 80 tu kwa mwaka. Unaweza kuona ni kiasi gani jinsi shamba hili limeshindwa kutekeleza mahitaji ya wananchi. Lakini kwenye changamoto hii ambayo nadhani wenzetu wa taasisi hii watakapokuwa wameanza baada ya kupewa kibali na Bunge hili Tukufu ni kuhusu utafiti kwenye malisho, kwenye majani haya. Ni kweli tunategemea majani mbegu toka nje, lakini namna gani sisi tufanye utafiti kwa kutumia majani yetu wenyewe ambayo yangeweza kufaa kuongeza uzalishaji au kutoa chakula kizuri na kuboresha mifugo yetu na hasa kwa shamba hili la ng'ombe wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo hapa ni kwamba, wataalam wengi wa Kitanzania wamebobea kwenye utafiti wa majani ya kwenye *tropical, tropical* kwa maana kwamba maeneo ya wafugaji sehemu kubwa ni kuanzia nyuzi za *degree* za joto 20 na kwenda juu. Lakini kwenye *temperature* ambayo inakuwa chini ya 20 kama iliyopo pale Kitulo hatuna watafiti kama hawa kwa sababu Kitulo pale pana baridi na kuna wakati tunapata mpaka barafu kwa hiyo maana yake tunakwenda kwenye *minus*. Kwa hiyo, tunahitaji sasa taasisi hii ifanye utafiti itakapokuwa imepitishwa wa kuona namna gani watashirikiana na wenzetu wa nchi za nje kwenye maeneo ambayo *temperature* iko chini kupata majani ambayo yanaweza yakasaidia kwa ajili ya ng'ombe wale walioko Nyanda za Juu Kusini hasa kwenye sehemu hizi za baridi. Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa ambayo naamini kwamba wenzetu wataifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba, tuwaombe sasa Wizara hii ya Mifugo kwamba ni vizuri katika

vipaumbele vyetu badala ya kugawa hela kidogo kidogo kwenye hili la kuendeleza shamba la ng'ombe la Kitulo, ni vizuri tukawapa fedha za kutosha; kwa sababu kama leo utawapa fedha kwa ajili ya kununua mbegu peke yake, utakuwa hujatatua tatizo kwa sababu utanunua mbegu, lakini itahitajika uwe na eneo la malisho. Kwa hiyo, lazima kuwe na fedha za malisho, lakini ukiwa na fedha za malisho, ni lazima uwe na fedha za kununua matrekta kwa ajili ya kulima na lazima uwe na fedha kwa ajili ya watu wataofanya kazi hiyo ya kilimo. Kwa hiyo, ni *programme* ambayo inatakiwa ijitosheleze yote. Kwa hiyo, naamini pengine kwa kuliona hili sasa kusiwe na tabia ya kutoa kidogo kidogo kama ilivyo kwenye Halmashauri ambako ametoa asilimia 30, 25 na matokeo imekuwa vigumu kutekeleza majukumu yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Wizara hii kwamba watengeneze programme inayojitosheleza ya kuhakikisha kwamba majukumu yote yanatekelezwa na kuona kwamba moja linaweza likashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nataka nichangie ni kuhusu umuhimu wa taasisi hii kufanya tafiti zake ambazo zitalenga kuondoa umasikini Vijijini, kwa lugha ya kigeni tungesema *livestock research for rural development.* Kwa hiyo, ziko tafiti nyingi zimefanywa, lakini haziendi kule kwa wananchi ambao ndiyo wafugaji. Naamini kwamba kama taasisi hii ikiwa na kitengo sasa ambacho kitakuwa ni kwa ajili ya *Livestock Research for Rural Development*, kitajielekeza kwa ajili ya kuboresha suala la mifugo kwa wafugaji waliko vijijini na lazima lihusishwe na kuondoa umaskini ulioko kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ziko tafiti ambazo zikifanywa na zikapelekwa kwa wananchi zitawaambia kabisa kwamba, kuwa na ng'ombe 100 ambao hawali chakula vizuri hakuna tija kuliko kuwa na ng'ombe 10 ambao wakilishwa vizuri wanakuwa na tija nzuri zaidi. Sasa haya yanatakiwa yaende kwa wananchi, kwa mfano, kwa ulinganisho

uliofanyiwa utafiti ili wananchi waweze kuona umuhimu wa kupunguza mifugo na kuwa na mifugo michache ambayo inakuwa na tija zaidi, hilo ni la msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tunaamini kwamba kwa kupitia kitengo hiki ambacho kinaweza kikaanzishwa kwenye Taasisi hii ya Utafiti wa Mifugo, kitengo cha *Livestock Research for Rural Development (LRRD)* kinaweza vile vile kikasaidia kuishauri Serikali kwamba, sasa ni muda muafaka kuweza kutoa dawa za ruzuku kwenye sehemu hii ya ruzuku. Nimeshuhudia sekta ya kilimo ikifaidika na ruzuku lakini kwenye mifugo hiyo sekta haijapewa vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba sekta hii ikiwepo na kitengo kama hiki kitasaidia kuona kwamba kwa wakulima wafugaji wale wanapewa ruzuku ya madawa na hivyo kuwa-*encourage* waweze kufanya kazi vizuri. Lakini naamini vile vile kwamba kuwepo kwa Taasisi hii na kitengo ninachopendekeza kutasaidia maeneo yale ambayo kuna sehemu kama za wafugaji, *ranches* kama za Kitulo, basi namna gani wananchi wale wanaozunguka yale maeneo waweze sasa kutumia lile shamba kwa kupewa wale ng'ombe au kwa kununua, lakini kwa kutumia wataalam wa kwenye lile shamba. Wale wataalam wakiwapa ule utaalam mzuri, wakatoa maziwa mazuri, baadaye yale maziwa yatanunuliwa pamoja na wale ng'ombe kwenye *ranch* ya Serikali. Hivyo, wananchi kupata soko na hivyo kupunguza umaskini kwa kupata kipato ambacho kinaeleweka kwa sababu wana *ranch* pale karibu ambayo inawasaidia kitaalamu, lakini vile vile iko karibu nao katika mambo mbalimbali. Kwa hiyo nilidhani hili ni jambo ambalo ni la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni wazi kabisa kwamba ukiangalia wakulima wetu ama wafugaji wetu wana mifugo na wanahitaji hizi bidhaa zao zinapoanza kama vile maziwa, lazima awe na soko. Sasa leo angalia shamba la ng'ombe la Kitulo, maziwa yanayotolewa pale, yanakwenda Mbeya kwa

gari, yakitoka Mbeya yanakwenda Iringa, ni wazi kwamba kiwanda cha maziwa kiko mbali sana. Pengine ingewezekana kuongeza thamani ya yale maziwa pale Kitulo kama kungekuwa na Kiwanda cha Maziwa pale cha ku-*process* na ambacho kingesaidia hata wafugaji wadogo kupeleka maziwa yao pale kiwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri alione hili kwamba ili kuongeza thamani ya maziwa yale kwenye shamba la ng'ombe la Kitulo, ni muhimu sana wakaona uwezo wa kufungua Kiwanda cha Maziwa pale Kitulo. Mpaka hivi ninavyoongea, wale wanafanya kazi kwa hasara kwa sababu usafiri wa kutoka Kitulo mpaka Mbeya mpaka Iringa wanaulipia wao. Kwa hiyo, matokeo maana yake bei ya lita moja inakuwa ni kama shilingi 500 mpaka 600 ambayo kwa kweli shirika letu la Kitulo pale linapata hasara. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali ilione hili kwamba, hata kama Serikali yetu sera yake sio kuwekeza kwenye viwanda tu, basi pengine tutumie wawekezaji wadogo, lakini wakiwezeshwa na Serikali ili kuwa na viwanda vya kutengeneza bidhaa zinazotokana na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu ni haya, lakini nimwombe sana Mheshimiwa Waziri alione hili kwamba, tunaamini Taasisi hii ikipitishwa itafanya utafiti wa malisho, itafanya utafiti wa mbegu, lakini iangalie sana mazingira ya shamba letu la ng'ombe la Kitulo kwamba kule hali ya hewa ni tofauti na maeneo mengine ambayo wafugaji ni wengi. Hali ya kule ni baridi inayohitaji utafiti kwa watu ambao wamebobea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii na naishukuru sana Serikali kwa kuleta Muswada huu kipindi hiki ambapo tuna

changamoto nyingi za mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika kifungu cha 5(1), kifungu cha 18(1), kifungu cha 19 na cha 38. Kwa miaka mingi Kituo cha Uzalishaji wa Mbegu Bora za Mifugo, Arusha kimekuwepo na takriban miaka kama minne Serikali imekuwa inajitahidi kupeleka viongozi wa Wilaya zile zilizoko kwenye maeneo ya wafugaji wengi kwenda Arusha kwa ajili ya kupata ujuzi na hatimaye kuwaelekeza wafugaji wao namna bora ya kupata ng'ombe bora. Lakini mpaka sasa hivi tumeshuhudia wafugaji kutembea nchi nzima na mifugo yao na ng'ombe hawa wamekonda, hawana tija na wala Serikali haipati tija. Kwa hiyo, ng'ombe bora laiti wangekubali kuboresha mifugo yao kwa kuhamilisha kama Kituo cha Arusha kinavyoelekeza, mfugaji anaweza kupata maziwa lita nane kwa siku badala ya lita mbili kwa siku kwa ng'ombe wa kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii sasa ikianzishwa maana yake ni kwamba, iwe ni kituo kikubwa au ifanye kazi kubwa ya kuangalia njia gani rahisi za kufikisha utaalam kwa mfugaji namna ya kuboresha mifugo yake, namna ya kuboresha madume yake ili aweze kuyatumia kwa kilimo bora zaidi ili pengine madume haya yaweze kumsaidia kubeba madume zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kabisa kwamba mifugo mingi inaharibu sana mazingira? Mkoa wa Shinyanga umekuwa jangwa, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Tabora na Mbeya umeharibika, Hifadhi za Taifa zimevamiwa na sasa hivi mifugo mingi inaelekezwa kwenye Bonde la Mto Malagarasi Kigoma. Ningeshauri pia vile vituo vya zamani vya utafiti wa mifugo ambavyo vipo kama *TALIRO*, kituo ambacho kipo Mkoani Kilimanjaro, West Kilimajaro, vifunguliwe ili viweze kusaidia katika utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Umoja wa Ulaya zinatoa ruzuku kwa wafugaji wao na wakulima wao na nchi hizi hata zinatoa masharti kwa wafugaji au wafanyabiashara wa Tanzania au kwa nchi za dunia ya tatu kwamba ni namna gani wanahitaji ng'ombe wa hizi nchi za dunia za tatu walishwe? Wanafanya kitu kinaitwa *traceability* kwamba wanataka kujua huyo ng'ombe amezaliwa lini, amekula nini na ndiyo hapo aweze kununua nyama ya hizi nchi za dunia ya tatu. Lakini kwa masharti hayo ni kwamba nchi za dunia ya tatu zitashindwa kushindana katika soko la dunia kwa zile *products* za mifugo. Kwa hiyo, kuna haja kufanya utafiti kwa ajili ya uzalishaji na namna gani watahifadhi na namna gani utumiaji uwe na namna gani tutauza ili kuweza kupata masoko ya bidhaa zetu nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hii inatakiwa pia ifanye utafiti kuhusu malisho ya mifugo. Wakishirikiana na Wizara ya Kilimo, inawezekana kabisa Wizara ya Kilimo ikaweka *schemes* za *irrigation* na kwa hiyo kama watakuwa wametenga maeneo ya *blocks* za kuotesha majani, inawezekana kabisa ikawa ndiyo chanzo kizuri cha *land use plan*. Kwa hiyo, badala ya mifugo kuzagaa nchi nzima, mifugo itakuwa kwenye eneo fulani, mwezi huu ng'ombe wanakula hapa, mwezi kesho wanakula eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko pia kifungo cha 18(1) kinachosema kuhusu mazao ya mifugo kama ngozi. Kuna haja ya viwanda vya ngozi vifufuliwe au viboreshwe. Kuna kiwanda kiko Moshi ambacho kina *process* ngozi, lakini wana-*semi process* pale Moshi, lakini *final process* inafanyika Nairobi. Kwa hiyo, utaona huyu mkulima au muuzaji wa Kilimanjaro hapati kipato cha kutosha na Taifa linakosa kwa sababu baada ya ku-*add value* hii ngozi inakwenda kuuzwa au kupelekwa Nairobi. Nashauri pia viwanda vya nyama vifunguliwe, tuuze nyama yetu ikiwa imesindikwa, ikiwa *packaged*, viko viwanda kule Mbeya na Shinyanga ambavyo vimefungwa na sisi tunasema Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa mifugo mingi

lakini hatuna kiwanda. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kwa utafiti huu, kuna haja hivi viwanda vifunguliwe ili tuweze kupata tija zaidi kutokana na mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujio wa soko la Afrika Mashariki na *SADC* na Umoja wa Ulaya na sasa kuna soko lingine linaitwa *BRICS* la Brazil, Russia, *South Africa*, China na India. Ningeshauri iwe basi ni chachu kwa Taasisi hii kuweza kufanya utafiti zaidi kwa ajili ya kuweza kugundua ni namna gani tunaweza kupata masoko mengine. Ni namna gani tunaweza kuingiza kwenye hili soko lingine jipya badala ya kutegemea tu soko la Umoja wa Ulaya ambalo kwa kweli linakandamiza nchi za Kiafrika na hata nchi za *Caribbean* na za *Pacific.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfugaji wa Tanzania anahitaji kufundishwa namna ya kufuga kwa kutumia mbegu bora, namna ya kunenepesha mnyama au ng'ombe kwa ajili ya nyama. Pia anahitaji elimu ya biashara kwamba afanye biashara na mifugo aliyonayo, auze ng'ombe wengine abaki na wachache, awaboreshe wale wachache apate maziwa zaidi na nyama zaidi. Lakini pia afanye biashara za aina nyingine kama majengo au usafirishaji wa anga, usafirishaji wa majini lakini apate pesa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niingie kwenye ufugaji wa kuku. Ufugaji wa kuku kwa *style* yake unavyokuwa hasa kuku wa kienyeji unaweza sana kumfaidisha mjasiriamali mdogo au mfugaji mdogo na hususani wanawake. Wengi wanachukua mikopo benki wakitegemea kufuga na kuuza na kupata fedha, lakini unatokea ugonjwa wa kideli kuku mmoja anakufa na banda lote linatoweka. Naomba Taasisi hii ya utafiti ilete usuluhisho katika tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19(1) kimetaja vijana, kimetaja watafiti wa Tanzania na naomba niipongeze Serikali na tukumbuke kwamba utafiti ni ajira tena nzuri sana. Kwa hiyo, niombe basi Serikali iweke mpango kwamba tuvutie

vijana waingie kwenye tafiti na watakavyokuwa wametoka na matokeo yao ya utafiti basi wakumbukwe, yaani wapate tuzo pengine wapewe fedha, pengine wapate mishahara mizuri zaidi ili kuendelea kuwavutia katika tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 38(1) kinaongelea kuhusu kanuni. Nimeambiwa kwamba Bunge hili lako Tukufu katika Mabunge yaliyopita limetunga Sheria nyingi ambazo zinashindwa kutekelezeka kwa sababu Kanuni zinakuwa zimechelewa kutungwa. Nashauri Kanuni zitungwe haraka ili kuepuka sasa migongano katika utekelezaji wa Sheria hii tunayotaka kuiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Cheyo na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii mchana huu na nataka kuanza kwa kuipongeza sana Serikali kwa kuamua kuleta Muswada huu mbele yetu na zaidi Muswada kwenye Ibara ya tano (5) unaposisitiza utafiti juu ya maendeleo ya uzalishaji mifugo na kuhimiza uzalishaji bora na pia utafiti juu ya uzalishaji na utengenezaji, uhifadhi, utumiaji na uuzaji wa mazao yatokanayo na mifugo na zaidi inazungumzia utafiti juu ya malisho na maendeleo ya vyakula vya mifugo na hapa ndiyo ningependa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningeshauri Serikali iache kabisa dhana kila wakati wanapozungumzia juu ya ng'ombe wanadhalilisha ng'ombe, eti ng'ombe wanatembea wamekonda. Eti yule mchungaji na mwenyewe amekonda, watu wote hawapati faida ya aina yoyote. Hii dhana ni potofu. Wale wafugaji wakiacha kutuletea nyama Dar es

Salaam mara moja kutakuwa *Peoples power* katika barabara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyama choma zote zitafungwa, ajira za watu hazitakuwepo, ng'ombe wasipokuwepo watu wengine hawataoa, ng'ombe wasipokuwepo watu wengine hawatalipa kodi na ng'ombe wasipokuwepo watu wengine hawatapeleka watu shule. Kwa hiyo, hii *business* ya kila wakati, ukizungumzia ng'ombe unaidhalilisha, sijui haina faida, ng'ombe katika Taifa hili ndiyo msingi unaotuweka na ni mtu mmoja mmoja mdogo kabisa ambaye tunamwita sisi maskini, lakini mimi namwita mtu mwenye ng'ombe ni tajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikuta mfugaji ana ng'ombe 1,000 maana yake ana akiba ya fedha isiyopungua milioni 400. Huyo mtu ni maskini huyu? Tatizo ambalo tunalo tumeshindwa, Wazungu wanasema *how to manage plenty,* namna ya kutawala uwingi na Serikali ina matatizo *actually* tukipata mahindi tunashindwa, tukipata ng'ombe wengi tunashindwa. Hii dhana ng'ombe wengi sijui punguzeni, sijui kitu gani, tusizungumze mambo ya kupunguza hapa. Tuzungumze namna ya kufanya ng'ombe wawe zaidi, wazaliwe wengi zaidi na tuwafanyie kazi, *that is the key message.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana likija tatizo la malisho, tumetenga hifadhi kubwa mno katika nchi hii kulisha wanyamapori na kila wakati tunanyang'anya ng'ombe malisho, tunaweka *hunting blocks.* Ndiyo hata ukiangalia mapato ambayo tunayapata kwa *hunting blocks* ni afadhali tungefanya kuwa ni *ng'ombe blocks.* Mahali pa watu kuchangia na hili watafiti ningependa watueleze, kama Wamasai wanaweza wakachunga Ngorongoro na ng'ombe wakaweza kukaa Ngorongoro na simba yuko pale na pundamilia yuko pale, ni kwa nini ng'ombe ambao tunapakana sehemu kwa mfano ile *Maswa Reserve* yote tangu Mwasware kuendelea mpaka Meatu kule kwa nini hizi siziwe

sehemu ambapo hii ni hifadhi kwa ajili ya kuweza kuchunga ng'ombe wetu. Watafiti watuambie kuna madhara gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni mbung'o siku hizi kuna ile *violate* nguo ambayo inawekwa katika kila sehemu. Hiyo inazuia mbung'o na mbung'o wanakufa. Kama ni mbung'o basi tutafute njia ya kuweza kuwamaliza ili ng'ombe wetu waweze wakachungwa pamoja na wanyamapori. Hii inawezekana Ngorongoro kama inawezekana Ngorongoro sioni kwa nini isiwezekane Bariadi, sioni kwa nini isiwezekane Simiyu, sioni kwa nini isiwezekane Meatu. Lakini kwa sababu ya hii dhana kwamba ng'ombe wengi punguza, punguza ndiyo maana hatufikirii na ndiyo maana nimefurahi sana kuona hapa kwamba tuangalie na malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini malisho ya Ng'ombe siyo majani tu, leo ukienda barabara ya Mwanza kwenda Musoma utashangaa jinsi watu walivyogundua namna ya kunenepesha ng'ombe. Ng'ombe unaweza kumkukuta amekonda lakini ukimpatia mapumba ya pamba, ukimpatia *cotton cake* utashangaa na nyama yake ni nyororo na nasema hili kwa uhakika. Maana yake niliposhinda Ubunge nilichinja ng'ombe wa namna hiyo wawili na watu wote wanasema Mheshimiwa umetutafutia wapi nyororo kama hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lakini Wizara inafanya nini kuboresha sehemu hiyo. Ningependa wafanye utafiti zaidi. Ni *dosage* kiasi gani ya *cotton cake?* Uzuri wa kuendelea hivyo itatusaidia sisi hata wakulima wa pamba katika ku-*stabilize price.* Kwa sababu badala ya kukaa tunategemea kwamba bei yetu itoke Ulaya, sasa tuna soko la ndani. Asilimia 66 ya pamba ni mbegu na asilimia 50 ni *cotton cake*. Mwaka jana tumelima kule zaidi ya kilo milioni 234 ndiyo kusema nusu ya hiyo milioni 107 ni keki. Tufanyie utafiti basi na usiishie utafiti na uhamasishaji, watu watumie hiyo *cotton cake* ili kuweza kunenepesha mifugo yao na wakifanya hivyo ndiyo njia ya kuanza kupunguza watu kuhamahama kwa sababu watajua kama ni wakati wa kiangazi tutakwenda kwenye pori, wakati

mwingine tutaweza kunenepesha hapa. Siyo hivyo tu, hiyo ndiyo njia ya kumtayarisha huyu mfugaji kuona biashara ya ng'ombe kama biashara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mfugaji hajioni kwamba yeye anafanya biashara, *but is a big business.* Nenda leo pale Pugu, ng'ombe mmoja ni laki saba. Rafiki yangu Mheshimiwa Laizer hayupo, juzi hapa ameuza ng'ombe mmoja kwa milioni 1.5. Sasa haya ndiyo maarifa ambayo tunataka kuuza kwa wafugaji siyo kuuza chuki ya ng'ombe. Siyo kuuza kwamba wao hawafai. Siyo wa kuwauzia kwamba wao ni maskini. Mfugaji siyo maskini, mfugaji ni tajiri. Sasa ningependa Taasisi hii isaidie zaidi katika eneo lao la malisho, isaidie katika kutuangalia ni jinsi gani unaweza kutumia hiyo pamba yetu kuhakikisha kwamba ng'ombe wetu wananenepa na wanapata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimefurahishwa kwenye hii Ibara ya tano (5), naambiwa kwamba utafiti pia utakuwa ni utafiti wa masoko. Masoko yenyewe ndani kwanza. Naungana kabisa na watu waliozungumzia hivi viwanda vya nyama. Hivi Mheshimiwa Waziri ni kitu gani kinachozuia Kiwanda cha Shinyanga kesho kisianze kuchinja nyama 800 kwa kila siku. Kiwanda cha Ruvu ambacho kimewekewa jiwe la msingi karibu mwaka mmoja na nusu na Rais kwa nini kisichinje ng'ombe 800 kila siku. Kwa nini Kiwanda cha Mbeya cha Ng'ombe kisifunguliwe na chenyewe kianze kuchinja ng'ombe 800. Hata tukamsaidia na rafiki yangu kule Mzindakaya na yeye ana kiwanda na yeye achinje ng'ombe 800 kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukichinja ng'ombe 800 kila siku ndiyo kusema kila siku tunachinja karibu ng'ombe 3,200. Wanaozungumzia juu ya kupunguza ndiyo wataona sasa tuanze kuongeza. Kwa sababu hatutakuwa na ng'ombe wa kutosha kuweza kufikia masoko na masoko yako wazi siyo lazima twende *European Union.* Watu wa Kinshasa kule

wanakula nyani, siyo kwa utashi wao, hawana ng'ombe. Ukiweza kupeleka *40 metric tone* kila wiki ambayo inawezekana. Ndege zima unakodisha pale unalipeleka kule. Fedha inaingia ndani ni fedha ya kigeni. Waarabu kule hawana ng'ombe, wanahitaji ng'ombe wa Tanzania. Lakini Wizara na Serikali hatujaweka umuhimu wa kuhakikisha kwamba ng'ombe wanachinjwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti hata Dar es Salaam soko la Dar es Salaam ni ng'ombe 1,000 kila siku. Lakini tunavyofanya mambo yetu siyo vizuri. Kuna baadhi ya machinjio ukienda kuyaangalia hutakula nyama maisha yako yote. Kwa hiyo, ningependa tuangalie zaidi hili jambo la masoko ili kweli ng'ombe wetu waweze kuwa na nafasi katika uchumi wa Taifa letu, unaonekana na kweli wafugaji wakafaidika. Serikali iache mambo ya kukamata ng'ombe kama Kilosa, kama Kilombero na sehemu nyingine bali tuwahakikishie hao maisha yao kwamba hapatakuwa na mtu atakayewabugudhi tena. Hicho ndicho kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nimeangalia hii Taasisi tunayoitengeneza, kwamba itapata fedha ya Bunge na nini. Nina hakika hii ndiyo njia ya kuinua hii Taasisi. Tutaitengeneza hapa kwa Sheria sawasawa lakini haitafanya kazi kama hakuna misingi ya pesa. Ningeshauri zaidi tutafute njia ya kuweza kuunganisha hii Taasisi na biashara ya ng'ombe kwa sababu inatoa *service* kwa ng'ombe au kwa mifugo kwa ujumla. Tukifanya hivyo watakuwa na uhakika wa kuweza kupata fedha inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka kutumia hii nafasi kuzungumzia neno moja juu ya watu wangu. Mwaka huu Kanda hiyo ya Ziwa na zaidi Mkoa wa Simiyu na sisi Bariadi na Itilima tutakuwa na njaa kuu kwa sababu watu walilima mahindi kibao mvua ilipoanza kunyesha mwanzoni lakini baadaye jua likaja na mahindi mengi yaliungua na watu wa sehemu hiyo ni takriban milioni sita, saba, nane. Nikiangalia

hesabu ya Serikali hapa sioni Serikali ambayo inaweza kuwa na uwezo wa kulisha takriban watu milioni saba. Kimbilio letu ni moja tu pamoja na kwamba tumekuwa na ukame lakini tumepata pamba nyingi sana ila Serikali kwa kupitia Bodi inaleta mizengwe namna ya kununua pamba.

Kuna mtu mmoja ametuletea hapa na unajua sisi Watanzania tunapenda sana mambo ya kuiga vitu. Kuna mtu mmoja ambaye anatoka anaitwa sijui *Lord* Swariby kutoka Uingereza sijui amefanya kazi sehemu za Zimbabwe, mambo ya kilimo cha mkataba. Sasa imekuwa lazima mnunuzi…

Kengele ya pili hiyo?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** *Oh I did not hear the first one.* Tusaidiwe na Serikali juu ya jambo hili.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana, Mheshimiwa John Momose Cheyo. Nakushukuru sana kwa mchango mzuri. Sasa nitamwita kwa namna muda wetu unavyokwenda, ikitimia saa kumi na mbili ndiyo wachangiaji waishe, basi nitajitahidi angalau wawili. Nimwite sasa Mheshimiwa Murtaza Mangungu na baadaye mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada wa kuanzisha Sheria hii muhimu ambayo iko mbele yetu hapa. Kutokana na muda naomba niende moja kwa moja katika Muswada husika. Ukianza na sehemu nyingine ambazo wachangiaji wengine wamechangia, ningependa niende kwenye sehemu ya pili ambapo imeainisha kazi ambazo zitakuwa zinafanywa na Taasisi hii ambayo imekusudiwa kuundwa. Sehemu ya 5(1) (a) (i) inazungumzia kwamba pamoja na mambo mengine Taasisi itashughulika

kuendesha shughuli za utafiti, maendeleo ya uzalishaji mifugo na kuhimiza uzalishaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya uanzishwaji wa Taasisi na malengo mahususi kama ilivyoainishwa katika Muswada nakubaliana nayo. Lakini ipo kazi kubwa kwa hao ambao watakuwa wanafanya utafiti kwa mujibu wa Sheria hizi ni jinsi gani ambavyo tutaweza kuwabadilisha watu kuendesha mifugo kwa njia za asili na kuja kuingiza katika ufugaji wa kisasa. Hii ni changamoto kubwa sana na naomba Waziri husika aliangalie hili kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele (vi) kimezungumzia zaidi pamoja na mambo mengine tafiti zitakazohusu afya ya mifugo. Naomba Taasisi vile vile ifanye utafiti ni jinsi gani ambavyo tunaweza kuwekea bima mifugo. Mifugo inakufa sana na wananchi wanaingia kwenye umaskini mkubwa sana pale ambapo majanga yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye utendaji wa Taasisi kile kipengele cha 18(1)(h) kinasema pia kwamba: "Uongezaji thamani, masoko na biashara na sera".

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitamwomba Mheshimiwa Waziri, arejee kwenye kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kuna kitu ambacho kimeandikwa kwenye changamoto; naomba kwa ruhusa yako nikinukuu wamesema hivi: *"The Sector is also facing a problem of non compliance to new market demand like livestock identification and traceability system and animal walfare."* Tumezungumzia zaidi hapa masuala ya masoko, Mheshimiwa Cheyo, amezungumza tunaweza tukaingia katika biashara ya kupeleka wanyama hawa au mazao haya katika maeneo ya *Middle East* na hata nchi hizi za Afrika. Lakini vilevile tuangalie mfanyabiashara yeyote ambaye anakusudia kufanya biashara, hawezi kujiwekea mipaka ya kutafuta masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tulifanyie utafiti kwa sababu, wataalam wetu wamelifanyia kazi kwa muda mrefu na wameliona kwamba, moja ya changamoto zinazoikabili sekta ya ufugaji ni hilo. Katika ukurasa huo huo wa 20, kuna maeneo mengi ambayo yameainishwa katika kitabu hiki cha Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano; matatizo ya masoko na utumiaji wa bidhaa zinazotokana na mifugo. Utafiti huo sijaona mahali ambapo umeainisha ni jinsi gani ambavyo tutawaelimisha wananchi kuweza kuielewa thamani ya mifugo kwa maana kwamba, hakuna kitu katika mifugo ambacho kinaweza kutupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, damu inatumika, mifupa inatumika, ngozi inatumika, hakuna kitu ambacho kinatupwa. Tatizo kubwa, kama alivyozungumza Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Cheyo na wachangiaji wengine, tumeua Viwanda vya Ngozi, tumeua Viwanda vya Nyama na bado tunawahimiza wananchi waweze kuingia katika ushindani wa kuzalisha wanyama kibiashara. Hii sio kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utafiti unatakiwa kufanywa, naomba mwelekeze zaidi pia katika utafiti ambao sasa hivi tunazalisha ngozi nyingi ambazo zinasafirishwa moja kwa moja nje, bila ya kufanyiwa *processing* hapa Tanzania. Kiwango cha juu kabisa ambacho kinaweza kusafishwa hapa kufikia kiwango cha *wet-blue;* lakini mtu yeyote yule ambaye anaweza akasafirisha ngozi nje ya nchi, anachajiwa 15% *export levy.* Lakini kwa nchi ambazo zinajua nini maana ya kutengeneza ajira katika nchi zao, wana-*subsides,* wanawafidia ile pesa ambayo sisi tunawachaji hapa na nchi hizi wala sio siri, India, Pakistan. Kwa nini hatuchukui mifano ya nchi za wenzetu za hapa hapa Afrika, ikiwemo Ethiopia, ambao hawakubali ku-*export raw hides and skins?* Kwa nini tunafanya hivyo? Tafiti zifanyike, lakini vile vile tuangalie maslahi ambayo yatakuwa yanalenga kumsaidia mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utendaji, Ibara ya 18(2) imeainisha hivi, umesema kwamba taasisi itawajibika katika usimamizi na utoaji wa taarifa za tafiti. Hapa napo tupaangalie kwa makini kwa sababu, mara zote tumekuwa tuna tafiti nyingi ambazo zinafanyika, lakini hakuna utekelezaji. Tafiti hizi tutazitumia vipi kuweza kumfikisha mwananchi wa kawaida ambaye ndiye mfugaji mwenye mifugo yake. Hii ni changamoto na ni lazima tuangalie mfumo ambao utasaidia, hizi tafiti ziwe zinawafikia wahusika. Vinginevyo, tutakuwa tunafanya kazi ya bure, kila siku tutaanzisha taasisi, mtaleta Miswada, tutaunda Sheria, ambazo zitakuwa hazitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mimi niko kwenye Kamati za *Oversight.* Taasisi hii naamini kabisa Bunge hili likiridhia, itakuwa ni moja kati ya taasisi zinazokuja kuripoti kwenye Kamati ambayo mimi nipo. Kuna kipengele kwenye sehemu ya tano (5), tukiacha kile kipengele cha 26 lakini ukisoma kipengele cha 27(1) hii imenipa mashaka na nitaomba Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha, basi anipe majibu katika hili. Kipengele hiki kinasema hivi 27(1), *"Wajumbe wa Bodi watastahili kulipwa posho na maslahi mengineyo, kama Waziri anavyoweza baada ya kushauriwa na Bodi."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tuko kwenye Kamati hizi za *Oversight,* tunaona matatizo makubwa sana ya kuacha Bodi kujiendesha na kujiamulia mambo yake. Kuna kumbukumbu ambayo tulikuwa tunapitia hesabu za shirika moja ambalo sipendi kulitaja, Waziri aliidhinisha kabisa Bodi ikae ijiamulie kugawana posho kufuatana na mapato ambayo wanapata. Jiulize wewe kama Bodi hii ikiwa inaingiza mapato na wakajigawia wao posho kufuatana na mapato yao, ni kiasi gani cha pesa ambacho tunapoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipengele cha 27(2) kinasema: *"Waziri katika kutumia mamlaka aliyonayo chini ya Kifungu Kidogo cha (1), atazingatia ushauri wa Msajili wa Hazina."* Mimi nasema kwamba, hapa lisiwepo suala la

kuzingatia ushauri; hapa ilistahili itamkwe kabisa, Waziri atalazimika kuzingatia ushauri wa Msajili wa Hazina, kwa sababu Msajili wa Hazina, ndicho chombo ambacho tumekiidhinisha kwa mujibu wa Sheria za Bunge, kusimamia mali zote za Serikali. Sasa ni kwa nini mmiliki wa mali awe anashauriwa jinsi ya kutumia mali zake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, naunga mkono hoja kwa kuzingatia kwamba, haya ambayo nimeyachangia na wachangiaji wengine ambao wamechangia yatazingatiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo kwenye Muswada ambao uko mbele yetu, Muswada wa Kuanzisha Sheria ya kuwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo. Kwa sababu ya muda naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni mali na hapa Tanzania tumeona *data* zinatolewa kila siku, Mawaziri wanatupa *data,* tunayo mifugo milioni kadhaa, mbuzi milioni kadhaa, ng'ombe milioni kadhaa, kuku milioni kadhaa, lakini nilikuwa najiuliza kwamba, kutoa *data* kwamba tunao milioni kadhaa inatosha? Hatujakaa tukaangalia kwamba, haya mamilioni ya mifugo ambayo tunaitaja kila siku ambazo ziko kwenye karatasi, zimeinuaje kipato cha Watanzania au zimeingizaje pato kwa Taifa au zinachangiaje kwenye uchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tu ya kukosekana kwa mipango mizuri ya nchi, sekta ya mifugo imekuwa haina tija kwa wafugaji wenyewe na hata kwa Taifa kwa ujumla. Tukiangalia hii miaka ya nyuma, sababu na mimi nimezaliwa kwenye miaka ya sabini huko nyuma, sekta hii ililiingizia Taifa pesa nzuri kwa sababu, tulikuwa tunakwenda hata *Super Market* unapata *sausage fresh* kutoka kwenye viwanda vyetu; unapata nyama ya *beef fresh* kwenye makopo, nakumbuka

sijui ilikuwa inaitwaje, lakini ni *fresh* kutoka *Tanganyika Packers,* bado unasikia imetoka Mbeya, hii imetoka Mwanza, tulikuwa tunapata vitu vya ndani ya nchi yetu ambavyo ni *fresh* vimetoka kiwandani, tunapakiwa tunapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyote vile leo vimekufa na leo imekuwa mifugo, haina thamani, wafugaji wanaonekana kama ni wakimbizi ndani ya nchi yao kwa sababu, tu Serikali ilikuwa haijaona umuhimu wa mazao haya ya mifugo na mifugo hii ndani ya uchumi wetu. Lakini nishukuru kwamba, kwa haya yanayofanyika sasa hivi nina imani sasa angalau Serikali imeanza kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimshukuru Waziri na timu yake kwa kuleta Muswada huu ambao, nina imani kabisa kama ukitekelezwa vizuri utasaidia kuweza kuinua sekta ya mifugo. Kwa sababu, kama tunavyosema *"No Research No Right of Talk."* Huwezi kufanya kitu kwa ukamilifu wake na kikawa na tija vizuri, ukaweza kuzalisha vizuri, kama hufanyi utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tunayo ardhi kubwa sana, tunayo mifugo mingi sana, tunayo ardhi ya kutosha na ardhi kubwa ya nchi hii haitumiki. Lakini unashangaa ni kwa nini wafugaji kila siku wanakuwa ni wa kukimbizwa tu, nendeni hapa, tokeni hapa, nendeni hapa, tokeni hapa. Kwa hiyo, hakuna mikakati, hakuna mipango kamili kwamba, wafugaji hawa tunawahamisha tunawatoa hapa, tunawapeleka hapa, ng'ombe wao wataendelea vizuri, kila wanachokifanya Taifa litanufaika na wenyewe watanufaika, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nikianza, Serikali ilihamisha mifugo kutoka Ihefu, lakini ni kwamba, wakati wa lile zoezi la kutoa mifugo kutoka Ihefu kuwapeleka sijui Kisarawe, kuwapeleka sijui Lindi, hakuna utafiti wowote uliofanyika. Ndio maana ukiangalia asilimia kubwa ya mifugo iliyohamishwa Ihefu, mingi ilifia njiani na hata kule walikokwenda. Kwa mfano

Lindi, juzi nilikuwa nasikiliza Taarifa ya Habari, wafugaji walewale waliopelekwa Lindi leo wanaambiwa hameni; Wanalindi wanasema kwamba, sisi tunaona mifugo kwetu ni mingi, lakini Serikali ilipanga kwamba iende kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kwamba, Serikali ilipokuwa inahamishia mifugo maeneo hayo, haikuangalia kwamba, mazingira yaliyopo kule yanafaa mifugo kwenda kukaa? Kwa sababu, sio kwamba kila jani unaloliona linaliwa na mnyama. Kwa hiyo, ukiangalia kuna majani ambayo ni kwa ajili ya wanyama, lakini ukiangalia majani mengi yaliyoko maeneo ambayo Serikali imepeleka mifugo ni majani ambayo sio mazuri kwa ajili ya mifugo. Kwa hiyo, unakuta mifugo haipati chakula cha kutosha, miundombinu haikuwepo, maji hakuna, basi ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake pato kubwa limepotea kwa sababu ya kukosa mipango; lakini hapa Serikali haijawahi kutuambia kwamba, mifugo iliyohamishwa Ihefu ikaenda Lindi, ikaenda Kisarawe, Serikali imepata hasara kiasi gani? Haijawahi kusema kwa sababu, ilikuwa haioni umuhimu wa ile mifugo. Kwa hiyo, naomba sasa kwa kupitia tafiti, Serikali ifanye mambo yake kwa kufuata utaratibu ili kuhakikisha kwamba, mifugo hii ambayo ni pato la Taifa, inaliletea Taifa fedha nzuri ambayo pia itainua kipato chetu cha Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye Muswada wetu Kifungu cha *6(1);* inasema kuanzishwa kwa Vituo vya Utafiti maeneo mbalimbali kama Waziri atakavyoona. Hapa ningependa kujua, kwa sasa hivi tunavyo vituo vingi hapa nchini vya utafiti wa mifugo; tunavyo kanda ya Ziwa, Mwanza, kuna kule *West Kilimanjaro,* tunayo Mpwapwa hapa ambapo nadhani ndio *Centre* kubwa na vingine naviona kama vilivyoainishwa kwenye jedwali ambalo nimeliona. Ningependa kujua kwamba, kwa kupitia Sheria hii sasa, Muswada huu, vinaanzishwa vituo vingine, je ni nini hatima ya vituo hivi ambavyo vipo sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivi ambavyo vingi sana vimekuwepo miaka mingi, lakini vimeshindwa kufanya kazi ya utafiti kwa ufanisi kwa sababu, ya kukosekana kwa uwezeshaji. Pesa inayotolewa kwenye vituo hivi ikawa ni kidogo, bajeti inayokwenda ni kidogo, wana upungufu wa watumishi, miundombinu na kila kitu ni mibovu, maabara zao zimechoka, kwa hiyo ni matatizo. Kwa hiyo, unaona kwamba vituo vilikuwepo lakini bado tulikuwa hatujaona kwamba, utafiti wa mifugo unafanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa kujua kwa kupitia Sheria hii sasa, vituo hivi vinavyoanzishwa ni vingine? Au vile vilivyopo vitaboreshwa viwe kama ni sehemu ya huu Muswada? Ningependa Mheshimiwa Waziri, atutolee ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nipende kusema kuwa, kuna sababu kubwa na haja kubwa sana ya kuboresha vituo vya utafiti wa mifugo ambavyo vipo kwa sasa hivi. Mazingira ya vile vituo kwa kweli yanasikitisha; kwa jinsi ambavyo mifugo yenyewe imekuwa haithaminiki na hivyo hivyo hata vile vituo vimekuwa havipewi nguvu ya kutosha. Kwa hiyo, sambamba na kuboresha sekta hii nzima, lakini pia vituo hivi tuhakikishe kwamba vinafanya kazi kwa ufanisi wake wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo maabara kubwa kabisa Tanzania ambayo ni Temeke, *Central Veterinary Laboratory* iliyoko Temeke. Maabara ile kwa miaka ya nyuma, miaka ya 1986, 1987 ilikuwa inafanya kazi kwa ufanisi mkubwa kabisa. Ulikuwa unaweza kupeleka *sample* pale, ukiangalia vitu vyako pale Maabara mpaka unafurahi na siku moja kesho unaambiwa mtu anachukua *sample* yake. Lakini kwa kuwa, imesahaulika sijui kama ina hali gani na sijui kama iteendelea ku-*survive* kwa mwendo inaokwenda nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mifugo hii ambayo tunayo, lakini maabara ile moja ya Kitaifa, tumeshindwa

kuiboresha. Mtu anapeleka *sample* yake anakaa wiki hajapata majibu na wakati mtu mwingine anatoka Mikoani. Kwa hiyo, wiki majibu hayajatoka, hata ugonjwa wa ng'ombe wenyewe aliokuwa anaumwa inakuwa *may be* ameshakufa. Kwa hiyo, hata majibu yakija kutoka, yanakuwa hayana msaada. Kwa hiyo, ningependa kujua ni nini hatima? Waziri, atueleze kwamba, sambamba na Muswada huo, kwa sababu kituo kikubwa cha utafiti ni nini kimeandaliwa kuhusiana na ile *Laboratory* ya *Veterinary?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Ibara nyingine ya 13(1); naungana na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwamba, nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hii ambayo ni muhimu sana, isiwe ya kuteuliwa. Isiwe ya kuteuliwa kwa sababu, Waziri anaweza akawa yeye anaona kwamba huyu mtu kasoma ana-*level* fulani, lakini *actual fact* ikawa sio hivyo. Kwa hiyo, iwekwe kwenye matangazo kwa sababu ya umuhimu na *sensitivity* yake, iwekwe kwenye matangazo watu wa-*compete*, watu wakae ateuliwe mtu ambaye ni *professional,* ana uwezo mzuri, anaweza akaendesha Taasisi hii kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kwamba hakuna sababu ya kuwa na msaidizi, ni taasisi ambayo ni moja tu. Ni kama vile tunavyosema labda *TAWIRI, TAFIRI,* hakuna haja ya kuwa na Mkurugenzi Msaidizi; Mkurugenzi mmoja tu kwa sababu, kwenye vile Vituo watakuwepo Wakuu wa Vituo ambao watakuwa wanatosha kuendesha shughuli ambazo zitatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine ni kipengele cha *19(2),* kinasema; yeyote atakayetaka kuendesha tafiti za mifugo, aandae *proposal* na vitu vingine vimeainishwa pale. Ningependa tuongeze kwamba, pamoja na mambo yote yaliyoainishwa pia ni lazima kuwepo na *time frame; time frame* ya *proposal* yenyewe na *time frame* ya lini atawasilisha ile *research* yake baada ya kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumeshuhudia *research* za maeneo mengine zinachukua muda mrefu kabisa. Nina mfano halisi wa Taasisi moja inayofanya kazi *Mikumi National Park* ya *ABRU,* miaka 42 leo *research* haijawahi kutolewa majibu. Miaka 42, mimi nikiwa mdogo mpaka leo, *research* iko pale, wazungu wako pale wanafanya *research*. Anatoka huyu anakuja huyu, akitoka huyu anakuja huyu, sasa hebu niambie kama *research* inachukua miaka 42 hata majibu yake yakitoka leo, yana faida gani? Kwa hiyo, *research* ni lazima iwe na *time frame* na *research* yoyote inafanyika kwa ajili ya kutoa majibu ili yaweze kusaidia katika kile ambacho kinatarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na *foreign researchers;* kwa kweli hapa ni lazima kama nchi, tuwe *very sensitive.* Ni lazima tuwe makini, anapokuja *foreigner* ni lazima tujue kweli ana dhamira na kitu anachokuja kufanya? Tusije tukaruhusu tu kwa sababu ni *foreigner,* amekuja tu na Mtanzania ambaye ni *assistant* wake tukamkubalia. Tunao mfano halisi wa yule *foreigner* aliyekuja kufanya *research* pale Ziwa Tanganyika kuhusiana na samaki; aliingia kwenye taasisi ya utafiti wa samaki, amekaa pale na msaidizi wake, amefanya utafiti, tumeona yaliibuka mambo ya mapanki hapa yamekwenda kuibukia huko mbele kwa mbele. Kwa hiyo, ni lazima tuwe makini kwamba, tunapopokea hawa ma-*foreign researchers* tuwe na uhakika, kwanza mwenyewe tumchunguze vya kutosha ili tuwe na uhakika kwamba ni kweli ana dhamira ya kufanya *research* kwa ajili ya kuisaidia tasnia hiyo. Pia msaidizi wake tuhakikishe kwamba, kweli na yeye mwenyewe anaweza akatumika kwa ajili ya kazi hiyo kwa ajili ya manufaa ya Taifa na sio kwa ajili ya manufaa binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia kipengele namba 18, ambapo Mheshimiwa Mangungu amekichangia, kuhusiana na suala la Waziri kupendekeza posho na maslahi ya

Bodi kwa kushauriwa na Bodi. Sasa nikawa nauliza, inakuwaje mtu amshauri Waziri kuhusiana na posho yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni lazima pawepo na aidha Taasisi nyingine ambayo itapendekeza maslahi na posho za *Members* wa Bodi. Haiwezekani *Members* wa Bodi wapendekeze posho, halafu Waziri ndio akubaliane nayo, aanze kuwalipa; wanaweza wakaamua kulipana milioni kumi. Najua, kuna shirika moja kikao kimoja tu cha Bodi, wanalipana milioni tatu. Sasa unaona hata wale ambao wanaofanya kazi huko *ground* ya kusababisha kile kitu kuwepo, hawalipwi hata posho kidogo, lakini wale ambao wanakaa *may be six hours or one day,* milioni tatu *per day*. Kwa hiyo, ni lazima kuwepo na *standard* na kuwepo na viwango kuhakikisha kwamba, pesa za walipa kodi haziendi tofauti na inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa sababu ya muda niishie hapo. Ahsante sana kwa nafasi, nakushukuru. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwani matatizo ya mifugo iko mingi sana.

Naomba Taasisi hii itusaidie kuweka utaratibu mzuri wa wafugaji nao kupumua na kufurahia mifugo pamoja na ufugaji. Tunayo migogoro ya maeneo ya malisho, hali ya wafugaji, uvaaji wao na vifaa ambavyo wanatakiwa kuwa navyo wakati wa kufuga na kulisha mifugo.

- Utafiti wa maji ya mifugo na usalama wake.

- Utafiti wa masoko – minada ya kuuzia mifugo hiyo.

- Utafiti wa mwingiliano wa mifugo toka nchi mbalimbali.

- Utafiti wa bei za mifugo ya ng'ombe kuku, kondoo na mbuzi kwa masoko mbalimbali.

- Utafiti ulenge kujua kwa nini pato la Serikali linalotokana na mifugo ni dogo kabisa kulingana na wingi wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu wawezeshwe katika ngazi zote ili *sector* hii iweze kuainishwa na kutoa mchango mkubwa zaidi.

Mwisho, ombi langu ni mnada wa mifugo wa Muyama, Jimbo la Manyovu ambao umefungwa na kuathiri wafugaji.

Maswali Makuu kwenye Wizara:-

(1) Kwa nini hakuna eneo la ufugaji katika maeneo mengi?

(2) Masoko kutokuwepo maeneo mengi ni kwa nini?

(3) Wizara kuwa na *budget* ndogo.

(4) Mifugo kuwa chanzo cha migogoro na wakulima.

(5) Madawa ya mifugo kutotosha na kuelimisha wafugaji.

(6) Maji ya mifugo tatizo.

(7) Usindikaji wa nyama hafifu.

(8) Uwekezaji wa mazao hayo ni mdogo tutajitahidi tutaweza.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru Serikali juu ya kuona umuhimu wa

kuanzisha Sheria hii ya Utafiti wa Mifugo jambo ambalo litaleta picha mpya ya kuwafanya Watanzania ambao wameegemea katika sekta ya mifugo kuwa na moyo wakiendeleza sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya mifugo imedumazwa kiasi cha kuwafanya wafugaji kuwa watumwa wa mifugo yao. Hata hivyo, niseme nia hii iliyooneshwa na Serikali ya kuanzisha tTasisi ya Utafiti iwe ni nia inayoambatana na matendo isiwe ni maelezo yatakayobakia katika kumbukumbu ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Watanzania tumekuwa na tabia ya kuanzisha kitu cha maslahi ya watu wa Taifa letu, lakini hatimaye maamuzi yetu hubakia katika maandishi na kutumiwa na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima zote kwamba elimu ya kutosha inahitajika kwa wafugaji ili isije ikaonekana kwamba wamepata kibali cha kuanza kuleta ugomvi baina ya wao na wakulima. Hivyo basi, pande mbili hizi zote zinashiriki katika kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 13 ya Muswada inampa uwezo Waziri kuteua Mkurugenzi Mtendaji na Naibu Mkurugenzi Mtendaji. Napenda niungane na watu ambao wataamua kuwa nafasi hii si vyema kuongeza Naibu Mkurugenzi, lakini si vyema pia kwamba nafasi hii apewe mamlaka Waziri juu ya kuteua Mkurugenzi hivyo ila ni vema vijana wapewe nafasi ya kujaza fomu na hatimaye kufanyiwa mahojiano ili yule ambaye atachaguliwa kutokana na mahojiano hayo hatoweza kuzusha mgogoro kwa jamii kwamba, mteuliwa huyo amependekezwa tu kwa udugu, ujirani au mtoto wa mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi wa Viwanda vya Nyama Tanzania litanyanyua pato la Taifa na kufanya katika

kukuza sekta hii kwa Mikoa ambayo inafuga ng'ombe kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe wa zamani si ukweli kwamba hawana faida na ni wakondefu hilo haliingii akilini bali ng'ombe wanategemeana na malisho ambayo wanapewa ng'ombe hao, tusiwavunje moyo wale wafugaji wa ng'ombe wa zamani kwa kuwaambia kwamba ng'ombe hao hawana thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa Sheria hii ni wa maana sana, unahitaji upongezwe na kila Mtanzania, lakini zaidi usiwe wa maneno bali uwe wa vitendo. Sheria hii tuitumie wenyewe Watanzania, sisi tusibakie na kumbukumbu ya maandishi ikatumiwa na wengine.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja. Baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafarijika kwa Serikali kuja na Muswada huu nikiwa na matumaini kwamba nia ya dhati ya Serikali kuhakikisha kwamba tunatumia rasilimali tulizonazo ili kujiletea maendeleo kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu lina mifugo midogo sana kwa Taifa. Ifike wakati kwamba lazima mifugo ichangie katika kuleta pesa za kigeni kama Mataifa mengine ambavyo yamekuwa yakifaidi. Itoshe sasa Serikali kuchukua uamuzi wa kuhakikisha kwamba ruzuku inayotolewa na Serikali inawafikia wananchi wa Mikoa yote hususan wa Mkoa wa Rukwa na hasa Wilaya mpya ya Kalambo.

**MHE. ALIKO N. KIBONA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja hii pamoja na maudhui yake yote.

Taasisi hii itakumbana na changamoto nyingi sana wakati itakapoanza kwa sababu wakulima na wafugaji wengi wanakata tamaa kwa sababu Serikali ilionesha kama haina haja sana na uendelezaji wa sekta hii. Majosho hayapo tena vijijini, viwanda vya nyama Shinyanga na Mbeya havipo tena, mashamba ya Kitulo na sehemu nyingine na ubora wa mifugo na Bajeti imepungua na sehemu zingine hayapo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, taasisi ije na majawabu ya kufufua mashamba haya. Taasisi hii itafute mbinu na ije na majawabu ya hatima ya Viwanda vya Nyama hapa nchini. Kitu kitakachofanya watu wahamasike kutunza na kufanya mifugo iwe bora, ni kuwepo kwa soko maalum kama ilivyo kwa mazao kama kahawa ambayo muuzaji lazima aiweke bora kabla ya kupeleka sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ya kumbana mfugaji atunze mifugo bora ni kuwa na soko la mifugo. Atakapouza mifugo ile hafifu itakataliwa na hiyo itakuwa changamoto kwa mkulima kuhakikisha mifugo yake inakuwa bora.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara na Serikali yetu kwa ujumla kwa kuleta Muswada huu Bungeni kuunda chombo cha kusimamia utafiti wa maendeleo ya mifugo. Mifugo ni eneo muhimu sana na taasisi inayosimamia utafiti wa maendeleo ya mifugo ni chachu madhubuti ya kuleta maendeleo ya kumkomboa mfugaji mdogo vijijini kwa kuwapatia wananchi mifugo iliyo bora kwa makusudio bayana. Mfano, ng'ombe wa nyama, wa maziwa, mbuzi wa nyama, wa maziwa, watenda kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii muhimu itasaidia sana kubaini wagonjwa na namna za kitabibu. Pia kuendeleza mbegu bora zenye uwezo wa kukabili maradhi lakini pia hata ukuaji ni kiasi na uzalishaji *(productivity)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kuwa Wizara ya Kilimo na hata ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi ni Wizara zilizo na wasomi wengi waliosomeshwa na fedha za Serikali. Muda sasa umefika watumike vizuri katika kufanya tafiti kupitia taasisi hii. Tafiti hizi sasa zilenge kuboresha mifugo ya kienyeji iliyo na uhimili wa hali ya hewa na mazingira yetu. Utafiti wa majani yanayopatikana na kustawi kwa wingi katika maeneo ya ufugaji ili kupunguza ufugaji wa kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa utafiti huu ulenge kule vijijini, uangalie wafugaji wadogowadogo na kuendeleza mbegu za wanyama wao. Ili tafiti hizi zizae matunda zisiishie kwenye uzalishaji wa wanyama na majani tu bali pia waangalie usindikaji wa nyama na maziwa na bidhaa nyingine zitokanazo na wanyama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na kuishukuru Serikali kwa kuleta marekebisho na Sheria hii maana sasa Sheria hii itasaidia pia kupunguza uharibifu na ufugaji holela kwa mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Sheria hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara yake.

Baada ya pongezi hiyo naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhamasisha matumizi ya matokeo ya *research*. Tafiti nyingi zinazofanyika nchini matokeo yake hayaonekani sana kwenye jamii kwa mfano, watu wachache wanakunywa maziwa au kufuga ufugaji wa kisasa/sayansi. Huu ni wakati wa

kuhamasisha wananchi kufahamu na kutumia matokeo mazuri ya *research findings.*

Pia kuimarisha kituo cha *research* cha Taifa. Napendekeza tujenge na kuimarisha tafiti Kitaifa yaani *National Research Institute Dedicated for Livestock*. Vituo vingine vya utafiti vidokezwe na *Research Institute* ya Taifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja iliyoletwa hapa mbele kwani inafungua njia nyingine ya kulikomboa Taifa la wafugaji ambapo uchumi wa nchi utakuwa kama zao la mifugo litatumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba viwanda vingi vya nyama vimekufa, zao la ngozi halina thamani kabisa. Mfugaji anapata fedha kidogo sana wakati mnunuzi anayesafirisha nje anafaidi sana. Pia viwanda vya ngozi nchini vinasuasua licha ya kuwepo faida kubwa ya ngozi kwa kutengeneza viatu, mkanda, begi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasukumwa kuandika ili kutoa angalizo kwamba bajeti ya Wizara ya Mifugo kwa asilimia ndogo sana ndio inapelekwa kwenye maendeleo ya sekta ya mifugo. Kwa mfano bajeti ya mwaka 2011/2012 ni asilimia 5% ndio iliyoenda kwenye maendeleo. Hii ni hatari sana. Naomba bajeti ya maendeleo iwe na *vote* yake tegemezi na sio kuchanganya ili fedha halisi za maendeleo zionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasiliaha.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa kuwasilisha Muswada huu Bunge kwa ajili ya kupitiwa hatimaye kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utafiti ni muhimu sana katika hatua za maendeleo kwani matokeo ya tafiti

huwawezesha wapanga maendeleo kuwa na vielelezo *(evidence)* kama ushuhuda na vigezo katika kuweka mipango ya maendeleo na utekelezaji wake hususan katika suala hili husika la maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wenzangu ambao wamechangia katika hoja hii katika masuala ya kuongeza bajeti, kukamilisha sera, udhibiti wa uagizaji wa bidhaa za mifugo na kadhalika. Nashauri utafiti utakaofanywa ulenge pia katika changamoto ya masoko ya bidhaa za mifugo, sambamba na tafiti za magonjwa, uzalishaji, malisho na maji ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kifungu cha 19(2) cha *Research Proposal format* kiongezwe kama/au kufuata *format* ya *COSTECH* au taasisi/zingine za utafiti kama *NIMR* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada na naomba kuwasilisha.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono kuanzishwa kwa Taasisi ambayo itawajibika na kuangalia na kuthibitisha hali ya ufugaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizngatia hali ya sasa ya uharibifu wa mazingira ambapo tumeshuhudia wafugaji wakiwa wachungaji, badala ya kuwa wafugaji wanaofaidika na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Taasisi ya Utafiti ikianzishwa pamoja na udhibiti wa mifugo katika suala zima la ufugaji wa mifugo katika suala zima la ufugaji wa kisasa liwepo suala la ushuru wa mifugo, kuondoa ushuru huo kumeleta uholela katika suala zima la utunzaji wa ardhi. Vyanzo vya maji na mifugo hii inabaki si msaada tena kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya mifugo lazima idhibitiwe kulingana na uwezo wa ardhi ya kufugia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ipimwe ili kila mfugaji afugie kwenye eneo lake na awajibike kurekebisha mazingira katika eneo lake na Taasisi hii iweke utaratibu wa kudhibiti na kukagua maeneo ya ufugaji. Mkoa wa Rukwa umeathiriwa sana, Wilaya ya Nkasi pekee ina idadi ya mifugo inayokabiliana kulingana na idadi ya wakazi wake ambapo tunashuhudia uharibifu wa mazingira, migogoro ya wakulina na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa sheria hii itawezesha mashamba ya mifugo kama yale ya Ranchi ya Kalambo yataweza kutumika vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa. Wananchi wamekosa ardhi lakini shamba la mifugo limegawia kwa watu ambao hawana mifugo kabisa, kumbe lengo la kuwabinafsishia wananchi wachache kwa lengo la kuanzisha ufugaji wa kisasa haujaafikiwa na hakuna anayedhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuleta Muswada huu ambapo nchi imevamiwa na wafugaji kila mahali na mazingira yameharibika kabisa.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Taasisi ni vema mmoja wa Wajumbe wa Bodi awe mfugaji wa kati na mkubwa ili kuwe na mrejesho wa tafiti kwenye matokeo chanya.

Pia elimu ya ufugaji kuku wa kienyeji kupitia *DADPS* ienezwe zaidi vijijini ili pato liongezeke na maradhi ya mifugo kama kideri yadhibitiwe. Pia tafiti za samaki wafugwao katika mabwawa matokeo yasambazwe vijijni ili pato liongezeke na umaskini upotee hasa vijijini.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutanguliza shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kuchangia hoja hii ya uanzishaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania.

Nichukue fursa hii kumpongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa uamuzi huu wa busara wa kuanzisha taasisi hii ya utafiti. Uanzishwaji wa taasisi hii itasaidia sana kuboresha mbegu za wanyama au mifugo tuliyonayo ambayo ni mbegu hafifu, kwa mfano ng'ombe aina ya zebu. Kufanya hivyo itasaidia sana kuongeza kipato cha wafugaji kwa kuongezeka hasa uzalishaji wa maziwa, nyama na *by-products* nyinginezo kama vile ngozi na kwato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hii itasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuweka mifugo duni kwa wingi ambayo inaathiri upotevu wa uoto wa asili na pia *soil compaction* inayoleta kutokea kwa mmomonyoko wa ardhi na makorongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii pia itapunguza ugomvi wa kijamii unaotokea baina ya wafugaji na wakulima na hivyo kupungua kwa vifo vinavyosababishwa na ugomvi huo. Haya yote yanatokana na ufugaji mbovu usiokuwa na maelekezo ya kitafiti/utaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumeshuhudia Mheshimiwa Rais akitoa fidia ya mifugo kwa wafugaji wa Arusha ambao walipoteza mifugo yao kutokana na kukosa malisho kutokana na ukame. Taasisi hii pamoja na kazi nyingine ni lazima ifanye utafiti wa malisho *(pasture)* ili tuweze kupata mbegu za malisho ambazo zinastahimili ukame na kwa *agro-economic zones* za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pamoja na umuhimu wa taasisi hii, nashauri kwamba muundo na uendeshaji wake

uhakikishe kwamba unasaidia kupata fedha kwa ajili ya kazi zao. Tafiti zetu nyingi hazijawafaidisha wafugaji na Tanzania kwa ujumla. Hivyo kiungo cha taasisi hii ya utafiti na wa wafugaji ni muhimu sana ili kuhakikisha kuwa matokeo ya tafiti zinawafikia walengwa kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hii ni taasisi ya utafiti, zaidi ya kuwa na *Director* na *Deputy Director*, pia tufikirie kuwa na *Chief Researcher* ambaye atakuwa ndiye *coordinator* wa tafiti zote zitakazofanywa na utekelezaji wake. *Director* na *Deputy* wake zaidi watakuwa ni mambo ya *management* na *administration.*

Kuhusu kazi za Bodi katika kifungu cha 2(d) nashauri isomeke; "*approve plans and budgets of the Institute.*" Pia kifungu cha 2(g) nashauri kisomeke; "*Determine and authorize fees for services rendered under this Act.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nikushukuru wewe kwa kuendesha hili kwa ufasaha kabisa. Naomba kuchangia hoja na nashukuru sana. Ahsante.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nitoe pongezi kwa Serikali kwa kuja na Muswada huu ambao unahusu uundwaji wa taasisi ya mifugo nchini. Naamini hii itasaidia sana wananchi na nchi kwenye kuboresha mazao ya mifugo, kuongeza pato la watu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla na kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuondoa ufugaji wa wanyama wengi wasio na tija na kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya pili, Ibara ya 5(a)(ii) inaonyesha kazi za taasisi. Huu utafiti na hapo inaonyesha pamoja na kazi nyingi sana zilizoorodheshwa kuna kazi ya uzalishaji, utengenezaji, uhifadhi, utumiaji na uuzaji wa mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii ni kubwa na inaweza ikafanya taasisi ikaondoka kutoka kwenye utafiti na kwenda kwenye biashara na kuharibu mpango mzima.

Lakini pia taasisi inaweza kuhodhi kwa siri matokeo ya utafiti wao ili na mwingine asiutumie na kupata faida hasa wafugaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho kama hoja ni kufanya biashara, tunayo taasisi nyingine inafanya biashara ya mazao ya mifugo *(NARCO).* Ningependa nipate maelezo ni kwa nini basi ili kupunguza gharama kwa Serikali *NARCO* isiwezeshwe ili ifanye utafiti katika ranchi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Muswada huu hakuna mahali popote inaonyesha ni jinsi gani mkulima mdogo atafaidika na matokeo ya utafiti. Lakini mimi nadhani nia na madhumuni ni kubadili hali ya ufugaji duni wa sasa na kama ndiyo wengi najua nitaambiwa kutakuwa na kanuni zitakazoangalia suala hili. Lakini uzoefu umeonesha utekelezaji wa kanuni nyingi zinategemea kiongozi aliyekuwepo mezani. Hii ni hatari, kwa nini sheria isitambue moja kwa moja ni jinsi gani mfugaji mdogo atapata faida ya sheria hii ili aweze kuidai atakapoikosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalileta kwenye muundo wa Wajumbe wa Bodi sehemu ya tatu, Ibara ya 8(2) ambayo katika wajumbe hao hakuna mwakilishi yeyote kutoka kwa watumiaji wa utafiti huo yaani wafugaji wadogo wadogo na hata wakubwa. Hii ingesaidia kwa taasisi kupata taarifa ya haraka ya vipindi vifupi kama bodi inavyokaa ili kuweza kupata mrejesho wa mwanzo na matokeo ya utumiaji wa matokeo ya utafiti. Mimi napendekeza wawepo wawakilishi wa vyama vya wafugaji au kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne, Ibara ya 19(1) inaeleza masharti ya mtu binafsi anaweza kufanya utafiti na

Ibara ya 20 inaeleza adhabu ya mtafiti binafsi wa ndani au wa nje iwapo atashindwa kupeleka matokeo ya utafiti wake, lakini sheria haisemi ni jinsi gani italinda siri ya utafiti wake ili kama amegharamia mwenyewe aweze kuvuna kwa kuuza matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni muhimu sana ama sivyo *private researchers* hawataona haja ya kushiriki katika tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu, naomba hayo niliyoyaleta yafanyiwe kazi kuboresha sheria hiyo ilete tija kwa wananchi na nchi kwa ujumla. Naunga mkono hoja.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi naunga mkono hoja ya Muswada wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo. Tabora ni moja ya Mkoa ina ng'ombe wengi, mbuzi, kondoo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika sana kuona katika sheria hii Mkoa wa Tabora hakuna Taasisi ya Utafiti wa Mifugo pamoja na ukweli kwamba katika Ukanda wa Magharibi kuwa ng'ombe wengi kuliko ukanda wowote ule.

Naomba atakapokuwa anajibu majumuisho ya Muswada huu naomba Mkoa wa Tabora, Mji wa Tabora kwa kupitia Chuo cha Tumbi (Utafiti wa Kilimo) ambacho kina uwezo na eneo kubwa sana na niko tayari kusaidia ili kufanikisha maombi haya katika kuwakomboa wafugaji wa mifugo.

Vilevile nashauri taasisi hii ijishughulishe na masuala ya kutafiti masoko ya nje kwani tunahitaji fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja Muswada huu.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kuhusu Sheria ya Taasisi ya

Utafiti wa Mifugo. Naomba sana suala la tozo ya faini ya shilingi 50,000 kwa kila ng'ombe anayeingia katika eneo la *NARCO*, hasa kule Missenyi imekuwa adha kubwa kwa wananchi jambo ambalo wana Missenyi, wafugaji wa Kata ya Kakuyu wanateseka sana na ukizingatia wananchi wameporwa ardhi yao na kuuzwa kwa wawekezaji na hii imesababisha wananchi kukosa nafasi za kuchungia wanyama wao. Matokeo yake ng'ombe akiteleza tu inakuwa ni mateso makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, je, hizi pesa zinafanya kazi gani na kiasi gani kimeweza kukusanywa toka *NARCO* ya Missenyi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini wafugaji wa Wilaya ya Missenyi watasaidiwa mbegu bora za kuwawezesha kuwasaidia kuwa wafugaji bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Wizara ikishirikiana na Wizara ya Ardhi, watatatua mgogoro wa wafugaji wa Kata ya Kakuyu walionyang'anywa ardhi yao na kupewa wawekezaji wasiowekeza?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya tatu kwa mifugo Afrika. Hata hivyo, mchango wa mifugo katika pato la Taifa nchini ni mdogo ukilinganisha na mchango katika nchi zenye mifugo michache kuliko nchi yetu. Tanzania ina mifugo mingi lakini uzalishaji ni mdogo. Pia muunganiko kati ya mifugo na soko na mifugo na sekta nyingine ni mdogo kwa kiwango cha nchi kuagiza bidhaa za mifugo kutoka nje ya nchi. Hali ni kutokana na kasoro katika mifumo na miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti ni nyenzo muhimu katika kutafuta ufumbuzi. Hata hivyo, Serikali haijaeleza kwa takwimu, namna ambavyo vyombo vilivyopo vya utafiti nchini havijaweza kukidhi haja ya utafiti katika mifugo kwa kiwango

cha kuonekana haja ya kuanzishwa kwa taasisi maalum kwa ajili ya utafiti wa mifugo pekee. Hivyo, siungi mkono hoja mpaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu mosi, ni kwa kiasi gani Serikali imetenga fedha za kutosha kwa kadiri ya ahadi ya Serikali ya kutenga bajeti ya utafiti walau asilimia moja ya pato ghafi la Taifa?

Pili, ni kwa kiasi gani taasisi zilizopo za utafiti ambazo zimekuwa zikifanya utafiti katika masuala yanayohusiana na mifugo zimetimiza wajibu na ni upungufu upi wa kitaasisi umeonekana?

Tatu, tafiti mbalimbali ambazo zimefanyika na taasisi, vyuo na wataalam mbalimbali toka uhuru zimetumika kwa kiwango gani katika kuinua sekta ya mifugo nchini. Serikali badala ya kuanzisha utitiri wa taasisi ni muhimu ikaweka kipaumbele katika kuzijengea uwezo taasisi zilizopo na kutumia tafiti zilizofanyika mpaka sasa nchini katika sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Serikali itaendelea kutaka Muswada huu upitishwe Bungeni katika hatua zake zilizobaki kwenye mkutano huu wa Bunge basi izingatie marekebisho yafuatayo:-

Mosi, kuweka mfumo ambapo taasisi itaweza kufanya kazi kwa karibu na Tume ya Mipango ambayo imepewa wajibu pia wa kushughulikia masuala ya utafiti na upangaji wa mipango ya maendeleo.

Pili, kuboresha mfumo wa ushirikiano kati ya taasisi na Halmashauri za Wilaya kwa kuwa sehemu kubwa ya shughuli za mifugo husimamiwa na Halmashauri.

Tatu, kupanua wigo wa uteuzi wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ili kuwezesha uteuzi kuzingatia vigezo na ushindani na pia kuwe na mipaka kwa mamlaka makubwa aliyopewa Waziri katika vifungu mbalimbali.

Nne, kuboresha mchakato wa bajeti ya taasisi ili kuhakikisha masuala ya Bunge na Kamati zake katika usimamizi wa kisera, mipango na bajeti unapewa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza wajibu wa kisheria wa utafiti, taasisi iweke mkazo kwenye utafiti na kulipatia ufumbuzi tatizo la muda mrefu la migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, pamoja na utafiti kuhusu ufugaji, utafiti upewe mkazo katika usafirishaji wa mifugo na bidhaa za mifugo, usindikaji wa bidhaa za mifugo na usambazjai wa bidhaa husika. Lengo la tafiti zote liwe ni kuwezesha mifugo kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi na kuongeza ajira bora nchini hususani kwa vijana. Hatua hizi zitachangia pia kupunguza kiwango cha bidhaa za mifugo kinachoingizwa toka nje hususani katika Mkoa wa Dar es Salaam na Jimbo la Ubungo.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kuleta Muswada huu wa sekta ya mifugo iliyokuwa imesahaulika kwa muda mrefu katika utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

- Taasisi hii pindi itakapoanza, ni vema kwanza ikajikita katika kujitangaza na kuuelezea umma kwa njia mbalimbali za mawasiliano ili wananchi waweze kuifahamu taasisi kwa ujumla kazi zake na madhumuni yake kwa manufaa ya wananchi ambao wengi wao ni wakulima na wafugaji.

- Kutoa elimu kwa wananchi ambao wengi wako vijijini umuhimu wa kuwa na mifugo michache iliyo bora na ambayo kwa mazao yake pato linaweza kuongezeka na hivyo kuweza kupata habari sahihi kuhusu namna ya ufugaji bora na

pia namna ya kupata habari kuhusu masoko ya mazao yanayotokana na mifugo yao.

- Taasisi hii iweze kuelezea wananchi umuhimu wa tafiti na mahusiano yake katika kuleta maendeleo si tu ya Taifa bali hata ndani ya familia ili wananchi hawa waweze kupunguza umaskini na hata ikiwezekana kutoka kabisa katika umaskini ili kutimiza Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

- Taasisi ijikite katika kutoa elimu kuhusiana na hali halisi ya mazingira hasa katika utunzaji wa mazingira na maliasili zilizopo na zinazowazunguka katika maeneo yao.

- Taasisi iwasaidie wafugaji namna ya kuthaminisha mazao yatokanayo na mifugo yao ili mazao yao yawe na thamani kubwa ili waweze kujiongezea kipato cha familia na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Muswada huu umekuja wakati tumechelewa. Kama Idara hii ya Mifugo ingekuwa ikiangaliwa mapema, huenda tusingefikia hatua ya kuona mifugo ni bughudha katika Taifa hili. Utafiti usilenge katika kuboresha ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku tu bali utafiti uhusishe malisho, mazao yatokanayo na mifugo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha huduma muhimu za ugani juu ya sekta ya mifugo zinafanyiwa utafiti ili kuboresha afya ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja sasa kutenga maeneo ya malisho ya mifugo badala ya kuacha wafugaji wanahangaika kana kwamba mifugo yao haina faida. Aidha, suala la masoko ya mifugo na mazao yake nayo yanatakiwa yafanyiwe utafiti wa kutosha na kuwe na viwanda vya kusindika nyama na ngozi na maziwa.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu unaolenga kuimarisha na kupanua ustawi wa mifugo nchini. Nchi yetu asilimia kubwa ya wananchi ni wakulima na wafugaji na sekta ya ufugaji ingeweza kuchangia sehemu kubwa ya uchumi wa nchi. Sekta ya mifugo haijapewa umuhimu unaostahili ili kuhakikisha kwamba sekta hii inapanuka, inastawi na hivyo kuwanufaisha wananchi na Taifa kwa ujumla. Katika maeneo ya wafugaji, Serikali bado haijawapa elimu wafugaji ili waweze kufuga kwa mafanikio kwa kuwatengea wafugaji maeneo maalum ya kufugia na kuweka miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo kungeweza kusaidia kupunguza migogoro kati ya wafugaji na wakulima.

Matokeo ya utafiti unaotarajiwa yawe ni yale yanayolenga:-

(1) Kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo.

(2) Kuelimisha wafugaji kuwa na mifugo bora badala ya kuwa nayo mingi isiyo na tija.

(3) Kutambua kwamba mifugo siyo ng'ombe tu bali aina zote za wanyama wafugwao ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, bata, sungura, nguruwe na kadhalika. Aina zote hizi zifanyiwe utafiti katika maeneo yote ya nchi yetu.

(4) Kutafuta ufumbuzi juu ya migogoro baina ya wakulima na wafugaji kwa kuhakikisha kuna utaratibu rasmi wa matumizi bora ya ardhi.

(5) Taasisi hii iwe na matawi katika kanda zote za nchi yetu ili matokeo ya tafiti yaweze kuwafikia wafugaji kama namna bora ya ukamilishaji na kadhalika.

(6) Taasisi izame sana katika kutafiti namna bora ya mazao ya mifugo ili kuleta faida kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi ninashauri matokeo ya utafiti yasiandikwe katika mabuku makubwa na kuwekwa kwenye mashelfu bali yaandikwe katika lugha rahisi na kuyafikisha kwa walengwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu mkubwa wa kuleta sheria hii; hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwapongeza Wanakamati na Viongozi wa Kamati, kwa ushauri wao mzuri na wenye manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mifugo ni sehemu ya uchumi wa Taifa ni vizuri kuwa na vituo vya utafiti. Vituo vya Utafiti wa Mifugo ni vingi nchini Tanzania, lakini tatizo vituo hivi kikiwemo kile cha Dar es Salaam ambacho toka miaka ya nyuma kilikuwepo eneo la Temeke ambapo panajulikana kama Vetinary hatujui kama kipo au kimekufa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Muswada huu tukaupitisha labda hivi vituo navyo vitaweza kufanya kazi zake vizuri na kuonesha uhai. Pia maeneo ya Vituo vya Utafiti yanakuwa kama hayana wahusika. Niombe Muswada upite na Wizara iweke mpango mkakati wa kuviimarisha Vituo vya Utafiti wa Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu

kwa wakati, huku nchi yetu ya Tanzania ikishika nafasi ya tatu kwa wingi wa mifugo katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umeletwa makusudi ili uweze kuwakwamua wafugaji ambao ni wengi ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Pamoja na azma nzuri ya Serikali ya kutenga asilimia moja ya pato lake la Taifa kwa ajili ya maendeleo ya utafiti, pesa hizi ni ndogo ukilinganisha na uhalisia wa uwingi wa mifugo ndani ya nchi yetu. Ningeomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza kiwango kinachotengwa kutoka asilimia moja kwenda walau asilimia mbili na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 6(1) cha Muswada huu, inaelezwa kuwa "Waziri baada ya kushauriwa na Bodi ataanzisha vituo kadhaa vya taasisi ikiwa na lengo la kutekeleza kazi za taasisi kama inavyohitajika. Kabla ya kushauriwa na Bodi, Waziri ashirikiane na Viongozi wa Serikali au wa Siasa ili kuainisha maeneo ambayo hata vituo vikianzishwa vitaleta tija kwa wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo au mikoa ambayo asili yake ni ufugaji, ningeomba Waziri ayape kipaumbele anapotaka kuanzisha vituo. Pamoja na kuanzishwa vituo hivyo ni vyema vikawekwa karibu na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vituo vingi vya utafiti ambavyo vimekutwa na sheria hii. Ningependa kuiuliza Serikali vina maeneo ya kutosha kuwezesha kufanyika utafiti wenye tija; na kama havina ardhi ya kutosha Serikali inafanyeje sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Vituo vya Utafiti wa Mifugo kama Kilimanjaro Magharibi na kile cha Mpwapwa ambavyo vina hekta nyingi sana lakini sina uhakika kama zinaviletea tija vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ekari ni nyingi sana na pengine vituo vinashindwa kuzilinda, matokeo yake wananchi wanaozunguka maeneo hayo wamekuwa wakiyavamia maeneo hayo na matokeo yake migogoro inaanza kati ya vituo na wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie upya maeneo hayo kwani sasa hivi idadi ya watu imeongezeka na ndiyo maana ardhi inazidi kuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu kifungu cha 15(1), kinachoipa Bodi mamlaka ya kuajiri wataalam. Jambo hili mimi siliafiki. Bodi ni mamlaka ya nidhamu na siyo mamlaka ya ajira. Hivyo basi, naomba sana kifungu hiki kibadilishwe na jukumu hilo iachiwe mamlaka husika ambayo ni Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu iliyotajwa katika kifungu cha 20(a) ya faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kwenda jela kwa kipindi cha miezi sita. Tuna Watafiti wa nje ya nchi na ndani ya nchi na watafiti wa Serikali wanaolipwa kutokana na kodi za Watanzania. Je, ni watafiti gani sasa ambao watahusika na hii adhabu kama inavyojieleza katika kifungu cha 20 (a) cha Muswada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 cha Muswada huu kinampa Waziri anayehusika na dhamana ya mifugo, wajibu wa kupanga marupurupu kwa Wajumbe wa Bodi kwa kushauriana na Bodi. Hivi kweli inawezekana mtu kujipangia marupurupu mwenyewe? Ningeomba kifungu hiki kifutwe ili marupurupu yao yapangwe na Serikali kama Taasisi nyingine za Serikali zinavyofanya kwa Wajumbe wake wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini Taasisi hii sasa italiletea tija Taifa ikiwemo kuongezeka kwa Pato la Taifa, kwani mifugo ina mazao mengi sana na isitoshe bado tunaongoza kwa wingi wa mifugo Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nasisitiza vituo hivi vielekezwe kwa wafugaji na hasa katika maeneo yenye mifugo mingi. Nina matumaini tutakuwa na mifugo na mazao bora yatokanayo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara, kwa kuandaa Muswada huu ili kuboresha ufugaji na ili kuongeza kipato cha wananchi na Serikali kwa ujumla. Sisi wenyeji wa Dodoma, mifugo ni zao kubwa na muhimu; hivyo, tunaomba Serikali ikumbuke kuboresha mifugo yetu kwa kutumia utafiti unaofanywa na Watafiti. Mambo muhimu ya kuboreshwa ni:-

- Malisho ambayo katika kipindi cha kiangazi hufanya mifugo iathirike sana;

- Suala la dawa kuuzwa kwa bei kubwa na hivyo kuwafanya Wafugaji washindwe kuzinunua; tunaomba Serikali itueleze utaratibu ambao utasaidia bei hizo zipunguzwe;

- Kwa kuwa ufugaji ni kazi muhimu tunaomba Serikali ijitahidi kutoa elimu kwa Wafugaji ili ufugaji uboreshwe na uwanufaishe Wananchi;

- Majosho mengi yaliyojengwa hayana maji na hii inasababishwa na ukosefu wa maji katika vijiji. Naomba kujua kama kuna utafiti uliofanyika kuhusu upatikanaji wa maji kwa ajili ya Mifugo au ni vipi Wizara hii inavyoshirikiana na Wizara ya Maji;

- Naomba kujua ni vipi utafiti huu utasaidia wananchi kuboresha ufugaji ili wanufaike na pia kubadilisha kabisa ufugaji wanaoendelea nao sasa;

- Mpaka sasa Dodoma hatuna Kiwanda cha Maziwa; je, utafiti umeshafanyika kuhusu kiwango cha maziwa yanayopatikana ambacho kingewezesha kuanzishwa kiwanda na pia kuwezesha kuhamasisha wawekezaji?

- Watumishi wa Mifugo sasa hivi hawaonekani vijijini, hivyo huduma ya kutibu mifugo inakuwa shida, tunaomba Wizara hii iwaajiri watumishi wengine;

- Vyuo vya kufundisha Wataalam wa Utafiti vipo vingapi na Wataalam wanaomaliza masomo wanatosha? Naomba vyuo hivi vipanuliwe ili tupate Watafiti wa kutosha; na

- Naomba Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya suala zima la utafiti hata wa magonjwa mbalimbali ya mifugo wakiwemo kuku, bata na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipengele kinachomtaka Waziri anapoteua Bodi inabidi ateue Mbunge anayetoka kwenye jamii ya ufugaji. Kwa nini asiteuliwe mtaalam wa mambo ya mifugo kutoka kwenye maeneo ya ufugaji? Haimaanishi ni lazima ajue mambo hayo, mambo ya ufugaji yanahitaji utaalam na uzoefu. Tuna changamoto za ufugaji wa kisasa, tunahitaji utaalam wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuhakikishe kuna maafisa mifugo wa kutosha mikoani na wawe na vitendea kazi. Kuna changamoto kubwa, maafisa wengi wa mifugo hawaendi *field,* wamekuwa wakibaki ofisini huku wafugaji wetu wanakosa elimu ya utaalam wa kuendesha ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuhakikishe *ranch* zetu zinafanya kazi, zilizopo hazifanyi kazi na ni chache; hivyo ni vyema Serikali ihakikishe kuna *ranch* za kutosha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa kufikia kuleta Muswada huu wa Sheria hii ya Utafiti wa Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu sasa imekumbwa na migogoro mikubwa ya wakulima na wafugaji. Hivi sasa ni muda mwafaka kwa Serikali kuondoa migogoro hiyo kwa kuangalia vipengele ambavyo vinasababisha migogoro. Sababu ya kwanza inasababishwa na kutokuwa na sheria inayoeleza na kufafanua kuwa mkulima alime wapi na mfugaji afuge wapi. Lazima Serikali iainishe maeneo ya kilimo na maeneo ya ufugaji kusiwe na mwingiliano wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji unatakiwa uwe wa kisasa, unaozingatia ufugaji bora kama ifuatavyo:-

- Unaozingatia mbegu bora ya mifugo;

- Eneo la kutosha linalolingana na idadi ya mifugo ili kuwa na malisho ya kutosha;

- Hali ya hewa ya kuwezesha ustawi wa mifugo, upatikanaji wa wataalam wa kutosha na wa kuwajibika vizuri;

- Mafunzo kwa makundi mbalimbali ya wafugaji;
- Kuwa na ufugaji bora na siyo bora ufugaji;

- Upatikanaji wa soko la mifugo lenye kuleta tija kwa wafugaji;

- Kuzuia ufugaji wa uzururaji wa mifugo kila sehemu ya nchi yetu bila kufuata Sheria ya Ufugaji;

- Usindikaji wa nyama, ngozi, kuliko kuuza mali ghafi katika nchi nyingine;

- Kuwa na viwanda katika maeneo ya wafugaji; na

- Utoaji wa elimu mara kwa mara kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kusema kuwa ninaunga mkono hoja. Pia naipongeza Serikali kwa kuletwa Muswada huu Bungeni japo umekuja kwa kuchelewa sana. Mswahili anasema kawia ufike, bila shaka tutafika pale tunapokusudia kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafugaji wetu wa Tanzania wamekuwa wakijitahidi kufuga kwa nguvu zao wenyewe, bila Serikali kutoa mchango mkubwa. Wafugaji wanapata hasara kubwa sana mara ukame unapolikumba eneo ilipo mifugo hii, mfano ni ukame uliojitokeza maeneo ya Arusha, Kagera na kwingineko. Serikali imekuwa haitoi msaada wowote wa kumsaidia mfugaji kwa kumfidia mifugo yao au kuwatafutia eneo mbadala la kulisha mifugo yao. Kitendo cha wafugaji kupoteza mifugo kwa wingi kiasi hiki ni tatizo kubwa kwa wafugaji na kwa Taifa. Serikali inao wajibu mkubwa wa kutoa fidia kwa wafugaji na hilo linawezekana tu kwa kutenga Mfuko Maalum wa Taifa kwa ajili ya kuwafidia wafugaji mifugo yao kutokana na majanga kama ukame na ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu unaweza kuanzishwa kwa mtindo ule ule wa bima ya magari, nyumba na kadhalika. Kama kila kichwa cha ng’ombe kitatozwa shilingi elfu moja kwa mwaka, mbuzi shilingi mia tano, sungura, bata, kuku na kadhalika, shilingi mia mbili kila mmoja, nguruwe shilingi mia tano, ninaamini zitapatikana fedha nyingi za kuunda Mfuko wa Fidia na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama jambo hili haliwezekani leo, naomba Serikali ikae ijipange haraka sana ilete mabadiliko ya Sheria hii au ilete Muswada mpya wa kuunda Mfuko huu muhimu kwa ajili ya kuwalinda wafugaji mara wapatapo maafa ya ukame, ugonjwa, wizi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya mifugo hasa maziwa, yanaweza kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kama Serikali italeta mbegu bora, chakula bora, madawa na soko la uhakika kwa maana ya viwanda vya kusindika maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuthubutu inawezekana. Naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia muda huu kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu muhimu sana. Nina imani sheria hii ikitekelezwa vizuri, Serikali itaongeza pato lake kupitia mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa kazi ya kutafiti iwe inachukua muda mfupi sana na matokeo ya tafiti yawe yanafanyiwa kazi mapema ili faida yake iwe inapatikana mapema; mfano, madume ya kisasa kupandishwa ili kupata machotara ambao wana soko kubwa Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuanza kujenga vituo vya kusindika maziwa, nyama na kuwamba ngozi kwenye vijiji vya wafugaji; mfano, Kituo cha Kusindika Maziwa na Kuwamba Ngozi kilichopo Kijiji cha Musungua, Tarafa ya Sepuka, Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Ili vituo hivi viwe na tija ni vyema Serikali ipeleke wataalamu wa kutosha, vitendea kazi na fedha za uendeshaji.

Hii itasaidia vituo kuwa na utendaji wenye tija kwa lengo la kuinua pato la wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusaidia ufugaji ni vyema Serikali iwe na maeneo kila Kijiji ya kulishia mifugo yetu na malambo kwa kunyweshea mifugo. Hii itasaidia mifugo yetu kuzaana kwa wingi pia itanenepa na kuongeza bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kufurahisha sana kwani masoko ya nyama sasa ni mengi hivyo ni vyema Serikali kuboresha miundombinu ya usindikaji wa nyama na maziwa ili yaweze kuwa na kiwango cha Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazipongeza Ranchi za Serikali ambazo zinatumika kutunza mifugo ambayo hutumika kusindika nyama kwa ajili ya kuuza nchini na nje ya nchi. Ni ukweli usiofichika bado haijaonesha kuongeza pato ipasavyo. Hivyo ni vyema maelekezo ya tafiti yafuatwe ili kuinua Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumaliza mchango wangu kwa kuunga mkono Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania wa Mwaka 2011. Ninawaomba na Wabunge wenzangu wauunge mkono. Ninategemea sana utekelezaji wenye tija wa Muswada huu.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia katika Muswada huu muhimu.

Mheshimwia Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo haisimamiwi ipasavyo. Kwanza, wafugaji wetu nchini wamekuwa hawatengewi sehemu maalum za kulishia mifugo yao. Wamekuwa wakinyanyaswa kwa kuhamishwa hapa na pale bila makao maalum ambapo hupelekea kukumbwa na migogoro kati ya wakulima na wafugaji kutokana na kuvamia maeneo ya wakulima na kulishia mifugo yao.

Serikali iliangalie hili sana ili kumaliza ugomvi huu ambao umekuwa wa kudumu kila Mikoa yenye wafugaji ili kufanya sekta hii ipendwe na Watanzania na kwa manufaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viongozi wamegeuza wafugaji ni sehemu ya kujipatia kipato kwa ujanja kwa kuwatoza kodi za mifugo na wanapochelewa kulipa, viongozi hao kama Wakuu wa Wilaya, baadhi hunyang'anya mifugo kama ng'ombe na kuuza nchi jirani kwa manufaa yao binafsi. Huku ni kuwajenga wafugaji au kuwadididimiza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mipaka rasmi kwa wafugaji ili waelewe mipaka na maeneo yao kuepuka wafugaji hawa kuingiza mifugo yao katika Hifadhi za Taifa ambako wafugaji wengi wamepata hasara ya mifugo yao kupigwa risasi na askari wa wanyamapori.

Serikali iisimamie Sekta hii ipewe kipaumbele kama ilivyokuwa Sekta ya Kilimo kwa kuipa ruzuku iweze kuleta maendeleo ya kweli kutokana na mifugo kama ng'ombe, samaki, nyuki, mbuzi na kadhalika. Pia wafugaji wapatiwe madawa waweze kukabiliana na magonjwa na kuzalisha maziwa kwa wingi na kupata masoko yaliyo bora hata nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa uhai na afya yangu. Pili, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara hii, kwa kazi zao nzuri za kila siku. Tatu, ninamshukuru Waziri, kwa kuleta Muswada huu Bungeni ili uweze kujadiliwa na kulata faida kwa Wananchi (Wafugaji, Wakulima, Wafanyabiashara na Wananchi wengine Tanzania nzima).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwamba utafiti utakaofanywa utalenga juu ya malisho na maji kwa mifugo. Ni vizuri utafiti ufanywe ili wafugaji waweze kuwa na mifugo watakayomudu, mifugo michache itakayonufaika, lakini mazingira nayo yatahifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni muda mwafaka wananchi wapewe elimu juu ya ufugaji wenye tija ambao utazingatia uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mkoa wa Rukwa umevamiwa na wimbi la wafugaji wa ng'ombe kutoka Mikoa ya Shinyanga na Tabora. Wafugaji hawa wameendelea kukata misitu kwa kiwango kikubwa, hali ambayo itapelekea jangwa Mkoani Rukwa na hivyo mvua za uhakika na nyingi zitakoma, kutakuwa na ukame wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya za Nkasi, Mpanda na Sumbawanga, zimeanza kuathirika kwa kiwango kikubwa sana na wimbi la wafugaji wahamiaji/wavamizi. Rukwa siyo ile ya zamani inayofahamika yenye neema. Hofu yangu ni kuwa mika si mingi kilimo Rukwa kitashuka sana na Rukwa haitakuwa tena miongoni mwa Mikoa Mikuu (*The Big Four - Five),* inayozalisha na kulisha nchi na hata nchi jirani zetu za Zambia, DRC na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii itakapopitishwa basi ifanyiwe kazi ili wafugaji waweze kusaidia viwanda vifufuliwe ili mifugo hii ya ziada iweze kuuzwa na kuchinjwa na nyama na mazao mengine yauzwe ndani na nje. Hii ita-*stabilise* uharibifu unaofanywa na mifugo maeneo mbalimbali hususan Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii itakapotekelezwa vizuri, ugomvi kati ya wakulima na wafugaji utakoma, patakuwa na *harmony* kwani hawa wawili wanategemeana. Mfugaji anamtegemea mkulima kwa mazao ya chakula kama

mahindi, maharage na kadhalika lakini mkulima naye anamtegemea mfugaji kwa kitoweo kama nyama, maziwa, ngozi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja katika misingi ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni dhahabu inayotembea juu ya ardhi. Mifugo ni mali, ni chakula, ni fedha na inakidhi mahitaji muhimu ya binadamu hususan Wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha asilimia 40 ya Watanzania wanategemea mifugo na mazao yake wakiwa ama *pure pastoralists* au *agro-pastoralists* na soko la ndani ni kubwa kuliko la nje. Soko la nyama choma likiongoza katika Soko la Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwekezaji katika Sekta hii ni mdogo sana; ni Serikali pekee ndiyo inahangaika na Sekta hii ambayo nayo haifanyi vya kutosha. Wafugaji wameachwa washughulike wenyewe na ufugaji wa asili usiokuwa na tija stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa mifugo, malisho ya mifugo, mifumo ya wafugaji na kadhalika, Sheria hii itafanya mifugo itambuliwe na kuthaminiwa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua frusa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa siku ya leo na pia kwa kunipa nafasi kuchangia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania wa Mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii baada ya kupitishwa italeta manufaa makubwa sana katika Sekta ya Mifugo nchini, itatoa mamlaka ya kisheria kuundwa kwa Chombo, Bodi na uendeshaji wa Taasisi hiyo. Malengo ni kuboresha mifugo nchini ili Sekta hiyo pia ichangie Pato la Taifa na kuboresha maslahi ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali, baada ya Sheria hii kupitishwa iwe makini na itoe fedha ya kutosha kuimarisha TALIRI. Mazoea ni pesa zilizoahidiwa katika utafiti hazifiki kwa kiwango na wakati. Pia utafiti mwingi uliofanyika hapa nchini, matokeo yake hayawafikii Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishauri Serikali iangalie namna ya kuipa Wazara ya Mifugo, Sekta ya Utafiti, *Vote* katika bajeti. Kwa sasa ni vigumu kuchambua pesa za Maendeleo ya Sekta na ile ya mshahara na matumizi ya kawaida, tunaona bajeti kubwa kumbe asilimia 95 ni mshahara na pesa ya kuendesha Ofisi ni asilimia tano kwa maendeleo kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri katika kuundwa kwa Bodi ya TALIRI ni vyema ateuliwe mwakilishi wa wananchi (Mbunge), awe katika Bodi, mwenye uzoefu na sifa ya Sekta hiyo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu pia ni tafiti katika Sekta hii ifanyike zaidi panapowezekana katika maeneo ya wafugaji ili wapate uzoefu na waone matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu, kwa kunipatia nafasi kuchangia katika Bunge hili kwa maandishi. Pili, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa

Mifugo na Uvuvi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wananchi wa Morogoro hasa wanawake na ninawapongeza Wananchi wa Mkoa wa Iringa kwa kazi zote wanazozifanya hasa za kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ni muhimu sana na umeletwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitisha Muswada huu na kupata Sheria ya kuanzisha Taasisi hii ya Utafiti, itasaidia sana katika Tafiti kama ufugaji wenye tija; uzalishaji wa mifugo bora; malisho; vyakula vya wanyama *(Consentrates – feeds);* mazao ya mifugo; na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu wa sayansi na teknolojia, Muswada huu umekuja wakati mwafaka. Kwa wakati huu ufugaji katika nchi yetu asilimia 98 ni wa asili. Kwa kupitia katika Taasisi ya Utafiti, ufugaji wa tija utabainika na tutaweza kuendesha ufugaji wa kisasa na wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia watafiti, wafugaji na wadau wengine katika ulimwengu wa kisasa.

- Tafiti ni vyema ziwafikie wafugaji, wananchi na wadau wengine wote.

- Tafiti ni vyema zifanyike katika maeneo husika *(On Farm Research).*

- Tafiti zitokane na matakwa ya wananchi/wafugaji *(Demand Driven Research);* yaani tafiti ziguse hasa matatizo ya wafugaji au wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Muswada ujadiliwe na kupitishwa, utaratibu ufuatwe mpaka kupata na kupitisha Sheria kwa manufaa ya wadau na uchumi wa nchi yetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Rais wetu, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuunga mkono na kusukuma ufugaji Tanzania na hasa kutaka uwe wa tija na wa kisasa pamoja na viongozi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii.

**MHE. PETER. M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuwasilisha Muswada huu kwa wakati huu pamoja na ukweli kwamba Muswada huu ungekuwa umewasilishwa mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ukipitishwa utaleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Mifugo na kuwa na mifugo yenye tija zaidi *(livestock modernization)*. Mageuzi makubwa katika Sekta ya Mifugo yanawezekana tu kwa kuwekeza katika utafiti wa changamoto zinazoikabili sekta hii. Hili linawezekana kupitia taasisi ya utafiti wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya sasa kuna vituo vingi vinavyofanya utafiti katika Sekta ya Mifugo kama vile Mpwapwa, Mabuki, *ADRI, VIC, CVL* na kadhalika. Napendekeza vituo vyote hivi viwe chini ya *TALIRI* badala ya kuwa na taasisi mbili zinazofanya kazi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo ya mabadiliko, tafsiri ya maneno yaliyowasilishwa na Serikali, neno *"centre"* lisomeke *"means a livestock Research Centre established under Section 6"*. Maneno "*or deemed to have been established"* yaondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi. Wingi wa mifugo hiyo itakuwa ni bora zaidi kama mifugo hiyo itakuwa bora. Ubora wa mifugo unapatikana kutokana na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili utafiti uende, lazima taasisi hiyo itakayoundwa iwe na fedha za kutosha za kuwezesha kufanyia utafiti. Uzoefu uliopo katika suala la utafiti unaonyesha kuwa fedha zinazotolewa ni kidogo kiasi ambacho hakifiki hata asilimia moja ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Taasisi hii iweze kufanya kazi ipasavyo, ni vyema uundwe Mfuko wa Utafiti wa Mifugo. Kwa kutegemea fedha inayotolewa na Seriikali kwa ajili ya utafiti, basi uwepo wa chombo hicho hautakuwa na maana yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kifungu cha 25(2), Taasisi inaweza kununua kwa mtu yeyote utafiti ambao umefanywa ili umiliki wa utafiti huo uwe mali ya Taasisi. Je, kama mtu huyo ni mfanyakazi wa Taasisi, pia itabidi utafiti huo ununuliwe na Taasisi? Kama siyo hivyo: Je, hawa wafanyakazi watakaovumbua jambo kubwa katika mifugo watapatiwa motisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo moja la nchi yetu katika kutunga sheria mbalimbali ni kutohusisha uwepo wa sheria, utekelezaji wake na gharama ya utekelezaji wa sheria yenyewe. Matokeo yake sheria inapitishwa lakini utekelezaji wake unakuwa haupo. Mfano hai upo kwenye Muswada huu. Kuna mambo mbalimbali yanayohitajki gharama ili sheria iweze kufanya kazi. Je, Wizara imejipanga vipi katika utekelezaji Muswada utakapopita kuwa sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba kuwe na *linkage research* (utafiti) na *technology transfer.* Ni lazima kuwe na uhusiano wa karibu kati ya *agricultural communities,* Serikali na *funding agencies.* Ni lazima kuwe na uhusiano wa karibu na vyuo vingine ambavyo vinajishughulisha kwenye *livestock research*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *funding* kwenye mambo ya utafiti ni changamoto kubwa kwenye vyuo (vituo)vyetu vya utafiti. Ninashauri njia mbalimbali zitumike ili kuhakikisha fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti zinapatikana. Ni lazima Taasisi iwe na sera ambayo italazimisha watafiti kwenye *livestock* kutafuta *funds* kutoka sehemu mbalimbali. Kwa mfano, Serikali, *private funding sources, corporate and foundation grants* na kadhalika. Vinginevyo, kama Taasisi hii itategemea fedha kutoka Serikalini tu, itashindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mfano mzuri wa kuigwa ni wa Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *capacity building,* kama tunavyojua, vituo vyetu vya utafiti wa mifugo vina uhaba mkubwa wa watafiti. Kwa hiyo, nafikiria kazi moja ya taasisi hii iwe ni kutayarisha watalaam kwenye fani hii.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hii Taasisi tunayoiandikia Sheria hivi sasa, Makao Makuu yake yanatarajiwa kuwa wapi? Ni vigezo gani vitatumika kupata Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, endapo Sheria hii itapitishwa na Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo pendekezo la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo iliyopo Mpwapwa hivi sasa, kuwa Chuo Kikuu Kishiriki *(Affiliated University)* chini ya Chuo Kikuu, Sokoine Mkoani Morogoro. Je, pendekezo hili, ambalo nina imani kwamba liko katika utekelezaji kupitia ngazi za juu, utekelezaji

wa hatua hii ya maendeleo utakuwaje kwa kuzingatiwa uanzishaji wa Taasisi hii mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Mpwapwa kina mashamba matatu kwa ajili ya utafiti. Moja ya mashamba hayo, lipo shamba la Kiboriani lenye hekta takribani 1,500, lina mgogoro wa ardhi hivi sasa, kati ya Chuo cha Utafiti na wananchi wa Kijiji cha Kiboriani. Tatizo hili hivi sasa liko Mahakamani. Wizara itasaidia vipi mgogoro huu wa ardhi ufikie mwisho na kwa busara kubwa bila ya kuleta mapambano ya Chuo cha Utafiti pamoja na wananchi ili tuepuke mapambano ya Serikali na wananchi?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umekuja kwa wakati muafaka japo umechelewa sana, kwani ungeshakuwepo, ungesaidia sana Sekta ya Mifugo. Kwa kuwa, sasa Muswada huu utapitishwa na Bunge hili Tukufu, ninaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

(a) Serikali iboreshe ranchi za Taifa ili wafugaji wengi wapate nafasi katika ranchi hizo, badala ya kuacha Kitengo hiki kwa watu wachache;

(b) Serikali ianzishe viwanda vikubwa vya kutumia rasilimali ghafi ya ngozi, ili zitumike hapa nchini badala ya zao hili kupelekwa nje ya nchi;

(c) Serikali ianzishe miundombinu ya kukusanya maziwa katika kanda za wafugaji, ili hayo maziwa yafikie soko kwa uhakika na soko la ndani likijaa tusafirishe nje ya nchi;

(d) Serikali ianze kupunguza kasi ya kuingiza nyama toka nje ya nchi ili zao la nyama lisindikwe hapa nchini;

(e) Katika masoko yatakayoanzishwa, Serikali iwape vipaumbele wazawa na Watanzania wa ndani kuliko kuwapa nafasi kubwa watu kutoka nje; na

(f) Serikali ianzishe utaratibu wa kuwapatia mikopo midogo midogo wasindikaji wa mazao ya mifugo ndani ya nchi ili kupunguza tatizo kubwa la ajira linalolikumba Taifa letu hivi sasa.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Namba 7 ya 1986, Kifungu cha 5 (1), iliyoanzisha *COSTECH* inaeleza majukumu ya Tume hii kama Mshauri Mkuu wa Serikali, hususan kwa masuala yote yanayohusiana na tafiti za maendeleo ya teknolojia nchini. Kwa maoni yangu, nashauri Serikali iitumie Tume hii katika kufanya tafiti zote zinazohusiana na masuala ya mifugo kwa kuwa, tayari Serikali ilisharidhia kuipa 1% ya mapato yote ya nchi ili kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo, napingana na Muswada kwa kutaka kutoa ruzuku kwa Taasisi zilizoongezwa na Serikali. Naungana na maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba, kwa kufanya hivyo ni kuiongezea Serikali mzigo usiobebeka kwa kutoa fedha kwa taasisi hizi. Ikumbukwe kwamba, taasisi zinaweza kijitegemea kwa kufanya tafiti za kisayansi na kujiendesha zenyewe bila kutegemea ruzuku toka Serikalini. Uzoefu unaonyesha kwamba, taasisi nyingi zinazopokea ruzuku Serikalini, hukosa ubunifu na kubweteka zikitegemea pesa za ruzuku na hii inakuwa maendeleo ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Kifungu cha 6 (1) cha Muswada, kinachopendekeza kuwa: *"Waziri ataanzisha Vituo kadhaa vya Taasisi kwa kutekeleza kazi za Taasisi kama itakavyohitajika, baada ya kushauriana na Bodi."* Kifungu hiki kinabidi kuangaliwa kwa makini, kwani kumekuwepo na matukio mengi ya kunyang'anyana ardhi kati ya wakulima na wafugaji, kwani ardhi iliyopo humilikiwa kimila na hivyo Waziri

au Bodi, wanatakiwa kufanya utafiti wa kina na kujiridhisha kwamba, ardhi ipi itumike kwa malisho na ipi kwa kilimo, baada ya kuwashirikisha wananchi wanaoishi katika eneo husika, ili kuepusha migogoro na mapigano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 27, kinachompa Waziri anayeshughulika na masuala ya mifugo kwa kushauriana na Bodi ya wadhamini kupanga marupurupu na posho za Wajumbe wa Bodi. Naungana na maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba, Kifungu hicho kiondolewe na Hazina itoe utaratibu mzuri ambao utakuwa na mfanano wa malipo kwa Wajumbe wa Bodi zote, kwa taasisi au Wakala wa Serikali, ili kuondoa manung'uniko miongoni mwa Wajumbe wa Bodi fulani kulipwa zaidi kuliko wengine. Hii itasaidia kuinua morali ya Wajumbe wa Bodi na kuwa Wabunifu zaidi na hivyo kuinua tasnia ya ufugaji wa mifugo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii ya pekee kuchangia kwenye hoja hii iliyopo mbele yetu, ambayo kwangu, kwa Wizara pamoja na Tanzania kwa ujumla ni hoja ya muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza, kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuwa hapa, lakini pili niishukuru familia yangu, wapiga kura wangu wote Kiteto, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wataalam wa Wizara, Wadau, pamoja na Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na kwa kuzungumza, kwa ushirikiano waliotupa katika kuandaa na hata kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pole kwa kila Mtanzania, kwa Taifa kwa ujumla, kwa misiba iliyofululiza ambayo imetufanya tuwapoteze watu ambao wamekuwa wa muhimu

sana katika Taifa letu na wameshika nafasi za juu kwenye uongozi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwanza naunga hoja mkono Muswada huu kama wengi waliochangia walivyosema umekuja kwa wakati muafaka, wakati ambapo kinchi tunaongelea kuleta mapinduzi ya mifugo. Pia kama wengi walivyosema maendeleo ya mifugo bila utafiti wa kina katika sekta ya mifugo kwa kweli ni ndoto. Kwa hiyo nadhani tunajipanga vizuri zaidi kusudi tuweze kutekeleza azma yetu hiyo ya kuleta mapinduzi ya mifugo. Tayari kuna uzoefu wa kutosha kwenye Kituo hiki cha Utafiti wa Mifugo, Kituo cha Taifa ambacho Makao yake yamekuwa Mpwapwa. Kwa njia hii mengi yamefanyika na kwa uhakika kwa kupitisha sheria hii na kuunda taasisi tunaona kwamba manufaa mengi yatakuwa kwa kweli yamepatikana.

**MWENYEKITI:** Kwenye hilo la Makao Makuu kuwa Mpwapwa hebu rudia tena.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Najua wewe ni mdau, lakini niseme kwamba uzoefu tangu mwaka 1947 umekuwa ukitoa Mpwapwa na umetumika kwa kweli kwa manufaa ya watu wengi wadau wa ufugaji kila kona ya Tanzania wamenufaika na kazi nzuri ambayo imefanywa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia wametoa hoja nyingi, lakini nipitie tu chache zile ambazo nitaruhusiwa na muda. Wengi wamegusia hoja ya umuhimu wa mifugo nchini Tanzania, moja katika kuondoa umaskini, lakini la pili, ajira na tatu, mchango wa mifugo kama si kwenye *GDP* lakini kwa uhakika katika lishe na maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Christine Ishengoma, Mheshimiwa Masele, Mheshimiwa Profesa Peter

Msolla hawa wote wameongelea sana nafasi ya mifugo kwenye Taifa letu na haya kwa kweli yameelezwa vizuri katika Muswada huu hasa katika kifungu kile cha tano kuanzia ile (a) mpaka (s). Kwa uhakika ni tafsiri iliyo halisi ya Sera yetu ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006.

Hoja nyingine iliyogusiwa na wengi kwa kweli ni nafasi ya utafiti katika kuboresha mifugo kumekuwepo katika nchi zilizoendelea hata tukiongelea mifano kama ya Botswana kwa uhakika tunakuta wenzetu waliweza kuunga vizuri matokeo ya utafiti na mazao ya mifugo na ndiyo maana wameweza kuboresha mazao hayo. Hii pia imeongelewa bado katika kifungu kile cha tano hasa katika kuelezea majukumu na kazi za taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamechangia suala nzima la manufaa ya kuunda taasisi kama kuunda *TALIRI* pamoja na yale yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wangu asubuhi hii kwa uhakika suala la maamuzi ya haraka litaweza kutendeka kwa sababu ya kuunda taasisi hii, lakini utafiti pia wa kupata msukumo na kupata rasilimali za kutosha zaidi kuliko ilivyo sasa. Ushirikiano wa taasisi hii pamoja na taasisi nyingine za utafiti ndani ya nje ya nchi, ushirikiano huu ni rahisi uboreshwe lakini pia utakuwa na tija zaidi na maslahi ya watumishi kwa uhakika yatakuwa bora kwa sababu kama chombo ambacho kitakuwa ni sehemu ya *autonomies***,** hawa watakuwa na uwezo wa kuajiri, kuendeleza na kudumisha rasilimali watu katika taasisi hiyo.

Lakini pia kwa kuwa mpango utakuwa ni kuunga *performance* pamoja na kupanda cheo kwa wahusika, watu watafanya utafiti wa kina na wataandika. Kwa njia hii watapanda vyeo, kwa hiyo hakutakuwepo na watu wa kupanda vyeo tu wanapoketi, nadhani kutakuwepo zaidi na *incentives* kwa watu kufanya kazi ili waweze kupanda vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya nne, imeelezewa na Wabunge, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Telele, Mheshimiwa Christine Ishengoma, pamoja na Mheshimiwa Ester Bulaya. Hawa wote wameongelea suala zima la uwekezaji ambao ni mdogo katika sekta ya mifugo. Kwa sababu hii ndiyo maana jitihada zinafanyika ili kuweza kupanua uwezo wa taasisi hii kupata fedha zaidi na mfano tayari kwa kipindi hiki tunachoongelea sasa, wakiwa bado hawajawa taasisi kamili wameweza kupata bilioni tatu nukta moja kwa mwaka 2011/2012 kwa ajili tu ya utafiti. Pesa hii imetoka *COSTECH* kama sehemu ya zile bilioni 30 ambazo Mheshimiwa Rais alielekeza kwamba ziende kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, ni suala zima la kujaribu kuwa na uratibu wa karibu kati ya Taasisi inayopendekezwa kuundwa na sheria hii pamoja na taasisi nyingine ambazo zimekuwa pia zinafanya utafiti nchini. Suala la Maabara kuu ya Kitaifa limetajwa, lakini pia *VICs* ambao ziko katika kanda zetu na tayari pamoja na kwamba hawa nao wamekuwa ni wakala, lakini bado watashirikiana kwa karibu kuratibu hasa katika masuala yale yanayogusa magonjwa ya wanyama kwa sababu hili ni eneo lingine litatazamwa kwa karibu sana na taasisi inayoundwa.

Mheshimiwa Aloyce Malocha, ameongelea sana pamoja na Wabunge wengine kwamba lazima utafiti ulenge changamoto na mahitaji yetu ya sekta ya mifugo katika nchi. Kwenye ngazi ya Taifa, ngazi ya kaya na ngazi ya mfugaji mmoja mmoja. Niseme tu kwamba tayari katika kifungu cha 5(1) tayari Muswada umechukulia haya maanani na yapo kwenye Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya saba, tayari imegusiwa na Wabunge kama Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora na lenyewe linafana na hili hili la *VICs*, kuna shughuli ambazo zinafanyika za kiutafiti tayari Tabora na

kumbe Mheshimiwa Mbunge asiwe na hofu kwa sababu haya yatachukuliwa kwa njia ya uratibu na Taasisi hii tunayoipendekeza. Tayari kama nilivyosema katika kifungu cha 5(1) haya yameshawekwa kwenye Muswada.

Waheshimiwa wengine wameongelea sana kama hoja suala la kwamba Makao Makuu ya Taasisi haya yawe wapi. Wewe Mwenyekiti ni kati ya watu waliopendekeza kwamba yabaki pale ilipoanza kwa maana ya Mpwapwa, lakini Mheshimiwa Gregory Teu na yeye pia amekazia hilo na niseme kwenye Muswada, tayari ufafanuzi umeshatolewa na hata katika Muswada huu imeelezwa kwamba Mpwapwa kama itabaki kama kituo, Makao Makuu ya Taasisi Kitaifa lazima jitihada zifanyike kuhakikisha kwamba kuna kutenga kusiwepo na kuingiliana kwa majukumu kati ya taasisi kwa maana ya Makao Makuu na pia kituo cha Mpwapwa ambacho kimekuwa kinafanya kazi kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine pia imetolewa na Mheshimiwa Teu na kukazania kwamba mahusiano ya taasisi inayoundwa pamoja na vyuo vingine vya elimu ya juu hasa ametoa mfano wa *SUA*, lakini pamoja na taasisi nyingine kwamba kuwepo na ushirikiano wa karibu. Hili limeshazingatiwa kama nilivyosema katika kifungu kile cha tano kinachoongelea jinsi Taasisi hii itakavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoibuliwa na Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Mahenge pamoja na wengine ni suala zima la upatikanaji wa mbegu kwa maana ya mifugo hasa aina ya *friesian* lakini pia mbegu za malisho. Kumbe moja katika malengo ya taasisi kama ilivyopendekezwa na Muswada ni kuhakikisha kwamba utafiti wa kina utafanyika, mbegu zile zinazopatikana zitaboreshwa lakini pia zitakuzwa na kupatikana kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Cheyo, amezungumzia suala la msingi hapa kwamba kuna kasumba

kidogo inayomtazama mfugaji kama mtu mwenye matatizo na mifugo yake ni matatizo, lakini akapendekeza kwamba badala tu ya kumuona kwamba mfugaji kakonda, ng'ombe kakonda, niseme tu kwamba utafiti utakaofanyika utasaidia sana kubainisha *stereotypes* pia kupendekeza aina nzuri ya elimu kwa umma ili kuweza kuondosha tatizo hili ambalo kwa kweli ni tatizo la kimtazamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongelea pia bado suala zima la kugeuza malisho na kufanya kuwa ni maeneo ama ya hifadhi na kwa kiasi kikubwa malisho yamechukuliwa na maeneo kadhaa ama kwa matumizi mengine. Lakini niseme Muswada unaopendekezwa huenda utekelezaji wake Mheshimiwa Cheyo utakwenda sambamba na utekelezaji wa sheria nyingine ambazo zipo na hasa nikumbushe zaidi ile Sheria namba kumi na tatu (13) ya mwaka 2010 tuliyoipitisha kwenye Bunge hili inayoongelea kulinda maeneo ya nyanda za malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni fedha zaidi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mfuko upo wa kutosha kwa kazi za Taasisi, ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Cheyo, tutauchukua kwa uhakika, lakini tayari mawazo yameanza kutokea ili kuwa na namna ya kuwa na mfuko na maalum kwa ajili tu ya kuhakikisha kwamba fedha ziko za kutosha kwa ajili ya shughuli za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho nitakayoielezea kwa ajili ya muda imetolewa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Yeye ameongelea vituo vingine vya utafiti, kwamba mkazo kwa mtazamo wetu utakuwa ni uboreshaji wa vituo vilivyopo, lakini pale panapohitajika maana mahitaji yanazidi kukua, vituo vipya vitafunguliwa pale ambapo ikionekana kwamba kati ya hivyo vilivyopo hakuna kituo kitakachoweza kuwahudumia wafugaji na wadau wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu, nikushukuru tena, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote walioko hapa na waliochangia kwa maandishi ambao watatambuliwa na Mheshimiwa Waziri. Lakini nimalizie tu kwa kushukuru tena na kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ole Nangoro, sasa nitamuita Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Dokta Mathayo David Mathayo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala*, mwingi wa rehema kwa kunijali afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu baadhi ya hoja za Wabunge waliochangia Muswada huu wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania yaani *Tanzania Livestock Research Institute Act*, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa michango yao katika kuboresha Muswada. Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara yangu, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na wataalam wote. Kipekee nipende kushukuru ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kushirikiana katika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizo, naomba sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Dokta Titus Mlengeya Kamani, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Daktari Binilith Mahenge, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Ole-Nangoro, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi: Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Christine Ishengoma, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Rachel Mashishanga na Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Ali Hamis Seif, Mheshimiwa Mbarouk Ali, Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mheshimiwa Dokta Hadji Hussein Mponda, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Maria Mfaki, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Sylivester Koka, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Kombo Hamis Kombo, Mheshimiwa Assumpter

Mshama, Mheshimiwa Joseph Kandege, nadhani wamekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kujibu hoja; nitaanza na hoja za Kamati za Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Maoni ya Kamati ni kwamba Serikali iongeze bajeti ya utafiti ili ifikie angalau asilimia moja ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kutekeleza kwa kutenga fedha za utafiti kupitia *COSTECH* ambapo Taasisi za Utafiti wa Mifugo zimepatiwa jumla ya shilingi bilioni tatu nukta moja kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kwamba Serikali ikamilishe Sera ya Taifa ya Utafiti. Sera hii zoezi la kuikamilisha linaendelea kupitia *COSTECH,* kwa hiyo tunasubiri kwamba wanafikia hatua gani kwa *speed* gani kusudi hii sera iweze kukamilika na iweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kwamba utafiti ulilenga kutatua matatizo ya magonjwa, uzalishaji, malisho na maji ya mifugo. Suala hili au hoja hii na majukumu ya taasisi yatahusisha na yamehusisha maeneo haya. Ukisoma kwenye ibara ya 5(1) na aya ya (a) hadi (t) utakuta maelezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *TALIRI,* Serikali iweke utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya ufugaji wenye tija, Muswada huu wa sheria huzingatia hoja hii katika kifungu cha 5(1) aya ya (g). Bodi ya *TALIRI* ihakikishe utafiti unafanyika katika maeneo husika yaani kwa mfano ku-*search* ili kuleta ushirikishwaji wa matokeo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *on farm research* ni moja katika majukumu ya taasisi, kwa hiyo, hilo ni moja kwa moja limekubalika. Hoja ya kwamba Serikali idhibiti uingizwaji holela wa mazao ya mifugo ili kulinda soko la ndani, Sera ya Serikali inatoa viwango vya ada na uingizaji wa bidhaa yaani *import*

*duty* kwa mifugo zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Aidha, uingizaji wa nyama ya kuku na mayai ya kula haujaruhusiwa ili kuzuia mafua makali ya ndege. Najua kabisa kwamba wapo wengine wanavunja sheria wanaingiza mayai kutoka nchi jirani ambayo hayana viwango. Sasa mimi ninachowaomba ni kwamba, maofisa wetu ambao wako mipakani na njiani waweze kutusaidia katika kudhibiti hii. Hakuna kibali chochote kinachotolewa na Serikali katika kuingiza mayai ama kuingiza nyama ya kuku kwa maana hiyo, natoa wito kwa viongozi na watendaji walioko mipakani wahakikishe kwamba bidhaa hizo hazipiti. Kwa sababu hata kama mwingizaji anakuonesha kibali, kile kibali si halali kwa sababu haturuhusu, tumezuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TALIRI*, ihakikishe matokeo ya tafiti yanawafikia wadau. Maoni haya yatazingatiwa, katika utekelezaji wa hayo na kifungu cha 5(1)(g) kwenye Muswada huu kinaelezea masuala ya elimu mafunzo na usambazaji wa taarifa za tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *long title* ya Muswada huu inapendekezwa badala ya maneno *research on livestock production* yasomeke *livestock research.* Ushauri huu umezingatiwa na ukiangalia kwenye jedwali la marekebisho ukurasa wa kwanza utakuta kuna marekebisho haya, tayari tumeshayachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tafsiri ya maneno *laboratory* iwe *facility* badala ya kuwa *institution* katika *definition*. Ipo kwenye jedwali la marekebisho na tumeshafanya marekebisho hayo na *livestock by product* itafsiriwe. Imeshatafsiriwa kwa hiyo inaweza ikaonekana vizuri kabisa katika jedwali la marekebisho.

Pia kwamba *researcher means a person* na siyo *graduate*, ni kweli kwamba *graduate* ni mtu ambaye anamaliza Chuo Kikuu lakini siyo *graduate* wote ambao ni *researcher* na wapo ambao hawajamaliza Chuo Kikuu wana

*certificate* au wana *diploma* au *advance diploma* lakini ma-*researcher* wazuri. Kwa hiyo, kwa maana hiyo hatuwezi kusema kwamba *researcher* lazima awe ni mtu aliyemaliza Chuo Kikuu yaani mwenye *degree*, hapana! Ni mtu yeyote, *a person* na siyo *a graduate. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja kwamba usambazaji wa matokeo ya utafiti iwe mojawapo ya majukumu. Nadhani hili nimeshalisemea kwamba litafanyika hivyo na inaonyesha katika Ibara ya 5(1).

Kuhusu kutoa mafunzo ya utafiti wa mifugo kwa vijana wanaotoka Vyuo Vikuu, hili ni muhimu kwa sababu kwanza wapo wanaostaafu lakini vilevile ni lazima tuhakikishe kwamba wafanyakazi wanakuwepo kuendeleza *research* baada ya wale wengine kustaafu ama kuondoka kazini kwa namna moja au nyingine. Mafunzo ya utafiti yamezingatiwa kwenye kipengele cha 5(1)(i). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja kwamba kuanzishwe mfumo wa kutunza taarifa. Hii imezingatiwa katika Ibara ya 5(1)(k).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine kwamba liongezwe neno *sub region.* Wizara imekubali ushauri huu ila inapendekeza lisomeke *regional* kwa kuwa *sub regional* ni sehemu ya *regional*. Ibara ya 5(1)(n) inaonesha maneno ya *region*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majina ya vituo yabebe majina ya Taasisi yaani kwa mfano, *TALIRI* na *BUKI* au *TALIRI Mpwapwa* au *TALIRI Naliendele*. Wizara imekubali ushauri huu na itazingatia ushauri kuhusu wapi yawepo Makao Makuu ya Taasisi hii. Hatujasema itakuwa wapo lakini tutazingatia kwa kujadiliana na wadau mbalimbali kwamba Makao Makuu ya Taasisi yawe wapi lakini tunatambua kwamba Mpwapwa ni eneo zuri ambalo lina hali nzuri ya kuweza kuwa na sifa kama

hiyo lakini vilevile inawezekana yapo maeneo yenye sifa ama yenye sifa nzuri zaidi ya Mpwapwa. Kwa hiyo, tutayaangalia hayo.

Lakini pia nadhani suala siyo kwamba ni wingi yaani sehemu fulani ina wingi wa mifugo basi tupeleke makao makuu, hapana! Kila mtu atasema tumpelekee Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa sababu Simanjiro kuna mifugo, Mheshimiwa Lekule Laizer atasema na yeye kwake Longido tumpelekee kwa sababu ana mifugo mingi. Mimi nadhani kuna vigezo vingine ambavyo tutavifikiria zaidi.

Liongezwe neno *technical committee* kwenye Ibara ya 7. Ushauri huu tunaukubali na ukiangalia kwenye jedwali la marekebisho utaona maneno haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSTECH* iwe na mwakilishi kwenye *board*. Hili tunalikubali moja kwa moja kwamba *COSTECH* itakuwa na mwakilishi na hii ipo katika Ibara ya 8(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti Mamlaka ya Bodi kuajiri badala ya Sekretarieti ya Ajira, kusema kweli anayefanya mchakato wa kuajiri watendaji ni Sekretarieti ya Ajira kwa mujibu wa *Public Service Amendment Act* namba 18 ya mwaka 2007. Kwa hiyo, wao ndio watafanya kazi hiyo. Lakini anayeandika barua kwamba wewe umeajiriwa kwa *position* hii ni Bodi, Bodi ndiyo itamuajiri kwa sababu ndiyo inahusika na *discipline* ya mfanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia yapo mawazo kwamba badala ya *employ* katika Ibara ya 9(2)( c), badala ya *employ or authorize employment* isomeke *employ or authorize employment and termination of staff.* Wizara imekubali na imeshaweka kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyeo vibadilishwe kwa mfano mwanzo ilikuwa ni *Director* yaani Mkurugenzi Mkuu alikuwa anaitwa *Director* lakini sasa inashauriwa kwamba aitwe

*Director General*. Hili tunalikubali kwamba badala ya kuwa *Director* basi awe *Director General* na vilevile baada ya kushauriana na wenzangu Serikalini cheo cha *Deputy Director* tunakubali kwamba kiondoke kwa sababu kwenye *centers* tukisema Naliendele au Uyole au *West Kilimanjaro* au Tanga kutakuwa na *Directors* wapo kwenye maeneo yale. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba kwa sasa Mkurugenzi Mkuu atatosha kwa sababu watakuwepo ma-*directors* katika maeneo hayo ya hivyo vituo saba ambavyo tunavyo kwa sasa. Kwa hiyo, tumekubaliana na ushauri huo.

Suala lingine ni kwamba ukomo wa kumteua Mkurugenzi Mkuu utajwe. Tunakubali kwamba hatuwezi kuwa tunachagua Mkurugenzi anamaliza miaka mitano halafu tunasema ame-*perform* vizuri tunamchagua tena na mpaka miaka 20, hapana! Akishachaguliwa kwa mara ya kwanza anaweza akateuliwa tena na siyo kuchaguliwa bali ni kuteuliwa na Rais, anaweza akateuliwa tena kwa mara ya pili lakini hiyo mara ya pili ndiyo ya mwisho kwa miaka mitano. Kwa hiyo, akimaliza miaka 10 ameshamaliza muda wake hawezi kuteuliwa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kinga kwa Wajumbe wa Bodi iwe kwa nia njema. Hilo limezingatiwa katika Ibara ya 17.

Majukumu yaliyomo kwenye Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 yajumuishwe kwenye majukumu ya Taasisi, hilo tumelikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *animal welfare*, hiyo ipo katika Ibara ya 18(1)(g) iwe *animal welfare and behaviour.* Hii tumeikubali na tafsiri yake kwa Kiswahili ni ustawi wa siha na hulka za wanyama na hii iko katika Ibara ya 18(1)(g).

Ibara ya 18(2) inasema kwamba liongezwe neno *research ethics* yaani maadili. Ni kweli kwamba *research* zozote ambazo zinafanyika na tafiti zinazofanyika ni lazima zifanyike kwa

maadili na viwango ambavyo vimewekwa na vinavyokubalika. Hii ipo katika Ibara ya 18(2)(a).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo hiyo ya 18)(b) au aya ya (i) badala ya neno *study* liwekwe neno *research output*. Hilo linalibali na tumelikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya *co-researchers* iandikwe *coordinating researchers advisory centres.* Hili nalo tunalikubali.

*Research proposal* iwe pana kama ile ya *COSTECH* au ya *Sokoine University of Agriculture. Research proposal format* inaonyesha maeneo muhimu lakini hata hivyo neno *inter-alia* litaongezwa ili kuonyesha kwamba orodha inaweza kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19(3) inasema kwamba siku 14 za kupitia *research proposals* ziongezwe ili ziwe ndani ya siku 30. Wizara inakubaliana na ushauri huu kwa hiyo itakuwa kwamba ndani ya siku 30 *proposal* iwe imepitiwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20; kifungu namba 21 kiwe namba 20 na kile cha 20 kiwe namba 21. Wizara imekubaliana kutokana na matumizi ya yale maneno kwa hiyo hilo halina tatizo.

Pia kuna suala lingine kwamba kiongezwe kipengele kinachotaja *establishment of Livestock Research Fund.* Hili ni sawa, lina nia njema na kwa kweli ni suala zuri lakini kwa sababu *source of funds* za *institute* hii au za Taasisi hii ni Serikali, vyanzo vya fedha vya Taasisi hii ni Serikali peke yake, rasmi ni Serikali kwa hiyo, tunaona kwamba hili suala tunaweza tukalizungumza baadaye kwenye vikao vya juu zaidi halafu baadaye tukaweza kuleta mabadiliko kidogo ya Sheria ili kusudi tuweze kuli-*accommodate* vizuri kwa sababu linahitaji

kuwe na *objectives* za kuweka pale na itakuwa inafanya kazi gani *specifically*. Kwa hiyo, hili tunaomba kwa sasa lisubiri kwanza kwa nia njema halafu tutalipitia baadaye kwa sababu ya *source* ya *fund* za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti badala ya kuidhinishwa na Waziri iidhinishwe na Bunge. Ni kweli siku zote bajeti zinaidhinishwa na Bunge lakini Waziri anaridhia bajeti ya Idara zote na Taasisi zote kabla hazijaletwa Bungeni na hicho ndicho kitakachokuwa kinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kujitafutia fedha kutoka vyanzo mbalimbali liwe mojawapo ya majukumu ya Taasisi. Hili limezingatiwa katika kifungu namba 26 na 30 cha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa ya utafiti yalenge wafugaji na wadau wengine pamoja na hifadhi ya mazingira. Kifungu namba 5(1)(o) kitaboreshwa ili kuweka bayana manufaa ya utafiti kwa wafugaji na hifadhi za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Waziri mwenzangu lakini yeye ni kivuli ametoa hoja zake na nimeona zipo kama tano ambazo ninaweza nikazitolea majibu kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imesema kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania ni gharama, kwa nini isiwe chini ya Wizara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Taasisi tunayoizungumza sasa hivi itaendelea kuwa Taasisi ambayo ipo chini ya Wizara, haiwezi kuwa inajitegemea kwani ipo chini ya Wizara ila kwa sasa inapanuliwa uwezo wake na kupata vyanzo vingine vya fedha tofauti na hapa ambapo Wizara inaigawia fedha ambazo wakati mwingine hazitoshi katika masuala mazima ya utafiti. Hii ni *autonomies* inapewa *autonomy.*

Suala lingine la pili ni Taasisi kuwa na maeneo makubwa ya ardhi. Maeneo yaliyopo yanahitaka kwa ajili ya kazi za utafiti, pale yatakapoonekana hayahitajiki basi yatapangiwa matumizi mengine ikiwa ni pamoja na kuwapa wananchi lakini hayo yameshafanyika kwenye maeneo mengi tu lakini maeneo mengi yapo kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la tatu ambalo Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani amelizungumzia ni uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, anasema sheria inakinzana na Sheria ya Ajira. Nadhani hili nimeshalijibu kwamba Mkurugenzi Mkuu atakuwa anateuliwa na Mheshimiwa Rais na wafanyakazi au watendaji wengine, mchakato utakuwa unafanywa ndani ya Sekretarieti ya Ajira halafu Bodi inaajiri kwa maana ya kuandika barua kwa sababu wao ndiyo wako *responsible* na *discipline* ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watafiti wanaojigharamia wenyewe wasiadhibiwe kwa sheria kwa sababu kuna sheria inazungumzia kwamba ukichelewa kutoa taarifa kuna adhabu yake ama usipowasilisha kabisa taarifa za mwisho za tafiti kuna adhabu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kifungu namba 22(b) kinazingitia kuwa watakaoadhibiwa ni wale tu waliopewa fedha za Taasisi, huwezi kuadhibu mtu wala hujui *source* za *funds* amezitoa wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za bodi ama posho ziwe sawa kwa Bodi zote. Kwa kuwa kila Bodi huanzishwa kwa sheria yake, suala hili litafikishwa Serikalini ili liangaliwe kwa upana wake. Lakini Waziri na Bodi hawawezi wakapanga bila kushauriana na Msajili wa Hazina kwa maana hiyo hiyo ya kusema kwamba wanaweza wakapewa posho kubwa, si kweli! Haiwezi ikatokea kwa sababu hii siyo Taasisi ya kwanza bali hii ni Taasisi tu ambayo inaanzishwa zikiwepo nyingine

zimeshatangulia na kazi zake wanazifanya vizuri, Wizara kwa kushauriana na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makao makuu ya Taasisi na vituo vya Taasisi, Wizara italizingatia hili. Haya masuala sasa naanza kuzungumza yale ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja ama kwa kuandika ama kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa George Simbachawene amelizungumzia hili, Mheshimiwa Masele, Mheshimiwa Amina Mwidau pia amelizungumzia hili suala la kuangalia vizuri eneo ambalo tunaweka makao makuu ya Taasisi.

Vilevile Waheshimiwa Wabunge, hawa yaani Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Masele, Mheshimiwa Blandes na Mheshimiwa Madabida wamezungumzia suala la wawakilishi wa *NGO* na wafugaji wawepo kwenye Bodi. Ni suala la msingi na mimi nasema ndiyo na lipo tumeshalichukua lipo *considered* kwenye Ibara ya 8(2)(f) inazingatia makundi ya wafugaji na wadau wengine pamoja na wazalishaji na wasindikaji na wafanyabiashara za mifugo na pembejeo.

Kuhusu usambazaji wa matokeo ya utafiti. Kifungu namba 5(g) cha Muswada kimezingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusindika mazao ya mifugo, Taasisi hii ijishughulishe na eneo la viwanda vya kusindika. Kifungu cha 5(1)(a)(ii) cha Muswada huu imezingatia suala la usindikaji.

Mheshimiwa Masele amenikaribisha Shinyanga, ni kweli, mikoa hii ipo mingi ndiyo tunaendelea kuzungumza na tutafika Shinyanga ili tukaone mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Kamani pia wamezungumzia kutenga maeneo ya wafugaji na hii imezingatiwa katika kifungu namba 5(1)(a)(iv) katika Muswada huu.

Mheshimiwa Masele pia amezungumzia masuala ya *database* kwa wafugaji. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa *(NBS)* itaendelea kukusanya na kutunza takwimu za wafugaji, mifugo na mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutatua changamoto za ukoosaafu duni wa mifugo yaani koo za mifugo zile ambazo ni duni, malisho, maji na magonjwa na *embryo transfer.* Hili limezingatiwa katika Ibara ya 5(1)(a) ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu unakinzana na Sheria ya Ajira, hili nimeshalitolea ufafanuzi kwamba Mkurugenzi Mkuu atateuliwa na Mheshimiwa Rais. Hilo limezungumzwa na Mheshimiwa Peter Msolla, Mheshimiwa Amina Mwidau na Mheshimiwa Gosbert Blandes.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya jumla ya utafiti haipo, zoezi la kukamilisha sera hii linaendelea kama nilivyosema kwamba linaendelea na likikamilika basi tutaona matokeo yake.

Shughuli za *CVL* na *VIC*, tafiti za magonjwa ya wanyama zitafanyika katika vituo vya *TALIRI,* magonjwa ya wanyama yatafanyika katika vituo vya *TALIRI* na maabara za Wakala wa Maabara ya Taifa yaani *Tanzania Veterinary Laboratory Agency* na *VIC* zipo chini ya Wakala yaani *VIC* zote zipo chini ya Wakala. Lakini *TALIRI* yaani hii Taasisi ambayo tunaianzishia sheria yake yenyewe hasa itakuwa inafanya tafiti kwa wanyama walio hai lakini *laboratories* zitakuwa zinafanya tafiti zake kwenye maabara kama neno lenyewe linavyosema *laboratories* na *VICs* zitakuwa zinafanya tafiti na pia zitakuwa

zinafanya *diagnosis*. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti yake lakini *at the end of the day* zote zinakutana kwenye utafiti. Kwa mfano, *laboratories* pia zitakuwa zinazalisha chanjo ambazo tutakuwa tunazitumia kwa ajili ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tafsiri ya *livestock* itafsiriwe yaani itoe maana ya wanyama, hii ipo kwenye *schedule of amendment.* Pia mtaalamu kutoka *NIC* awepo kwenye Bodi, hii imezingatiwa kwenye kifungu cha 8(2)(d) kama mwakilishi wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Mpwapwa breed*, Mheshimiwa Kamani alikuwa anaulizia utafiti wa *Mpwapwa breed* unaendelea? Naomba kumjulisha kwamba utafiti huu unaendelea vizuri na ng'ombe hawa wamesambazwa kwa wafugaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini na Serikali imeanzisha kituo cha kusambaza ng'ombe *Sao Hill* Wilaya ya Mufindi.

Mtafiti binafsi matokeo yake yanalindwa vipi? Matokeo ya mtafiti binafsi yanalindwa kwa kuzingatia *interactual property right*. Kuna Sheria inaitwa *Cooperate and Neighbouring Act Cap 218* namba 17 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumtambua pia Mheshimiwa Athumani Mfutakamba na yeye amechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zingine ni za Mheshimiwa Betty Machangu amezungumzia suala la ruzuku kwamba kwa sababu tunatoa ruzuku kwenye maeneo mengine ya kilimo ni vyema pia tukatoa ruzuku kwenye mifugo. Labda nimkumbushe tu kwamba ruzuku inatolewa kwa baadhi ya chanjo za mifugo kama vile za *CBPP* kwa ugonjwa wa mapafu, *rabies* kwa kichaa cha mbwa pamoja na sotoka ya ngozi. Ruzuku hapa inatolewa, lakini pia tunatoa ruzuku kwenye dawa za kuogesha mifugo.

Lakini kwa sababu na mimi nahitaji wafugaji wangu waneemeke, nasema bado tunahitaji kuongeza ruzuku zaidi na kuangalia maeneo mengine ya ruzuku zaidi kwa wafugaji ili tuweze kuwapunguzia mzigo. Ni muhimu sana kwa sababu kama tunavyoona suala la njaa Tanzania lipengua kwa sababu tunatoa ruzuku ya mbolea pamoja na mbegu kwa wakulima waliopo kwenye maeneo ya kuzalisha chakula kwa wingi, basi nadhani hata kwenye mifugo na kwenye uvuvi tukitoa ruzuku tutakuwa tumewasaidia wale kwa sababu wapo watu ambao maisha yao wanategemea kabisa kwenye uvuvi na wapo wengine ambao wanategemea kwenye mifugo kabisa, ambao hawalimi na hata ruzuku ya mahindi haiwagusi, inawagusa labda katika kununua, lakini ile *direct* hawaipati.

Kwa hiyo, hili ni suala ambalo tunaweza tukalizungumza huko baadaye ili fedha zinavyopatikana basi na wafugaji na wavuvi wapate ruzuku ili na wao wajisikie kwamba wanaweza wakajiendeleza vizuri kwa kusaidiwa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uimarishwe Mheshimiwa Betty Machangu amesisitiza kuhusu hilo na ndilo tunalotaka hasa na ndiyo maana tunaunda sheria ya Taasisi hii.

Mheshimiwa John Cheyo amezungumzia utafiti kuhusu malisho ya vyakula vya mifugo. Ushauri huu wa Mheshimiwa Cheyo unakubaliwa hasa ukizingatia pia kuwa anatoka maeneo ya wafugaji. Kwa hiyo, tunalizingatia kabisa.

Mheshimiwa Silvestry Koka ameshauri utafiti uimarishwe. Hili tunalizingatia na kusema kweli ndiyo maana tunasema tunaifanya Taasisi hii iwe ya kisheria kama zile za nchi jirani. Ile ya Kenya ambayo inaitwa *(KARI)* inatambulika kisheria hata Kimataifa. Sasa hata unapozungumza na wenzako wa nchi nyingine wakati mmekaa meza moja, basi mnaelewana kwa sababu Taasisi yako inatambulika kisheria. Lakini ya kwetu

kidogo mambo mengine na *privileges* nyingine walikuwa wanazikosa kwa sababu Taasisi yao haitambuliki kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hii isipotambulika kisheria maana yake hata *research outputs* zitakazotokana na ule utafiti hazitakuwa zinatambulika vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Daktari Pudenciana Kikwembe ameshauri Taasisi ijitangaze. Kwa kweli ametupa wazo ambalo ni zuri sana kwamba Taasisi ijitangaze. Hili litazingatiwa kwamba ijitangaze ili watu wajitokeze kwa sababu unaweza ukawa una kuku unataka wakue haraka lakini unataka utumie njia nzuri wakue haraka au una ng'ombe unataka wakue haraka basi utafiti unaweza ukautumia kwa kutumia chombo hiki na wakaweza kukufanyia utafiti wa chakula kizuri ama cha kunenepesha mifugo yao ama chakula cha kuku na ukaweza kufaidika vizuri zaidi. Kwa hiyo, tukitangaza nadhani Watanzania wengi na wale wa nje ya nchi watatumia tafiti hizi. Kwa hiyo, huo ushauri naukubali kabisa.

Mheshimiwa Murtaza Mangungu amezungumzia bima ya mifugo. Hili la kuifanya Taasisi iwe ya kisheria maana yake ni kwamba ikishaanza kazi sasa kwa kushirikiana na vyombo vya kifedha wataangalia uwezekano wa kuweka bima kwenye mifugo. Nchi kama Botswana wanayo bima kwenye mifugo, lakini tafiti zao pia zipo mbalimbali vilevile na Taasisi zao zile zimekuwa *accredited* Kimataiafa, muda mrefu sana kwa sababu wanauza nyama Ulaya. Lakini na sisi tunaelekea huko huko, maana wenzetu wana ng'ombe milioni tatu tu lakini wanauza ng'ombe kila mwaka na wanawaingizia fedha nyingi sana. Nadhani na sisi inabidi tuelekee huko huko na ndiyo maana tumejaribu kuimarisha utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vifufuliwe. Hilo ni wazo zuri, Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kwa sababu Serikali yenyewe haijengi viwanda. Serikali ilijitoa kwenye

biashara, hatujengi viwanda na hizi ni biashara kubwa. Tunaposema kwamba Taasisi hii itakuwa inafanya mambo mengine kibiashara ni pale ambapo labda inazalisha utafiti fulani, mfugaji anaomba afanyiwe utafiti fulani basi anatoa *royalty* (mrabaha) kidogo kwa ajili ya kuchangia gharama *(cost)* za utafiti kidogo tu kwa ajili ya kui-*sustain* ile Taasisi ili iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali haifanya biashara lakini inatengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wale wanaotaka kuanzisha viwanda ama vya usindikaji, kwa mfano, sasa hivi tunazungumzia kile kiwanda cha nyama cha Mbeya ambacho kinatakiwa kipate mwekezaji. Sasa ingekuwa kwamba Serikali inafanya hiyo kazi, ingekuwa tayari imeshaendeleza hicho kiwanda. Lakini Serikali hatufanyi biashara na ndiyo maana tunahamasisha sekta binafsi. Mzee Cheyo ukisema unataka uingie ubia na Serikali basi unaweza ukaruhusiwa, ama ukatafuta mtu mwekezaji ungekuwa umetusaidia sana. Kiwanda cha nyama Mbeya ni mfano tu, lakini kipo kingine cha Shinyanga na vipo vingine vingi tu ambavyo vingeweza vikasaidia. Lakini Serikali haifanyi biashara na wala haijengi viwanda, yenyewe inaandaa tu mazingira mazuri kwa ajili ya wafanyabiashara kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngozi mbichi kusafirishwa nje ya nchi. Kusema kweli hili ni tatizo, niseme si tatizo kwa sababu tumeruhusu wasafirishe kwa kutozwa asilimia 40, lakini sasa hivi wengine wana-*misuse*. Kwanza wengine wana-*under declare* wanapeleka ngozi nyingi kuliko kiasi wanachokilipa Serikalini. Kwa hiyo, kuna wazo ambalo sasa hivi tunalifikiria kwamba ikiwezekana tuongeze ushuru wa kutoa badala ya asilimia 40 angalau ifikie 90 au tufunge kabisa uuzaji wa ngozi nje ya nchi ili viwanda vyetu viweze kupata malighafi. Lakini ni lazima pia tuweke *control mechanism* kusudi viwanda vya ndani visije vikateremsha bei kwa sababu watu hawa-*export*. Lazima tuweke *indicative price* au tuweke kama *warehouse receipt system* ambayo inafanyika kwenye korosho iweze kutumika pia

kwenye ngozi, tena ngozi haiwezi ikaharibika haraka kama korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza tukasema wanaotaka kununua ngozi waende kwenye Vyama vya Ushirika ili muuza ngozi apate bei nzuri lakini na yule ambaye ananunua ngozi kusafirisha hata kama anataka kusafirisha ashindane kwenye soko la ndani. Najua Mzee Cheyo hapendi hayo mambo ya *warehouse* lakini ndiyo mambo yenyewe ya kuleta usawa kwa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utafiti yatolewe. Hii imezingatiwa kwenye Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Desderius Mipata ameshauri migogoro idhibitiwe. Ushauri huu utazingatiwa na ndivyo tunavyofanya na ndiyo maana Serikali inaendelea kupima maeneo na kuyakabidhi kwa wafugaji ili wasiweze kuingiliana na watumiaji wengine wa ardhi. Serikali inaendelea na imeshapima zaidi ya hekta milioni mbili na inaendelea kuzikabidhi kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Modestus Kilufi ameshauri maeneo ya malisho yatengwe. Hili ni suala ambalo linaendelea na nimeishalielezea.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya amezungumzia utafiti ufanyike kabla ya kuhamisha mifugo. Ni kweli utafiti huwa unafanyika kabla ya kuhamisha mifugo, lakini wafugaji wengine wanakiuka taratibu ambazo zimewekwa, wanatoa ng'ombe kutoka sehemu moja kupeleka sehemu nyingine bila ruhusa na wanapoondolewa wanasema kwamba wananyanyaswa. Ni lazima tufuate sheria za nchi. Huwezi ukapeleka ng'ombe Rufiji wakati huna barua inayokualika kuleta wale ng'ombe pale na hujaomba ruhusa ya kuwapeleka. Ukiambiwa uwarudishe mahali unapowatoa hao ng'ombe usilalamike na utarudisha kwa gharama zako. Ni lazima tufuate taratibu na sheria zilizopo. Huwezi ukasema tu

sasa unapeleka ng'ombe Rufiji kwa sababu kuna eneo. Hapana! Lazima ufuate taratibu zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtanzania anaruhusiwa kukaa na kwenda sehemu yoyote anayotaka lakini asiende kwa kuvunja sheria. Ni lazima afuate sheria. Tunatetea, mimi ni Waziri wa Mifugo na natakiwa nitetee wafugaji lakini siwatetei wakivunja sheria. Wakivunja sheria na mimi nakandamiza, lazima tufuate sheria. Wasihamishe mifugo bila ruhusa maalum na bila kufuata taratibu. Lazima hizo taratibu zifuatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magdalena Sakaya amesema vituo vilivyopo sasa viimarishwe. Kwa kweli tukishapitisha hii *TALIRI* vituo vitaimarishwa kwa sababu hata uwezo wake kidogo utakuwa. Kwa hiyo, vituo vitaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara ya Temeke iimarishwe. Jibu ni kwamba imeshaboreshwa na sasa hivi siyo maabara tu ya kawaida, bali ni Wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla pia ameshauri kwamba tuwekeze kwenye utafiti. Ushauri huu utazingatiwa na vituo vya *CVL* na *VIC* vitakuwa chini ya Wakala ili viweze kufanya kazi kubwa ya uchunguzi wa magonjwa na kutengeneza chanjo ili Taifa lijitegemee kwa chanjo. Kama nilivyosema awali *VIC* na *CVL* zenyewe zitakuwa zinafanya kazi zaidi kwenye maabara, lakini Taasisi hii ya utafiti itakuwa inafanya kazi kwenye mifugo, japo na wao watakuwa na maabara kwa sababu hata hao wanyama (mifugo), wanaugua *east coast fever*, wanaugua *CBPP* ni lazima wachukue *sample* na kufanya *diagnosis* kwenye maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac yeye amaezungumzia kwamba wafugaji watengewe maeneo. Hilo nimeshalijibu kwamba tuna sheria yetu ya Matumizi ya Ardhi na Sheria ya Malisho na Vyakula vya Mifugo.

Mheshimiwa Gosbert Blandes anauliza kama kutakuwa na uwezekano wa mifugo ifidiwe ikifa au tuanzishe mfuko wa kufidia mifugo. Nadhani ushauri huu utaangaliwa huko mbeleni, lakini kwa hali yetu na mazingira ya kufuga na vile ambavyo wafugaji wengine hawataki kuogesha mifugo yao na hivyo kuifanya ife sana, sasa kama watu hawataki kufuata taratibu Serikali haiwezi ikabeba mzigo huo, *unless* kama kunatokea maafa kama ilivyotokea kule Longido, Monduli na Ngorongoro kutokana na matatizo ya ukame. Watu hawakufidiwa lakini walipewa mbegu za kuweza kuanzia kuzalisha tena mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, amezungumzia umuhimu wa kutoa elimu, ushauri utazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Binilith Mahenge amezungumzia mbegu za *Friesian* kupungua na malisho kupungua kule kwenye shamba la Kitulo. Ni kweli kabisa sasa tukishakuwa na Taasisi hii watakuwa na uwezo kidogo kwa hiyo, hata ule uwezo wa kuzalisha mbegu zaidi… maana kituo chetu cha *NAIC* kina uwezo wa kuzalisha mbegu, lakini hata kama mbegu zitahitajika kuagizwa basi tukishakuwa na Taasisi hii kwa kushauriana na mashamba haya basi tutaweza kupata mbegu za kutosha kwa ajili ya maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kuongeza utafiti katika uzalishaji wa malisho ya mifugo *(pasture).* Utafiti katika malisho na wanyama umezingatiwa kwenye Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa kitengo cha *Livestock Research for Rural Development,* hili litazingatiwa katika utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuhusisha wafugaji jirani. Kuhusiana na kuanzisha kiwanda Kitulo, Taasisi itapewa jukumu la kuona kama inawezekana. Lakini kama nilivyosema wanaweza wakaandaa mazingira mazuri ya kupata mwekezaji ambaye angeweza kufanya hii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa William Mgimwa ameshauri kwamba matumizi ya utafiti na vituo vya utafiti viimarishwe. Nadhani ushauri huu nilishauzungumza na utazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephat Kandege ameshauri Serikali itoe ruzuku kwa mifugo. Jibu ni kwamba Serikali itafanya hivyo kulingana na uwezo wa fedha kama ambavyo nimeeleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtambue aliyesoma maoni ya Kamati, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Seleman Jafo. Nampongeza sana, ameiwasilisha taarifa hiyo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kujibu hoja hizo sasa tunaingia hatua nyingine. *(Makofi)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania wa Mwaka 2011 (*The Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011)*

Jina refu la Muswada

*(Jina refu la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila ya marekebisho yoyote)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mapendekezo ninayopendekeza yaingizwe ni

kwenye Ibara 8(2) kuingiza katika *sub clause (g)* maneno; *"a representative from Ministry responsible for Local Government and Regional Administration."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mapendekezo haya ni kwamba kwenye majukumu ya Taasisi hii ni muhimu sana ambayo inakusudiwa kuundwa ya kufanya utafiti wa kuinua mifugo, kukuza uchumi wa nchi na kuongeza ajira kupitia sekta hiyo, ibara ya 5 inayozungumzia kazi za Taasisi, sehemu (f) inasema kwa kushirikiana na wakala wengine wanaohusika, kutoa mwongozo wa kisera kwa mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine kuhusu masuala yanayohusiana na utafiti wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jukumu zito sana. Taasisi hii inakwenda kupewa jukumu la kutoa miongozo ya kisera kwa Serikali za Mitaa, maana yake zile Halmashauri na kadhalika. Tunafahamu kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu kuna mgawanyo wa madaraka baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na hiki ni chombo kitakachokuwa chini ya Serikali Kuu kwa maana ya Wizara yenye dhamana husika lakini kinapewa mamlaka makubwa ya kutoa miongozo kwa Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri. Lakini kwa upande mwingine kazi nyingi za mifugo iwe ni masuala ya majosho ya mifugo, iwe ni masuala ya machinjio kama kule Dar es Salaam na kwinginepo kimsingi ni kazi za Halmashauri. Sasa ili taasisi hii ya utafiti inapofanya kazi zake za utafiti iweze kuzingatia vilevile masuala yanayotokana na Serikali na Halmashauri za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwe na mwakilishi kutoka Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye hii Bodi ili awe kiungo baina ya Halmashauri za Mitaa nchini na taasisi hii inapofanya utafiti wake. Kwa hiyo, ndio msingi wa kupendekeza kwamba kuongezwe hicho kifungu (g) kisomeke; *"A representative from the Ministry responsible for Local Government and Regional Administration."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi ya kitaalam. Idara nyingi za Serikali zinatoa miongozo kwa TAMISEMI, haina maana kwamba kila Bodi inavyoanzishwa basi TAMISEMI wawepo. Mimi nadhani kama ilivyo hii inatosha. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaomba hapa aingizwe Diwani au mtu mwingine asiyekuwa mtaalam. Nimeomba kuwepo na mwakilishi wa Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa kwa maana TAMISEMI. Kwa hiyo, TAMISEMI itakapoteua mwakilishi wake itazingatia vigezo vyote ambavyo vinahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo zito sana kwa sababu Tume imepewa mamlaka ya kutoa miongozo ya kisera kwa Halmashauri. Halafu chombo kinachohusika na Halmashauri na hapa kuna kituko kikubwa kwa sababu gani kwenye hiki kifungu cha nane cha sheria, kifungu kidogo cha pili, kipengele (c) na (d) Wizara inayohusika na mifugo imewakilishwa, mwakilishi wa Wizara husika na mifugo ambalo ni jambo muafaka. Halafu kuna mwakilishi wa Wizara inayohusika na chakula na mazao. Sasa kama katika hii Taasisi ya Utafiti inayohusika na utafiti wa mifugo kumeonekana haja ya kuweka mwakilishi wa Wizara inayohusika na chakula na mazao kinashindikana nini kuweka mwakilishi wa Wizara ambayo masuala yote haya ya mifugo, ng'ombe, migogoro ya ardhi, majosho, utafiti, usindikaji wa nyama, usambazaji wa kuku, sijui na mambo yote yanatekelezwa chini ya Halmashauri za Serikali za Mitaa ni kwa nini Serikali Kuu inaona Serikali za Mitaa hizi si muhimu kwa kiwango hicho hizi Halmashauri wakati kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu ni vyombo ambavyo vina mamlaka na ni vizuri vikawakilishwa na Wizara yenye dhamana ili kukawa na kiungo cha kisera kwenye masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kweli Wizara hili ni pendekezo ambalo lipo wazi sana na ni kwa ajili ya Serikali yenyewe. Wizara ilikubali kuwe na mwakilishi wa Wizara husika ili kusaidia uratibu. Sio Tume itoke ifanye utafiti irudi tena ika-*consult* na Wizara inayohusika wakati ambapo maamuzi yanaweza yakafanywa kwenye Bodi yenyewe inayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri pamoja na maelezo hayo unasema nini?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa mfano wa mwakilishi kutoka kwenye Wizara inayohusika na mazao. Nadhani Mheshimiwa Mnyika anaelewa kabisa mazao ndio chakula cha mifugo, kwa hiyo, ni lazima awepo mwakillishi kutoka kwenye vyakula vya mifugo. Ndio maana ya mahusiano ya *crop production* na *animal production.* Kwa sababu *animals they fit on crops*, ndiyo maana yake. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba ibaki kama ilivyokuwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaotunga sheria ni Wabunge wote tunapiga kura. Sasa nitawahoji ambao hawaafiki mabadiliko hayo waseme ndiyo na ambao wanaafiki waseme siyo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, rudia tena.

**MWENYEKITI:** Maana yake sijaeleweka eeh?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikusaidie tu.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Tuna Muswada ambao umewasilishwa na Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nafikiri ungewaambia kwamba wanaokubaliana na hoja ya Serikali waseme ndiyo na wasiokubali waseme siyo.

**MWENYEKITI:** *Anyway* nitachukua huo ushauri wa Mwanasheria Mkuu ingawa bado hata yenyewe hiyo ni shida kidogo kwa sababu sasa hoja inayoamuliwa ni ile iliyoletwa ambayo hoja hiyo ni ya Mheshimiwa Mnyika na ndiyo inayopigiwa kura. Sasa sina hakika katika hili kama tutafanya vizuri, lakini kwa nia ya kutenda haki tuhoji tu kwa maana ya hali halisi ilivyo, kwa maana ya wanaoafiki msimamo wa Serikali waseme ndiyo na wasioafiki msimamo wa Serikali waseme siyo.

Kwa sauti niliyosikia msimamo wa Serikali umepita. Tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeleta mabadiliko kwenye kifungu cha 8(2) nikipendekeza iingizwe (g) baada ya (h) na yenyewe nilikuwa napendekeza isomeke; *"The Director of National Artificial Insemination Centre."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini ni kwamba katika Wajumbe wa Bodi hii nilikuwa napendekeza awepo Mkurugenzi anayetoka kwenye Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji. Kwa nini nasema hivi kwanza ni kutokana na madhumuni na sababu ya Muswada huo. Ukisoma kwenye ukurasa wa 49 madhumuni ya kwanza inasema ni pamoja na kuainisha majukumu na mamlaka ya taasisi, katika kuhamasisha na kuendesha shughuli za utafiti wa uzalishaji wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukija kwenye ukurasa wa 31(5) kazi za taasisi zitakuwa ni zipi. Ya kwanza inasema ni kuendesha shughuli za utafiti katika:-

(i) Maendeleo ya uzalishaji mifugo na kuhimiza uzalishaji bora. Hii ndiyo kazi ya kwanza ya taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uzalishaji bora tuliundia taasisi ambayo ni taasisi yetu ya Kitaifa *(The National Artifical Insemination Centre)* na ndiyo hawa tu peke yao ambao wanafanya kazi hiyo kwa niaba ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani na niliona ni bora kwamba Mkurugenzi wa Kituo hiki au mwakilishi wake basi awemo ili kuweza kutoa mchango wake mkubwa sana katika kuhakikisha kwamba shughuli ya uzalishaji mifugo kwa njia ya uhamilishaji inafanyika kwa usahihi na mifugo bora inaenea katika Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemwomba Mheshimiwa Waziri alione jambo hili kwamba ni la muhimu sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wa *NAIC* au kiongozi wa *NAIC*, Mtendaji wa *NAIC* yupo chini ya Idara pale Wizarani kwangu na Wizara imeshawakilishwa tayari. Kwa maana hiyo sioni sababu ya kumuingiza humo kwa sababu kwanza hata *representation* ya watu ambao unajua *animal science, veterinary science* kwa sasa wanatosha na ni wengi wanatosha na wote hao wana *knowledge* ya *artificial insemination.* Kwa hiyo, naona kwamba hakuna umuhimu wa kumuweka kwa sababu tayari ile *NAIC* ipo chini ya Idara katika Wizara yangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Blandes kwa ufafanuzi huo wa Waziri bado una neno?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika vizuri kwa sababu pamoja na kwamba kweli Wizara imewakilishwa lakini tuangalie katika Wajumbe hawa kwa mfano mwakilishi (e), huyu tunasema awepo Mkurugenzi wa Maabara Kuu ya Mifugo. Sasa Mkurugenzi huyu hana tofauti kabisa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Taifa. Hapa nazungumzia Mkurugenzi wa Kituo cha Taifa, huyu ni Mkurugenzi katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tatizo kubwa sana la nchi hii ambalo tunalipata ni kuwa na mifugo ambayo haina ubora hata kidogo na kile kituo tunaki-*undermine.* Mimi nilidhani kama ambavyo ameingizwa Mkurugenzi wa Maabara Kuu ya Mifugo ningependa na ningeshauri Mheshimiwa Waziri unikubalie kwa sababu mimi ni mdau mkubwa sana wa mifugo na nimekuwa nikitumia kituo hiki cha *NAIC* na najua matatizo waliyonayo. Nilidhani ni vizuri wakiwemo watatoa mchango mzuri sana katika Bodi yako. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Baada ya maneno hayo Mheshimiwa Waziri unasemaje?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza *Laboratory Veterinary* wanahusika na *research*. Kwanza wanazalisha chanjo, lakini wanashirikiana na taasisi hii ambayo tunaitungia sheria kwa ajili ya kufanya *research.* Kwa maana hiyo katika masuala ya *research* lazima kuna masuala ya *diagnosis,* kuna masuala ya *epidemiology* hawa ndiyo wana mahusiano na kusema kwamba kila Idara iwe na mwakilishi hatutaweza. Lazima tuchukue Idara ambazo ziko kwenye *research oriented veterinary and central veterinary laboratory* inahusika na masuala ya *research* kila siku ya Mungu. Sasa hivi wanashughulikia chanjo ya mdondo, chanjo ya *anthrax*, kwa hiyo wanajihusisha katika masuala ya *research*. Sasa yule wa *NAIC* tayari kuna mwakilishi wa Wizara ambaye atamwakilisha

yeye. Kwa hiyo, hatuoni sababu kwa nini tuwajaze tu hapo kwa sababu wanataka waingie kwenye Bodi, hapana.

**MWENYEKITI:** Tunapiga kura simuoni mwingine, tunapiga kura wanaoafiki msimamo wa Serikali waseme ndiyo, wasioafiki msimamo wa Serikali waseme siyo. Uko peke yako walioafiki wameshinda tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zimap pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mapendekezo ya marekebisho niliyowasilisha ni ya kuomba Bunge lako Tukufu likubali kwamba karibu ya maneno *"shall"* na neno *"appoint"* kuongezwe maneno; *"upon recommendation of the Board."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mapendekezo haya ni kwamba kwa mujibu wa Muswada wa Sheria ambao tulikabidhiwa ilikuwa inasomeka kwamba kifungu cha 13(1) Waziri atateua Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi. Naelewa kwamba kuna mapendekezo ya Serikali mapya ambayo hayapo kwenye mapendekezo ya Kamati, lakini ni jambo jipya

kabisa la kurudisha tena mamlaka makubwa kwa Rais pamoja na mamlaka ya Rais ya kuteua Mwenyekiti wa Bodi ateue vilevile Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitaomba hilo pendekezo la Serikali baadae tupate wasaa wengine wa kulichangia, sasa hivi nizungumzie pendekezo nililoliwasilisha mimi kwa mujibu wa Muswada uliopo hapa mbele. Pendekezo hili ni la kutaka kwamba kabla ya Waziri kuteua apokee kwanza mapendekezo ya majina ya Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi kutoka kwenye Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi sana na hili jambo ni muhimu sana kwa Utawala Bora wa Taasisi zetu na Mashirika ya Umma kwamba Wakurugenzi wakiteuliwa na mamlaka sawa sawa na Mwenyekiti wa Bodi na Wajumbe wengine wa Bodi mara nyingi uwezo wa Bodi kuwasimamia Wakurugenzi huwa unapungua. Lakini mara nyingine vilevile uteuzi umekuwa haufanyiki kwa uwazi sana na kwa ushindani sana. Sasa hii taasisi ni muhimu sana na tumeelezwa umuhimu wake kwamba nchi yetu ni ya tatu kwa mifugo Barani Afrika, lakini bado kuna umaskini kwa wafugaji, taasisi hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ajili ya umuhimu wa taasisi hii napendekeza kwamba kabla ya Waziri kuteua pendekezo litoke kwenye Bodi na hili jambo halitakuwa jambo jipya. Nchi yetu ina Sheria ya Mashirika ya Umma pamoja na kuwa sio taasisi zote za umma ni Mashirika ya Umma, lakini tunaweza tukaiga mfano wa Sheria yetu ya Mashirika ya Umma. Sheria ya Mashirika ya Umma kifungu cha 13 kinasema; *"The Board with the prior concept of the Minister shall appoint Director or Director General on the case may be"* tafsiri yake ni nini? Kwa sheria yetu ya sasa ya Mashirika ya Umma Wakurugenzi wanapaswa kuteuliwa na Bodi, sheria yetu hii inataka kumpa Waziri mamlaka ya kuteua. Sasa hii ni taasisi ni

tofauti kidogo na Mashirika mengine ya umma pamoja ni kuwa ni Taasisi ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ili kuendana na *spirit* hii ya Sheria ya Mashirika ya Umma, Waziri kabla ya kuteua alazimishwe na sheria kupokea mapendekezo kutoka kwa Bodi ili hiyo michango ya Wabunge wengi waliokuwa wanasema kwamba uteuzi uzingatie uwezo, uzingatie vigezo, uzingatie ushindani, Bodi itakapoandaa mapendekezo itazingatia masuala yote hayo halafu itampelekea Waziri, Waziri atateua. Kama Waziri hataridhika na namna ambavyo Bodi imefanya, Waziri ana uwezo wa kukataa uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba pendekezo hili likubaliwe kwa msingi ule ule kwamba uteuzi ufanywe na Waziri kwa sababu Rais ameshateua Mwenyekiti, tumeshampa mamlaka Rais ya kuteua Mwenyekiti, Mkurugenzi ambaye ni Mtendaji ateuliwe na Waziri lakini kwa kupokea mapendekezo kutoka kwenye Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maamuzi kutoka katika kifungu hiki nitaomba maamuzi kuhusiana na mapendekezo ya Serikali yafuate.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali ilishaleta mabadiliko kuwa anayeteua Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi sio Waziri ni Rais. Sasa Bodi haiwezi ikamshauri Rais, Bodi imeteuliwa na Waziri, Bodi haiwezi ikarudi tena ikamshauri Rais. Rais amechaguliwa na watu mamilioni atashauriwaje na watu 12, lazima tumuamini Rais wetu afanye kazi yake ili aweze kututeulia Mkurugenzi Mkuu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili lingetoka kwa Kamati ningesema pengine Bunge lilikuwa na fikra za upande wa pili. Lakini pendekezo la kubadili huu Muswada wa Sheria lililetwa na Serikali, Serikali

yenyewe kwenye Muswada ambao tumepewa Wabunge iliweka kwamba Waziri ndiye atateua. Inahitaji kupata ufunuo kujua ni nini kiliifanya Serikali ikafikiri tena mara ya pili ikaleta marekebisho ya kwenda kuongeza mamlaka kwa Rais, mamlaka ambayo Rais tayari anayo kwa mujibu wa sheria hii ya kuteua Mwenyekiti wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais tena akateue na Mkurugenzi Mtendaji tunampa Rais mamlaka ambayo mwisho wa siku kazi haifanyi yeye. Kama Rais anateua Wakurugenzi wote, Watendaji wote anateua yeye mtu mmoja tafsiri yake ni nini. Kuna watu wengine wamekaa huko pembeni ndio wanaoteua wanakwenda kupeleka mapendekezo kwa Rais wanasema huyu mteue. Lakini kama tunaiamini hii Bodi ambayo Mwenyekiti wake ameteuliwa na Rais mwenyewe, Wajumbe wameteuliwa na Waziri, tukiiamini hii Bodi itoe mapendekezo tutaweza kwanza kuifanya Bodi yenyewe ijihisi kwamba ina mamlaka, Mkurugenzi atakayeteuliwa atawajibika kwa Bodi, lakini kama Mwenyekiti anateuliwa na Rais, Mkurugenzi wa Bodi anateuliwa na Rais nani atawajibika kwa nani kwa maana uwajibikaji na dhamana ya misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pendekezo sio jipya sana. Nchi yetu ina sheria, nimenukuu hapa kifungu cha Sheria ya Mashirika ya Umma inasema bayana kwamba Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma wanapaswa kuteuliwa na Bodi. Sasa hii ni taasisi ya umma sio Shirika la Umma. Lakini ni taasisi ya umma ipo chini ya Wizara, Rais anakwenda kuteua Mkurugenzi kwa taasisi ambayo iko chini ya Wizara ni ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine tufanye mabadiliko tuanze na haya. Kama sheria za nyuma zilikuwa tofauti tuanze na sheria hizi kwa maslahi ya nchi yetu kuongeza uwajibikaji. Nakushukuru. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Muswada haujaja Bungeni Serikali inaupeleka kwenye Kamati yake inayohusika na Wizara hii. Mwanzoni ilikuwa Waziri ndiyo anamteua Mkurugenzi Mkuu lakini Kamati ikashauri na kwa kweli katika Taasisi nyingi Rais ndiyo anafanya hiyo kazi. Kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba wametoa mapendekezo ya mabadiliko na wameingizwa kwenye *schedule of amendments*. Kwa hiyo, ipo kwenye jedwali la marekebisho.

Kwa hiyo, mimi sidhani kama kuna tatizo hapo. Kwa hiyo, ninachojaribu kueleza hapa ni kwamba usiseme Waziri atashauriwa na Bodi na Rais haiwezekani kushauriwa na Bodi. Kwa hiyo, ninachoeleza ni kwamba haya ni mapendekezo ya Kamati na yamepitishwa na katika *schedule of amendments* na yapo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani iko kwenye *schedule* na mimi nimeiona hapa na marekebisho yapo na kwamba Waziri anatuhakikishia kwamba ni mazingatio ya ushauri wa Kamati. Lakini Mheshimiwa Mnyika ni kwamba hapa ni afadhali ungeshangaa sana kama katika sheria ile ya Mashirika ya Umma ingesema Rais ndiyo anateua kuliko kushangaa huku maana kwenye taasisi haya ni mambo ya kisera sana na Rais ndiyo Mkuu anayeteua Mawaziri na hivyo anaweza kuteua watu wengine kuliko kule. Kwa hiyo, mimi nadhani kidogo kama iko kinyume. Lakini niseme tu kwamba kwa hatua hii tunachofanya ni kupiga kura. Sasa nitawahoji.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mwongozo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna marekebisho mawili. Kuna marekebisho niliyowasilisha mimi. Naamini uamuzi wa sasa unahusu marekebisho niliyowasilisha mimi. Halafu kuna jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Serikali. Sasa kwa mujibu wa Kanuni zetu tunapaswa kuamua jedwali ama rekebisho baada ya rekebisho. Nitaomba tuamue kuhusu mapendekezo niliyowasilisha halafu tuamue kuhusu mapendekezo ya Serikali ili wengine tupate fursa ya kuchangia kuhusu mapendekezo ya Serikali. Kwa sababu ni marekebisho mapya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Labda tu nikueleweshe. Serikali ikileta marekebisho yake hatuwezi kuwahoji tena hapa kwa sababu Muswada ni wa kwao ndiyo walioleta Muswada. Kwa hiyo, hatuwahoji ila tunachukulia kwamba wameona, wameweka mezani na imepokelewa, kwa hiyo, ndiyo maana nahoji hapa; kifungu fulani pamoja na marekebisho ya Serikali kinaafikiwa? Kinaafikiwa. Ila kama kuna Mbunge ambaye ame-*move schedule* yake ni lazima tumpe nafasi na Serikali ijibu. Sasa Serikali kama ikiwasilisha *schedule* yake nani atajibu. Naomba niwahoji, Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashakuru jicho lako limeniona sasa. Lakini nilisimama tulipofika kwenye kifungu hiki.

Mimi hoja yangu iko kwenye kifungu kidogo cha pili. Wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho ya hoja yake alisema Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hii anaweza akaongezewa kipindi cha uongozi cha miaka mitano na kweli kwenye *schedule of amendments* dhana hiyo ya *addition term* ya *five years* ipo. Lakini ule ukomo kwamba ndiyo wa mwisho hakionekani. Lakini ameyasema na yameingia kwenye *Hansard* lakini kwa vile sasa tunatunga sheria ni vizuri basi kwenye eneo hili tulinyooshe na mimi sio mwandishi wa sheria lakini ningeweza kusema tu, *for another final term of five years*. Sasa niiachie Serikali ione kama haya ninayoyasema kwa

maana ya uandishi wa sheria yanakidhi matakwa ya uandishi wa sheria. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa naomba Mwanasheria Mkuu usubiri, nilikuwa naomba tufanye maamuzi ya ile ya Mheshimiwa Mnyika halafu tutakuja kwenye hii. Tutakuwa na *sequence* nzuri kidogo na kwa kuwa hatua za kumpa fursa ya kutoa hoja yake Mheshimiwa Mnyika iliyopo kwenye *schedule* na tulikuwa kwenye hatua ya kupiga kura na nilishahoji sehemu ya kwanza ya wanaounga mkono msimamo wa Serikali.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Sasa tunakuja kwenye hili ambalo amelisema Mheshimiwa Chenge kwa ajili ya kuweka utungaji sawasawa. Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yaliyopo kwenye *schedule of amendments* na haya ambayo Mheshimiwa Chenge amezungumza ninashauri tukubaliane kwamba yasomeke *for an addition final term of five years* kama alivyosema nakubaliana nae. Lakini pia kwenye kifungu kidogo cha tano kwa sababu Mheshimiwa Waziri alipokuwa anahitimisha alisema Mkurugenzi Mkuu peke yake anatosha na hakuna haja ya kuwa na *Deputy Director.*

Nilikuwa napenda kwamba kifungu kidogo cha tano kifutwe na kikishafutwa yanayobaki ni ya uandishi kwenye 13(1) sentensi ya mwisho inaposema *as the Minister may specify in the letters of appointments* kwa sababu ni mmoja sasa iwe ni *letter of appointment.* Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, itabidi nihoji tena eneo hili, ufafanuzi uliotolewa na Serikali juu ya marekebisho haya na ufutwaji wa kifungu kile cha tano na pale kwenye 13(2) kwenye muda unaongezeka kwa maelezo aliyotoa na

*Hansard* nafikiri imechukua. Eneo hilo la kifungu hicho linaafikiwa?

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuondoa mapendekezo yangu ya marekebisho kwenye hicho kifungu.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

**MWENYEKITI:** Kifungu 32 kina marekebisho ya Mheshimiwa Mnyika. Nimekuona Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwangu ni dogo sana. Kwenye hiyo Ibara ya 32(1) mstari wa mwisho tunaongelea mwaka wa fedha wa taasisi. Sasa nadhani neno 31 pale ya Juni, imewekwa kwa makosa. Ilipaswa iwe 30 Juni, hakuna tarehe 31 Juni. Nadhani ilikuwa ni hilo. Lakini kwa kutegemeana na haya yanayokuja kwenye marekebisho ya hoja nime-*register* pia baadae. Kwa hiyo, utambue kusimama kwangu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge na mamlaka ya Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 ni pamoja na kupitisha bajeti. Sasa kwenye kifungu cha 32(6), kinasema kwamba Waziri baada ya kupokea bajeti ya mwaka au bajeti ya nyongeza ataikubali au ataikataa bajeti au nyongeza ya bajeti kwa kuzingatia marekebisho yoyote ambayo anaweza kuona yanafaa.

Kwa hiyo, bajeti ya taasisi hii itapitishwa na Waziri na Mheshimiwa Waziri katika majibu yake wakati wa majumuisho alisema hili ni jambo la kawaida kwa sababu hii ni taasisi chini ya Wizara na bajeti za idara na taasisi zake zinapitishwa kwa

utaratibu huo. Kwa maana ya mazoea na mifumo ya sasa ya kitaasisi inaonekana ni jambo la kawaida. Lakini kumekuwa na *tendency* ya taasisi mbalimbali za Serikali na Mashirika ya Umma kupanga bajeti na kinachokuja Bungeni ni sehemu ndogo tu za bajeti zao inayohusu ruzuku inayotoka kwenye Serikali. Lakini taasisi hizi na mimi ni Waziri Kivuli wa Nishati na Madini najua kule kuna *TANESCO, TPDC, EWURA,* zinakusanya mapato, zinatengeneza bajeti lakini bajeti zinaishia kwenye Wizara zenye dhamana isipokuwa kwenye vifungu vichache vinavyokuja kupitishwa Bungeni.

Sasa utamaduni huu unahitaji kubadilika na natambua kwamba kuna sheria ya nchi yetu. Sheria namba nne inayohusu masuala ya Katiba ambayo imeweka mamlaka kwa mihimili hii. Sasa kwa misingi hiyo hiyo ya sheria hiyo tunaweza kwa kuanzia maana hata baadae itabidi hiyo sheria ifanyiwe marekebisho. Kwa kuanzia tutakubali tukaongeza kifungu kidogo kwenye hiki kifungu cha saba ambacho kitasomeka; *"the Minister shall, as soon as practicable after lay before the responsible Parliamentary Committee the approved annual budget and supplementary budget of the institute."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kifungu hiki kitakubalika hakipokonyi mamlaka ya Waziri ambayo kwa mujibu wa utaratibu wa sasa ambayo baadae itabidi ifanyiwe mabadiliko ya kutunga bajeti. Lakini baada ya Waziri kuipitisha, Kamati husika ya Bunge ipewe hiyo bajeti na jambo hili halitakuwa jipya sana. Uganda wana mfumo wa namna hii. Tofauti ni kwamba Uganda wana sheria inaitwa *Parliamentary Budget Office* ambayo inatoa fursa. Kwa sababu kengele imelia ninahitaji ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Labda kabla ya ufafanuzi maana *schedule* yenyewe hii kama ndiyo hii niliyonayo sina hakika kama ipo sawasawa kwa maana ya kiingereza hapa; *"the Minister shall, as soon as practicable after lay before the responsible…"* naona kama neno *after* linapaswa kuondolewa. Kwa hiyo, ni

*amendment of the amendment,* haya. Lakini kabla hatujafikia kwenye hatua ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri nafikiri kwa mamlaka ninayopewa na Kanuni ya 28(5) nitaongeza dakika 30 ili tuweze kumaliza shughuli yetu. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mihimili hii kwa maana ya Serikali, mipango inapangwa na Serikali, Serikali ndiyo ina *executive power* za kupanga mipango. Sasa kule Wizarani kinachofanyika ni kuridhia tu. Lakini wanaopitisha bajeti ni Bunge ndiyo maana tunakuja hapa mwezi wa sita mpaka mwezi wa tisa tunajadili bajeti za Wizara hadi Wizara zingine kuzikubali na kuzirekebisha hapa na pale. Lakini kule Wizarani lazima tukae tukubaliane kwamba hapa iwe hivi na hivi, ni lazima niridhie kama Waziri. Siwezi nikasema bajeti ya Wizara ya Mifugo ni trilioni 13 halafu nilete Bungeni. Lazima kule tukae tuzungumze kutokana na *ceilings* ambazo tumepewa. Kwa maana hiyo kule Wizarani mimi sipitishi au Waziri hapitishi bajeti, yeye anaridhia kwamba hii ipo sawa kutokana na *ceiling* ambayo tumepewa. Sasa Bunge ndiyo lenye mamlaka ya kupitisha bajeti ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Kabla sijahoji, Mheshimiwa Chenge ni katika hili hili?

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunatunga sheria ya nchi na tunapofanya kazi hii naomba sana Wajumbe wa Kamati yako tuwe makini kama siku zote. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya Nne inatamka kabisa mamlaka ya utendaji yako wapi. Lakini pia inasema mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma yatakuwa ya Bunge. Sasa pendekezo linaloletwa na Mheshimiwa Mnyika kwa heshima zote linataka kutuletea utaratibu ambao haupo na hatujawahi kuwa na sheria katika nchi hii ambayo ina utaratibu ambao unapendekezwa.

Mheshimiwa Waziri amelielezea vizuri kwa nini isije na sura anayopendekeza Mheshimiwa Mnyika, hapa tunaongelea kuidhinisha bajeti ya chombo hiki. Sasa ikishaidhinishwa utekelezaji wake ndiyo inaachiwa sasa bodi ifanye hayo. Lakini kwa vile tumeona fedha na rasilimali za chombo hiki sehemu kubwa inatokana na uamuzi wa Bunge hili kwenye bajeti ya Wizara hilo fungu ndilo litaonekana na ndiyo pale Bunge sasa linakuwa na majukumu yake ya kuweza kuisimamia utekelezaji wa Wizara hii katika eneo hilo. Ndiyo maana nilikuwa nasema nilipoiona hii nikasema yawezekana mwenzetu labda anataka kuleta kitu ambacho tunaweza tukakianza. Huwezi ukakianza kitu kipya bila kwanza kutambua na kutengua msingi ulio kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimesimama kutoa tahadhari hiyo na kuishauri Kamati yako kwamba kwa vyovyote vile pendekezo hili mimi linanisumbua sana kutokana na taaluma yangu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeshauri wachangiaji wakasoma mstari kwa mstari pendekezo lililopo mezani. Hakuna mahali kwenye pendekezo hili ambapo kumetamkwa kwamba Bunge litafanya kazi ya kutunga bajeti ya taasisi kama ambavyo inajaribu kujengwa. Kinachoelezwa hapa ni kwamba bajeti ikishaidhinishwa, iletwe Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inawezekana, tunaweza tukawa tunazungumza lugha tofauti tukiwa na uelewa tofauti. Ukisoma kifungu cha 26 cha hii sheria, vyanzo vya pesa vya hii taasisi; chanzo cha Bunge ni kimoja tu, chanzo A ni chanzo cha pesa kitakachotengwa na Bunge. Hiki kitakuja Bungeni, hata kwa sheria ilivyo sasa kupitia kwa bajeti ya Wizara yenye dhamana. Lakini sheria inakwenda mbele zaidi, inataja vyanzo vingine, kiasi cha fedha ambacho taasisi itapokea kama tuzo kwa huduma, michango, misaada, urithi wa fedha ambayo

bodi inaweza kupokea, kiasi kingine cha fedha ambacho kinaweza kulipwa kwa taasisi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu wangu nimekaa kwenye Bunge hili zaidi ya mwaka mmoja sasa. Tumeshapanga bajeti, ukiletewa bajeti ya mashirika ya umma na taasisi za Serikali, iwe ni *TANESCO, EWURA,* iwe ni *TPDC,* iwe ni taasisi nyingine yoyote, kinachokuja Bungeni kwenye bajeti ya Wizara zile zenye dhamana ni hiki kiwango kilichotengwa na Bunge kwa ajili ya kuchangia kwenye taasisi au matumizi yanayoelekezwa. Lakini haya mashirika yote na taasisi zote, zinakusanya pesa na zinapanga matumizi bila Bunge kujua, bila hata Bunge kutaarifiwa ambacho ni kinyume kabisa ya mamlaka ya Bunge ya kusimamia fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaweza tukaenda na mabadiliko awamu kwa awamu. Hatua *ideal* ingekuwa ni kwa nchi kutunga Muswada wa Sheria ya Bajeti kama wanavyofanya Uganda, tungeweza kufanya hivyo. Kabla ya kutunga hilo, walau kwa sasa tupewe *information* ya hicho ambacho kimepitishwa ili sisi tuweze ku-*play oversight function better* na hatuta-*contradict* Katiba, hatuta-*contradict* sheria yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sasa hivi kwa sheria hii hii, kuna kifungu hapa sasa hivi kwenye hii sheria, kifungu cha 35 na kifungu cha 36 kinalazimisha kwamba ile taasisi hesabu zake za mwaka tuletewe taarifa iwasilishwe Bungeni kama hati inayowasilishwa Bungeni. Sasa sisi tunaletewa hesabu, lakini bajeti iliyopangwa hatuletewi, tunafanyaje kazi ya kuisimamia Serikali?

Kwa hiyo, ni jambo ambalo linawezekana hata kwa sheria za sasa na hatu-*contradict* sheria yoyote kwa kufanya hivyo. Lakini *in the future* tunahitaji marekebisho makubwa zaidi kwa kuwepo na *Parliamentary Budget Office*. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. *In future* tunahitaji, kwa sasa tunafanyaje? Lazima tupige kura, tuamue!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kukataliwa)*

Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Jedwali la1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na kupitisha Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(Tanzania Livestock Research Institute Act, 2012)* na kuupitisha pamoja na marekebisho yake. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liukubali Muswada huu kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki! *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

***Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kutunga Sheria Itakayoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, Kuainisha Kazi na Mamlaka ya Taasisi Kuhusiana na Uendeshaji wa Utafiti wa Mifugo na Kuainisha Masuala Mengine Yanayohusiana nayo (A Bill for an Act to Establish The Tanzania Livestock Research Institute, to Provide for Functions and Powers of the Institute in Relation to the Conduct of Livestock Research and to Provide for the Related Matters)***

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada ukishasomwa kwa mara ya tatu ndiyo tumeshahitimisha utungaji wa sheria na kwa maana hiyo sisi kwa maana ya Bunge tumekamilisha utungaji wa sheria. Kwa maana hiyo tumemaliza kutunga sheria ya *The Tanzania Livestock Research Institute Act* ya mwaka 2011. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana watendaji wa Wizara, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa mliyoifanya na Serikali kwa ujumla. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango na hata tumefikia hatua hii. Sheria ikitungwa siyo ndiyo mwisho wa kila kitu, tunaweza kama pale ambapo mambo hayakwenda vizuri, tukaja tukarekebisha, tukaweka vizuri zaidi. Lakini sasa inangojea hatua ya kwenda kusainiwa na Mhifadhi Mkuu wa Sheria ambaye ni Rais. Niwapongeze sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapa ninalo tangazo, mtakumbuka hivi karibuni Mheshimiwa Rais ameteua Tume ya Kukusanya Maoni kwa ajili ya Kuunda Katiba Mpya na shughuli ya kuwaapisha hao wateule wa Tume itafanyika kesho, na

kwa maana hiyo kwa sababu tukio hilo ni kubwa na ni muhimu na la kihistoria, *TBC* watarusha *live* na hivyo sisi hapa Bungeni tutashindwa kuonekana *live.* Kwa hiyo, nilitaka tu mtambue hivyo kwamba shughuli hiyo itafanyika kesho Dar es Salaam.

**MBUNGE FULANI:** Saa ngapi?

**MWENYEKITI:** Saa ngapi, wewe hujateuliwa, huendi, kwa hiyo hakuna haja ya kujua saa ngapi. Itakuwa kuanzia asubuhi, lakini Naibu Spika atatuwakilisha, amekwenda na Wabunge wenzetu wengine10 na sasa hivi wapo safarini wanaelekea Dar es Salaam kwa ajili ya shughuli hiyo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.50 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 13 Aprili, 2012 saa tatu asubuhi)*

**KIAMBATISHO I**

**ISSN 0856 – 01001X**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***BILL SUPPLEMENT***

***No. 9*** ***23rd December, 2011***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 51 Vol. 92 dated 23rd December, 2011*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

THE TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE ACT, 2011

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

PART 1
PRELIMNARY PROVISIONS

2. Short title and commencement.
3. Application.
4. Interpretation.

PART II
THE TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE

5. Establishment of the Institute.
6. Functions of the Institute.
7. Centres of the Institute.
8. Departments and Sections.

PART III
THE TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE BOARD

9. Establishment of the Board.
10. Functions of the Board.
11. Committees of the Board.
12. Delegation of powers of Board.
13. Direction by the Minister.

PART IV
ADMINISTRATION AND OPERATIONS OF THE INSTITUTE

*(a) Administration*

14. Appointment of Director and Deputy Director.
15. Appointment of other senior officers of the Institute.
16. Employment of other staff.
17. Procedure for appointment.
18. Protection from personal liability.

*(b) Operations of the Institute*

19. Livestock research activities
20. Conduct of research by local researchers
21. Failure to submit final report on research
22. Foreign researchers
23. Termination of research
24. Institute may call for information.
25. Co-ordination of research carried outside Mainland Tanzania.
26. Provisions relating to discoveries.

PART V
FINANCIAL PROVISIONS

27. Funds of Institute.
28. Remuneration of members of the Board..

29. Terminal benefits.
30. Power of Board to charge fees.
31. Investment of funds.
32. Power to borrow.
33. Annual and supplementary budget.
34. Budget implementation.
35. Accounts and audit.
36. Annual report.
37. Laying of accounts before National Assembly.

PART VI
GENERAL PROVISIONS

38. Offences and penalties.
39. Powers of the Minister to make regulations.

---

SCHEDULES

---

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam PHILLEMON L. LUHANJO,
17th October, 2011 *Secretary to the Cabinet*

# A BILL

*for*

**An Act to establish the Tanzania Livestock Research Institute; to provide for functions and powers of the Institute in relation to the conduct of research on livestock production and to provide for other related matters.**

ENACTED by Parliament of the United Republic of Tanzania.

## PART I
## PRELIMINARY PROVISIONS

Short title and commencement

1. This Act may be cited as the Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011 and shall come into operation on such date as the Minister may, by notice published in the *Gazette*, appoint.

Application

2. This Act shall apply to Mainland Tanzania.

Interpretation

3. In this Act, unless the context require otherwise:

"animal" means any vertebrate or invertebrate other than human being;

"Board" means the Board of the Institute established by section 8;

"bio-safety" means protection of the health of livestock and human beings from diseases;

"bio-technology" means the use of biological systems to produce a product, process or services;

"Centre" means a Livestock Research Centre established or deemed to have been established by, or under section 6;

"Director" means the Director of the Institute, appointed under section 13 (1);

"diseases" means any deviation from normal physiological functioning of the body and includes the clinical and pathological manifestation;

"foreign researcher" means a researcher who is not a citizen of Tanzania;

"gene bank" means a physical repository in one or more locations where samples of animal or plant genetic resource populations are being preserved or kept, and includes embryos, oocytes, sperms, ova and Deoxyribo Nucleic Acid material;

"Institute" means the Tanzania Livestock Research Institute, established under this Act;

"laboratory" means a properly equipped institution staffed by technically competent personnel;

"livestock" means any domesticated animals and includes cattle, sheep, goats, pigs, chicken, dogs, cats, donkeys and game;

"local researcher" means a researcher who is a citizen of Tanzania;

"member" in relation to the Board, means a member of the Board appointed under section 8;

"Minister" means the Minister responsible for livestock;

"research" means any systematic study conducted in order to develop, verify and disseminate appropriate technologies for the benefit of stakeholders in the livestock industry; and

"researcher" means a graduate trained to design and implement research protocols, collect, analyse and interpret data relating to livestock, and report results in a scientific format.

## PART II
## THE TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE

Establishment of the Institute

4.-(1) There shall be an Institute to be known as the Tanzania Livestock Research Institute also known by acronym TALIRI.

(2) The Institute shall be a body corporate and shall—

(a) have perpetual succession and an official seal;

(b) in its corporate name, be capable of suing and being sued;

(c) subject to this Act, be capable of holding, purchasing, or acquiring in any other way, any movable or immovable property, and of disposing of any of its property;

(d) have all the rights and privileges of a natural person;

(e) in its own name, enter into contracts and agreements; and

(f) subject to section 31, have power to borrow such sums as it may require for its purpose.

Functions of the Institute

5-(1) The functions of the Institute shall be to—

(a) carry out research on—

(i) livestock breeding development and promotion of high yielding breeds;

(ii) production, processing, storage, utilization and marketing of animal products and by-products;

(iii) pasture and forage development, management and utilization and livestock nutrition including feeding and feedstuff evaluation;

(iv) proper utilization and management of rangeland resources;

(v) animal husbandry aspects including animal welfare and organic livestock farming;

(vi) animal health;

(vii) socio-economic aspects of the livestock industry; and

(viii) local and indigenous knowledge in animal production;

(b) plan, undertake, aid, promote and co-ordinate research and its application in livestock production and allied sciences;

(c) set national priorities and harmonize livestock research activities of the public livestock research institutes, civil society organizations, private sectors and farmers organizations;

(d) develop mechanism for assessment of progress and updating the livestock research programmes;

(e) provide guidelines, guidance and ensure delivery of quality livestock research by livestock research service providers;

(f) in collaboration with other relevant agencies, provide policy guidance to local government authorities and other stakeholders on matters relating to livestock research;

(g) provide, undertake and promote consultancy services in the fields of research, education, training and dissemination of information in livestock production and allied sciences;
(h) plan and evaluate the human resources requirements in livestock research;
(i) develop appropriate training programmes and collaborate with other organizations and institutions of higher learning for purposes of attaining high level scientific manpower in livestock production sciences;
(j) coordinate formulation of research standards, codes of ethics, conduct and practice, and guidelines for delivery of livestock research services;
(k) register potential livestock research service providers in the public and private sectors, and maintain a central register of livestock research and development;
(l) keep and maintain gene banks for purposes of characterizing, evaluating and conserving farm animal and forage genetic resources;
(m) promote the use of biotechnology and bio-safety measures to improve livestock production;

(n) collaborate with national, international institutions and individuals in carrying out livestock research;
(o) develop appropriate technologies for the livestock industry in order to increase production and productivity while conserving the environment;
(p) encourage, promote and support investment in livestock research in collaboration with other stakeholders for the purpose of seeking livestock research funds;
(q) strengthen infrastructure and facilities for livestock research, extension, and farmer linkages;
(r) carry out and promote the carrying out of research in livestock production while conserving the environment; and
(s) perform such other functions as are conferred upon TALIRI for the purpose of promoting livestock research and development.

(2) Without prejudice to the generality of subsection (1), the Institute may carry out and promote basic and applied research or any other type designated to provide effective measures for reference by scientists in co-operation with any person within or outside Mainland Tanzania.

(3) For the purposes of the better performance of its functions, the Institute shall establish and maintain a system of consultation and cooperation with any person having functions related to those specified in subsection (1) or which relate to livestock or environmental research or to scientific development generally.

Centres of the Institute

6.-(1) The Minister shall, upon the advice of the Board, establish such number of centres of the Institute for the purpose of performing functions of the Institute as may be required.

(2) The Centres specified in the First Schedule to this Act shall be deemed to have been established under this section and the control and management of their business and affairs is hereby vested in the Institute.

(3) The Minister may, upon advice of the Board and by order published in the *Gazette*, amend, add to, vary or replace the names of the Centres specified in the First Schedule.

(4) The Minister may, after consultation with the Board and by order published in the *Gazette*, establish other Centres and vest in the Institute the control and management of the business and affairs of the Centres.

(5) The Institute shall, upon application in terms of the provisions of the relevant laws, be granted a right of occupancy over the land on which a Centre exists or is intended to be established.

(6) All land held by the Institute in accordance with this section shall be exclusively used for the purposes of the livestock research, and the Institute may, in relation to the land—

(a) manage or use it in such manner as may be desirable for the better performance of the functions of the Institute;
(b) graze livestock and do any other thing in relation to the land or livestock;
(c) enforce within that area of land, such restrictions or regulations as the Board may approve; or
(d) provide for the depositing and propagating of species of livestock as the Board may, with the advice of the Director, determine for the purpose of improving, conserving or experimenting such species of livestock.

Departments and sections

7. The Institute may form such number of departments and sections or units with prescribed functions as the Board may determine.

PART III
THE TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE BOARD

Establishment of the Board

8.-(1) There is established a board to be known as the Tanzania Livestock Research Institute Board.

(2) The Board shall consist of the Chairman to be appointed by the

President from amongst persons with knowledge and experience in livestock and other members to be appointed by the Minister as follows:

(a) a representative from university faculty responsible for livestock sciences;

(b) a representative from the professional association responsible for animal production;

(c) a representative from the Ministry responsible for crop research;

(d) a representative from the Ministry responsible for livestock research;

(e) the Director of Central Veterinary Laboratory; and

(f) two representatives from private sector organizations dealing with livestock industry.

(3) The provisions of the Second Schedule to this Act shall have effect in respect of the tenure of office of members, proceedings of the Board and other matters relating to the Board.

(4) The Minister may, by order published in the *Gazette*, amend the Second Schedule.

(5) The Director shall be the secretary to the Board.

Functions of the Board

9.-(1) The Board shall, subject to the provisions of this Act, be responsible for the performance of the functions and management of the affairs of the Institute.

(2) Without prejudice to the generality of subsection (1), the functions of the Board shall be to—

(b) advise the Minister on all matters relating to livestock research;
(c) ensure efficiency in the performance of the Institute;
(d) employ or authorize employment of staff of the Institute;
(e) approve budgets of the Institute;
(f) advise the Minister on the establishment of centres under this Act;
(g) issue directives to the Director on the performance of his functions;
(h) determine and charge fees for services rendered under this Act; and
(i) perform such other functions as may be directed by the Minister.

Committees of the Board

10.-(1) The Board may, for purposes of facilitating performance of its functions and upon such terms and conditions as the Board may specify, form committees to perform any specific functions.

(2) The provisions of the Second Schedule to this Act shall, unless otherwise stated in writing by the Board, apply *mutatis mutandis* in relation to the committees and sub-committees appointed under this section.

Delegation of powers of the Board

11.-(1) Subject to subsection (4), the Board may, upon such terms and conditions as it may determine, delegate to a committee or to any employee of the Institute any of its functions under this Act.

(2) A delegation may be made to the holder of an office, under the Institute specifying the office but without naming the holder, and in that case each successive holder of the office in question, and each person who occupies or performs the duties of that office, may, without any further authority, exercise the delegated functions or powers in accordance with the delegation made.

(3) The Board may revoke a delegation made and no delegation so made shall prevent the Board from exercising the function or power delegated.

(4) The Board shall not delegate its power of delegation or the power to approve the annual budget, the annual balance sheet or a statement of accounts.

Direction by the Minister

12. The Minister may, subject to the provisions of this Act, give to the Board directives of a general or specific nature regarding the performance of functions by the Institute and the Board shall give effect to such directives.

## PART IV
## ADMINISTRATION AND OPERATIONS OF THE INSTITUTE

### *(a) Administration*

Appointment of Director and Deputy Director

13.-(1) The Minister shall appoint a Director and Deputy Director from amongst persons with knowledge and experience in research on livestock production and upon such terms and

conditions as the Minister may specify in the letters of appointment.

(2) The Director shall hold office for a term of five years and may be eligible for re-appointment subject to his satisfactory performance.

(3) The Director shall-

(a) be the chief executive officer of the Institute;

(b) be responsible to the Board for administration and management of the Institute;

(c) be a disciplinary authority in respect of the staff of the Institute; and

(d) discharge such other duties relating to the Institute as may be directed by the Board.

(4) In the discharge of duty, the Director may, subject to such general or specific directions given to him by the Board, issue operational guidelines to all or to any of the officer in-charge.

(5) The Deputy Director shall be the principal assistant of the Director and shall perform all functions of the Institute as may be assigned to him by the Director or the Board.

Appointment of other senior officers of the Institute

14.-(1) The Board shall, in respect of each centre, department and section of the Institute, appoint qualified persons from amongst senior officers to be officers in charge of the Centre, Heads of Departments and Head of Sections.

(2) The terms and conditions for appointment under this section shall be prescribed in the letters of appointment.

Employment of other staff

15.-(1) The Board may employ such number of other professional and non-professional employees of the Institute as it may consider necessary for the proper and efficient conduct of the business and activities of the Institute.

(2) Subject to sub-section (1), remunerations and other matters relating to the employees of the Institute shall be prescribed by regulations.

(3) Subject to the general or specific directions given by the Board in that behalf, the Director may employ such number of supporting staff for the proper performance of the functions of the Institute.

Procedure for appointment

16. The Minister may, by regulations, prescribe procedures for appointment of various categories of employees and other staff of the Institute.

Protection from personal liability

17. No act or thing done in good faith by any member of the Board or a committee or by any employee of the Institute in the execution or purported execution of his duties under this Act shall render such member or employee personally liable for the act or thing done.

*(b) Operations of the Institute*

Livestock research activities

18.-(1) Research on livestock carried out by the Institute shall focus on the following areas:

(a) milk – dairy cattle, dairy goats and other milch animals;
(b) meat – beef cattle, sheep, goats, poultry and pigs;
(c) livestock by-products – hides and skins;
(d) animal feed resources; pastures and forages, compounded feeds, crop residues;
(e) animal genetic resources of cattle, sheep, goats, chicken, ducks, pigeons and other livestock species;
(f) animal health;
(g) draught power, biogas, animal welfare;
(h) value addition, marketing and trade as well as policy;
(i) socio-economic aspects of livestock production; and
(j) any other area the Board may consider necessary.

(2) In undertaking research activities, the Institute shall-

(a) ensure that research is carried out in accordance with the standards prescribed by guidelines;
(b) be responsible for-
    (i) the management and reporting of the study to the Institute; and
    (ii) co-ordinating the co-researchers who take the

lead at each site involved in the study.

Conduct of research by local researcher

19.-(1) A person who wishes to conduct research on livestock shall develop a proposal in an identified priority research area and furnish the proposal to the Institute for approval.

(2) The proposal shall contain the following:

(a) title of the intended research;
(b) background information;
(c) materials and methods to be used;
(d) cost of research and source of funding;
(e) results on data analysis; and
(f) references or bibliography.

(3) The Institute shall, where it is satisfied with the contents of the proposal and within fourteen days, approve the proposal.

(4) The Institute shall, where it has approved the proposal under subsection (3) -

(a) determine the provision of funds for the approved research proposal;
(b) specify a timeframe within which the proposed research shall be accomplished; and
(c) require the researcher to submit his completed research to the Institute for registration and custody.

(5) A researcher whose proposal is approved under this sections shall be obliged to furnish the Institute with the

progress report on the research at such intervals as the Institute may determine.

Failure to submit final report on research

20. A researcher who fails or refuses to submit to the Institute the final report of the research as required under section 19, commits an offence and on conviction is liable-

(a) in the case of local researcher, to a fine not less than ten million shillings or to imprisonment for a term of six months;

(b) in the case of foreign researcher, to a fine not less than twenty million shillings or to imprisonment for a term of one year.

Foreign researchers

21.-(1) A foreign researcher who wishes to carry out research under this Act shall, prior to submission of research proposal to the Institute, apply to the Commission for Science and Technology for certificate of clearance.

(2) The Institute shall, upon approval of the proposal submitted by foreign researcher, ensure that the foreign researcher has a local co-researcher.

(3) Notwithstanding subsection (2), the Institute shall not approve the research proposal by foreign researcher if the foreign researcher has no local co-researcher.

(4) The provisions of sections 18 and 19 shall apply *mutatis mutandis* to foreign researcher.

Termination of research

22. Where the researcher-

(a) fails, without good cause, to submit the progress report within the intervals as determined by the Institute; or

(b) submits a report which is not satisfactory,

the Institute may terminate the research and require the researcher to refund the Institute all the funds granted to him for the purpose of the terminated research.

Institute may call for information

23.-(1) The Institute may, in writing, require any person who engages in livestock research or other allied scientific research to provide to the Institute information relating to the research or other allied scientific research conducted as the Institute may specify.

(2) A person who fails or refuses to submit information as required under subsection (1), commits on offence and shall be liable, on conviction to a fine not exceeding two million shillings or to imprisonment for a term not exceeding twelve months.

Co-ordination of researches carried out outside Tanzania

24.-(1) Where a person desires to sponsor any livestock production research using scientific materials from Tanzania to be carried out outside the country or to make payments for the purpose of participating in livestock production research project outside Tanzania using

such materials, that person shall submit in writing his proposal to the Director.

(2) Upon receipt of proposals submitted pursuant to subsection (1), the Director shall within seven days after consultation with the person who submitted the proposals, make the decision on the proposal for the best interests of livestock research or other allied scientific research in Tanzania.

(3) Every decision made by the Director under subsection (2) shall be binding upon persons to whom the proposal relates.

(4) A person who is aggrieved by the decision of the Director may, within twenty one days from the date of such decision, appeal to the Board.

(5) For the purpose of giving effect to the provisions of this section, the Board may issue guidelines specifying the conditions to be considered in making proposals and matters which the Director shall take into consideration in making any decision under this section.

(6) The Minister may, in writing, exempt any person from the provisions of subsection (1).

Provisions relating to discoveries

25.-(1) Where as a result of any research carried out by or on behalf of the Institute anything is discovered, the discovery shall become the property of the Institute.

(2) The Institute may, for the purposes of commercial exploitation of any discovery which the Institute considers

important for the improvement of animal production, arrange with any person to buy, sell, take or grant patent rights in the discovery, subject to such terms and conditions as the Board may determine.

(3) Every discovery made as a result of livestock production research or other allied scientific research carried out under this Act shall be registered by the Institute in such form and upon such conditions as the Minister may, by regulations prescribe.

(4) The Institute shall, a with the prior approval of the Minister, develop a rewarding system and grant reward to any person who makes a discovery or who materially assist or contributes to the making of that discovery to appreciate and honour the researcher.

## PART V
## FINANCIAL PROVISIONS

Funds of the Institute

26. The funds and resources of the Institute shall consist of—

(a) such sums as may be appropriated by Parliament;
(b) such sums as the Institute may receive as fees for any services rendered;
(c) such donations, grants, bequests and loans as the Board may receive from any person; and
(d) any sums or property which may become payable to the Institute under this Act.

Remuneration of members of the Board

27.-(1) The members of the Board shall be entitled to such remuneration or allowances as the Minister may, upon the recommendation of the Board, prescribe.

(2) The Minister shall, in excising his power under subsection (1), have regard to the advice of the Treasury Registrar.

Terminal benefits

28. Subject to the provisions of any written law for the time being in force relating to pensions, the Board shall ensure that gratuities or other retirement allowances or benefits are granted to the employees of the Institute.

Power of Board to charge fees

29. The Board may, for the proper performance of the functions of the Institute, charge fees for any services or category of services rendered by the Institute, subject to any directions which the Minister may issue.

Investment of funds
Cap. 53

30. With the prior approval of the Minister, the Board may, invest any part of the moneys available in any fund of the Institute as is authorized in relation to investment of fund by a trustee under the Trustees Investments Act.

Power to borrow

31. The Board may, with prior approval of the Minister, borrow moneys for the purposes of the Institute by way of loan or overdraft, and upon such security and on such terms and conditions relating to the repayment of the principal and payment of interest as the Board may consider appropriate.

Annual and Supplementary Budget

32.-(1) Subject to subsection (2), "a financial year" in this Act means any period not exceeding twelve consecutive months commencing from the 1st day of July to the 31st day of June, of each year.

(2) The first financial year of the Institute shall commence, on the date when this Act comes into operation and may be of a period longer or shorter than twelve months.

(3) Not less than two months before the beginning of every financial year the Board shall, at a meeting, pass a detailed budget of the amounts respectively expected to be received and expected to be disbursed, by the Institute during that financial year, and whenever circumstances so require, the Board may pass a supplementary budget in any financial year.

(4) The annual budget and every supplementary budget shall be in such form and include such details as the Minister may approve.

(5) Upon passing any budget or any supplementary budget, the Board shall submit to the Minister for his approval the annual budget or the supplementary budget.

(6) The Minister shall, upon receipt of the annual budget or supplementary budget, approve, disapprove, or may approve the budget or supplementary budget subject to any amendments which he may consider necessary.

Budget implementation

33.-(1) Where the Minister approves any annual or supplementary budget with or without amendment, the budget, as approved by him, shall be binding on the Board which, subject to subsection (2), shall confine the disbursements of the Institute within the items and amounts contained in the applicable estimates, as approved by the Minister.

(2) The Board may—

(a) with the written sanction of the Minister, make a disbursement notwithstanding that disbursement is not provided for in any budget;

(b) adjust expenditure limits to take account of circumstances not reasonably foreseeable at the time the budget was prepared, subject to submitting a supplementary budget to the Minister within two months of the alteration of expenditure limits become necessary.

Accounts and Audit

34.-(1) The Board shall cause to be provided and kept proper books of accounts and records with respect to—

(a) the receipt and expenditure of money by, and other financial transactions of the Institute;

(b) the assets and liabilities of the Institute,

and shall cause to be made out for every financial year a balance sheet showing the details of the income and expenditure

of the Institute and all its assets and liabilities.

(2) Within three months of the close of every financial year the accounts, including the balance sheet, of the Institute in respect of that financial year shall be audited in accordance with the Public Audit Act.

Cap. 418

(3) Every audited accounts shall be placed before a meeting of the Board which, if adopted, shall be endorsed with a certificate that it has been so adopted.

(4) As soon as the accounts of the Institute have been audited, and in any case not later than six months after the close of the financial year, the Board shall submit to the Minister a copy of the audited statement of accounts, together with a copy of the report made by the auditors on the statement of accounts.

Annual report

35. The Board shall, within six months after the close of the financial year, cause to be prepared and submitted to the Minister a report on activities and operations undertaken by the Institute during that financial year and accompanied by—

(a) a copy of the audited accounts;
(b) a copy of the auditors' report on the accounts; and
(c) such other information as the Minister may direct.

Laying of accounts before National

36. The Minister shall, as soon as practicable after receiving the reports, lay before the National Assembly the audited

Assembly

accounts of the Institute together with the auditors' report of the accounts and the annual report of the Institute.

PART VI
GENERAL PROVISIONS

Offences and penalties

37. A person who is convicted of an offence under this Act to which no specific penalty has been prescribed shall be liable:

(a) in the case of an individual, to a fine of not less than five hundred thousand shillings and not exceeding one million shillings, or imprisonment for a term of six months or to both such fine and imprisonment;

(b) in the case of a continuing offence, to a further fine of not less than one hundred thousand shillings for each day during which the offence continues; and

(c) in the case of a corporation, to a fine of not less than one million shillings and in the case of a continuing offence, to a further fine of not less than five hundred thousand shillings for each day during which the offence continues.

Power of Minister to make regulations

38.-(1) The Minister may, upon advice by the Board, make regulations for the better carrying out the provisions of this Act.

(2) Without prejudice to the

generality of the power conferred by subsection (1), the Minister may make regulations—

(a) requiring persons who engage in livestock or other allied scientific research to furnish the Institute with information relating to any aspect of their activities;

(b) prescribing the form, manner and the period within which an information shall be furnished or made available to the Institute;

(c) regulating the involvement of the Institute in the conservation and management of livestock or the collection and use of livestock and livestock products;

(d) regulating the utilization by specified institutions engaged in livestock research or livestock industry, of the technical expertise and services of the Institute in environment or livestock conservation, or in the management, collection or use of livestock or livestock products;

(e) prescribing national standards for establishment of a livestock research centre;

(f) prescribing the procedure for the submission to the Institute of proposals for the carrying out of research into any particular aspect of livestock;

(g) prescribing the manner in which proposals for the carrying out of research shall be dealt with by the

Institute;

(h) prescribing the powers, rights and obligations of persons carrying out research;

(i) prescribing procedures for appeals under this Act;

(j) prescribing standards and ethics for carrying out research activities under this Act;

(k) prescribing the procedure to be adopted with regard to livestock research being carried out on behalf of, or for the benefit of, the Institute;

(l) prescribing rewarding systems for researchers under this Act; and

(m) prescribing any other regulations for livestock production research pursuant to this Act.

## FIRST SCHEDULE

*(Made under section 6(2))*

LIVESTOCK RESEARCH CENTRES

1. Livestock Research Centre Mpwapwa
2. Livestock Research Centre – Kongwa;
3. Livestock Research Centre –Mabuki;
4. Livestock Research Centre – Naliendele;
5. Livestock Research Centre – Tanga;
6. Livestock Research Centre – West Kilimanjaro
7. Livestock Research Centre – Uyole

## SECOND SCHEDULE

(Under section 8(3))

PROVISIONS RELATING TO THE BOARD

Vice-Chairman

1. The members shall elect one of their members to be the Vice-chairman of the Board and any member so elected shall, subject to his continuing to be a member, hold office for a term of one year from the date of his election, and may be eligible for re-election.

Tenure of office for Board members

2.-(1) Subject to sub-paragraph (2), a member of the Board shall unless his appointment is sooner terminated by the appointing authority, or he otherwise ceases to be a member, hold office for such period as the appointing authority may specify in his appointment, or if no period is so specified, shall hold office for term of three years from the date of his appointment, and is eligible for re-appointment.

(2) In the case of the member who is a member by virtue of his holding some other office, he shall cease to be a member upon his ceasing to hold that office.

(3) Any member, other than member referred to in sub-paragraph (2), may at any time resign by giving notice in writing to the Minister, and upon receipt of the notice by the Minister, he shall cease to be a member.

Absent member may be represented at meetings

3. If a member of the Board who is a member by virtue of his holding some other office is unable for any reason to attend any meeting of the Board, he may nominate in writing another person from his organization to attend that meeting in his behalf.

Vacancies in the Board

4. Where any member ceases to be a member for any reason before the expiration of his term of office, the appointing authority may appoint another person in his place and the persons so appointed shall hold office for the remainder of term of office of his predecessor.

Meetings of the Board

5.-(1) The Board shall ordinarily meet for the transaction of its business at the time and at

the place determined by it, but shall meet four times in a year.

(2) The Chairman, or in his absence the Vice-Chairman, may at any time call a special meeting of the Board, and shall call a special meeting upon a written request by the majority of the members in office.

(3) The Chairman, or in his absence the Vice-Chairman, shall preside at every meeting of the Board, in the absence of both Chairman and Vice-Chairman, the members present shall appoint one member amongst themselves to preside over the meeting.

(4) The Chairman, or in his absence the Vice-Chairman, may invite any person who is not a member to participate in the deliberations at any meeting of the Board, but any person so invited shall not be entitled to vote.

Quorum

6. The quorum at any meeting of the Board shall be half of the members in office.

Decision of the Board

7. Questions proposed at a meeting of the Board, shall be decided by a majority of the votes of the members present and voting and in the event of an equality of votes the person presiding shall have a second or casting vote in addition to his original or deliberative vote.

Minutes of Meetings

8.-(1) The Board shall cause to be recorded and kept minutes of all business conducted or transacted at its meetings, and the minutes of each meeting of the Board shall be read and confirmed, or amended and confirmed, at the next meeting of the Board and signed by the person presiding at the meeting.

(2) Any minutes purporting to be signed by the person presiding at a meeting of the Board shall, in the absence of proof of error, be deemed to be a correct record of the meeting whose minutes they purport to be.

Vacancies not to invalidate proceedings

9. The validity of any act or proceeding of the Board shall not be affected by any vacancy among its members or by any defect in the appointment of any of them.

Orders, directions etc.

10. All orders, directions, notices or documents made or issued on behalf of the Board shall be signed by:

(a) the Chairman of the Board; or

(b) the Director or any other officer of the National Livestock Research Institute authorized in writing in that behalf by the Director.

Seal of the Institute

11. The seal of the Institute shall not be affixed to any instruments except in the presence of the Chairman or the Vice-Chairman or the Director or some other officer of the Institute and at least one member of the Board.

Board may regulate its own proceedings

12. Subject to the provisions of this schedule, the Board may regulate its own proceedings.

---

## OBJECTS AND REASONS

---

This Bill is intended to provide for an enactment of the Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011 with a view to establish the Tanzania Livestock Research Institute, to provide for the functions and powers of the Institute in relation to the conduct of research on livestock production and for other matters connected thereto.

The Bill is divided into six Major Parts.

Part I contains preliminary provisions which include short title and commencement date of the proposed law, application and the interpretation of various terms and phrases used in the proposed Act.

Part II of the Bill contains provisions relating to the establishment of the Tanzania Livestock Research Institute, functions of the Institute, Centres of the Institute and the powers of Institute to form departments and sections.

Part III of this Bill provides for the establishment and composition of the Tanzania Livestock Research Institute Board, functions of the Board, powers of the Board to form various committees for purposes of facilitating the performance of various activities of the Board, powers of the Board to delegate and the directions issued by the Minister.

Part IV of the Bill provides for Administration and Operations of the Tanzania Livestock Research Institute. It makes provisions relating to the appointment and functions of the Director and Deputy Director of the Institute, appointment of senior officers of the Institute, employment of other staff of the Institute and the procedure for appointment. It further

stipulates the areas on which livestock research activities may be carried out, the conduct of research by local researchers, failure to submit final report on research, the conduct of research by foreign researchers and the termination of research. Moreover, it provides for powers of the institute to call for information,, discoveries made as a result of livestock research and the co-ordination of research carried outside Mainland Tanzania.

Part V provides for Financial provisions. It contains provisions relating to Funds of the institute, remuneration of members of the Board and Institute, investment of funds, accounts and audit, annual report and Laying of accounts before National Assembly.

Part VI provides for offences and penalties under the proposed law and powers of Minister to make Regulations.

Dar es Salaam,<br>04 October, 2011

DAVID M. DAVID,<br>*Minister for Livestock and Fisheries Development*

**KIAMBATISHO II**

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. DAVID M. DAVID, MINISTER FOR LIVESTOCK DEVELOPMENT AND FISHERIES AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE ACT, 2011"**

*(Made under S. O. 86 (10) (b))*

A Bill entitled "The Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011" is generally amended as follows:

**A:** In the long title, by deleting the phrase "research on livestock production" and substituting for it the words "livestock research".

**B:** In Clause 3, by-

(a) deleting the definition of the term "Centre" and substituting for it the following new definition:

"Centre" means a Livestock Research Centre established by, or deemed to have been established under section 6;";

(b) deleting the term "Director" and substituting for it the term "Director General";

(c) deleting the word "institution" appearing in the definition of the term "laboratory" and substituting for it the word "facility";

(d) deleting the words "in relation to the Board," appearing in the definition of the term "member";

(e) deleting the word "graduate" appearing in the definition of the term "researcher" and substituting for it the word "person";

(f) inserting in its appropriate alphabetical order, the following new definition:

"Deputy Director" means the Deputy Director of the Institute appointed under section 13";

(g) inserting in its appropriate alphabetical order, the following new definition:

"livestock by-product" includes wool, blood, bones, horns, hooves, bristles, feathers, hair and fur."

**C:** In Clause 5(1),

(a) in paragraph (a), by-

(i) deleting the phrase "and livestock nutrition including feeding" and feedstuff evaluation" appearing, in sub paragraph (iii) and substituting for it the phrase "of livestock feeds";

(ii) adding the words "and diseases" after the words "animal health" appearing in sub paragraph (vi).

(a) in paragraph (n), by deleting that paragraph and substituting for it the following new paragraph:

"(n) collaborate with national, international and regional institutions and stake holders in carrying out livestock research;"

(b) adding the following new paragraph after paragraph (g):

"(h) keep and maintain a database of information relating to livestock research from researchers, institutions and other stakeholders;"

(c) re-naming paragraphs (h) to (s) as paragraphs (i) to (t) respectively.

**D:** In Clause 6(6), by inserting the words "General" after the word "Director" appearing in paragraph (d).

**E:** In Clause 7, by inserting the words ", technical committees" between the word "departments" and the word "and".

**F:** In Clause 8(2), by-

(a) deleting in paragraph (a), the words "livestock sciences" and substituting for them the words "veterinary sciences";

(b) deleting paragraph (b) and substituting for it the following new paragraph:

"(b) a representative from an association of livestock professionals;"

(c) adding immediately after paragraph (b) the following new paragraphs:

"(c) a representative from an institution of higher learning offering a course in livestock production;

(d) a representative from the Commission for Science and Technology;";

(d) renaming paragraphs (c) to (f) as paragraphs (d) to (h) respectively.

**G:** In Clause 9(2), by deleting paragraph (c) and substituting for it the following new paragraph:

"(c) employ or authorize the employment or termination of staff".

**H:** In Clause 13, by-

(a) deleting in sub-clause (1), the designation "Minister" and substituting for it the designation "President";

(b) deleting in sub-clause (2), the phrase "subject to his satisfactory performance" and substituting for it the phrase "for an additional term of five years";

(c) deleting the words "Deputy Director" wherever they appear in the Bill and substituting for them the words "Deputy Director-General".

**I:** In Clause 17, by deleting that Clause and substituting for it the following:

"Protection from personal liability

**17**. Anything done in good faith by any member of the Board or a Committee or by an employee of the Institute in the execution or purported execution of his duties under this Act shall not render such member or employee personally liable for the act or thing done."

**J:** In Clause 18,

(a) by deleting in sub-clause (1), paragraphs (a), (b), (c) and (g) and substituting for them the following new paragraphs:

"(a) milk production;

(b) meat production;

(c) livestock by products;

(g) draught power, biogas, animal welfare and behavior;"

(a) in sub-clause (2), by-

(i) inserting the words "ethics and" between the words "with the" and "standards" appearing in paragraph (a);

(ii) deleting the word "study" appearing in paragraph (b)(i) and substituting for it the words "research outputs"; and

(iii) deleting the sub-paragraph (ii) of paragraph (b) and substituting for it the following new sub-paragraph:

"(ii) coordinating researchers at various Centres;"

**K:** In Clause 19,

(a) in sub-clause (2), by-

(i) deleting the word "and" appearing at the end of paragraph (e);

(ii) deleting the "full stop" appearing at the end of paragraph (f) and substituting for it a "semi colon";

(iii) adding immediately after paragraph (f) the following new paragraph:

"(g) any other information the Institute may consider necessary."

(b) by deleting in sub-clause (3), the word "fourteen" and substituting for it the word "thirty".

**L:** By designating Clause 21 as Clause 20 and Clause 20 as Clause 21;

**M:** By deleting the First Schedule and substituting for it the following new Schedule:

## FIRST SCHEDULE

(Made under section 6(2))

CENTRES OF THE INSTITUTE

1. TALIRI – Mpwapwa;
2. TALIRI – Kongwa;
3. TALIRI – Mabuki;
4. TALIRI – Naliendele;
5. TALIRI – Tanga;
6. TALIRI – West Kilimanjaro;
7. TALIRI – Uyole."

Dodoma,
12th April, 2012

**DMD**
MLFD

OFISI YA BUNGE
12 APR
S.L.P. 941 DODOMA

**KIAMBATISHO III**

## SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. JOHN JOHN MNYIKA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR A BILL ENTITLED THE TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE ACT, 2011"

---

**(Made under Standing Order 86(11) and 88(2)**

---

A Bill entitled "The Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011" is amended as follows:

**A: In clause 8:**
Add (g) in sub clause (2)- "a representative from Ministry responsible for local government and regional administration"

**B: In clause 13:**
Insert in sub clause (1) between "shall" and "appoint" – "upon recommendation of the board"

**C: In clause 24:**
Insert in sub clause (6) between "The Minister" and "may"- "as prescribed by the regulations"

**D: In clause 32:**
Add sub clause- (7) "The Minister shall, as soon as practicable after lay before the responsible parliamentary Committee the approved annual budget and supplementary budget of the institute"

..................................

**JOHN JOHN MNYIKA (MP)**
**UBUNGO CONSTITUENCY**
**12/04/2012**

**KIAMBATISHO IV**

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. GOSBERT BEGUMISA BLANDES, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KARAGWE CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE TANZANIA LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE ACT, 2011"**


---

*(Made under Standing Order 86(9) and (11))*

---

A Bill entitled "The Tanzania Livestock Research Institute Act, 2011" is amended in Clause 8(2) by inserting the following new paragraph:-

"(g) the Director of National Artificial Insemination Centre."



Hon. Gosbert Begumisa Blandes (MP.)
**KARAGWE CONSTITUENCY**